

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Thelathini na Tisa - Tarehe 3 Agosti, 2004

(Mkutano Ulianiza Saa Satu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

MHE. HADIJA K. KUSAGA (k.n.y. MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE):

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 365

Takwimu za Sensa ya 2002

MHE. PAUL P. KIMITI aliuliza:-

Kwa kuwa gharama iliyotumika kwa zoezi lote la sensa ni kubwa sana na tusingependa gharama hiyo ikapotea bila Wananchi kufaidika na matokeo ya sensa hiyo ya mwaka 2002:-

(a) Je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kuhakikisha kuwa takwimu hizo zinawafikia walengwa na wanazitumia kwa mipango yao kuanzia mwaka 2003/2004?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Kamisheni ya Idadi ya Watu ili isimamie shughuli zote hizo za mipango ya watu?

(c) Kwa kuzingatia kuwa sasa kila kaya itakuwa ana daftari la wakazi wake ambao watakuwa wanaandikisha wanaozaliwa, wanaokufa na hata wageni, je, kwa msingi huo kuna haja ya kuwa na sensa nyingine ya watu baada ya miaka kumi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha takwimu za sensa zinawafikia walengwa na wanazitumia katika mipango yao ya maendeleo, Serikali imeandaa mikakati ifuatayo: Kuchapisha na kusambaza taarifa zenye takwimu za sensa kwa wadau mbalimbali, kuweka takwimu za sensa kwenye Tovuti ya Taifa na kuhamasisha utumiaji wake na kutoa mafunzo ya namna ya kutumia takwimu za Sensa kwa Watendaji katika ngazi mbalimbali za Wilaya, Mikoa na Taifa.

Aidha, Bunge lako Tukufu lilikuwa miongoni mwa Taasisi za kwanza za wadau zilizofikishiwa taarifa ya matokeo ya sensa ya mwaka 2002. Hivyo, ni matumaini yetu kwamba, Waheshimiwa Wabunge nao watasaidia katika kuhamasisha na kuelimisha watu mbalimbali wazitumie takwimu zilizopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hoja ya kuwepo Chombo cha Kuratibu Utekelezaji wa Sera ya Idadi ya Watu. Kwa wakati huu Serikali inaendelea na uhuishwaji wa Sera ya Idadi ya Watu ya Mwaka 1992. Rasimu ya sera inapendekeza uundaji wa Baraza la Taifa la Idadi ya Watu na Maendeleo. Kwa hiyo, dhana ya kuanzisha Kamisheni itatekelezwa kuititia Baraza hili.

(c) Mheshimiwa Spika, pamoja na kila kaya kuwa na Daftari la wakazi wake litakalojazwa taarifa za wanaozaliwa, wanaokufa na hata wageni, bado zoezi la sensa ya watu na Makazi linapaswa kufanyika kila baada ya miaka kumi kwa sababu zifuatazo:-

(i) Zoezi la sensa hukusanya takwimu nyingi zaidi ya hizo, kama vile takwimu za elimu, shughuli za kiuchumi zikwemo za sekta rasmi na isiyo rasmi, hali ya ulemavu, hali ya makazi, hali ya ndoa, takwimu zinazopima hali ya umaskini.

(ii) Katika nchi zilizoendelea, pamoja na kwamba wao wanazo kumbukumbu nzuri za vizazi, vifo na uhamaji/uhamiaji kupitia mfumo wa Rejesta hata hivyo wanafanya zoezi la sensa katika kipindi maalum. Njia ambazo nchi hizi hutumia ni kutuma madodoso kwa wahojiba kwa njia ya Posta na njia hii hupunguza gharama za sensa na hutoa fursa ya kulinganisha takwimu za sensa na zile zitokanazo na Rejesta.

(iii) Zoezi la sensa huendeshwa kwa misingi ya kisayansi ili kuweza kupata takwimu sahihi na pia ili takwimu za nchi yetu ziweze kufanana na kulinganishwa na takwimu za nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ni dhahiri kuwa hata kama tunaweza kuwa na mfumo imara wa Daftari la Wakazi kwa kila kaya, bado kutakuwa na umuhimu wa kufanya sensa kila baada ya miaka kumi. Muhimu ni kuendelea kubuni mbinu za kupunguza gharama za sensa kwa kuimarisha kitengo kinachohusika na kufanya baadhi ya kazi za sensa kama vile utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu kuwa kazi ya kudumu.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, Waziri anaweza kutuambia ni kitu gani kilichosababisha ya kwamba Tume au Baraza la Idadi ya Watu na Maendeleo lilishindikana kuanzishwa hapa Tanzania licha ya Viongozi wa Wakuu wa Afrika kuagiza mwaka 1994 ya kwamba kila nchi ya Afrika iunde Baraza hilo? (*Makofi*)

(ii) Pili, ili tuwe na mipango ya uhakika na endelevu katika Sekta mbalimbali, Mheshimiwa Waziri, atakubaliana nami ya kwamba sasa utaratibu wa kuwa na Maafisa Mipango Wasaidizi katika kila Kata, uanzishwe ili tuwe na uhakika kwamba mipango sasa inaanza kwa Wananchi wenyewe katika Mji wao wenyewe na hasa kuanzia Sumbawanga Mjini? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Paul Kimiti, kama Mwenyekiti wa Tume ya Idadi ya Watu Afrika, kwa kuwa mstari wa mbele katika kufuatilia mambo ya idadi ya watu na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, sasa hivi tumeshatayarisha sera ya idadi ya watu ambayo tulitafuta toka mwaka 1992, lakini vilevile sera hiyo inapendekeza uundaji wa Baraza hilo. Kwa vile yote hayo tumeshayatimiza, ni hakika kabisa kwamba, Serikali iko mbioni kuanzisha Baraza hilo kutoptera na maagizo yaliyotolewa na Kamisheni ya Idadi ya Watu ya Afrika.

Ni kweli kwamba, tunahitaji kuimarisha nguzo za kupanga mipango yetu toka ngazi za kaya. Hivi sasa tuna tatizo moja, Chuo chetu cha Mipango Dodoma, kina tatizo la upatikanaji wa rasilimali kwa sababu kila mwaka wanafunzi wanaoomba kuingia pale kujifunza mambo ya mipango wamekuwa ni zaidi ya ile *allocation* iliyokuwepo. Lakini

hili tunalifanyia kazi ili tufundishe wanamipango wengi watakaoanza kupanga toka ngazi za kaya. (*Makof*)

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, ninalo swali dogo la nyongeza.

Kumekuwa na mafanikio ya sensa hii iliyopita, lakini bado Wananchi wengi wanasita kuandikisha ndugu zao hasa pale wanapokufa kule Vijiji au kuzaliwa. Sasa ni jinsi gani Serikali itahamasisha pamoja na majibu yaliyotolewa na Waziri, jinsi ya kuondoa hofu hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, inawezekana katika baadhi ya Vijiji, Wananchi wana wasiwasi wa kuandikisha wale waliozaliwa na wale waliokufa, labda ni kwa sababu ya kutokuelewa. Hapa nadhani suala la msingi ni sisi sote kama Wabunge, kuendelea kuwahamasisha kuwaeleza umuhimu wa kujaza rejesta hizo ili ziweze kusaidia katika kufuatilia idadi ya watu katika Taifa letu mara wakati tunapohitaji takwimu za aina hiyo.

Na. 366

Uwekezaji

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI aliuliza:-

Kwa kuwa yapo baadhi ya Mashirika ambayo *PSRC* imewekeana Mikataba ya Mauzo na Wawekezaji na kwa kuwa ni Wawekezaji wachache tu waliolipa vizuri na waliobakia wanasusasua katika kukamilisha malipo na kwa kuwa Wawekezaji wengi wameshindwa kuyaendeleza Mashirika hayo:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwashughulikia wale Wawekezaji ambao hawajalipa na wale ambao wanasusasua kulipa madeni yao?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kwa hali inavyoendelea, katu, malengo ya ubinafsishaji hayatafanikiwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa baadhi ya Wawekezaji wanashindwa kutekeleza Mikataba ya Mauzo waliyowekeana na Serikali. Aidha, kwa kushindwa kulipia gharama za mauzo au kushindwa kutekeleza mipango ya uwekezaji katika Mashirika hayo. Serikali katika kuhakikisha kuwa Wawekezaji wa Mashirika haya

wanatekeleza Mikataba ya Mauzo ikiwa ni pamoja na kulipia gharama za ununuzi wa Mashirika hayo, imechukua hatua mbalimbali zikiwemo:-

(i) Kuongeza vifungu katika Mikataba hiyo vinavyoipa Serikali nguvu ya Kisheria kutengua Mikataba ya Mauzo kwa kuwanyang'anya Wawekezaji watakaoshindwa kulipia gharama za mauzo au watakaoshindwa kutekeleza mipango ya uwekezaji katika Mashirika yaliyonunuliwa.

(ii) Kuwafanya uchambuzi yakinifu Wawekezaji wote wanaoonyesha nia ya kuwekeza katika Mashirika ya Umma ili kubaini historia yao katika uwekezaji, uwezo wao kifedha, kiteknolojia, ujuzi na uzoefu katika shughuli hizo endapo Wawekezaji wameendelea kuwa na uzoefu katika nyanja hiyo sehemu nyingine duniani.

(iii) Kuhimiza, kutoa maonyo na kuwakumbusha Wawekezaji kupitia barua, majorida na matangazo mbalimbali umuhimu wa kutekeleza makubaliano yaliyomo kwenye Mikataba ya Mauzo ili kuepuka adhabu zinazotokana na kutotekeleza Mikataba hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeajiri Makampuni kumi ya kukusanya madeni ambayo yameweza kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 2,746 kati ya kipindi cha Julai, 2001 hadi Machi, 2004.

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Ni Mashirika gani ambayo hayajalipa madeni yake na wanadaiwa kiasi gani? (*Makofi*)

(ii) Je, Serikali ina mipango gani juu ya wale Wawekezaji ambao hawajaendeleza vizuri Mashirika waliyowekeana Mikataba na Serikali kama vile *TAFICO* na kadhalika? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, bado yako baadhi ya Mashirika mengi ambayo yanadaiwa. Lakini nikiri kwamba, sasa hivi kwa sababu ameulizia kwamba ni kiasi gani yanadaiwa mpaka sasa, takwimu hizo siwezi kuzitoa hapa, mpaka nifanye rejea na ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, tunaweza tukawasiliana ili tukampa idadi ya Mashirika yanayodaiwa.

Lakini pili, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, katika yale Mashirika ambayo Wawekezaji wameshindwa kuyaendeleza, Serikali inafanya utaratibu wa kutafuta Wawekezaji ambao wanaweza kuendeleza Mashirika hayo na vilevile kuendelea kuwakumbusha Wawekezaji hao, kuheshimu Mikataba tuliyowekeana. Mfano mmoja ni Wawekezaji wa *Katani Limited*, ambao walichukua mashamba mengi zaidi ya uwezo wao na katika utaratibu tuliofutilia ni kuwaambia Wawekezaji wengine wenye uwezo wayaendeleze mashamba hayo.

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swalii moja la nyongeza. Wakati Mashirika yanabinafsishwa wapo watu waliochukua Mashirika na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kuna Mashirika yameingiza hasara. Je, zile hasara ambazo zimeingia, watakaohusika na kulipa ni wale waliochukua Mashirika au Serikali yetu? Ahsante sana. (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, kabla ya zoezi la ubinafsishaji kuanza, karibu Mashirika yote yalikuwa yanaingiza hasara na ndiyo maana tukaamua tufuate utaratibu wa kuyabinafsisha Mashirika haya kwa kuhamisha umiliki kutoka Sekta ya Umma kwenda Sekta binafsi. Tatizo moja tunalolipata hivi sasa ni kwamba, pamoja na Wawekezaji wengine kuchukua Mashirika hayo, kutokana na madeni makubwa yaliyojitokeza hapo nyuma, Mashirika haya yamekuwa yakiendelea polepole katika kukarabatiwa kwao. Lakini Serikali inaendelea na jitihada za kuweka vivutio mbalimbali kuwawezesha Wawekezaji hawa hususan Wawekezaji wa ndani ya nchi kuweza kuwapa afueni ya kuweza kuyakarabati na kuyaboresha Mashirika yale. (*Makofî*)

Na.367

Fedha za Mikopo ya Vifaa vya Ujenzi

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkoa wa Singida hadi sasa wapo Walimu wanaodai kurudishiwa fedha walizotoa kwa ajili ya kukopeshwa vifaa vya ujenzi na kadhalika na Mfuko wa Ustawi wa Walimu uliodhaminiwa na TSC na kwa kuwa Walimu hao walikwishatiwa moyo na kurejeshewa fedha hizo:-

- (a) Je, Serikali bado inalikumbuka tatizo hilo?
- (b) Kama inalikumbuka, je, ina mipango gani ya haraka ya kuondoa kero hiyo ambayo imewafanya Walimu hao wakate tamaa na kufikiri kuwa Serikali yao imewadhlumu?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa ufanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, iliyokuwa Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers Service Commission*) ilianzisha Mfuko wenye jina la Inua Hadhi ya Walimu mwaka 1993, ambao ulikuwa na lengo la kuwasaidia Walimu katika kuwapunguzia matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwakopesha vyombo vya usafiri kama vile balskeli, pikipiki na magari, kuwawezesha kununua vifaa vya ujenzi au nyumba zilizokuwa zinazozwa na Shirika la

Nyumba la Taifa na kuwasaidia kulipa ada ya masomo ya watoto na Walimu wanaojiendeza.

Mheshimiwa Spika, uchangiaji wa Mfuko huo ulianza rasmi mwezi Juni, 1997 baada ya baadhi ya Walimu kuelewa madhumuni yake. Mfuko ulianza na mafanikio ambapo Walimu 60 walipewa mikopo ikiwepo 30 ya magari, 16 ya pikipiki, tisa ya nyumba na mitano ya ada za masomo. Baada ya Mfuko kukumbwa na matatizo ya uendeshaji, Wizara yangu kupitia *TSC*, ilichukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kusimamisha kupokea Wanachama wapya, kukagua mahesabu ya Mfuko na kuhakiki madai ya Walimu katika Mfuko kwa kutumia Kamati Maalum iliyoteuliwa na Wizara yangu kufanya kazi hiyo. Aidha, Kamati hiyo ilihakiki madai ya Walimu 188 katika Mikoa yote wakiwemo Walimu 10 wa Mkoa wa Singida waliokuwa wanadai jumla ya shilingi 3,780,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Diana Chilolo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2003/2004, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh.82,690,620/= ili ziweze kutumika kuwarejeshea Walimu fedha zao walizokuwa wamechangia katika Mfuko wa Inua Hadhi ya Mwalimu. Hivi sasa Walimu wote waliokuwa na madai katika Mfuko huo, wamekwishalipwa fedha zao. Kwa hiyo, Serikali haijamsahau Mwalimu yeoyote ambaye alikuwemo katika orodha iliyohakikiwa.

Napenda nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa kuuliza swalii hili ili niweze kutoa tamko kwamba, madai hayo ya Walimu, yamekwishalipwa yote na kama yupo ambaye amebakia, basi awasiliane na Wizara.

Na. 368

Wanafunzi Wanaolazimishwa Kufanya Mitihani ya Binafsi (*Private Candidates*)

MHE. ESTHERINA KILASI aliuliza:-

Kwa kuwa kumejitokeza ushindani wa Shule za Sekondari za watu binafsi kwa kutoa wanafunzi wengi wanaofaulu kwa kiwango cha *Division One* ili kuvutia wanafunzi wengi kujiunga na Shule zinazofanya vizuri na kwa kuwa inapotokea kuwa kuna wanafunzi wanaotegemea kuingia Kidato cha IV na maendeleo yao sio mazuri sana hulazimishwa wafanye mitihani ya binafsi (*Private Candidate*) bila kutumia jina la Shule wanayosoma:-

(a) Je, kuna tofauti yoyote katika utoaji wa alama kati ya wanaofanya mitihani ya *Private* na wanaofanya mitihani ya kawaida ya kupitia Shule wanazosoma na kama zipo ni zipi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kitendo hicho cha kuzuia watoto wasifanye mitihani kwa jina la shule wanazosoma kinapojitokeza kinawanyima haki?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna tofauti katika utoaji wa alama wakati wa kusahihisha mitihani kati ya Watahiniwa wa Shule (*School Candidates*) na Watahiniwa wa kujitegemea (*Private Candidates*). Tofauti inatokea kwenye kutunuku, ambapo 50% ya alama walizopewa Watahiniwa wa Shule hujumlishwa na 50% ya alama za maendeleo ya kila siku darasani (*Continuous Assessment*), wakati alama za Watahiniwa wa kujitegemea, 100% zinatokana na mtihani wa mwisho (*Final Examination*) peke yake.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kitendo cha kuzuia watoto wasifanye mtihani kwa jina la Shule wanayosoma ni kuwanyima haki yao wanafunzi hao na kwa kweli ni kuwaibia wanafunzi hao na wazazi wao karo waliyolipa. Aidha, ni kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Afisa Elimu Kiongozi katika Waraka wa Elimu Na.5 wa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kutamka humu Bungeni kuwa, kuanzia sasa ni marufuku kabisa wanafunzi wa Shulenii kufanya mtihani kama wanafunzi binafsi. Nimekwishatoa maagizo ya kuweka utaratibu wa kompyuta utakaohakikisha kuwa wanafunzi wote waliofaulu mtihani wa Kidato cha Pili na kuingia Kidato cha Tatu, watafanya mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha Nne katika Shule zao walizoingia Kidato cha Tatu. Hatua kali itachukuliwa kwa yejote atakayekiuka utaratibu huo.

MHE. ESTHERINA KILASI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, nina swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa wanafunzi hawa wanaofanya mitihani ya *Private Candidate*, hata wakifafulu vizuri hawapati nafasi ya kuchaguliwa au hawafikiriwi na Serikali kuingia kwenye Shule za Serikali kwenye Kidato cha Tano, je, Serikali ina utaratibu gani kuhakikisha kwamba inarekebisha utaratibu huu pale ambapo mtu amefanya mtihani wa *Private* na amepata *Division One* ili aweze kuchaguliwa kwenda Kidato cha Tano kwenye Shule za Serikali? (*Makofî*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya tatizo hili ilitokana na ufinyu wa nafasi za Kidato cha Tano. Sasa hivi katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari tunaongeza sana nafasi za Kidato cha Tano. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na ushauri wake kwamba, tuweke utaratibu ambapo wote waliofaulu wawe ni watahiniwa wa Shulenii au Watahiniwa wa kujitegemea wapewe fursa sawa kutokana na matokeo ya mitihani. Hilo tutalitekeleza. (*Makofî*)

MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA: Mheshimiwa Spika, kwanza ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na kwa kuwa mwaka huu kuna baadhi ya Shule zilifutiwa matokeo kwa kile kilichoelezwa kwamba ni kutokana na makosa ya udanganyifu na baadhi ya Shule zimefutiwa Vituo vyta Mitihani, sasa kwa sababu katika hizo shule tayari kuna vijana amba wako Kidato cha Nne, Wizara inasema nini? Hawa wanafunzi watatakiwa kufanya mitihani, kama watafanya, hizo alama zao za *Continuous Assessment* zitapatikana namna gani? (*Makofî*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kuna baadhi ya Shule zimefutiwa mitihani ile ya mwaka 2003 na kwamba zimepewa adhabu kwamba, hazitakuwa vituo vyta mitihani kwa muda wa miaka miwili. Huu ni utaratibu wa kawaida kwamba, ilidhahirika kwamba ile mitihani waliyopewa ya mwaka 2003 waliwafanya wanafunzi, kwa hiyo, hawaaminiki kusimamia.

Baraza la Mitihani limeamua kutowaamini kusimamia tena mitihani ya Kidato cha Nne ya Kitaifa, lakini utaratibu umewekwa kwamba, wale wanafunzi amba wako katika Kidato cha Nne mwaka huu na wale walio Kidato cha Tatu amba watakuwa Kidato cha Nne mwaka kesho, watafanya mitihani yao katika Vituo vingine ambavyo Baraza litaelekeza, vitakuwa katika Shule za jirani amba hawajawa na kasoro yoyote katika kusimamia mitihani.

Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kusema wanafunzi hao walioko Shuleni wasiwe na wasiwasi, kilicho futwa ni wale wasimamiaji wa mitihani, yaani ile Shule kwa kutokuwa waaminifu, lakini wanafunzi pamoja na mazoezi yao kama kawaida, mitihani ya ndani ya Shule wanayoifanya itachukuliwa ile ile na Kituo watafanya katika Vituo vyta jirani kama watakavyo elekezwa na Baraza la Mitihani siku chache zijazo. (*Makofî*)

Na.369

Miradi Isiyokamilika

MHE. STEPHEN M. KAZI aliuliza:-

(a) Je, Serikali inatoa maelezo gani kuhusu Miradi ya Kitaifa ambayo imeachwa bila kukamilishwa?

(b) Je, kuna Miradi mingapi ya Maji chini ya Wizara hii ambayo imeachwa bila kukamilika na ina thamani gani?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Setephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingi hapa nchini ambayo ilianzishwa na Serikali lakini haikukamilishwa kama ilivyokuwa imepangwa hapo awali. Utekelezaji wa miradi hii ulisimama kutokana na hali mbaya ya uchumi wa nchi yetu ambapo tulishindwa kuiendeleza na kuikamilisha. Aidha, ipo miradi mingine ambayo haikukamilika kutokana na Wafadhili wa miradi hiyo kusitisha misaada au kumalizika kwa fedha zilizotengwa.

Pia, ipo miradi mingine ambayo ilikamilika lakini haikuendelea kutoa huduma kikamilifu kutokana na kuharibika au kuchakaa kwa miundombinu kama kukosa matunzo yanayostahili kuendeleza miradi hiyo na mingine kuibiwa vifaa muhimu katika miundombinu na mfumo wa mradi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara yangu ilishirikiana na Halmashauri za Wilaya na Miji kufanya tathmini ya miradi ya namna hiyo na kuainisha jumla ya miradi 794 ambayo bado ilikuwa haijakamilishwa au ilikamilishwa lakini haitoi huduma. Baada ya kuitathmini miradi hiyo, ilibainika kuwa gharama za ukarabati na ukamilishaji huo ni takriban Shilingi bilioni 43.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutoa kipaumbele katika kuikamilisha na kukarabati miradi hii hatua kwa hatua kwa kuitengea fedha katika Bajeti zake za kila mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara ilitenga jumla ya Sh.1,837,407,900/= kwa ajili ya kukarabati miradi 30 kati ya miradi 794 nilioitaja. Katika mwaka 2004/2005, Serikali imetenga Sh.1,440,000,000/= kwa ajili ya kukarabati miradi 47 ya namna hiyo. Serikali itaendelea kutenga fedha zaidi kwa kazi hii. Tunatarajia kwamba, Wananchi watashirikishwa kikamilifu katika kufufua miradi hii ili iwe endelevu kulingana na Sera yetu ya Maji.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalı dogo la nyongeza. Pamoja na juhudı za Serikali hasa nia yangu ilikuwa kufahamu tu na kutaka kuiomba Serikali iendeleze Miradi ya Maji iliyoko katika Jiji la Mwanza ambayo sasa inafanyika ambayo ni pamoja na maji machafu. Kwa hili naishukuru sana Serikali. Kitu ambacho nataka kufahamu ni kwamba, katika Miradi ya Maji ya Mwanza ambayo inaendelea sasa, je, katika hali ya utumiaji wa kawaida na teknolojia inayotumika itasaidiaje wakazi wa Mwanza katika kupata unafuu wa gharama ya maji baada ya miradi hiyo kukamilika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi wa maji Mjini Mwanza shughuli ya ukamilishaji imeshaanza na hivi juzi tu tarehe 27 *re-qualification documents* zilifunguliwa ambapo mradi huu ukikamilika katika vipengele vyote viwili, utakidhi mahitaji ya maji ya Jiji la Mwanza na maeneo yanayozunguka jiji hilo na kama anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge, juzi juzi tu tumekamilisha mradi wa maji taka ambao kwa sasa hivi unakidhi kwa asilimia karibu 30 ya mahitaji ya usafishaji wa majitaka kwa ajili ya Jiji la Mwanza ambayo iligharimu zaidi ya shilingi bilioni tano.

Sasa huu mradi mpya ambao utagharimu karibu shilingi bilioni 52 ukikamilika, nina hakika kwamba, matatizo ya maji kwa Jiji la Mwanza yatakuwa yamekwisha na hivyo hivyo, tunajaribu kwa kutumia vyanzo vingine vingi nya hapa nchini na nya wahisani ili kutatua matatizo madogo madogo yanayojitokeza wakati tunakamilisha mradi huu.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa kuna mitambo mingi ya kuchimbia mabwawa ambayo yamechakaa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba mitambo hiyo ikikarabatiwa itasaidia kuchimba mabwawa katika Wilaya zetu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, ni kweli mitambo ya maji ya uchimbaji wa visima na ukarabati wa malambo au ujenzi wa malambo ni ya siku nyingi sana na ni kweli kwamba, imechakaa.

Lakini kwa ushirikiano na Wizara ya Fedha, tumeweza kufanya mpango wa kupata mkopo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vipyta kwa ajili ya wakala wetu wa uchimbaji malambo na visima. Kwa hiyo, nina uhakika kwamba, baada ya muda mfupi ujao, mitambo hiyo itakuwa inakidhi mahitaji ambayo tunayahitaji katika miradi mbalimbali.

Lakini wakati huo huo, *private sector* pia wanakaribishwa kuingia kwenye shughuli hiyo na tayari wameshaingia katika shughuli ya uchimbaji wa maji. Lakini pia kuna mipango mingine mingi ambayo inaleta mitambo kama hiyo na wa karibuni kabisa ni huu ambao Shirika moja kutoka Marekani wametoa mashine kama hiyo hiyo kwa ajili ya matumizi kwa Mkoa wa Singida.

Na. 370

Kituo cha Polisi cha Matangatuani

MHE. MCHANDE SALIM MCHANDE aliuliza:-

Kwa kuwa, Kituo cha Polisi (*FFU*) cha Matangatuani Konde kipo kati ya barabara itokayo Konde - Wete pia kituo hicho kipo katikati ya kijiji cha Matangatuani na kwa kuwa Wananchi wengi hulazimika kupita mara kwa mara au magari yanayopita kwenda na kurudi Wete, lakini katika kituo hicho ifikapo saa 12.00 jioni hadi 12.00 asubuhi raia au madereva wa magari hulazimika kubisha hodi wanapopita katika eneo hilo hali ambayo imekuwepo kwa miaka 40 sasa na unapokosa kufanya hivyo basi hupata mkong'oto wa nguvu kwa hiyo Wananchi wengi wamechoshwa na hali hiyo:-

- (a) Je, kubisha hodi katika Vituo nya Polisi ni sheria?
- (b) Je, ni sheria iwe ni kituo hicho pekee Pemba nzima?

(c) Je, ikiwa sio sheria kwa nini itumike katika kituo kilichotajwa tu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mbunge wa Jimbo la Konde, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuweka vizuizi nya Polisi barabarani (*Road Blocks*) unatumika nchi nzima na sio Matangatuani pekee kama Mheshimiwa Mbunge anavyooleza. Vizuizi hivi huwekwa kwa mujibu wa Sheria ya Polisi (*Police Force Ordinance No. 332*), kifungu cha 38. Lengo la vizuizi hivi ni mbinu ya kubaini wahalifu na sio kuwanyanya raia wema. Aidha, katika kituo cha Matangatuani, kama ilivyo katika vituo vingine, raia wema hupita bila kubughudhiwa na askari walio katika zamu za ulinzi. Iwapo Mheshimiwa Mbunge, anao ushahidi wa raia wema kubughudhiwa na Polisi bila sababu ya msingi, atupatie ushahidi huo na Wizara yangu itaufanyia kazi.

Hata hivyo, Wizara yangu itaangalia uwezekano wa kukipunguzia masharti ya kubisha hodi kituo hicho ikiridhika kwamba, hatua hiyo haitaleta taathira ambazo zimekuwa zikihofiya, hasa ile ya kuitishia bidhaa za magendo.

Na. 371

Vyombo nya Zimamoto

MHE. MARGARETH J. BWANA aliuliza:-

Kwa kuwa uwezo wa vyombo vyetu vilivyoko chini ya huduma ya zimamoto nchini haviwezi kuzima moto kwenye majengo yenyе ghorofa zaidi ya tano:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuagiza vyombo nya kisasa vinavyoweza kuzima moto kwenye majengo yenyе ghorofa zaidi ya tano?

(b) Kama jambo hilo haliwezekani, je, Serikali haioni umuhimu wa kuleta Sheria ya kusitisha ujenzi wa majengo marefu kupita uwezo wa vyombo vyetu nya kuzima moto?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Bwana, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba maendeleo ya miji ya kisasa ni pamoja na ujenzi wa majengo marefu, Serikali imeanza kununua magari ya zimamoto

yenye uwezo wa kuzima moto katika nyumba zenyе maghorofa mafuru. Kwa kuanzia Serikali imekwisha nunua gari lenye uwezo wa kuzima moto hadi ghorofa ya kumi na nane kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam. Gari hili limekabidhiwa rasmi kwa Jiji la Dar es Salaam tarehe 22 Mei, 2004.

Aidha, Serikali inaona sio busara kwa sasa kutunga sheria ya kusitisha ujenzi wa majengo mafuru wakati tunahimiza maendeleo ya makazi katika miji yetu. Serikali inachofanya kwa sasa ni kuimarisha vyombo vyetu vinavyotoa huduma ya kuzima moto kwa kasi inayolingana na kasi ya maendeleo ya ujenzi wa majengo makubwa. Vilevile wamiliki wa majengo hayo wameelekezwa, kwa mujibu wa Sheria kuweka viashiria moto (*Fire Detectors*) na vizima moto vyenyewe (*Automatic Fire Extinguishers*). Vilevile wanashauriwa kuhakikisha majengo yao yanakaguliwa na Wataalamu wa Zimamoto mara kwa mara na kuzingatia ushauri wanaopewa na Wataalamu hao.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini kuna swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, ameongelea kwamba, imepatikana gari moja tu katika Jiji la Dar es Salaam ambayo inawezekana kuzima huo moto kwa majumba makubwa. Lakini cha kushangaza na maeneo mengine pia yapo majumba makubwa kama hayo, je, Serikali itachukua hatua gani kupeleka magari sehemu nyingine?

SPIKA: Kama wapi? (*Kicheko*)

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Kama Mwanza, Arusha na Zanzibar. (*Makofu/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba, tumeanza. Hilo gari ambalo limekuja ni mwanzo na mengine ambayo yatakuja na kusema kweli kwa Dar es Salaam siyo moja tu, hili ni la Serikali. Lakini vilevile ziko kampuni za zimamoto za binafsi ambazo vilevile zina magari kama haya. Kwa hiyo, kwa Dar es Salaam liko hili la Serikali lakini yako makampuni ya binafsi ambayo yanazima moto, yenye magari yenye urefu kama huu.

Kwa hiyo, ningependa kutoa wito kwamba, kampuni za binafsi za zimamoto, zishirikiane na Serikali katika kusambaza magari haya katika miji mbalimbali aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Wawi. (*Kicheko*)

Na. 372

Wanyamaporи Wanaoharibu Mazao Nanyumbu

MHE. ARIDI M. ULEDI aliuliza:-

Kwa kuwa sehemu kubwa ya Jimbo la Nanyumbu limo kwenye njia za wanyamaporи wanaosafiri kutoka katika hifadhi za *Selous* na Msanjesi upande wa

Kaskazini na Msumbiji upande wa Kusini na kwa kuwa hali hiyo husababisha uharibu wa mazao ya wakulima hivyo kuwepo kwa upungufu mkubwa wa chakula katika vijiji vingi vya Jimbo la Nanyumbu hata vile vilivyo mbali na hifadhi ya Lukwika-Lumesule:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia wanyama hao ili wasiendelee kuleta uharibifu wa mazao?

(b) Je, unapotokea uharibifu wa mazao ya Wananchi, Serikali itakuwa tayari kuwafidia Wananchi hao?

(c) Je, Serikali itawasaidiaje Wananchi hao katika kujilinda na wanyama wakali wanaohatarisha maisha yao na mazao yao?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Tatizo la wanyamapori wakali na waharibifu linaendelea kujitokeza katika sehemu mbalimbali za nchi, hasa katika hali ya sasa ambapo kuna ongezeko la watu na mahitaji yao. Hii ni kwa sababu shughuli nyingi za vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi za wanyamaporri kwa kiwango kikubwa zinaingiliana na shughuli za uhifadhi wanyamaporri. Aidha, tatizo la wanyamaporri waharibifu linaongezeka pale ambapo Wananchi wamevamia maeneo ya hifadhi au kusogea karibu na mipaka ya maeneo ya hifadhi yakiwemo mapito ya wanyamaporri kwa ajili ya makazi, kilimo na ulishaji mifugo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwalinda Wananchi na mali zao dhidi ya wanyamaporri wakali na waharibifu. Aidha, Wizara yangu itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendesha doria za msako wa wanyamaporri waharibifu, kununua risasi za kutosha na kutoa mafunzo kwa askari wa vijiji, viongozi na Wananchi kwa ujumla. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Aridi Uledi kuwa, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na wadau wote muhimu pamoja na vyombo vingine katika kutekeleza jukumu la kudhibiti wanyama wakali na waharibifu.

(b) Mheshimiwa Spika, dhana ya kulipa fidia kwa uharibifu wa mazao ya Wananchi unaosababishwa na wanyamaporri ni nzuri lakini kutookana na mtawanyiko wa maeneo ya wanyamaporri na ukubwa wa tatizo la uharibifu wa mazao, suala la fidia kwa Wananchi litakuwa la gharama kubwa ambayo itakuwa ni mzigo mkubwa kwa Serikali kuweza kumudu.

(c) Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya kijiji, Serikali inajenga uwezo wa Wananchi kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya wanayamaporu kupitia mpango wa kuanzisha maeneo ya Jumuia ya Kuhifadhi Wanyamaporu (*Wildlife Management Areas - WMAs*).

Kutokana na mpango huu na kuwashirikisha Wananchi katika shughuli za uhifadhi likiwepo suala la ulinzi wa mali na maisha dhidi ya wanayamaporu wakali na waharibifu katika vijiji, ni dhahiri kuwa Wananchi katika Jimbo la Nanyumbu sasa watachukua hatua muafaka za kujilinda na madhara yanayoweza kusababishwa na wanyamaporu, kwa kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji vyao, kutumia elimu wanayopata pamoja na kuwatumia askari wa vijiji kudhibiti wanyamaporu.

Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, kuwa Wizara itaendelea kusaidia jitihada hizo.

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wanyama hao wanaohama huleta uharibifu mkubwa wa mazao ya Wananchi na wakati mwagine maisha ya watu kupotea:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kuweka walinzi katika vijiji hivyo kama inavyofanya katika vijiji vinavyozunguka hifadhi?

(b) Je, pale ambapo askari wanyamaporu huchelewa kwenda au kushindwa kutoa msaada, Wananchi wachukue hatua za kupambana na wanyama hao? (*Makofi*)

WAZIRI WA MALISILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kusema kwamba, katika Bunge hili theluthi moja ya maswali ya Wizara yangu yametoka kwa Mheshimiwa Aridi Uledi na napenda kumpongeza anavyoonyesha kwamba ni jinsi gani anaonyesha jitihada zake kwa Wananchi wa Jimbo lake. (*Makofi*)

Suala la mazao kuharibika na maisha ya watu, napenda kusema kwamba, tutajitahidi kama vile tunavyofanya kupeleka askari mara moja pale panapotokea matatizo. Suala la Wananchi kuamua kuwaa wanyamaporu, napenda kusema kwamba, Sheria ya Wanyamaporu ya mwaka 1974, kifungu Na. 50, kinatoa uwezo kwa Wananchi kuwaa wanyamaporu pale ambapo inatoka kwamba, wanaleta matatizo, lakini tu baada ya hapo, kutoa taarifa kwa Afisa Wanyamaporu katika maeneo hayo. (*Makofi*)

MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali dogo la nyongeza. Kutokana na jinsi ambavyo Warufiji wameliwa karibu watu 29 mwaka huu na kwamba Serikali ilichelewa, Mabwana wanyamaporu kule kuwashughulikia. Je, Serikali inasemaje inapochelewa maisha ya watu yanapoteketea hivyo ni sawa? (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, pale ambapo tumepata taarifa kwa kweli tumejitahidi mara moja kupeleka Maafisa Wanyamaporu katika maeneo hayo ili kuweza kusaidiana na Wananchi. Lakini kama kwa kweli

imechelewa labda pengine taarifa nayo pia ilichelewa kutufikia sisi Wizarani. Lakini pale ambapo taarifa inatokea na tunashirikiana na Wabunge hapa kupeleka Afisa Wanyamapori katika maeneo hayo. Lakini sielewi kama pengine taarifa ilichelewa upande wa kule katika Wilaya husika.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa kuna hali ya utata katika mpaka wa hifadhi ya Msanjesi na vijiji vya karibu vya Chingulungulu na Namalembو. Je, Waziri atawapa matumaini gani Wananchi wa maeneo hayo kwamba, sasa Serikali imefikiria kuuhamisha ule mpaka ili kuwapa nafuu kidogo Wananchi wa maeneo yale kwa kuwa mara kwa mara wanyamapori huwa wanahama kutoka pori hili la Msanjesi na kuingia katika vijiji mbalimbali na kufanya uharibifu mkubwa?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, pale ambapo kumetokea tatizo la mpaka na mara nyingine inatokea kwamba ni Wananchi ambao wanaingia katika maeneo ya wanyamapori, basi suala hili kwa kweli linazungumzwa katika ngazi ya kijiji linakwenda katika ngazi ya Wilaya, ngazi ya Mkoa, halafu linafika kwetu na pale tunaona kwamba, kwa kweli kuna tatizo, basi mara nyingi sana tunatuma Maafisa wetu kuja kuangalia na kutathmini huo mpaka ambapo upo. Kama kuna tatizo hilo basi ningemwomba Mheshimiwa Raynald Mrope, atumie ngazi hizo mpaka ifike katika ngazi ya Taifa.

Na. 373

Timu zetu Kushindwa kwenye Mashindano ya Kimataifa

MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME aliuliza:-

Kwa kuwa michezo inapendwa sana na Watanzania walio wengi, lakini wanamichezo wetu mara nyingi wanapoliwakilisha Taifa kwenye mashindano mbalimbali ya Kimataifa hushindwa:-

(a) Je, ni kitu gsani kinachosababisha wanamichezo wetu kushindwa mara kwa mara katika mashindano ya Kimataifa?

(b) Je, Serikali inazisaidia kwa kiwango gani timu zetu zinazowakilisha Taifa letu katika mashindano hayo ya Kimataifa?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, si michezo yote tunayoshindwa katika mashindano ya Kimataifa. Kwa mfano, Timu ya Taifa ya Mpira wa Mikono ya Wanawake ni mabingwa

wa Afrika. Timu ya kriketi chini ya miaka 19 hivi sasa inawania kucheza katika mashindano ya dunia, wakimbiasi wetu wa mbio ndefu wamekuwa washindi wa kwanza na pili katika mashindano ya *Sydney Marathon* huko Australia. Hata hivyo, sababu kubwa zinazofanya badhi ya timu zetu zishindwe katika mashindano ya Kimataifa ni uongozi mbaya wa baadhi ya vyama vya michezo vya Taifa, ukosefu wa vifaa vya kuimarisha uwezo wa mwili wa mchezaji na maandalizi yasiyoridhisha. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu timu zetu zinazoliwakilisha Taifa katika mashindano ya Kimataifa, Serikali inazigharamia iwapo mahitaji yake ya fedha yanaletwa Wizarani na makisio yake kuitishwa na Bunge, kutegemeana na kiwango cha juu cha bajeti. Mfano mzuri ni Timu ya Taifa iliyokwenda Abuja katika mashindano ya Mataifa Huru ya Afrika mwezi Oktoba, 2003, ambapo Serikali ilitoa shilingi milioni themanini na moja kwa ajili ya usafiri, malazi, chakula, posho na vifaa.

MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa vyama hivi vya michezo ni vyama vya hiari na kwa kuwa vyama vingi vinaelekea havina uwezo wa kuendesha michezo hiyo kufikia kiwango cha Kimataifa. Je, sasa Serikali haionti kama ni vyema ichukue jukumu la kushughulikia masuala ya michezo?

(ii) Kama haitaweza kushughulikia masuala ya michezo, je haionti ni vizuri sasa ikatoa ruzuku kwa vyama vyote ili kuvipa uwezo wa kuweza kuwafundisha wachezaji wetu kufikia kiwango cha Kimataifa?

SPIKA: Swali la kwanza hukulisikia vizuri. Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, rudia swali lako la kwanza.

MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME: Mheshimiwa Spika, ni kwamba, kwa kuwa michezo inaendeshwa na vyama vya hiari na kwa kuwa vyama hivi havina uwezo. Je, Serikali inaweza ikabeba jukumu la kuendesha michezo badala ya kuachia vyama vya hiari?

SPIKA: Sawa amelipata vizuri. Sasa unaweza kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naafikiana naye kwamba, baadhi ya vyama vya michezo havina uwezo. Lakini bado la msingi ni lile lile kwamba, matumizi ya Serikali yanapangiliwa kwa mfumo wa bajeti. Pesa ambazo tumeidhinishiwa wiki iliyopita zinatumika kwa mujibu wa yale mambo tuliyoyaombea. Kama klubu haina ushirikiano, chama cha michezo, hatuwezi kupeleka mambo yao na kuyaweka kwenye makisio. Inakuwa si rahisi Serikali kugutushwa katikati ya bajeti na kuweza kutoa pesa papo kwa papo.

Lakini suala la kutoa ruzuku tuna masharti, tunasema kama chama fulani cha mchezo ngazi ya Taifa kinataka ruzuku kwetu, basi tukubaliane maana kupeana ni kikoa. Wao watupe mapato yao ya milangoni, ya wafadhili na sisi tuweze kuleta kile ambacho kinakosekana katika kuja kufidia. Lakini haiwezekani tuwe tunatoa pesa halafu hatuna uwezo hata wa kuhoji na hizo pesa zetu wala zao zinazotoka nje. Katika hali kama hiyo, hatuwezi kwenda. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kutokana na kufanya vibaya katika mchezo wa mpira wa miguu, Serikali bado haijaona haja ya kuzuia mashindano ya nje kujitoa ili tuweze kuijandaa na kupata timu nzuri zaidi kwenda nje?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, hatuoni sababu ya kuzuia mashindano ya mpira wa miguu nje mpaka pale tutakapokaa vizuri kwa sababu tunafikiria tu kwamba, tatizo si kubwa kiasi hicho ukitoa lile la uongozi. Itakumbukwa kwamba, mwaka 2003, timu yetu ya Tanzania hapa ilikuwa imefika robo fainali ya Afrika na hivyo kuwa mionganoni mwa timu nane bora za Afrika. Sasa katika hali kama hiyo, tunachohitaji kwa kweli ni uongozi tu, bado vipaji viro, dhamira ipo na suala la uongozi linaendelea kurekebishwa kuitia ngazi za mikoa, *inshallah* uchaguzi utakaofuata utakuwa mzuri. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa utaratibu uliopo sasa ni kwamba klabu bingwa za Tanzania zinazowasilisha nchi kwa maana ya Tanzania katika mashindano ya Kimataifa, zinalazimika kujilipia gharama zote wenyewe. Na kwa kuwa klabu hizi hazina uwezo wa kufanya hivyo na hivyo kushindwa kwenda katika nchi hiyo kama walivyoshindwa ndugu zangu wa Mtibwa na kusababisha faini kubwa kutoka *CAF* na kwa kuwa sasa Bunge hili limepitisha Sheria inayoitwa *Gaming Act* ambayo inatoa fedha kwenye Serikali kwa ajili ya michezo. Je, haingekuwa busara sasa Serikali kuchukua jukumu la kugharamia klabu zinazowakilisha mashindano ya Kimataifa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ni kweli Sheria ya asilimia fulani ya michezo ya kubahatisha kwenda Serikalini kuja kwenye Wizara ya Michezo ilipitishwa na Bunge hili lakini ningependa kuarifu kwamba, Sheria hiyo bado haijaanza kutumika lakini kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mwaka huu Sheria itatumika na imeshakubalika, hatuoni sababu ya kushindwa kusaidia, sio tu vilabu lakini hata timu zetu za Taifa. Lakini kwa makubaliano yale yale kwamba lazima abebwaye awe anajishika, kwa sababu klabu ina wanachama wake, linalofanywa na Serikali ni kusaidia tu.

Lakini vilevile tumezungumza kati ya BMT, Wizara na *FAT*, kuweka mkazo juu ya makusanyo yale ya asilimia 10, BMT wako katika nafasi nzuri zaidi ya kusaidia michezo, siyo mpira wa miguu tu, lakini michezo yote ambayo nchi itakuwa inashiriki huko nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongeza kidogo tu kwenye jibu zuri alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu suala la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Missanga. Si sahihi kusema kwamba, Serikali haisaidii kabisa vilabu, Serikali ina rekodi ya kusaidia vilabu na kusaidia hata timu za Taifa. Tunapozungumza Serikali ni pamoja Wahisani ambao Serikali inawahamasisha kushirikiana ili kuweza kuwezesha michezo kufanyika. Kwa mfano, kulikuwa na mashindano ya *Youth Challenge Cup* kule Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa mgeni rasmi, wakaweza kukusanya shilingi milioni 29 mashindano yale yakafanyika kwa ufanisi mkubwa.

Kwa mfano, Serikali ilichangia Timu ya Simba ilipokwenda kucheza na El-Merreck, Serikali hiyo hiyo iliisaidia Timu ya Mtibwa kwa kuchangia kiasi cha shilingi milioni mbili, Serikali hiyo hiyo iliweza kuhamasisha na kuipeleka *Twiga Stars* kule Zimbabwe kwenda kucheza *return match*. Kwa hiyo, si sahihi kudhani kwamba, Serikali haisaidii. (*Makofsi*)

Na. 374

Kudidimia kwa Mpira wa Miguu

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA aliuliza:-

Kwa kuwa ni wazi kabisa kwamba, kiwango cha mchezo wa mpira wa miguu kimeshuka sana nchini kwa kipindi cha karibu mwongo mmoja na nusu hivi; na kwa kuwa hali ya timu zetu ni mbaya kiuchumi/kimapato na *ki-standard* kiwango cha kucheza kimeshuka mno kiasi kwamba, mashabiki na Wananchi kwa ujumla wamekata tamaa kwa kuwa timu zetu zinakuwa zikishindwa na kuwa msindikizaji wa timu nyingine; na kwa kuwa Wananchi wanayo ari/hamu ya kutaka kuona mchezo huo unafuliwa kwa nguvu zote:-

- (a) Je, ni sababu gani zilizoua mchezo huo nchini?
- (b) Je, Serikali itachukua hatua gani ili kuinua kiwango cha mpira huo ili kurudisha matumaini ya mashabiki na Wananchi kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, napata mashaka kukubaliana na maeleo ya Mheshimiwa Eliachim Simpasa kuwa, kiwango cha soka kimeshuka kwa kuwa sina vigezo vya kuthibitisha hayo. Unathibitishaje au unaelezaje wakati timu moja ya Tanzania imefuzu kuwa mionganii mwa timu nane bora Afrika katika mashindano ya *CAF - Africa Cup of Club Champion*. Tunachokiona sisi ni kwamba, kiwango cha soka

hana kwetu hakikui sambamba na wenzetu kuto kana na uongozi dhaifu unaotokana na Katiba mbovu ambazo zimepitwa na wakati katika Vilabu na Vyama vy a Michezo na ambavyo kwa sehemu kubwa unatokana na ubinafsi uliokithiri mi ongoni mwa viongozi wen yewe na wanachama na hata wapenzi wa soka.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa vyama na vilabu vy a Michezo ni mali ya wanachama wen yewe walioviunda na kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora, Wizara yangu itaendelea bila kuchoka, kutoa maelekezo na kuelimisha wadau wote kwa ujumla, kuzingatia katiba zao katika utekelezaji wa kazi za vilabu na vyama husika ili kuboresha utawala wa vyama hivyo na hatimaye mchezo wen yewe.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Pamoja na majibu mazuri kidogo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza ni kwamba, mpira haukui sambamba na wenzetu kwa sababu ya uongozi dhaifu na amba o unatokana na katiba mbovu. Je, wanafanya nini ili uongozi dhaifu usiwepo na Katiba mbovu zisiwepo? (*Makofit*)

Pili, kiwango hakikui kwa sababu ya ubinafsi wa watu katika uongozi katika vilabu au mashabiki. Sasa ubinafsi huo kama Wizara au kama Serikali wao wana uondo a vi pi, sisi hatupendi kutaja majina ya watu, maana yake wana watetezi wao hapa siku hizi? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua kadhaa ili kupambana na uongozi dhaifu unaotokana na katiba mbovu au zilizopitwa na wakati za vilabu na vyama vy a Michezo.

Miongoni mwa hatua hizo kwanza, ilikuwa ni kuwakusanya viongozi wote wa ngazi ya Taifa na kueleza udhaifu uliomo ndani ya Katiba zao na ningependa kupitia Bunge lako hili kueleza kwamba, baadhi ya vyama vy a Michezo vimetekeleza na leo hatuna migogoro tena katika ngumi, leo mgogoro umepungua katika riadha.

Mgogoro umeondoka kabisa katika *TAVA* na hatua zinazochukuliwa sasa na *FAT* kurekebisha Katiba yao kwa kweli lazima tuseme kwamba, juhud i zilizofanywa na Bunge hili kupitia Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Serikali kwa ujumla, imewafikisha wenzetu pale walipofika.

Lakini vilevile tumekuwa tukiendesa mafunzo, mtakumbuka mwaka huu tulikuwa na mafunzo Morogoro lakini mwaka 2003 kanda zote za Tanzania Bara zilihu shwa ku wahamasisha basi na wale wanachama wao wa one umuhimu wa kuwabana viongozi wao kupitia Katiba zao wen yewe.

La pili kuhusu ubia binafsi, wanachama na mashabiki tunafanya nini? Moja, ni kutoa elimu tu kupitia vyombo vy a habari waelewe lakini kama alivyosema Mheshimiwa Eliachim Simpasa kwamba, baadhi ya watu wana watetezi wao humu ndani ya Bunge, lakini ndani ya Bunge vilevile napo tuna ushabiki unaoharibu hata viongozi wa Vilabu vyetu. Tunafikia wakati tunasahau umuhimu wa kuwa na mchezo bora. Tunajikuta

tunagawanyika humu kwenye *Yanga Family* na *Friends of Simba* na ushabiki wa namna hiyo nao unachangia vilevile kushusha nidhamu katika uongozi. (*Kicheko*)

SPIKA: Napenda kuwaarifu mashabiki waliosimama sasa kuuliza maswali ya nyongeza kwamba, muda wa maswali umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na matangazo ya vikao vya leo. Kamati za Kudumu, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Athuman Janguo anaomba Wajumbe wa Kamati hii wakutane kuanzia saa nne asubuhi mara baada ya kipindi cha maswali katika chumba Na. 231 ghorofa ya pili. Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kuanzia saa tano asubuhi chumba cha Kamati Na. 219 ghorofa ya pili.

Kamati ya mwisho ni Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kuanzia saa tano chumba Na. 227. Kikao kingine ni Kikao cha Waheshimiwa Wabunge wa CCM wanaotoka Zanzibar, Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, anawaomba Wabunge hao wakutane leo saa saba mchana baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge cha asubuhi, watakuwa kwenye chumba Na. 231.

Mwisho wa matangazo, Katibu tuendelee na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na Wabunge wenzangu walionitangulia, kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mbunge mwenzetu wa Jimbo la Bariadi Mashariki, Mheshimiwa Danhi Makanga, wa Chama cha Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwake. Ni ushindi alioustahili na tunamwombea mafanikio mema.

Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wenzangu walionitangulia, kwa hotuba zao nzuri ambazo zimefanua maeneo muhimu ya ushirikiano wa Kimataifa ambayo Serikali itayapa umuhimu wa juu katika mwaka huu wa fedha.

Naomba pia kutumia nafasi hii kuipongeza Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje inayoongozwa na Mheshimiwa Dr. William Shija, iliyojadili Bajeti hii kabla ya kuifikisha hapa leo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa majonzi makubwa, nikupe mkono wa pole na rambi rambi kwa misiba miwili mikubwa iliyotukuta ya kufiwa na Wabunge wenzetu, Marehemu Mheshimiwa Yetet Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki. Vifo vyao vya ghafla sio tu vimewanyang'anya familia na Wananchi wa Majimbo yao, wazazi na wawakilishi hodari, bali pia vimetuondolea marafiki wapendwa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwape pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi na Mheshimiwa Dr. Lawrence Mtazama Gama na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na watoto wao wapendwa. Tuendelee kuwaombea Marehemu wetu hawa kwa Mungu, awape mapumziko mema. *Amina*.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, namshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluwaye Sumaye, kwa kutaja bayana katika hotuba yake, maeneo muhimu ya ushirikiano wa Kimataifa, ambayo Serikali yetu itayapa umuhimu wa juu katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje na majukumu ya Wizara yangu. Nawashukuru pia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa hotuba zao nzuri zilizoainisha maeneo mbalimbali ya ushirikiano wa Kimataifa. Naomba shukrani ziwafikie Mawaziri wenzangu wote waliotangulia kwa kuzungumzia kwa ufasaha maeneo ya ushirikiano wa Kimataifa mnayoyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, naomba niitumie nafasi hii vilevile kuwashukuru kwa dhati kabisa, Wabunge wenzangu ambaa ni Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, inayoongozwa na Mwenyekiti wake makini, Mheshimiwa Dr. William Shija. Kamati yetu hii ilijadili makadiryo ya Wizara yangu kabla ya kuyafikisha hapa leo. Kamati ilifanya uchambuzi mzuri, tena wa kina na kutoa ushauri mwingi muhimu ambaa utaisaidia Wizara yangu katika utekelezaji wa malengo ya bajeti hii na majukumu yetu kwa jumla. Sina budi kukiri mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, ni kawaida ya Kamati yetu hii kila wakati wanapojadili mambo yanayohusu Wizara yangu, mimi na wenzangu wote Wizarani tunaona fahari kuwa na Kamati yenye Wajumbe mahiri kama hawa. Tunaomba waendelee na moyo huo huo.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, Katibu Mkuu, Ndugu Phillemon Luhanjo, Wakurugenzi, Mabalozi wetu walioko nchi za nje pamoja na wafanyakazi wenzangu wote Wizarani na katika Balozi zetu. Kwanza kabisa, nawashukuru kwa kuwezesha kukamilisha bajeti na hotuba hii kwa wakati. Pili, nawashukuru na kuwapongeza kwa juhudhi wanazozifanya kutetea na kuendeleza maslahi ya Taifa letu nje. Nawapongeza kwa uchapakazi wao mzuri na moyo wao wa kujituma na kuipenda nchi yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha wa 2003/2004, ulikuwa wa kuridhisha kwa upande wa upatikanaji wa fedha. Tumeweza kupata fedha zote kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu ilipangiwa kutumia Shilingi 32,079,101,100.00/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 21 Mei 2004, Wizara yangu ilikwisha pokea kutoka Wizara ya Fedha kiasi cha Sh. 33,586,435,955.00/=, ikiwa ni sawa na ongezeko la Shilingi 1,507,334,855.00/. Matumizi haya ya ziada yamesababishwa na gharama za ziada zilizojitokeza kugharamia nyongeza za mishahara ya wafanyakazi, mikutano ya *SADC*, mikutano ya usuluhishi wa migogoro ya Nchi za Maziwa Makuu na michango katika mashirika ya kimataifa na yale ya ushirikiano wa kikanda. Kufungua Ubalozi Mpya Malawi na ununuvi wa majengo nako kumechangia nyongeza hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, watakumbuka kuwa mwaka wa 2003 nilielezea ugumu wa kuendesha Balozi zetu kwa mgao wa mwezi mmoja mmoja. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utaratibu huo sasa umerekebishwa na kwamba kuanzia Julai, 2003 tumekuwa tunapata mgao wa robo mwaka. Kwa ajili hiyo, hivi sasa tunaweza kupanga vizuri zaidi shughuli za kufanya Balozini na Wizarani. Utaratibu huu umetusaidia sana kupunguza migogoro ya malipo ya kodi za nyumba. Napenda kuitumia nafasi hii kuwashukuru wenzetu wa Hazina kwa hatua hiyo na Waheshimiwa Wabunge kwa msaada wenu. Hali yetu siku hizi imekuwa nafuu zaidi kuliko huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, suala la kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania ukilinganisha na dola ya Kimarekani limeendelea kuwa tatizo. Kwa sababu hiyo mara kwa mara kumekuwepo na pengo la kuziba kati ya fedha kwa dola zinazostahili kupelekwa Ubalozini na kiasi halisi kinachofikishwa. Bado hatujafikia muafaka kuhusu maombi yetu ya kutaka bajeti za Balozi zetu kuwa kwa dola badala ya shilingi za Tanzania ili Balozi zetu zilipwe stahili zao kwa ukamilifu. Mashauriano yanaendelea. Pamoja na hayo tunaishukuru Hazina kwa kuboresha hali ya ulipaji wa tofauti ya malipo inayotokana na kushuka kwa thamani ya sarafu yetu. Siku hizi hali si mbaya, tunaomba tuendelee hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mazungumzo kati ya Wizara yetu na Hazina kuhusu kufanya malipo kwa Balozi zetu kwa sarafu ya nchi zao za uwakilishi yamefikia hatua nzuri. Huenda katika bajeti zijazo fedha ya mishahara na matumizi mengineyo ikatolewa na kutumwa kwa sarafu za nchi zao za uwakilishi. Hii itawapunguzia wana Balozi wetu usumbufu wa kubadilisha fedha tunazowatumia kwa dola na kuwa sarafu ya nchi zao za uwakilishi. Wakati mwingine kufanya hivyo kumekuwa kunawapunguzia stahili zao.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa maduhuli katika Balozi zetu umekwenda vizuri na kwamba tulivuka lengo lililokadirwa. Makadirio ya bajeti kwa mwaka 2003/2004, yalikuwa kiasi cha Sh. 3,262,680,640.00/= na makusanyo halisi hadi tarehe 30 Juni, 2004 yalikuwa Sh.6,221,144,236.00/= Hivyo basi kumekuwa na makusanyo ya ziada ya Sh. 2,958,463,596.00/= hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2003/2004

na tumevuka lengo kwa asilimia 90.67. Mafanikio haya makubwa, yametokana na kazi nzuri waifanyayo wana Balozi wetu huko nchi za nje ya kuwavutia wawekezaji, watalii na wafanyabiashara wa kimataifa kuja nchini kwa wingi. Hatuna budi kuwapongeza wana diplomasia wetu kwa kazi yao nzuri hasa, tukizingatia kwamba bado nchi yetu ilikuwa mlengwa mmojawapo wa tahadhari za baadhi ya mataifa makubwa kwa raia wao kutembelea nchi yetu kwa madai ya kuwepo tishio la ugaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya hali ya upatikanaji wa fedha kuwa nzuri kwa ujumla utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2003/2004, ulikuwa wa kiwango cha kuridhisha pia. Tumeweza pia kufungua Ubalozi mpya nchini Malawi katika Mji wa Lilongwe. Balozi na watumishi wote muhimu tayari wapo kituoni. Bahati nzuri tumeanza vizuri kwa upande wa majengo maana nyumba za kuishi maofisa na Balozi Mjini Lilongwe ni mali yetu, tumenunua nyumba tano kwa mara moja. Kwa sasa tunapanga jengo la Ofisi ya Ubalozi lakini kiwanja tumepewa na mipango iko mbioni kujenga siku za usoni. Ubalozi huo tumeupatia mahitaji yake ya msingi ya vitendea kazi yakiwemo magari matatu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na majengo yetu wenyewe Balozini ni jambo tulilolipa kipaumbele cha juu. Kwa ajili hiyo tumebuni Mpango Kabambe wa Kununua na Kujenga Majengo katika Balozi zetu. Mpango huo wa miaka 15 ukitekelezwa kwa ukamilifu utatufanya tuwe na majengo ya ofisi na nyumba za kuishi Mabalozi na Maafisa wetu ambazo ni mali yetu. Inakadirwa kuwa dola 177,100,000 zitahitajika. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa mpango huo umeanza. Tumenunua jengo la Ofisi ya Ubalozi wetu mjini London, Uingereza kwa gharama ya *pound* 6,000,000 ambazo ni karibu sawa na Tshs. 12 bilioni. Tumeshalipa Sh. 3,601,200,000/= kutokana na fedha zetu na zilizosalia ni mkopo kutoka *Barclays Bank*. Mkopo huu wa *Pound* 4,200,000 tutaulipa kwa miaka 30. Kuweza kununua jengo la Ofisi London ni ushindi kwani hatimaye tunaweza kuhama kutoka jengo tulilokuwa tumepanga kwa zaidi ya miaka 40. Kuanzia sasa kodi ya nyumba tuliyokuwa tunalipa kwa jengo la sasa tutaitumia kulipia mkopo wa *pound* milioni sita kutoka *Backlays Bank*. Naomba nitoe shukrani maalum kwa Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa uamuzi wake thabiti na wenzetu wa Hazina kwa utekelezaji wao makini na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa majengo ya ofisi za Balozi ambayo ni mali yetu ni 15 tu katika balozi zetu 29 duniani. Makazi ya Mabalozi wetu ambayo ni nyumba zetu ni 22 na nyumba za maafisa ni 34. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba tumepanga majengo 14 kwa ajili ya Ofisi za Balozi, nyumba nane kwa ajili ya makazi ya Mabalozi na nyumba 77 kwa ajili ya makazi ya maofisa. Upangaji wa nyumba hizi hutugharimu takribani fedha kiasi cha US\$ 3,199,334.15 ambazo ni sawa na Sh. 3,583,255,383.00/= kwa mwaka. Kutokana na kutumia sehemu kubwa ya Bajeti kulipia pango za nyumba tulizopanga ndiyo maana Wizara imeweka mikakati ya muda wa kati na muda mrefu kuhakikisha kuwa Serikali inamiliki nyumba zake katika miaka 10 hadi 15 ijayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka uliopita wa fedha Wizara yangu imeendelea kuboresha hali ya utendaji kazi. Tumekarabati ofisi zetu Makao Makuu ya Wizara na

katika baadhi ya balozi zetu nje ili kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi. Vile vile tumeendelea kuweka vifaa vya kazi vipyta na vya kisasa maofisini. Kadhalika, tumenunua samani mpya kwa ajili ya ofisi zetu na tumeweka *heating systems* mpya pale palipohitajika. Tumenunua magari mapya matatu kwa ajili ya Makao Makuu ya Wizara na Ofisi za Ubalozi za New York, Harare, Lilongwe, Abuja na Lusaka nazo zimepatiwa magari mapya. Tunakusudia kuendelea kufanya hayo katika mwaka huu wa Fedha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nafurahi pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tulipata msaada wa magari 12 ya aina ya *Mercedes Benz* kutoka Dubai katika Umoja wa Falme za Kiarabu. Magari hayo yaliyofika nchini muda mfupi kabla ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa *SADC* Agosti, 2003 yalitusaidia sana kuboresha huduma ya usafiri wakati wa mkutano huo. Kupatikana kwa magari hayo kumetuongezea idadi ya magari ya Idara ya Itifikasi, tunayoyatumia kwa ajili ya kupokelea wageni wa kitaifa. Hivi sasa Wizara yangu inayo jumla ya magari 24. Kati ya hayo, magari 21 ni ya aina ya *Mercedes Benz* na matatu ni *Hyundai*. Kuwa na magari hayo kumeipa nchi yetu heshima katika masuala ya Itifikasi. Naomba niitumie nafasi hii kuzishukuru kwa dhati kabisa Serikali za Libya, Korea ya Kusini na Dubai kwa misaada yao mikubwa ya magari.

Mheshimiwa Spika, bado tunaendelea kutafuta magari zaidi ya kupokelea wageni ili hatimaye siku moja na sisi tuweze kuwa wenyeji wa mikutano mikubwa ya Kimataifa kama vile Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika au Wakuu wa Nchi na Jumuiya ya Madola, au mkutano wa mwaka wa Benki ya Dunia na *IMF* au wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hatuna budi pia, Watanzania tuendelee kuboresha miundombinu muhimu ya mikutano kama vile mahoteli na kumbi za mikutano ili nchi yetu iweze kuvutia mikutano mingi ya kimataifa na kikanda hapa nchini. Naomba kuitumia nafasi hii kutoa wito kwa wawekezaji na viongozi wa Halmashauri za Miji na Wilaya hapa nchini kutoa msukumo maalum wa kuwekeza katika mahoteli na kumbi za mikutano. Ni vyema tukatambua kuwa kuhudhuria mikutano huchangia sehemu kubwa ya utalii duniani. Zipo nchi nyingi duniani zinazonufaika na sisi pia tunawenza kunufaika ili mradi tu tufanye yale yanayovutia utalii wa mikutano (*Conference Tourism*).

Mheshimiwa Spika, katika miezi ya hivi karibuni tatizo la kukatika umeme mara kwa mara limegeuka kuwa kero na kikwazo kwa ufanisi wa kazi Wizarani. Kwa ajili ya kukabili tatizo hili tumenunua jenereta mpya. Kupatikana kwa jenereta hiyo kutatumalizia kilio na tatizo letu hilo.

Mheshimiwa Spika, sina haja ya kusisitiza umuhimu wa Wizara yangu kuwa na watumishi wa kutosha wenyewe uzoefu na ujuzi muafaka. Kufanya hivyo ndiko kunakoihakikishia Wizara yangu na Taifa kwa jumla ufanisi wa hali ya juu wa utekelezaji wa malengo na majukumu yetu. Bahati mbaya Wizara yangu imekuwa inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi takriban wa kada zote, Wizarani na Balozini, kwa miaka kadhaa. Athari ya upungufu huu ni wafanyakazi wachache kubeba

mzigo mkubwa kiasi cha kurudisha nyuma ufanisi. Naomba kutoa shukrani maalum kwa Idara Kuu ya Utumishi wa Umma, hususan iliyokuwa Tumeajiri, kwa kutambua kilio chetu na mara kwa mara kuchukua hatua za kutusaidia.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Mheshimiwa Spika, tulipewa nafasi ya kuajiri vijana 10 wenye Shahada ya Sheria na Uhushiano wa Kimataifa. Tumeshafanya hivyo. Kadhalika, tunawashukuru kwa kutupatia Wachumi watano waliohamishwa kutoka Wizara nyingine za Serikali na kuja Wizara yetu. Watumishi hao wapya 15 wamesaidia sana kutupunguzia pengo ingawa bado tuna mahitaji. Tunashukuru vile vile, kwamba tumepewaa nafasi ya kuajiri maafisa 20 katи ya mwaka 2004 na 2006. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la kuongeza ujuzi na maarifa kwa maafisa na wafanyakazi wa Wizara yangu ni jambo tulilolipa kipaumbele cha juu. Kwa ajili hiyo tumekuwa tunagharamia mafunzo kwa maofisa na wafanyakazi wetu. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, tuliwagharamia watumishi tisa kwa kozi za muda mrefu katika fani za Uhushiano wa Kimataifa, Diplomasia ya Uchumi na Ukatibu Muhtasi. Baada ya mafunzo hayo, watumishi hao watatunukiwa Shahada ya Pili, Stashahada ya Uzamili na Stashahada. Wizara yangu pia imegharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi tisa waliosomea fani za Utunzaji Kumbukumbu, Ukatibu Muhtasi, Udereva na Kompyuta. Baada ya kufuzu mafunzo yao watumishi hao watatunukiwa vyeti (*Certificates*).

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa maslahi bora kwa wafanyakazi katika kuongeza ari ya kufanya kazi wakati wote tumetoa umuhimu kwa suala zima la kuboresha maslahi ya maofisa na watumishi wetu. Katika mwaka uliopita wa fedha, maofisa 13 walipandishwa vyeo na kati yao kumi waliteuliwa kuwa Mabalozi. Mambo mawili muhimu kukumbukwa katika uteuzi wa Mabalozi aliofanya Rais wetu mwaka wa fedha uliopita. Jambo la kwanza ni kwamba, sehemu kubwa sana ya Mabalozi inatokana na watumishi wa Wizara yetu hivyo kuwapa motisha ya aina yake maofisa wetu. Pili, kwamba hata Wakurugenzi wa Makao Makuu na maofisa wetu waliko kwenye Idara nyingine za Serikali yetu walioteuliwa kuwa Mabalozi walikula kiapo mbele ya Rais. Zamani haikuwa hivyo. Kufanya hivyo kumewaongezea kauli na uwezo wa kuzungumza na kufanya maamuzi kwa niaba ya nchi yetu hasa mamlaka zaidi ya kujiamini.

Mheshimiwa Spika, tumetekeleza kwa ukamilifu nyongeza za mishahara kwa maofisa na watumishi wote. Kadhalika, tumezitazama upya Kanuni za Utumishi wa Nje na Posho za Utumishi wa Nje kwa nia ya kuziboresha. Ni matumaini yangu kuwa kazi hiyo tutaikamilisha mwaka huu na kwamba mapendekezo mapya yakikubaliwa yataanza kutumika kuanzia bajeti ya mwakani au mwaka unaofuatia huo.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba, uanachama wetu na ushiriki wetu katika mashirika ya kimataifa na kikanda huenda sambamba na wajibu kwetu wa kutoa michango katika Mashirika hayo. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, tumetumia kiasi cha Sh. 4,503,515,403.40/= katи ya Sh. 5,588,395,150.45/= tunazotakiwa kulipa. Hii ni michango yetu ya mwaka na malimbikizo ya michango ya nyuma kwa Mashirika ambayo Wizara yangu ni mratibu, yaani, Umoja wa Mataifa na baadhi ya mashirika

yake, Umoja wa Afrika, *SADC*, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Madola na kadhalika. Kwa jumla hali ya ulipaji wa michango ni wa kiwango cha kuridhisha. Mpaka sasa hatudaiwi michango katika mashirika ya Umoja wa Afrika, *SADC*, Jumuiya ya Madola na *EAC*. Bado hatujamaliza michango yetu ya Umoja wa Mataifa, *EAC*, *ADC* na mazungumzo na wenzetu wa Hazina kupatiwa fedha hizo ili tulipe, yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, moja ya jukumu la msingi la Wizara yangu ni kuratibu ziara za Viongozi kwa maana ya viongozi wetu kutembelea nchi za nje na viongozi wa nje kutembelea nchi yetu. Nafurahi kusema kwamba tumetekeleza vyema kazi hiyo. Tumefanya hivyo huku tukiwa tunazingatia ukweli kwamba ziara za Viongozi ni mojawapo ya njia muhimu ya kukuza na kuendeleza urafiki na uhusiano mwema na mataifa mengine duniani kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa jumla mwaka 2003/2004, ulikuwa wa shughuli nyingi na mafanikio kwa upande wa ziara za Viongozi wetu, kutembelea nchi za nje. Tangu mwezi Julai, 2003 hadi sasa, Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa amefanya ziara za kikazi katika nchi za Uswisi, Japan, Malawi, Uingereza, Afrika Kusini, China, Botswana na Msumbiji. Kwa ziara za Kitaifa, Mheshimiwa Rais wetu ametembelea Ujerumani na China. Rais pia alienda Uswisi kwa ajili ya matibabu. Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein ametembelea Lesotho, Kenya, Zimbabwe, Rwanda, Oman na Umoja wa Falme za Kiarabu kwa ziara za kikazi. Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume ametembelea Saudi Arabia kwa ibada ya Hijja, Malaysia, India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Malawi na Msumbiji kwa ziara za kikazi. Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye ametembelea Uingereza, Austria, Ujerumani, Norway, Ethiopia, Rwanda na Burundi kwa ziara za kikazi. Aidha, tumeratibu ziara nyingine za kikazi, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alitembelea China na Umoja wa Falme za Kiarabu. Aidha, tumeratibu ziara nyingine za kikazi ambazo Mheshimiwa Rais aliwakilishwa na Mawaziri na viongozi mbalimbali ukiwemo wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika ulipomuwakilisha huko Marekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ziara za Viongozi wa nchi za nje walioitembelea nchi yetu, katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2003/2004, nchi yetu ilibahatika kutembelewa na viongozi wengi. Kwa ziara za kikazi, tumetembelewa na Viongozi kadhaa wakiwemo, Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*), ambao walikuja kuhudhuria kikao cha kawaida cha Mkutano wa Wakuu wa Nchi za *SADC*, na mkutano wa dharura kuhusu Kilimo na Usalama wa Chakula katika *SADC* uliofanyika tarehe 15 Mei, 2004. Viongozi wengine ambao wametutembelea kwa ziara za kikazi katika kipindi hiki ni kutoka nchi za Maziwa Makuu waliokuja kutafuta amani ya Burundi.

Aidha, kwa ziara za Kitaifa, tumetembelewa na Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mheshimiwa Mwai Kibaki, tarehe 12 Januari, 2004, alikuwa mgeni rasmi katika sherehe za miaka 40 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia aliyekuwa Rais wa Malawi, Mheshimiwa Bakili Muluzi, alitembelea Tanzania tarehe 30 Juni - 3 Julai, 2003 na aliyekuwa Rais

wa Ujerumani, Mheshimiwa Dr. Johannes Rau, alifanya ziara nchini tarehe 19 - 24 Machi, 2004. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2003 nilieleza katika Bunge lako Tukufu, mambo mawili kuhusu Sera Mpya ya Mambo ya Nje, ambayo leo napenda kutoa taarifa ya utekelezaji wake. Kwanza, nilieleza kuhusu kuendelea kwa kazi ya kufanya tafsiri ya Kiswahili ya Sera hiyo na kwamba baada ya kazi hiyo kukamilika tutashughulikia uchapishaji wa vitabu. Na, pili, nilieleza dhamira yetu ya kufanya uzinduzi rasmi wa Sera hiyo kwa heshima na uzito stahiki kwa jambo muhimu kama Sera ya Mambo ya Nje ya taifa. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi ya kufanya tafsiri ya Kiswahili na kuchapisha vitabu vya Sera hiyo kwa lugha ya Kiswahili zimekwisha kamilika. Tutajitahidi kuhakikisha kuwa kila Mbunge anapata nakala yake ya kitabu hicho.

Mheshimiwa Spika, uzinduzi rasmi wa Sera ya Mambo ya Nje ulifanywa na Rais Benjamin W. Mkapa tarehe 30 Aprili, 2004 wakati wa Mkutano wa Mabalozi uliofanyika katika Hoteli ya Serena iliyoko katika Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro. Pamoja na kuzindua Sera ya Mambo ya Nje, Rais wetu pia alizindua Mkakati wa Utekelezaji (*Strategic Plan*). Mkakati wa Utekelezaji siyo tu ni mwongozo muhimu wa utekelezaji wa Sera bali pia ni kigezo cha kupima mwenendo wa utekelezaji wa Sera na majukumu mbali mbali ya Wizara yetu. Napenda kuitumia nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Rais wetu kwa kukubali kufanya uzinduzi huo na kutoa maelekezo muhimu yatakayoboresha Sera yenewe na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje umekuwa unaendelea vizuri na mafanikio yake yanaonekana dhahiri. Tanzania leo ni nchi inayong'ara katika medani ya diplomasia ya Kimataifa. Tuna marafiki wengi sana mionganoni mwa mataifa na mashirika ya kimataifa pengine kuliko wakati mwingine wo wote katika historia ya nchi yetu. Hatuna adui wa dhahiri wala wa siri mionganoni mwa mataifa na hakuna shirika lolote la Kimataifa ambalo tuna mgogoro nalo.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya sifa zote hizo na ukweli huo Tanzania imekuwa na sauti yenyeye uzito wa aina yake katika majukwaa ya kimataifa. Pengine sauti hiyo haifanani na nguvu yetu ya kiuchumi na kijeshi, mambo ambayo kwa kawaida huwa chanzo kikubwa cha nguvu na heshima ya taifa duniani. Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, amekuwa anahusishwa na kushirikishwa katika kutoa maoni na ushauri wake katika Tume za Kimataifa na mikutano mbalimbali. Kama tujuavyo Rais wetu alikuwa Mwenyekiti-Mwenza na Rais wa Finland Mheshimiwa Tarja Harlonnen wa Tume ya Utandawazi iliyomaliza kazi yake hivi karibuni. Hata kabla ya kumaliza kazi ya Tume ya Utandawazi, Rais wetu aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Afrika iliyoundwa na Waziri Mkuu wa Uingereza Mheshimiwa Tonny Blair. Tume hiyo inajumuisha watu wengi mashuhuru wakiwemo wanasiasa, wasomi na wafanyabiashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka uliopita Rais wetu alialikwa kuhudhuria na kuzungumza katika mikutano mingi. Mialiko yake imekuwa mingi kiasi cha kutupa ugumu sisi wasaidizi wake Wizarani kwangu na Ikulu kuhusu ipi tupendekeze

ashiriki na ipi atume mwakilishi. Nafurahi kusema kuwa Rais alikubali mialiko mingi kwa heshima yake na manufaa ya nchi yetu. Aliweza kushiriki na kuzungumza kama mtoa hotuba ya msingi katika Mkutano wa *Tokyo International Conference on Africa's Development (TICAD III)* uliofanyika Tokyo, Japan Septemba 29 hadi Oktoba 1, 2003. Rais Benjamin William Mkapa pia alishiriki katika mkutano ulioitishwa na Rais wa Benki ya Dunia, Bw. James Wolfenson huko Shangai, China tarehe 25 Mei, 2004. Rais wetu alizungumzia jitihada za kupambana na umaskini duniani hususan uzoefu wa Tanzania katika harakati hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii, kuomba Bunge lako Tukufu kutoa pongezi maalum kwa Rais wetu kwa uongozi wake makini, mzuri na uliotukuka katika medani ya Kimataifa. Naamini kuwa anastahili pongezi hizo maalum hasa tukizingatia kuwa tangu nusu ya pili ya mwaka wa jana Rais wetu amekuwa na matatizo ya kiafya hata kulazimika kufanyiwa upasuaaji mara mbili. Lakini, pamoja na hali hiyo Rais wetu aliweza kutimiza majukumu makubwa ya kimataifa kwa kiwango cha kutukuka. Waswahili wanasema: "Mcheza kwao hutunzwa". Nadhani Bunge hili kwa niaba ya Watanzania wote tumpongeze Rais wetu kwa sifa na heshima kubwa anayoiletea nchi yetu. Nasema hivyo kwa sababu tukizingatia kwamba mwaka wote huu alikuwa anajiguza lakini bado kazi za nje hazikulala. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya sifa na heshima kubwa ya Rais wetu na nchi yetu imekuwa ya manufaa kwa nchi na raia wake. Hivi karibuni tumependekezwa kwa heshima kubwa kuwa wagombea wa ujumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa niaba ya Afrika. Wagombea wenzetu walijittoa kwa heshima yetu kwa imani kuwa ikiwepo Tanzania maslahi yao pia yataangaliwa. Miongoni mwa mifano ya karibuni ya dhahiri ya Watanzania kunufaika ni ushindi wa Mheshimiwa Getrude Mongella kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Umoja wa Afrika na Mheshimiwa Balozi Ali Mchumo kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la *Common Fund for Commodities*, lenye makao makuu huko Amsterdam, Uhlanzi. Yupo pia Mheshimiwa Daudi Mwakawago, aliyekuwa Balozi wetu Umoja wa Mataifa ambaye amechaguliwa kuwa Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa nchini Sierra Leone. Balozi Shani Lweno aliyekuwa Balozi wetu nchini Zambia pia amechaguliwa kuwa Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Sahara Magharibi. Naomba kutumia nafasi hii, kwa mara nyingine tena niwapongeze viongozi wenzetu hawa kwa ushindi na uteuzi wao. Napenda kuwahakikisha kuwa kama vile ambavyo tuliwasaidia katika kupata ushindi tuko tayari kuwasaidia katika kufanikisha majukumu yao na wasisite kututumia iwapo wataona inafaa kufanya hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia tarehe 27 Aprili, 2004 hadi tarehe 7 Mei, 2004 Wizara yangu ilifanya Mkutano wa Mabalozi katika Hoteli ya Serena iliyoko katika Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, Mkoani Arusha. Mkutano huu uliojumuisha Mabalozi wetu walioko nchi za nje na Wakurugenzi waliopo Makao Makuu ya Wizara. Mkutano huo ulikuwa chini ya Uenyekiti wangu nikisaidiwa na Naibu Waziri Dr. Abdulkader Shareef na Katibu Mkuu Ndugu Philemon Luhanjo. Rais wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alitufungulia Mkutano wetu na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa

Amani Abeid Karume aliufunga. Pamoja na kufunga na kufungua Mkutano huo viongozi wetu hao wawili wakuu wa nchi yetu walipata nafasi ya kuzungumza na Mabalozi katika kikao cha ndani. Rais Benjamin William Mkapa alifanya hivyo pale Ngorongoro na Rais Amani Abeid Karume alifanya Ikulu, Zanzibar. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Mabalozi ni mkutano wa kazi kwa maana kwamba madhumuni yake ya msingi ni kuzungumzia wajibu na majukumu ya Wizara kwa jumla na Balozi zetu. Ni mkutano ambao lengo kuu ni kufanya tathmini ya utendaji wetu kwa nia ya kuimarisha na kuboresha utekelezaji wa wajibu na majukumu yetu. Huu ni mkutano wa pili wa Mabalozi kufanyika katika kipindi cha uongozi wa Rais Benjamin Mkapa. Mkutano wa kwanza ulifanyika Dar es Salaam mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, kwa jumla mkutano huu ulikuwa wa mafanikio makubwa. Pamoja na kuzungumzia majukumu ya Wizara yetu na wajibu wetu wa kiutendaji ili kuboresha utekelezaji, Mabalozi wetu walifahamishwa kwa kina mambo muhimu ya kisera na kiutendaji yanayotokea na kufanyika hapa nchini katika nyanja za siasa, uchumi, maendeleo ya jamii na ulinzi na usalama. Jambo la msingi lililofanyika ni kwamba, kwa kila eneo wajibu wa Mabalozi na Wizara yetu kwa jumla viliainishwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mabalozi wetu wamenufaika sana na maelekezo ya Viongozi wetu Wakuu pamoja na mada zilizotolewa na Mawaziri, Wakuu wa Idara za Serikali, Mashirika ya Umma na watu binafsi walioshiriki mkutanoni. Nathubutu kusema kuwa lengo letu la kuwafanya wawe watendaji bora, watetezi hodari na wenye kujihamini wa maslahi ya taifa, bila ya shaka limetimia. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa upeo wao na kina chao cha ufahamu wa masuala ya utendaji kazi na wa mambo muhimu ya taifa umeongezeka. Mabalozi wetu wameondoka mkutanoni wakiwa watu tofauti na wale walioingia kabla ya mkutano.

Naomba kuitumia nafasi hii, Mheshimiwa Spika, kuwashukuru kwa mara nyingine tena viongozi wakuu wa nchi yetu na baadhi ya Mawaziri, Wakuu wa vyombo vyaa dola na taasisi za Serikali, wakuu wa mashirika ya umma na asasi za umma kwa kutumia muda wao adimu na kuja kuzungumza na Mabalozi wetu. Naomba uniruhusu kwa ajili hiyo niwataje baadhi yao kama ifuatavyo: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Kiongozi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Spika wa Bunge, Mheshimiwa Pius Msekwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho. Orodha ni ndefu, naomba hawa watosheleze kuwa wawakilishi wa wengine wengi. Naomba wale ambao sikuwataja, waniwie radhi lakini tunatoa shukrani zisizo na kifani kwao kwa mchango katika kufanikisha shughuli hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. (*Makofî*)

Naomba pia niwashukuru wale wote waliofanya maandalizi ya mkutano huo chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wetu mchapa kazi hodari Ndugu Phillemon Luhanjo. Kazi

yao nzuri ndiyo iliyotuletea mafanikio yote hayo. Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawashukuru wenyiji wetu wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa mapokezi mazuri na ukarimu. Kwa Hoteli ya Serena, *Ngorongoro Crater Lodge* na *Ngorongoro Wildlife Lodge*, tunawashukuru kwa kutupokea na kutuangalia vizuri. Mwisho kabisa, nawashukuru Mabalozi na Washiriki wote kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya mapitio ya hali ya dunia naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa jumla hali ilivyo mwaka huu kwa upande wa usalama na maendeleo duniani haina tofauti kubwa na ilivyokuwa mwaka 2003 nilipokuwa natoa taarifa kama hii. Kwa kweli kwa baadhi ya mambo hali ni mbaya zaidi sasa kuliko ilivyokuwa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, hapa duniani leo taarifa za vita, mashambulizi ya kigaidi, machafuko ya kisiasa na migogoro ya kijamii na kibinadamu zimeendelea kusikika pembe zote za dunia. Ndizo habari zinazopamba vichwa vya habari vya magazeti, radio na televisheni duniani. Kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Mataifa, zaidi ya nchi 27 duniani zimekuwa katika vita au migogoro na machafuko makubwa ya kisiasa na kiusalama. Nchi 17 zinakabiliwa na hali ya vita nazo ni: Burundi, Ivory Coast, Liberia, Sierra Leone, Sudan, Eritrea na Ethiopia katika bara la Afrika. Nyingine ni Afghanistan, Iraq, Srilanka, Lebanon, Syria, Palestina, Nepal, India na Pakistan katika Asia. Katika Bara la Amerika ni nchi za Haiti na Colombia ndizo zilizoko katika hali ya vita. Nchi ambazo zina migogoro mikubwa yenyе kutishia amani ni pamoja na Cyprus, Georgia, Kosovo, *East Timor*, *Western Sahara*, Spain (*Basque Separatist*) na Uingereza (*Northern Ireland*).

Mheshimiwa Spika, Vita na migogoro hiyo duniani vimeigharimu sana Jumuiya ya Kimataifa katika jitihada za kutafuta amani ya kudumu na gharama za ujenzi wa nchi baada ya vita na ujenzi wa taasisi za kiutawala na demokrasia. Vilevile jumuiya ya kimataifa, kupitia Umoja wa Mataifa, imeingia gharama kubwa ya kuunda amani. Kwa sasa hivi Umoja wa Mataifa unaendesha operesheni za kulinda amani zipatazo 16, zinazohusisha wanajeshi wapatao 56,000 na kugharimu dola za Kimarekani milioni 2,600. Mbali na gharama hizo kwa Jumuiya ya kimataifa, katika nchi au jamii husika vita vina madhara mengi ikiwemo kupotea kwa maisha ya watu wengi, wengi zaidi kujueruhija, uharibifu wa mali kufanyika na kuleta hasara nyingine nyingi. Bahati mbaya sana nchi za Mashariki ya Kati, na Bara la Afrika ndizo zilizoathirika zaidi kwa maana ya kuwa na migogoro ya kiusalama iliyo mikubwa zaidi na iliyoathiri watu wengi zaidi na kuvuma sana duniani. Nchi hizo ziko nyuma kwa maendeleo hivyo rasilimali chache zilizopo zinahitajika sana kuleta maendeleo, hutumika kwa vita.

Mheshimiwa Spika, Barani Afrika, mwaka huu ulikuwa kwa kiasi fulani wa matumaini na maendeleo ya kutia moyo kwa upande wa amani na usalama. Migogoro mingi iliyokuwa kero imeelekea kudhibitiwa na jitihada za kupata ufumbuzi wa kudumu zina muelekeo wa matumaini. Migogoro hiyo ni ile ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*), Liberia, Siera Leone, Guinea Bissau, Comoros, Eritrea-Ethiopia, Sudan ya Kusini na Somalia.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kutafuta amani ya kudumu kwa nchi ya Burundi ziliendelea kwa kasi na msisitizo wa kuridhisha. Viongozi wa nchi za Maziwa Makuu waliyoanzisha jitihada hizo mwaka 1996, waliendelea nazo kwa kushirikiana kwa karibu sana na viongozi wa Afrika Kusini na Umoja wa Afrika. Nchi husika za Maziwa Makuu kwa suala hili ni: Uganda (Mwenyekiti), Tanzania (Makamu Mwenyekiti), Kenya, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia na Zambia. Juhudi zao zilipata msukumo mkubwa Novemba, 2003 baada ya kikundi kikuu cha waasi cha *CNDD-FDD* ya Pierre Nkurunziza kilipotiliana saini na Serikali ya Mpito makubaliano ya kuacha mapigano na kugawana madaraka ya kuitawala na kijeshi. Tayari viongozi wa chama hicho wameshajunga na Serikali ya Mpito na wanashiriki vizuri shughuli za Serikali. Wapiganaji wa *CNDD-FDD* pia wanashiriki katika shughuli za ulinzi wa nchi yao wakati ambapo mipango inafanywa ya kuundwa Jeshi jipya la Taifa la Burundi.

Mheshimiwa Spika, makubaliano baina ya Serikali na kikundi hicho cha waasi na utekelezaji wake yameiwezesha Burundi kupata amani kwa karibu asilimia 95 ya nchi hiyo. Asilimia tano iliyosalia ni katika maeneo ya Bujumbura Vijijini ambako bado kumekuwa na hali ya mapigano kati ya majeshi ya Serikali na kikundi cha waasi cha *PALIPEHUTU-FNL* kinachoongozwa na Bw. Agathon Rwasa. Viongozi wa kikundi hicho wamekuwa wakikaidi rai zote zinazotolewa na viongozi wa Kanda na jumuiya za kimataifa ya kuwataka wazungumze na Serikali ya Mpito bila masharti yoyote ili hatimaye nchi yote ya Burundi ipate amani na mauaji, mateso kwa raia na uharibifu wa mali vikomeshwe.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wao uliofanyika tarehe 5 Juni, 2004 mjini Dar es Salaam viongozi wa nchi za Maziwa Makuu, Afrika Kusini na Mozambique (Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika wakati ule) waliendelea kuwasihii viongozi wa *PALIPEHUTU-FNL* wakubali njia ya mazungumzo badala ya bunduki. Kwa sababu ya ukaidi wao, viongozi hao waliamua kuweka kikwazo cha usafiri kwa viongozi wa chama hicho. Kwa mujibu wa uamuzi huo viongozi wa kikundi hicho hawataruhusiwa kutembea tembea katika nchi za Maziwa Makuu na wameiomba jumuiya ya kimataifa nayo kusaidia. Aidha, viongozi waliamua kuwa iwapo viongozi *PALIPEHUTU-FNL* hawataacha mapigano na kufanya mazungumzo na Serikali ya Burundi, watachukua hatua kuomba Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa kikitangaza kikundi hicho kuwa cha kigaidi na kupendekeza kishughulikiwe ipasavyo.

Mheshishiwa Spika, Tanzania inaunga mkono na inasisitiza msimamo huo wa viongozi wa nchi za Maziwa Makuu kwamba wakati umefika kwa Bw. Agathon Rwasa na wenzake wa *PALIPEHUTU-FNL* kusikiliza ushauri wa wengi, waache mapambano na wafanye mazungumzo na Serikali ya Mpito. Sisi tunaamini kuwa hakuna chochote wanachokipigania ambacho hakiwezi kumalizwa kwa njia ya mazungumzo. Wenzao wa kundi la *CNDD-FDD* ya Peter Nkurunziza wameonyesha mfano na wao ni busara kuiga mfano huo mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wao wa Juni 5, 2004, Viongozi wa Ukanda wa Maziwa Makuu pia, walizungumzia maendeleo ya utekelezaji wa hatua zinazofuatia za Mkataba wa Arusha kuhusu Amani ya Burundi hususan matayarisho ya uchaguzi

unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2004. Viongozi wa Nchi za Kanda ya Maziwa Makuu walisisitiza kwamba jitihada zifanywe na viongozi wa Burundi ili uchaguzi ufanyike kama ilivyoamuliwa katika Mkataba wa Amani wa Arusha wa Agosti, 2000. Viongozi wa Kanda, walimwagiza Naibu Rais wa Afrika Kusini, Mheshimiwa Jacob Zuma aende Bujumbura kufanya mazungumzo na vyama vyta siasa ili wamalize tofauti zao na kufungua nia ya uchaguzi kufanyika. Tanzania inaamini kuwa kufanyika kwa uchaguzi ndiko kutakakoashiria kumalizika kwa mgogoro wa kisiasa na kiusalama ulioikumba Burundi tangu Oktoba, 1993 alipouawa Rais Melchior Ndадaye wa nchi hiyo. Hivyo basi, tunawasihi viongozi wa vikundi vyote vyta siasa na kijamii nchini Burundi kutoa uzito unaostahili kwa uamuzi na ushauri wa viongozi wa Kanda.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu kukamilika kwa mazungumzo ya Wakongomani juu ya hatma ya kisiasa na kiusalama ya nchi yao yaliyokuwa yanafanyika *Sun City*, Afrika Kusini. Katika taarifa hiyo, nilisema kuwa Wakongomani walikubaliana kuwa na Serikali ya Mpito na asasi za mpito za kiutawala na kijamii zitakazojumuisha makundi yote ya kisiasa, kijeshi na kijamii yaliyopo nchini. Serikali ya Mpito imeshaundwa chini ya uongozi wa Rais Mheshimiwa Mejor Jenerali Joseph Kabilo. Ina Makamu wa Rais wanne: Mheshimiwa Abilahi Yerodia Ndumbasi (Serikali), Mheshimiwa Jean Pierre Bemba (*Movement for the Liberation of Congo - MLC*), Mheshimiwa Azarius Ruberwa (*RCD - Goma*) na Mheshimiwa Arthur Zaidu Ngoma (*Non Armed Opposition*). Asasi zote za utawala na kijamii kama vile Bunge na Tume mbalimbali zimekwisha undwa na zinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo moja muhimu ambalo halijakamilika ni kuundwa kwa Jeshi la Taifa linalotokana na makundi mbali mbali yenye silaha nchini. Mpaka sasa uongozi wa juu wa Jeshi hilo na kamandi mbali mbali umeshateuliwa lakini utendaji wake unatatizwa na kutokuwepo kwa Jeshi la Taifa. Hali kadhalika, hali ya usalama hasa Mashariki mwa Kongo bado ni ya kutia wasiwasi hasa kutokana na matukio ya mara kwa mara ya mapigano katika majimbo ya Ituri na Kivu. Vilevile hali ya uhusiano wa kutoaminiana na majirani zao wa Uganda na Rwanda ni mambo yanayozidisha wasiwasi kuhusu utulivu wa Kongo.

Naomba niitumie nafasi hii, Mheshimiwa Spika, kusisitiza msimamo wa Tanzania wa kuunga mkono makubaliano ya kuleta amani Kongo na kutoa wito kwa nchi zote kuisaidia Kongo ipate amani ya kudumu. Kwa upande wetu, Tanzania itaendelea kuiunga mkono Serikali ya Mpito ya *DRC* na asasi zake. Tunaahidi kuchangia kwa kadri uwezo wetu kuisaidia Serikali hiyo iweze kutimiza ipasavyo wajibu wake na kuisaidia Kongo kupata amani ya kudumu. Aidha, tunatoa wito kwa Wakongomani kutambua thamani ya amani na hivyo kuwasihii kuutumia vizuri muda huu kujenga misingi imara ya kuihakikishia nchi yao amani na utulivu. Kwa ajili hiyo basi, tunawahimiza Viongozi wa Serikali ya Mpito kukamilisha mapema iwezekanavyo uundaji wa Jeshi la Kitaifa. Umuhimu wa jambo hili hauna haja ya kukumbushwa kwani hakuna kiashirio kikubwa na mdhamini mkubwa wa amani nchini humo kushinda kuwepo kwa Jeshi la Kitaifa. Kadhalika, tunawasihi kudumisha upendo na mshikamano mionganii mwao ili waiwezeshe Serikali yao kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nilieleza Bunge lako tukufu kwamba hali nchini Sudan inatia matumaini baada ya Serikali Kuu na wapiganaji wa *SPLM* kukubaliana kumaliza mapigano na kujumuika kwa pamoja katika Serikali ya Shirikisho. Makubaliano hayo yamezidi kupata nguvu baada ya hivi karibuni, kunako tarehe 26 Mei, 2004 pande hizo kutia saini maridhiano yanayohitimisha mazungumzo baina ya pande mbili hizo huko Naivasha, Kenya 2004. Maridhiano hayo, pamoja na mambo mengine, yanaainisha mgawanyo wa madaraka kati ya pande hizo katika kipindi cha mpito cha miaka sita. Tanzania inazipongeza Serikali ya Sudan na Chama cha waasi cha *SPLM* kwa kupata muafaka unaomaliza vita vya zaidi ya miaka 30 huko Sudan ya Kusini. Tunawasihi viongozi wa Serikali na *SPLM* watekeleze kwa dhati makubaliano yao ili watu wa Sudan wapate amani ambayo ni haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, matumaini ya kupata amani ya kudumu nchini Sudan yameingia dosari kubwa baada ya kuzuka mapigano mapya katika jimbo la Darfur lililoko Magharibi mwa Sudan. Mapigano hayo yanayowahusisha wanamgambo wa Kiarabu (Janjaweed Militia) na makabila ya Kiafrika yamesababisha vifo vya maelfu ya watu na kuacha wengine zaidi ya milioni moja wakiwa wakimbizi ndani ya nchi yao na nchi jirani ya Chad. Watu wengi wanateseka kwa mazingira mabaya wanayoishi uhamishoni. Mzozo wa Darfur unaleta mgogoro mkubwa wa kibinadamu. Mapigano ya Darfur yasipodhibitiwa na wakimbizi kuhudumiwa ipasavyo na kwa haraka, yanaweza kusabibisha maafa makubwa kwa wanadamu wasiokuwa na hatia. Dunia inaanza kushuhudia maafa makubwa ya halaiki kwa mara nyingine tena.

Napenda kuchukua fursa hii, Mheshimiwa Spika kumshukuru Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mheshimiwa Kofi Annan na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika Mheshimiwa Alpha Omar Konare kwa uongozi wao na hatua madhubuti walizochukua na wanazoendelea kuchukua katika kupata ufumbuzi wa kudumu wa mzozo wa Darfur. Katika jitihada hizo Umoja wa Mataifa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika wameunda Tume ya Kusimamia Usitishaji wa Mapigano na kukubaliana kupeleka waangalizi wa Kijeshi (*Military Observer Mission*). Aidha, hivi karibuni Baraza la Usalama lilipitisha azimio la kuitaka Serikali ya Sudan kuwadhibiti wanamgambo wa Janjawied wanaona raia wenzao wenye ngozi nyeusi. Ni matumaini yetu kuwa Serikali ya Sudan itatekeleza agizo hilo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mionganoni mwa nchi zilizoombwa kupeleka wanajeshi nchini Sudan kujiunga na kundi la waangalizi wa kijeshi huko Darfur. Kama alivyokwisha eleza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Phillemon Sarungi, Tanzania itatimiza ipasavyo wajibu wake kwa wananchi wa Sudan na Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe kumalizika nchini Cote d'Ivoire takriban miaka miwili iliyopita, kulikuwa na matumaini makubwa kwamba amani itarejea tena nchini humo. Kutiwa saini kwa mkataba wa kusitisha mapigano wa Linas-Marcoussis, huko Ufaransa kulizidisha matumaini yetu. Hata hivyo, matumaini hayo yameathiriwa vibaya na kukwama kwa utekelezaji wa mkataba huo baada ya pande zinazohisika kushindwa kuheshimu ipasavyo makubaliano yao. Matokeo yake ni

wawakilishi wa Vikundi nya Upinzani kujiondoa kwenye Serikali ya mseto. Aidha, hali ya wasiwasi imeongezeka baada ya mapambano kuzuka tena kaskazini mwa nchi hiyo kati ya tarehe 20 na 21 Juni, 2004. Tumepokea kwa furaha jitihada za Katibu Mkuu Kofi Annan na viongozi wa ECOWAS kuzileta pande zinazohusika katika meza ya mazungumzo na makubaliano mapya yaliyofikiwa. Napenda kuchukua fursa hii kuzitaka pande zote zinazopingana nchini Cote d'Ivoire kuhakikisha kwamba zinafanya kila njia ili kurahisisha utekelezaji wa mkataba wa Lina-Marcoussis na makubaliano yao ya hivi majuzi (tarehe 30 Julai, 2004) huko Accra, Ghana.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Liberia imeendelea kuleta matumaini hasa baada ya Bwana Charles Taylor kwenda uhamishoni nchini Nigeria na Liberia kupata uongozi mpya. Tangu wakati huo na hasa baada ya kutiwa saini kwa mkataba wa amani kati ya waasi na Serikali ya Liberia, maendeleo mbali mbali ya kutia moyo yamepatikana. Jeshi la kulinda amani la Umoja wa nchi za Afrika Magharibi (ECOMOG) pamoja na Jeshi la kulinda amani la Umoja wa Mataifa yameweza kupelekwa nchini Liberia. Zoezi la kuwanyang'anya silaha wapiganaji linaendelea vizuri na mpango wa kuwasaidia wapiganaji hao kurudi katika maisha ya kawaida uraiani upo katika muelekeo mzuri. Tanzania inawapongeza sana wananchi wa Liberia kwa hatua kubwa waliyoipiga mpaka sasa katika kurejesha amani na utulivu nchini mwao. Ni matumaini yetu kuwa pande zinazohusika na mgogoro huo zitatekeleza kwa ukamilifu wajibu wao kwa mujibu wa Mkataba wao ambao hatma yake ni kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2005.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa migogoro ya kisiasa katika visiwa nya majirani zetu Comoro, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba juhudzi za kimataifa, hususan, hatua za makusudi za Umoja wa Afrika, zimewezesha pande zinazopingana visiwani humo kufikia makubaliano/suluhu. Kunako tarehe 20 Desemba, 2003, pande hizo zilitiliana saini mkataba wa kuacha kabisa malumbano yao. Tanzania ni moja ya nchi zilizounda kamati ya usuluhishi ya AU na imeshiriki kwa ukamilifu toka hatua ya mwanzo hadi kupatikana kwa huo Mkataba wa Amani Visiwani humo. Makubaliano yao katika mkataba huo yalihusisha kujengwa mazingira ya utulivu visiwani humo ili wananchi wake weweze kuendesha uchaguzi wa Wabunge wa kuunda Bunge la Serikali ya Muungano (*Union Government*) na Mabunge ya visiwa vyote vitatu (Ngazidja, Anjouan na Moheli) ulishafanyika Aprili, 2004.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Bunge la Muungano wameshaapishwa na Serikali ya Muungano imeundwa hivi karibuni. Tunatazamia Bunge hilo kuanza kazi zake hivi karibuni. Kamati ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba wa amani Comoro inaendelea kufuatilia utekelezaji wa Mkataba wa Desemba, 2003. Tanzania ni moja ya nchi zinazounda Kamati hiyo na tunaaminu kuwa Mkataba huo ndiyo njia pekee ya uhakika ya kuleta amani ya kudumu Visiwani humo.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya Mabunge hayo (kwa ngazi zake) ni kutoa tafsiri sahihi ya Katiba ya nchi, hususan katika masuala ya mgawanyo wa madaraka kwenye taasisi na vyombo mbali mbali nya Serikali, mgawanyo wa bajeti ya nchi na mgawanyo wa madaraka katika vyombo nya ulinzi na usalama, mambo ambayo kimsingi ndiyo chimbuko la mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, Bunge bado halijaanza kazi yake baada ya Serikali ya Kisiwa cha Ngazidja kuomba masuala kadhaa yafanyiwe marekebisho na hivyo kusababisha kuahirishwa kwa shughuli za uzinduzi rasmi wa Bunge hilo zilizokuwa zimepangwa tarehe 27 Mei, 2004. Kamati ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba wa amani Comoro inaendelea kuyatafutia ufumbuzi masuala yaliyoletwa na Kisiwa cha Ngazidja ili Bunge lizinduliwe mara moja na kuanza kazi yake. Kamati hiyo iliundwa kwa mujibu wa makubaliano yaliyo kwenye Mkataba wa Desemba, 2003. Ni matumaini yetu kuwa pande zinazohusika zitaendelea kuheshimu na kutekeleza Mkataba wao huo.

Mheshimiwa Spika, bila shaka mmekuwa mkifuatilia taarifa mbalimbali kuhusu mgogoro wa Sahara Magharibi kati ya Chama cha Wapigania Uhuru cha *POLISARIO* na Morocco. Baada ya Morocco kukataa Azimio la Umoja wa Mataifa linalotaka kuitishwa kwa kura ya maoni ili wananchi wa Saharawi wajiamulie mustakabali wao yaani ama kuwa taifa huru au kujunga na Morocco, Bwana James Baker, Msuluhishi wa mgogoro huo alipendekeza marekebisho katika mpango huo. Kwa mujibu wa marekebisho hayo ambayo yalikubaliwa na Umoja wa Mataifa, Saharawi itapewa nafasi ya kuwa na Serikali ya madaraka ya ndani (*Autonomous Status*) chini ya Morocco kwa kipindi cha mpito cha miaka mitano. Baada ya hapo wananchi wa Saharawi watapiga kura ya maoni kuamua kama watapenda kuendelea kuwa chini ya Morocco au kupata uhuru kamili. Chama cha Polisario kimeukubali uamuza huo wa Umoja wa Mataifa lakini Serikali ya Morocco inaupinga. Tanzania inaona uamuza huu mpya wa Umoja wa Mataifa ni jaribio na njia nyingine muafaka ya kuelekea kumalizika kwa mgogoro huu wa zaidi ya miongo mitatu sasa. Hivyo basi, jumuiya ya kimataifa haina budi iweke shinikizo kwa Morocco kukubali ili utekelezaji wa mpango huo uanze.

Mheshimiwa Spika, balaa la mamluki limejitokeza tena katika Bara letu la Afrika. Bila ya shaka itakumbukwa kuwa tarehe 7 Machi, 2004 Serikali ya Zimbabwe ilikamata ndege iliyokuwa na mamluki sabini, pamoja na vifaa mbalimbali vyta kijeshi. Mamluki hao walikuwa wakielekea nchini *Equatorial Guinea* kwa madhumuni ya kuipindua Serikali halali ya nchi hiyo. Kukamatwa kwa mamluki hao na wengine 15 waliokamatwa wakiwa tayari ndani ya *Equatorial Guinea* kulitokana na ushirikiano wa vyombo vyta usalama vyta Zimbabwe, Angola na Afrika Kusini. Katika mkutano wa Wakuu wa nchi za Umoja wa Afrika uliomalizika hivi karibuni, Wakuu hao kwa kauli moja wa nchi za Umoja huo wamelaani vikali kuibuka upya kwa umamluki katika Bara letu. Wamesisitiza azma yao ya kupambana na umamluki na kuzitaka nchi wanachama kuzidisha ushirikiano katika suala hilo hususan katika kubadilishana taarifa za usalama zinazohusu umamluki na kuwadhibiti.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililiarifu Bunge lako tukufu kuhusu Tanzania kupewa heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Maziwa Makuu uliotarajiwa kufanyika mwezi Juni, 2004. Mkutano huo wa aina yake unaitishwa na Umoja wa Mataifa kwa ushirikiano na Umoja wa Afrika kujadili mikakati na mbinu za kulifanya eneo la nchi za Maziwa makuu kuwa ni eneo lisilokuwa na migogoro, lina amani na utulivu na ambalo linakuwa kitovu cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi na ushirikiano wa kanda. Aidha, eneo hili linatarajiwa kuwa eneo lenye utawala bora, demokrasia na

haki za binadamu zinaheshimiwa. Mkutano huo sasa unatarajiwa kufanyika Novemba, 2004. Ulichelewa kufanyika kwa sababu kuu mbili. Kwanza, kutokana na matatizo ya kifedha kugharamia mkutano baada ya baadhi ya mataifa wajumbe wa Baraza la Usalama kutaka Umoja wa Mataifa usigharamie mkutano huo kutoka fedha zake bali vitafutwe vyanzo vingine. Suala la gharama linalekeea kupatiwa ufumbuzi baada ya nchi kadhaa zinazojiita “Marafiki wa Maziwa Makuu” kuamua kuchangia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo limejitokeza hivi karibuni na kuchangia kucheleweshwa kwa mkutano ni madai ya kutaka Angola na Kongo Brazaville zihesabiwe kuwa ni nchi za Maziwa Makuu na hivyo zishirikishwe kwa hadhi hiyo katika Mkutano huo. Jambo hilo limezua mzozo usiokuwa na msingi kabisa. Kwa miaka karibu miwili sasa ya matayarisho ya Mkutano huu nchi zilizohusishwa ni Burundi, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda, Tanzania, Uganda na Zambia. Hizi ndizo nchi ambazo kihistoria zinazunguka maziwa makuu yaani Tanganyika, Victoria, Kivu na Albert. Ilipojitokeza tafsiri mpya imezua mjadala mkali na kuibua hisia za kutilia shaka dhamira ya wale walioleta hoja hiyo. Bado mjadala unaendelea lakini tunaamini kuwa tutapata muafaka mzuri muda si mrefu kutoka sasa na mkutano kufanyika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wetu maandalizi ya kuupokea mkutano huo yanaendelea vizuri. Tanzania itafanya kila tuwezalo kuhakikisha kuwa Mkutano huu unafanikiwa. Tunatambua fika athari za kutofanikiwa kwa Mkutano huu kwa sababu ya mapungufu yetu. Tutajitahidi isiwe hivyo. Kadhalika, matayarisho ya ushiriki wetu kwa maana ya Serikali, sekta binafsi na vyama vyama kijamii (*Civil Societies*) yanaendelea vizuri. Kwa upande wa vyama vya kijamii tuliwaomba wenzetu wa *Mwalimu Nyerere Foundation* wawe waratibu. Wamekubali na wamekuwa wanafanya kazi nzuri. Napenda kuitumia nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wale wote ambao wamechangia na wanaendelea kuchangia katika kufanikisha Mkutano huu muhimu na ushiriki wa Tanzania katika Mkutano huo. Tuendeleze ushirikiano wetu huo mpaka hapo mkutano utakapoanza na kuisha.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu Mpango wa Amani ya Mashariki ya Kati uitwao *Road Map*, uliobuniwa na mataifa makubwa manne duniani yaani Marekani, Urusi, Uingereza na Ufaransa. Mpango huo unalenga kupatikana kwa taifa huru la Wapalestina ifikapo mwaka 2005. Inasikitisha kuona kuwa utekelezaji wa mpango huo umekwama na hasa kutokana na kukosekana kwa utashi wa kisiasa kwa upande wa Israel wa kuwepo kwa taifa huru la Palestina. Badala yake dunia imeshuhudia Israel ikifanya vitendo vinavyovuruga muelekeo mzima wa Mpango huo wa Road Map. Kwanza, ni ule uamuzi wake wa kujenga ukuta ambao kimsingi una mpaka mpya kati ya Israel na Palestina.

Bahati mbaya, mpaka huo haujazingatia mipaka inayotambulika Kimataifa kati ya mataifa hayo mawili. Baya zaidi ni kuwa ukuta huo umepona zaidi ardhi ya Wapalestina na kumeleta mateso kwa watu wengi. Katika sehemu nyngi ulimopita ukuta huo, vijiji vimemegwa katikati, familia zimetenganishwa na jamaa zao, watu wengine

wametenganishwa na mashamba yao au hata vyanzo vy a huduma muhimu kama vile maji, hospitali, shule, ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Waziri Mkuu wa Israel, Mheshimiwa Ariel Sharon, alitangaza mpango wa kuondoka ukanda wa Gaza na sehemu za ukingo wa Magharibi mwa Mto Jordan. Kwa upande mmoja ni hatua ya maendeleo kuelekea kupatikana kwa taifa la Palestina. Hata hivyo, kwa vile bado makazi ya Wayahudi wanaowajibika Israel na watakaolindwa na Israel yataendelea kuwepo katika ukanda wa Ukingo wa Magharibi wa Mto Jordan, uamuzi huo bado haukidhi haja ya kupata jawabu la tatizo la Palestina na Israel. Isitoshe ukichanganya na ujenzi wa ukuta na matatizo yanayohusiana nayo bado uamuzi wa Waziri Mkuu wa Israel una mapungufu mengi.

Tanzania inaamini kuwa jawabu la kudumu la mgogoro kati ya Wayahudi na Wapalestina lipo katika kupatikana kwa Taifa huru la Palestina linaloishi kwa amani na Israel, taifa ambalo limekamilika na lina mipaka endelevu na ya kudumu. Sisi tunaamini kuwa Mpango wa Road Map ndiyo njia ya uhakika ya kufikia kwenye hatma hiyo ya amani na utulivu. Hivyo basi, Israel haina budi kufufua utashi wa kisiasa wa kuwepo Taifa la Palestina na kusaidia kwa dhati hatua za kuelekea huko. Aidha, tunarudia kutoa wito kwa pande zote zinazohusika kufanya kila wavezalo kurudi kwenye meza ya mazungumzo kwa ajili ya kutekeleza *Road Map*. Waepuke kufanya vitendo vinavyozidisha chuki na kuvuruga Mpango huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Iraq bado ni kitendawili kinachohitaji ufumbuzi. Baada ya Serikali ya Saddam Hussein kuangushwa na mwenyewe kukamatwa, tulidhani hali ya amani ingerejea. Bahati mbaya hali haikuwa hivyo, vitendo vy a kigaidi viliongezeka sana na Iraq imeendelea kuwa mahali pasipokuwa na usalama. Tulitegemea pia kwamba baada ya Marekani na Uingereza kukabidhi madaraka kwa Serikali ya Mpito inayoongozwa na Wairaq wenyewe, mashambulizi ya kigaidi yangepungua lakini haijawa hivyo. Mashambulizi yanaendelea na taarifa za watu kupoteza maisha, kujeruhiwa na mali kuharibiwa zimekuwa ni habari za kawaida. Hali hii ni mbaya tena ya hatari na hairidhishi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, hatuna ushauri wa uhakika juu ya nini kifanyike kuibadili hali hiyo. Sote tunaendelea kutumaini kwamba, wakati utasaidia kupata jawabu ambalo kwa hakika ni jawabu la mtu aliyehemewa na kupungukiwa hoja. Pengine, uchaguzi huru na wa haki mwishoni mwa kipindi cha Serikali ya sasa ya Mpito huenda itakuwa mwanzo wa kupatikana amani na utulivu nchini humo. Pamoja na kusubiri wakati huo Tanzania inatoa wito kwa wanamgambo kuisaidia nchi yao kupata amani. Wananchi wa Iraq wanaistahili haki yao hiyo baada ya miaka minge ya mateso na kukandamizwa chini ya udikteta wa Saddam Hussein na vita mbili kubwa.

Mheshimiwa Spika, ugaidi bado ni tishio kubwakwa amni na usalama duniani. Matukio ya kigaidi yameendelea kutikisa sehemu mbalimbali za dunia na kusababisha kuongezeka kwa hofu mionganoni mwa watu. Kwa mwaka uliopita, dunia imeshuhudia matukio makubwa ya kigaidi huko Hispania, Saudi Arabia, Urusi na Mashariki ya Kati

ambapo mamia ya watu wamepoteza maisha na wengine wengi kujeruhiwa na mali kuharibiwa.

Mheshimiwa Spika, dunia haina budi kuendelea kulaani na kupambana na vitendo vyote nya kigaidi bila huruma na woga. Kuendelea kuwepo matukio ya kigaidi kunaimarisha haja ya dunia kuendelea kuweka mikakati ya pamoja ya kupambana dhidi ya maovu haya. Kadhalika, dunia iendelee na hatua mbali mbali zinazochukuliwa kupata ufumbuzi wa matatizo na hasa mazingira yanayokuwa mboji ya kumea kwa ugaidi na kuzaa magaidi wa kimataifa. Tanzania inaendelea kuahidi kutoa mchango wake wa hali na mali katika vita dhidi ya ugaidi. Tukiwa wahanga wa ukatili wa ugaidi kwa tukio la Agosti 7, 1998 nchi yetu inayo kila sababu na nia ya kufanya hivyo. Bahati nzuri siku hizi na uwezo pia tunao. Tunashukuru pia kwa misaada tuipatayo kutoka kwa Mataifa rafiki inayotuungezea uwezo wetu wa kuzuia na kukabiliana na vitendo nya ugaidi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha uliopita nilielezea masikitiko yetu kwa athari tuzipatazo kutokana na ushauri wa usafiri (*Travel Advisories*) uliokuwa unatolewa na baadhi ya nchi za Ulaya na Marekani unaotahadharisha raia wa nchi zao dhidi ya kutembelea Tanzania na nchi za Afrika Mashariki kwa sababu ya kuwepo tishio la mashambulizi ya kigaidi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali yetu kuititia Wizara yangu na Ofisi zetu za Kibalozi nje ililivalia njuga suala hili ili kuzuia athari zake kwa uchumi wetu na hasa kwa sekta ya utalii. Dalili za mafanikio zinaanza kuonekana kwani taarifa za aina hiyo zimeanza kupungua sana. Aidha, hata utoaji wa taarifa hizo pale ambapo hapana budi umeboreshwa. Kuna mashauriano au hata kupeana taarifa za tahadhari ya kutolewa taarifa ya namna hiyo kabla haijatoka. Ni mabadiliko mema. Ni matumaini yetu kuwa ushirikiano huu mpya utadumu.

Mheshimiwa Spika, sura ya maendeleo duniani bado haipendezi. Bado duniani kuna nchi na watu maskini sana wakati ambapo kuna mataifa na watu matajiri sana. Ubaya wake unakuja pale ambapo jitihada zinazofanywa na mataifa tajiri husaidia mataifa maskini kujinasua kutoka katika dimbwi la umaskini zinapoonekana kutokutosheleza na hivyo kuacha watu wengi wakihoji kudhani kuwa kuna upungufu wa utashi wa kisiasa kiasi cha kufanya watu wahoji usahihi wa sera za kiuchumi na za maendeleo za nchi husika na wafadhili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Maendeleo Duniani (*The World Development Report*) ya mwaka wa 2003, idadi ya watu maskini duniani imekuwa inaongezeka badala ya kupungua. Kwa mwaka 1990 kulikuwa na watu wapatao milioni 917 waliokuwa wanaishi chini ya dola moja kwa siku na watu wapatao milioni 2,712 wakiishi kwa chini ya dola mbili kwa siku katika kipindi hicho hicho. Idadi ya watu wanaoishi kwa kipato cha dola moja kwa siku iliongezeka na kuwa milioni 945 na wale wa kipato cha dola mbili kikaongezeka na kufikia watu milioni 2802. Inakadiriwa kwamba hadi kufikia mwaka wa 2015 zaidi ya nusu ya watu wote duniani watakuwa na kipato pungufu ya dola mbili kwa siku. Hali hii si tu ni mbaya bali inatisha na kusikitisha.

Aidha, mzigo wa madeni kwa nchi maskini duniani unazidi kuongezeka uzito na hivyo kuathiri sana uwezo wa nchi hizo kumudu mahitaji ya msingi ya kujiondoa katika lindi la umaskini. Kwa mujibu wa taarifa za *SADC* nchi za wanachama wa umoja huo kwa mfano wanadaiwa jumla ya \$ 69.12 bilioni. Maradhi, hasa malaria, kifua kikuu na UKIMWI yameendelea kuathiri na kuua mamilioni ya watu duniani na wengi wao wakiwa katika nchi zinazoendelea. Kwa mfano, takwimu zinaonyesha kwamba duniani kuna wagonjwa wa Ukimwi Milioni 47 na zaidi ya asilimia 95 ni kutoka nchi zinazoendelea na asilimia 70 wako nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Inakadirisha kuwa kati ya 2002 na 2010 watu milioni 45 zaidi watakuwa wameathirika na UKIMWI. Idadi ya watoto yatima wanaotokana na UKIMWI imeongezeka kutoka 11.5 milioni hadi 15 milioni kati ya mwaka 2001 na 2003.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuwepo na hasa kuongezeka kwa watu na nchi maskini sana duniani badala ya kupungua, kuendelea kukua kwa mzigo wa madeni badala ya kupungua, kuendelea kuongezeka kwa maradhi badala ya kupungua kunadhihirisha kasoro na mapungufu mengi mionganoni mwa wanadamu na mataifa. Kuna mikataba, mingi na makubaliano na maazimio mengi duniani ambayo kama yangezingatiwa na kutekelezwa hali ingekuwa bora badala ya kudumaa na kurudi nyuma tunakokushuhudia sasa. Ni dhahiri basi kuna pengo kubwa kati ya ahadi na utekelezaji wake na baadhi ya sera bado hazikidhi haja ya kukabili matatizo yanayoisibu dunia. Hatuna budi kuongeza mshikamano na mataifa yaliyoendelea kutimiza kwa dhati wajibu na ahadi zao wanazozitoa katika majukumu ya kimataifa na hata ya Mataifa yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuitumia fursa hii kwa Mara nyingine tena kuwasihii wenzetu wa Mataifa yaliyoendelea kuongeza kasi ya kuelekea kwenye kutimiza ahadi yao ya kuchangia asilimia 0.7 ya Pato la Taifa la nchi zao kwa ajili ya misaada ya maendeleo. Mpaka sasa karibu miaka 20 tangu azimio hilo litolewe tupo kwenye asilimia 0.23 tu. Kama mataifa hayo yangefikia kiwango hicho utekelezaji wa Malengo Manne ya Milenia ungekwenda vizuri sana. Hivi sasa unasua sua tu kwa sababu ya upungufu wa rasilimali. Naomba niitumie nafasi hii kuzipongeza nchi za Luxembourg, Sweden, Denmark, Norway na Netherlands kwa kufikia lengo. Tunawapongeza kwa kuongoza njia, tunaomba na wengine wafuate mapema iwezekanavyo. Kwa upande wa madeni naomba kuirudia kauli ambayo tumekuwa tunaitoa mara kwa mara kwamba nchi maskini na dhana ya uendelevu na madeni (*Debt Sustainability*) imepoteza maana. Kwa nchi maskini madeni hayalipiki, hivyo jambo la busara ni kusamehewa madeni yote. Ni kweli pia kwamba hata mpango wa *HIPC* haujatatua tatizo pamoja na nafuu tuipatayo ambayo tunatoa shukrani za dhati.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana, Tanzania ni mwanachama wa ushirikiano wa kanda nne. Kwanza kabisa ni mwanachama wa *Kagera River Basin Organisation* kwa pamoja na nchi za Uganda, Rwanda na Burundi. Pili, ni mwananchama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), inayojumuisha nchi nyingine 12 yaani Afrika Kusini, Botswana, Angola, Namibia, Lesotho, Swaziland, *DRC*, Mauritius, Msumbiji, Malawi, Zambia na Zimbabwe. *SADC* imepungukiwa mwanachama mmoja baada ya Seychelles kujitoa. Rai zote za kuwataka wabaki hazikufanikiwa. Tatu, ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika

Mashariki (*EAC*) pamoja na Kenya na Uganda. Nne ni mwanachama wa Umoja wa Nchi zinazopakana na Bahari Kuu ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association of Regional Cooperation - IOR-ARC*). Umoja huu unajumuisha nchi 19 zifuatazo Tanzania, Kenya, Msumbiji, Afrika Kusini, Yemeni, Oman, *EAE*, Iran, India, Singapore, Indonesia, Malaysia, Japan, New Zeland, Madagascar, Maldives, Sri Lanka, Mauritius na Seychelles. Uanachama wa jumuiya hizo ni fursa muhimu ya kuendeleza maslahi ya kiuchumi, kisiasa na hata kiusalama ya nchi yetu. Pia inatusaidia kujenga nguvu muhimu ya umoja wa kupigania haki duniani na kujenga uwezo wa ushindani katika dunia ya leo ya utandawazi.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyokumbuka, Agosti, 2003, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*). Katika mkutano huo Tanzania ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo na hivyo Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa akachukua hatamu za uongozi wa *SADC*. Mara baada ya kuchukua uongozi wa *SADC* tulijipangia malengo ya kazi za kufanya pamoja na wajibu wa kawaida wa kufuutilia utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya Jumuiya. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa pamoja na kwamba kwa sehemu kubwa ya uongozi wake Rais wetu alikuwa anajiuguza, malengo mengi tuliyojiwekea yameweza kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niyataje baadhi ya malengo muhimu tuliyoyatekeleza. Jambo moja ni kukamilika kwa Mkakati wa Maendeleo wa Kanda (*The Regional Indicative Strategic Development Plan*). Baada ya kukamilika kwake Rais wetu aliuzindua rasmi mpango huo tarehe 12 Machi, 2004, wakati wa Mkutano wa Baraza la Mawaziri la *SADC* uliofanyika Arusha. Huu ni mpango wa kimkakati wa kusukuma maendeleo ya nchi za *SADC* ulioangalia na kuhusisha sekta zote za ushirikiano. Shabaha ya msingi ya mpango huu ni kutokomeza umaskini wa nchi na Wananchi katika nchi wanachama wa Jumuiya yetu.

Jambo la pili muhimu lililotekeliza Mheshimiwa Spika, ni kufanyika kwa Mkutano wa Kilimo na Usalama wa Chakula katika *SADC* kunako tarehe 15 Mei, 2004. Mjini Dar es Salaam Mkutano huu wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* uliitishwa na Mwenyekiti wa *SADC* Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kujadili hali ya kilimo na upatikanaji wa chakula katika ukanda wetu. Lengo kuu la kuitisha Mkutano lilikuwa ni kujadiliana na kupanga mikakati na mbinu za kuinua hali ya kilimo katika Jumuiya ili tuweze kuondokana na aibu ya upungufu wa chakula na njaa. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mkutano huo ulikuwa wa mafanikio makubwa na kwamba kwa kauli moja viongozi wetu walikubaliana kushirikiana na kuchukua hatua kadhaa za kuendeleza kilimo ili kutokomeza upungufu wa chakula na hivyo basi kumaliza tatizo la njaa katika *SADC*. Katika kipindi hiki pia Tanzania iliongoza *SADC* katika majadiliano na Umoja wa Ulaya kuhusu Mkataba wa Ushirikiano (*Economic Partnership Agreement*) baina yetu. Mkutano wa hivi karibuni uliofanyika Windhoek, Namibia tarehe 8 Julai, 2004 ulikuwa mzuri na wa mafanikio. Ni matumaini yetu kuwa mazungumzo yanayofuatia nayo yatakuwa mazuri na hatimaye tutapata mkataba wenyе maslahi kwetu sote.

Kwa jumla mikutano yote tuliyopanga kufanya, yaani, Baraza la Mawaziri, Kamati ya Pamoja ya Mawaziri na sekta mbali mbali ilifanyika kama ilivyopangwa. Ni mkutano mmoja tu wa Baraza la Mawaziri ndio hatukuweza kuufanya. Huo ni ule tuliyopanga kuzungumzia *NEPAD* ambao haukuweza kufanyika kwa sababu ya kuingiliwa na tarehe za Uchaguzi Mkuu nchini Malawi baada ya tarehe hizo kufanyiwa mabadiliko. Hata hivyo, mkutano umepangwa kufanyika Mauritius tarehe 7 - 9 Agosti, 2004. Katika moja ya malengo muhimu ya Rais wetu wakati akipokea Uenyekiti ilikuwa kutembelea Makao Makuu ya *SADC* huko Gaborone, Botswana. Lengo ambalo amelikamilisha kuanzia tarehe 26 mpaka 28 Julai, 2004.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi chetu cha Uenyekiti, Tanzania imeongoza Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika kwa ufanisi mkubwa. Hivyo basi, katika kikao kijacho cha *SADC* kitakachokuwa Port Louis, Mauritius kuanzia tarehe 9 mpaka 17 Agosti, 2004 Tanzania itakabidhi uongozi wa Jumuiya kwa Mauritius ikiwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2003/2004, nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba majadiliano ya kufikia Mkataba wa Umoja wa Forodha yalikuwa katika hatua za mwisho. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kazi hiyo ilishakamilika. Mnamo tarehe 2 Machi 2004, Wakuu wa Nchi zetu tatu Wanachama wa Jumuiya, yaani Mheshimiwa Benjamin William Mkapa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mwai Kibaki, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda walikutana Mjini Arusha na kuitisha rasimu na hatimaye kuweka saini Mkataba wa kuanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkataba wa Umoja huo unategemewa kuanza kutumika tarehe 1 Januari, 2005 baada ya nchi wanachama kuridhia.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Forodha, utachochea na kurahisisha shughuli za kibiashara na kiuchumi katika nchi zetu za Afrika Mashariki na kati ya nchi na watu wa Afrika Mashariki, wakiwemo wazalishaji mali, mawakala, wafanyakishara na watumiaji kwa ujumla wao. Mkataba huu pia utakuwa chachu ya kuanza kuunganisha na kufungamanisha tena uchumi wa nchi zetu tatu kama ilivyokuwa wakati wa Jumuiya ya zamani ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba huo hatukuwa na ushuru wa forodha kwa bidhaa zitokazo Tanzania na Uganda zinapouzwa katika soko la Afrika Mashariki. Kwa upande mwingine, bidhaa za Kenya zinazoingia katika soko la Tanzania na lile la Uganda zitakuwa zinatozwa ushuru kwa miaka mitano. Hata hivyo, ushuru huo utakuwa unapunguzwa taratibu hadi kufikia kiwango cha sifuri kwa mwaka wa sita tangu Mkataba wa Umoja wa Forodha utakapoanza kutumika. Orodha ya bidhaa zitakuwemo katika utaratibu imeshakamilishwa na kukubaliwa, Tanzania ina bidhaa 899 wakati Uganda wana bidhaa 426. Aidha, zipo bidhaa chache ambazo nchi wanachama zimekubaliana kuwa hazitahusishwa katika utaratibu wa kuondoleana au kupunguziana ushuru. Bidhaa zote za kiusalama na zile zinazokatazwa kwa mujibu wa Mikataba ya

Kimataifa hazimo kabisa katika utaratibu wa kufutiana ushuru. Hivyo basi, ushuru utaendelea kuwepo kwa bidhaa husika.

Mheshimiwa Spika, Katika Mkataba wa Umoja wa Forodha nchi zetu zilikubaliana kuweka wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha kwa bidhaa zitokazo nje ya nchi zetu tatu. Imekubaliwa kuwepo na viwango vitatu vya msingi. Viwango hivyo ni asilimia sifuri kwa malighafi na asilimia 10 kwa bidhaa za kat. Hizi ni bidhaa ambazo zimetengenezwa kwa kiasi fulani lakini hazikufikia mwisho. Ni bidhaa mbazo zinaweza kutumika zilivyo na kuwa mali ghafi ya kutengeneza bidhaa nyingine. Kiwango cha tatu ni asilimia 25 ambacho hutozwa bidhaa zilizokamilika kabisa tayarikutumika. Pamoja na hayo kumekuwapo na bidhaa zilizowekwa kundi lijulikanalo kama “Bidhaa Nyeti”. Hizi ni bidhaa ambazo kwa umuhimu wake kwa uchumi na nchi zinastahili kulindwa dhidi ya ushindani wa nje. Kwa ajili hiyo imeamuliwa kuwa bidhaa hizo zitozwe ushuru mkubwa kuliko kiwango cha juu cha asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kutoza ushuru kwa muda wa miaka mitano kwa bidhaa za Kenya ni kutaka kulinda viwanda vichanga vya Tanzania na Uganda dhidi ya viwanda vya Kenya vilivyo imara. Lengo ni kutoa nafasi kwa viwanda vya Tanzania na Uganda kukua, kujijenga na kujiimarisha, ili baada ya kipindi hicho vimudu ushindani. Ili kuratibu mwenendo na shughuli za Umoja wa Forodha, imeundwa idara katika Sekretariati itakayoongozwa na afisa mwandamizi atakayekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Umoja wa Forodha mwenye hadhi sawa na Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya. Uteuzi wa afisa mtendaji mkuu huyo utafanywa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wale wote walioshiriki bila kuchoka katika majadiliano ya kufikia Mkataba wa Umoja wa Forodha. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Mawaziri wenzangu na Makatibu Wakuu wote tulioshirikiana bega kwa bega kutetea maslahi ya Afrika Mashariki na hasa yale ya Tanzania. Aidha, nawashukuru wenzetu wa sekta binafsi na jamii kwa kupitia *TCCIA, CTI, NBC, ESRF, ERB - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Private Sector Foundation* na wasomi kwa jumla kwa mchangwo katika kufanikisha hatua hii muhimu. Naamini kwa dhati kuwa umoja wetu, mshikamano wetu, ushirikiano wetu pamoja na uvumilivu wetu na moyo wa ndivyo vilivyo tuwezesha kupata Mkataba ambao kwa kiasi kikubwa umepata muafaka wa wengi.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umetoa fursa ya kukuza na kuendeleza uchumi wa nchi zetu kwa kufungua soko kubwa la watu 80 milioni kuwa soko moja. Lakini, fursa hii mtu haletewi mkononi au mdomoni bali anaipata kwa kuzalisha bidhaa na huduma za kuuza katika soko hilo. Nayasema haya kusisitiza ukweli kwamba hatuna budi kujipanga vizuri kisera na kiutendaji kukuza uzalishaji mali katika nchi zetu ili tuweze kunufaika na fursa inayotolewa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali na sekta binafsi kila mmoja wetu peke yake na kwa Umoja wetu tunao wajibu wa kufanya. Sasa wakati umefika wa kuanza kutimiza wajibu wetu. Tusipofanya hivyo sijui kama kuna mtu wa kumnyooshea kidole cha lawama.

Mheshimiwa Spika, kwa jumla mambo yanakwenda vizuri katika kujenga Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya inazidi kujengeka na kuimarika siku hadi siku. Vikao vinafanyika kama ilivyopangwa na hata kuzidi. Tena hufanyika katika mazingira ya upendo na udugu. Tutajadiliana tutabishana lakini mwishowe tunaelewana. Sekretariat inazidi kuimarika kwa kuongezewa watumishi kila ilipojitokeza haja ya kufanya hivyo. Idara mpya, vitengo vipyta pamoja na Kamisheni ya Ziwa Victoria vimeundwa kuimarisha utendaji na utekelezaji wa majukumu. Bunge la Jumuiya limeendelea kutimiza vizuri wajibu wake wa msingi pamoja na kufanya kazi nzuri ya kuhamasisha wana Afrika Mashariki kuiunga mkono Jumuiya. Wanastahili pongozi zetu za dhati. Mahakama bado haijanza kazi ya usuluhishi wa migogoro iliyoundiwa kufanya. Naamini baada ya Umoja wa Forodha kuanza kutakuwa na shughuli za kutosha za kufanywa na Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 27 Machi, 2004, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipata pigo kubwa kwa kumpoteza aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ambaye pia alikuwa Naibu Waziri Mkuu wa Pili na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Uganda kutokana na kifo. Marehemu Wapakhabulo siyo tu alikuwa mwana diplomasia mahiri aliyesaidia kwa wakati muafaka kutatua migogoro, bali alikuwa mwana Afrika Mashariki wa kweli. Mke wake alikuwa Mtanzania na atakumbukwa kwa mchango wake muhimu katika hatua mbalimbali za kuanzishwa tena kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mungu aiweke roho ya Marehemu wetu huyo mahala pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, shughuli za uendelezaji wa Bonde la Mto Kagera zilisimama kuanzia mwaka 1994 baada ya matatizo ya kiusalama yaliyoikumba Rwanda. Tangu wakati huo juhudhi za kufufua shughuli na miradi ya Umoja huo hazijafanikiwa na matumaini ya baadae ni madogo. Kwa kutambua ukweli huo, Baraza la Mawaziri wa *KBO* lilipokutana Kigali, Rwanda mwezi Februari, 2004 kuangalia hatma ya *KBO*. Baraza la Mawaziri lilikubaliana kwa kauli moja kuuvunja *Kagera River Basin Organisation* na na kuzielekeza shughuli na miradi yote ya *KBO* kuwa chini ya *EAC* na *Nile Basin Initiative*. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mapendekezo hayo ya Mawaziri yamepata idhini ya Marais wa Nchi zetu wanachama katika kikao chao cha dharura kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia tarehe 7 Julai, 2004. Baada ya kufikia uamuzi huo Marais wetu wametiliana saini Mkataba wa kuvunja KBO. Katika mkataba huo pia kuna makubaliano ya kuteua Mfilisi atakayeshughulikia kugawana mali na madeni ya *KBO* mionganoni mwa nchi wanachama. Ni uamuzi mgumu lakini katika hali ya sasa ya *KBO* ni heri kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kushiriki katika mikutano ya Umoja wa nchi zinazopakana na Bahari Kuu ya Hindi ambayo madhumuni makubwa ya Jumuiya hii ni kukuza biashara na uwekezaji katika nchi wanachama. Mwezi Oktoba, 2003 Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya hii uliofanyika Colombo, ambapo Mawaziri walipitisha ripoti ya *High Level Task Force*, iliyoundwa kuangalia upya muundo wa Sekretariati na kupendekeza hatua mbalimbali za kuboresha utendaji kazi na ufanisi katika Sekretariati iliyoko Mauritius. Baadhi ya maeneo yanayofikiriwa kutiliwa mkazo ni uendelezaji wa sekta ya uvuvi, sayansi na teknolojia, nishati,

uboreshaji wa shughuli za bandari na usafiri wa bahari. Nchi hizi pia zina lengo la kuanzisha *Preferential Trade Area*, ambapo nchi itajiunga pale inapofikiri ni wakati muafaka. Tanzania itaendelea kufuatilia kwa karibu shughuli za *IOR-ARC* na kukuza ushirikiano na nchi wanachama kwani kuna fursa kubwa ya kunufaika pia.

Mheshimiwa Spika, uhusiano na ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine katika mabara yote duniani ni mzuri. Vivyo hivyo ushirikiano wa nchi yetu na mashirika ya Kimataifa ni mzuri. Ni dhamira ya Wizara yangu na Balozi zetu zote kuidumisha hali hiyo na hasa kuifanya iwe bora zaidi. Katika mikakati na mbinu muafaka za kujenga na kuimarisha uhusiano na ushirikiano na mataifa mengine duniani ambazo tumekuwa tunazitumia ni pamoja na kuwa na uhusiano wa Kibalozi na nchi mbali mbali, kufungua Balozi zetu nje, kuwa na Tume za Pamoja za Ushirikiano na ziara za viongozi. Katika baadhi ya nchi na maeneo tumekuwa tunateua Makonseli wa Heshima. Kwa kawaida tumekuwa tunateua watu wenyе sifa nzuri, wenyе kufahamika vizuri na kukubalika mahali hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa nia ya kuimarisha uhusiano na ushirikiano wetu na nchi jirani ya Malawi Rais wetu aliamua kufungua Ubalozi katika nchi hiyo. Ubalozi huo umekwisha funguliwa na kazi zinaendelea vizuri. Baada ya kufungua Ubalozi wa Malawi Tanzania sasa inazo Balozi 29. Katika Bajeti hii hatuna mpango wa kufungua Ubalozi mpya popote duniani. Hata hivyo, kufuatia ziara ya Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein nchini Oman na mazungumzo aliyofanya na viongozi wa nchi hiyo Oman sasa iko tayari kupandisha hadhi ya Ubalozi wao mdogo uliopo nchini na kuwa Ubalozi kamili. Aidha, wametuomba na sisi tufungue Ubalozi nchini Oman, na kuahidi kutoa kila msaada wa kufanikisha lengo hilo. Makamu wa Rais amelikubali kimsingi ombi na pendeleko hilo. Hivi sasa Wizara yangu, imeanza mashauriano ya ndani Wizarani na Serikalini kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, inafanya mashauri ya ndani kuhusu utekelezaji wake, ili itoe ushauri muafaka kwa Mheshimiwa Rais.

Aidha, Mheshimiwa Spika, Wakati wa Ziara yake huko Tawala za Kifalme za Kiarabu, Mheshimiwa Makamu wa Rais alikuwa na mazungumzo na Uongozi wa Serikali ya Muungano wa *UAE* na pia uongozi wa Serikali ya Dubai. Katika mazungumzo hayo, suala la kuimarisha fungamanisho zetu za kiuchumi na kidiplomasia lilizungumzwa, ambapo Serikali ya Muungano wa UAE ingefikiria kufungua Ubalozi kamili nchini Tanzania na Tanzania ingefikia kufungua Ubalozi mdogo mjini Dubai. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali mbili zimo katika hatua za mwisho za kukamilisha mapendekezo hayo. Baraza la Mawaziri la *UAE* limepitisha uamuzi wa kufungua Ubalozi kamili Tanzania na Serikali ya Tanzania imo katika hatu za mwisho kufungua Ubalozi mdogo mjini Dubai.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha uliopita, tulikusudia kufanya mikutano ya Tume za Pamoja za Ushirikiano na nchi za Afrika ya Kusini, Cuba Zimbabwe na Nigeria. Kwa sababu mbali mbali ikiwemo tatizo la fedha na wakati mwininge kuingiliana kwa mipango mbali mbali ya Viongozi wa pande zote mbili, iliwezekana kufanya mkutano wa Tume na Cuba tu mwezi Oktoba, 2003, Mjini Havana. Kikao hicho kilikuwa kizuri, cha kirafiki na cha mafanikio makubwa. Kiliboresha ushirikiano wa muda mrefu kati

yetu na Cuba na matokeo yake yameanza kuonekana. Katika sekta ya afya tayari madaktari kumi na mmoja kutoka Cuba wamewasili nchini na wameanza kazi. Wengine 59 watawasili wakati wowote mipango ya kuwasafirisha na kuwapokea itakapokamilika. Katika mwaka huu wa fedha tunakusudia kukamilisha viporo vya mwaka wa jana vya Afrika Kusini na Nigeria pamoja na kufanya vikao na Zimbabwe, Rwanda, DRC na Burundi.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi za Ulaya na Marekani sera yetu inaelekeza kuwa pamoja na kuimarisha uhusiano wa kisiasa, lengo letu kuu ni kupata kutoka katika nchi hizo, misaada zaidi ya maendeleo, misamaha ya madeni, masoko kwa bidhaa za nchi yetu, wawekezaji na watalii kuja kwa wingi nchini na teknolojia ya kisasa. Kadhalika tunataka kupata misaada ya kiufundi kwa maana ya kupatiwa nafasi nyingi za masomo kwa Watanzania na kupata wataalamu/mabingwa watakaokuja nchini kufanya kazi katika maeneo ambayo tuna upungufu. Katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita Wizara yangu na Balozi zetu kwa kushirikiana na wadau wengine katika Wizara na Idara za Serikali na jumuiya za wafanyakazi na za kijamii tumefanya jitihada kubwa za kutekeleza malengo hayo ya sera. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mafanikio kadhaa tumeweza kuyapata.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada ya maendeleo kumekuwepo na ongezeko la kutia moyo. Kwa jumla tumepata kutoka nchi za Ulaya na Marekani kiasi cha shilingi milioni 308,711 za misaada ya maendeleo ambayo ni nyongeza ukilinganisha na shilingi milioni 231,760 tulizopata mwaka uliopita. Kwa upande wa msamaha wa madeni mwaka huu tulisamehewa kiasi cha US\$ 84.6 Mil kutoka nchi za Bulgaria na Urusi. Aidha kupitia mpango wa *HIPC* tumeweza kusamehewa kiasi cha shilingi 82.1 bilioni katika mwaka huu wa fedha. Mazungumzo yanaendelea na nchi zingine zinazotudai ili kukamilisha upatikanaji wa misamaha ya madeni chini ya mpango wa *HIPC* na nchi moja moja. Juhudi zaidi zitaimarishwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwekezaji na biashara nafurahi kueleza kuwa wako watu na makampuni kadhaa yanayojiteza na kuonyesha nia ya kuja kuwekeza nchini na kufanya biashara na Tanzania. Idadi ya watu na makampuni yanayofika Balozini au kuwasiliana nasi Wizarani kutafuta habari za uwekezaji na biashara inaongezeka kila mwaka. Ujumbe wa wafanyabiashara kutembelea nchi yetu umekuwa unaongezeka. Mwaka jana tulipokea ujumbe wa aina hiyo toka Uingereza, anada, Italia, Ujeruman na Ufaransa. Upande wetu pia mwaka 2003 kwa kushirikiana na Ubalanzi wetu wa Roma Italia tuliandaa ziara ya wafanyabiashara 20 kutoka nchini kutembelea nchi za Italia, Ugiriki, Croatia, Uturuki na Slovenia. Kote huko walipokelewa vizuri na makubaliano kadhaa ya biashara na uwekezaji yalitiwa saini baina yao na wenzao wa nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kupata masoko kwa bidhaa zetu, fursa ipo tele kwa nchi za Ulaya na Marekani. Kwa Umoja wa Ulaya fursa imetolewa kupitia Mpango maalum wa upendeleo kwa nchi za Afrika kuuza bidhaa zao zote, isipokuwa silaha, bila ushuru wala ukomo wa kiasi cha kuuza. Vivyo hivyo, kwa Marekani kwa kupitia mpango maalum wa upendeleo uitwao *Africa Growth and Opportunities Act*

(*AGOA*), tunayo pia fursa ya namna hiyo. Nchi ya Canada nayo imeanzisha mpango wake unaofanana na mipango hiyo.

Bahati mbaya sana, Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania bado hatujazitumia vya kutosha fursa hizo na nyingine zitolewazo na China na Japan. Tunalo tatizo la kutokuwa na bidhaa za kutosha za kuuza katika masoko hayo. Hatuna budi kufanya kila tuwezalo kumaliza kasoro zetu hizo ili kunufaika ipasavyo. Fursa hizi ni za muda tu si za milele na muda hautusubiri sisi. Naomba kuitumia nafasi hii kutoa shukrani maalum kwa Serikali ya Marekani hususan Rais George W. Bush na Bunge la Marekani kwa uamuzi wake wa kuongeza muda wa mpango wa *AGOA* mpaka mwaka 2015. Ni misaada mkubwa na dalili ya upendo kwa Afrika. Kama nilivyosema awali kuwa hii ni changamoto kubwa kwetu kuitumia fursa hiyo kabla haijatoweka.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu na Serikali kwa jumla, inatambua umuhimu wa uhusiano na ushirikiano na nchi za Caribbean na Marekani ya Kusini kwa ujumla, uhusiano na mshikamano wetu wa kisiasi ni mkubwa. Uhusiano wetu huo umekuwa jambo muhimu sana kwani tumeutumia kwa mafanikio katika majukwaa ya Kimataifa kudai haki zetu za nchi zilizoko kwenye kundi la nchi zinazoendelea na zile maskini sana. Tutajitahidi kuuendeleza uhusiano huo wakati huo huo tutaaendelea kutafuta namna ya kushirikiana kiuchumi. Nafurahi, kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka huu wa fedha Rais wetu atafanya ziara ya kitaifa katika nchi za Cuba na Jamaica kwa nia ya kusisitiza umuhimu tunaouomba kwa uhusiano na ushirikiano na nchi za Caribbean na Marikani ya Kusini na Kati.

Mheshimiwa Spika, uhusiano wa Tanzania na nchi za Asia na Australasia ni mzuri na unaendelea kushamiri. Ni makusudio yetu kuuboresha zaidi kwani eneo hili la dunia lina umuhimu wa aina yake kwa nchi yetu. Nchi za Japan, China, Australia, India, Korea ya Kusini, Malaysia na Indonesia ni vyanzo muhimu vya misaada ya maendeleo na kiufundi kwa nchi yetu. Kadhalika, nchi nyingi za Asia ni muhimu sana kwa biashara na nchi yetu. Wafanyabiashara wetu wengi hupata bidhaa zao nyingi kutoka nchi za Asia hususan China, Japan, India, Vietnam, Thailand, Korea ya Kusini, Indonesia, Malaysia na Singapore. Nchi za Asia pia ni wanunuzi wakubwa wa mazao na bidhaa toka nchini mwetu. Pamoja na hayo, mataifa ya Asia yanajulikana duniani kwa kuwa na watalii wengi na wawekezaji wengi. Bahati mbaya wawekezaji vitega uchumi na watalii wao hawajatoa umuhimu stahiki kwa Tanzania, hivyo basi tunayo nia ya kuvutia waje nchini.

Mheshimiwa Spika, uhusiano wetu na Japan unazidi kustawi na nchi yetu imenafaika sana na misaada ya maendeleo kutoka nchi hiyo. Japan pia ni nchi ambayo tumekuwa tunasaidiana na kushirikiana kwa karibu katika majukwaa ya Kimataifa na kwa masuala ya kimataifa. Kwa nia ya kuimarisha uhusiano wetu Rais wetu Alishiriki katika Mkutano wa Tatu wa Tokyo kuhusu maendeleo ya Afrika (*TICAD III*) uliofanyika Tokyo tarehe 29 Septemba mpaka 1 Oktoba, 2003. Waziri wa Fedha Mhe. Basil P. Mramba alitembelea Japan tarehe 24 - 28, Februari, 2004 na mimi nilifuatia mara baada yake kunako 26 - 30 Mei, 2004. Muelekeo wetu kisera kwa Japan ni kuhimiza uwekezaji na utalii toka Japan kuja nchini. Kwa ajili hiyo, nilipokuwa Osaka Japan tulikubaliana na Viongozi wa Serikali, Jiji na wafanyabiashara kuwa watume ujumbe

wa biashara nchini kuangalia fursa za uwekezaji, biashara na utalii. Tunaendelea na mawasiliano kuhusu utekelezaji wa maelewano hayo.

Mheshimiwa Spika, uhusiano wetu na China ni wa aina yake. Ni uhusiano spesheli kabisa. Katika uhusiano huu nchi zetu mbili zimesaidiana kwa mengi na sisi tumenufaika sana kwa misaada ya maendeleo tuliyopata kutoka China na tunaendelea kunufaika. Tarehe 28 Mei mpaka 2 Juni, 2004 Rais wetu alitembelea China na kupata fursa ya kuonana na kuzungumza na Waziri Mkuu Hu Yia Bao na Rais Hu Jintao. Ilikuwa ziara fupi na yenye mafanikio mengi. Uhusiano wa kidugu ulisisitizwa kudumishwa. Ndoto ya miaka mingi ya Watanzania ya kuwa na kiwanja cha michezo cha kisasa hatimaye itatimia kufuatia Rais wa nchi hiyo kukubali maombi ya Rais wetu kutaka Wachina watusaidie. Kampeni yetu ya kutaka kuongeza watalii ilipata msukumo pale Rais wa China alipomwarifu Rais wetu kukariri uamuzi kwamba, Tanzania imeteuliwa kuwa moja ya nchi ya kutembelewa na watalii kutoka China. Kadhalika, kumekuwepo na ahadi kadhaa za ushirikiano katika maeneo mengine kama vile huduma ya afya, uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, China ni rafiki wa Afrika pia wa miaka mingi. Kwa ajili hiyo nchi hiyo imeanzisha China-Africa Forum ambalo ni jukwaa la kuzungumzia mipango ya ushirikiano na Afrika. Tarehe 15 na 16 Desemba, 2003 Mkutano wa *China-Africa Forum* ulifanyika Addis Ababa, Ethiopia. Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Frederick Sumaye aliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye mkutano huo ambao ulikuwa wa mafanikio makubwa. Mambo mengi ya manufaa kwa maendeleo ya nchi yetu na Afrika kwa jumla yalijitokeza. Mionganoni mwa hayo ni ahadi ya China kuendelea kutoa misaada ya maendeleo, kupunguza mzigo wa madeni, kuleta watalii na kukuza biashara kwa kutoa fursa ya kuingiza bidhaa katika soko la China kwa upendeleo.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tumezidi kuimarisha uhusiano wetu na Indonesia. Nilitembelea Indonesia tarehe 31 Machi mpaka tarehe 2 Aprili, 2004 baada ya kutembelea Japan. Tumekubaliana kuanzisha Tume ya Pamoja ya Ushirikiano ambayo tutaitumia kukuza na kuendeleza uhusiano wa nchi zetu. Niliitumia fursa hiyo kuishukuru Serikali ya Indonesia kwa msaada wao wa kiufundi wanaoipatia nchi yetu katika kuendeleza uzalishaji wa kilimo na kuwasihhi waendelee kutusaidia. Nchi hiyo imeeleza utayari wake wa kuendelea kushirikiana nasi katika eneo la kuongeza uzalishaji wa chakula. Kwa sasa, Indonesia inao wakufunzi wanaofundisha wakulima wadogo wadogo wa mpunga katika kijiji cha Mkindo, Wilayani Mvomero ambapo uzalishaji umeongezeka maradufu kutoka tani 3.8 hadi tani 6 kwa hekta.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madeni nchi za Asia zimetupa nafuu ya kuridhisha. Japan wametusamehe madeni yote, China wametusamehe deni la US \$ 37.7 milioni na India \$ 32.25 milioni. Naomba kuitumia nafasi hii kuzishukuru nchi hizi rafiki kwa uamuzi wao huo. Tunawasihi marafiki zetu wengine nao wafanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu litakavyokumbuka, katika kikao kilichopita, nilitaja mambo mbalimbali ambayo Wizara yangu inatarajia kufanya katika kipindi cha fedha cha mwaka 2003/2004. Mionganoni mwa mambo hayo, ilikuwa ni

kutengeneza mwongozo wa kazi na masharti na sifa za mtu kuwa Konseli wa Heshima wa Tanzania. Aidha, kazi nyingine ilikuwa ni kuratibu ziara za nje za Viongozi wa kitaifa na Viongozi wa nchi za nje walioitembelea Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi hizo zimetekelawa kwa ufanisi mkubwa. Tumefanikiwa kutoa rasimu ya Mwongozo ambayo inaorodhesha sifa zinazotakiwa kwa mtu anayetaka kuteuliwa kuwa Konseli wa Heshima wa Tanzania pamoja na hatua mbali mbali za uteuzi wa Konseli wa Heshima wa Tanzania tangu hatua ya kuanza kupokea maombi au kupendekeza mtu kushika nafasi ya Konseli wa Heshima hadi hatua ya mwisho ya uteuzi na ufunguzi rasmi wa Ofisi na kazi anayotarajiwa kuifanya Konseli huyo wa Heshima wa Tanzania katika sehemu atakayoteuliwa. Hatua inayofuatia ni kupata maoni ya adau wetu, kwa nia ya kuuboresha zaidi mwongozo huo.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa mwongozo huu mara ukikamilika na kuanza kutumika, utasidia katika kufanikisha azma yetu ya kuteua Makonseli wa Heshima wa kuwakilisha nchi yetu katika sehemu mbalimbali duniani. Hii itasidia kuendeleza na kuimarishe uhusiano na ushirikiano wa nchi yetu na nchi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa mashirika na asasi mbali mbali za Kimataifa kama vile Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola, Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote, Kundi la 77 na China, Tume ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini na mengineyo. Tanzania itaendelea kuwa mwanachama wa mashirika na asasi hizi muhimu kwani zinatoa nafasi muhimu ya kutetea na kuendeleza maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika ulioasisiwa rasmi Julai, 2002 huko Durban, Afrika Kusini umeendelea kuimari. Baada ya kukamilisha uteuzi wa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika Mhe. Alpha Konare na Makamishna wa Kamisheni mbali mbali Julai, 2003 mjini Maputo Mozambique Umoja wa Afrika umezidi kujimarishe kimuundo. Tarehe 18 Machi, 2004 Bunge la Afrika (*The Pan-African Parliament*) lilizinduliwa rasmi na Rais Joachim Chissano wa Msumbiji, wakati akiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Tanzania ilipata heshima maalum katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge hilo pale Mtanzania mwenzetu Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, alipochaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge hilo. Nachukua fursa hii kwa mara nyingine tena, kumpongeza Mheshimiwa Getrude Mongella kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika. Hii ni heshima kubwa sana kwa nchi yetu. Aidha, nawapongeza pia wabunge wenzetu, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Remedius Kissassi na Mheshimiwa Athuman Janguo kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge la Umoja wa Afrika. Kwa mara nyingine naomba nirudie ahadi yangu ya kuwapa kila aina ya msaada utakaofanikisha uwakilishi wao huu adhimu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Mei, 2004, Umoja wa Afrika ulizindua rasmi Baraza la Amani na Usalama la Afrika (*Peace and Security Council*). Hii ni hatua

muhimu sana kwa Afrika bara ambalo lina migogoro mingi. Baraza hili ni chombo muhimu katika kuzuia na kutatua migogoro katika Bara la Afrika. Inafurahisha na kutia moyo kuona kuwa ipo dhamira ya dhati mionganoni mwa viongozi wa Bara letu kushughulikia migogoro inayoisibu Afrika. Baraza la Amani na Usalama limeonesha manufaa yake kwa jinsi lilivyotoa uongozi katika kushughulikia mzozo wa Darfur na mgogoro wa Ivory Coast.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Tatu wa Wakuu wa nchi za Umoja wa Afrika ulifanyika Addis Ababa Ethiopia kuanzia tarehe 6 hadi 8 Julai, 2004. Mbali na kujadili masuala mengi muhimu kwa bara letu la Afrika kulikuwa na masuala yaliyokuwa na umuhimu wa kipekee kwa Tanzania. Kwanza kabisa, Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliwasilisha rasmi kwenye mkutano huo Ripoti ya Tume ya Utandawazi. Rais wetu alikuwa Mwenyekiti mwenza wa Tume hiyo pamoja na Rais Tarja Harlonnen wa Finland.

Mheshimiwa Spika, nafurahi pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya juhudzi za muda mrefu, mwaka huu Kiswahili kimezinduliwa rasmi kuwa mionganoni mwa lugha sita zinazotumiwa na Umoja wa Afrika. Lugha nyingine ni Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kihispania. Tukio hili limekifanya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza ya kiafrika kutumika katika umoja huo. Tanzania imekuwa mstari wa mbele kupendekeza matumizi ya Kiswahili na sasa katika kuhakikisha kwamba, Kiswahili kinatumika katika shughuli za *AU*. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wale wote waliolisenea na kulifanya kazi suala hili na hatimaye kulifanikisha. Natoa shukrani za pekee kwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika Mheshimiwa Alfa Omar Konare kwani msimamo wake thabiti ndiyo hatimaye umewezesha Kiswahili kitumike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo pia, Tanzania imependekezwa kwa kauli moja kugombea nafasi ya Afrika ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia 2005 hadi 2006. Nafasi hiyo inaachwa wazi na Angola inayomaliza muda wake mwishoni mwa mwaka huu. Nchi za Uganda, Sudan na Ethiopia zilizokuwa zikiwania nafasi hiyo zilijitoa kuipisha nchi yetu. Kupendekezwa kwa Tanzania kunatokana na imani kubwa waliiyonayo nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kwa Tanzania. Uchaguzi rasmi wa kuingia katika Baraza la Usalama utafanyika wakati wa mkutano ujao wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Tuna imani kwamba msimamo wa nchi za *AU* kupendekeza nchi yetu utatufanya tupate nafasi hiyo. Tanzania imejitokeza kuomba nafasi hii kwa sababu katika miaka miwili ijayo kutakuwa na kazi kubwa ya kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya mkutano wa Maziwa Makuu utakaofanyika hapa nchini. Pia kutakuwa na kazi ya kufuatilia utekelezaji wa mpango wa amani ya Burundi. Yote hayo ni mambo yaliyoamuliwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na ufuatiliaji wake hufanywa na Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, wakati wa kikao cha Umoja wa Afrika kilichopita, Tanzania imetia saini na hivyo kuijunga na *African Peer Review Mechanism (APRM)*. Huu ni utaratibu wa kutoa ahadi ya kuwa tayari kujenga mazingira ya Utawala Bora wa kiuchumi na kisiasa katika nchi wanachama wa

Umoja wa Afrika. Ni mionganini mwa vipengele muhimu vya NEPAD. Ni mpango unaotoa nafasi kwa nchi wanachama kukumbushana au hata kubanana wenyewe kwa wenyewe pale mmoja wao anapovunja misingi na maadili ya utawala bora. Baraza la Mawaziri lilishakubali la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ijiunge na APRM. Hivi sasa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji anaandaa utaratibu wa kuleta Bungeni mapendekezo ya kuridhia kujiunga kwetu huko.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inathamini sana uanachama wake katika Umoja wa mataifa na tutaendelea kuunga mkono. Tunafanya hivyo kutokana na kutambua umuhimu wa Umoja wa Mataifa kwa nchi yetu na kwa Mataifa yote duniani. Tanzania imenufaika sana na uanachama wake katika Umoja huo. Kupitia mashirika yake, nchi yetu imepata misaada mingi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kupitia shirika lake la Wakimbizi, Tanzania imeweza kusaidiwa katika kubeba mzigo mzito wa majirani zetu wanaozikimbia nchi zao kwa ajili ya vita. Tutaendelea kuwa wanachama waaminifu wa Umoja huo na kuutetea pale misingi ya kuanzishwa kwake inapokiukwa au kupuuzwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa ajili hiyo, Tanzania inaunga mkono jithada za Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Koffi Annan zenye lengo la kuleta mabadiliko ya kimuundo, kiutendaji na kimtazamo katika Umoja wa Mataifa. Mabadiliko hayo ni pamoja na kuwepo kwa uwezekano uwezekano wa kuongeza nafasi zaidi za wanachama wa kudumu na wa muda katika Baraza la Usalama (*Security Council*) la Umoja wa Mataifa. Mabadiliko haya yakikubaliwa yatazipa nafasi na sauti nchi masikini katika kufikia maamuzi yanayotuhusu sisi na ulimwengu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2003 Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliunda kamati maalum ya watu mashuhuri ya kutoa maoni na ya ushauri kuhusu mageuzi katika Umoja wa Mataifa. Bahati nzuri, Mtanzania mwenzetu, Dr. Salim Ahmed Salim, amekuwa mionganini wa Wajumbe wa Kamati hiyo. Kamati hiyo inatarajiwa kutoa taarifa yake katika kikao cha 59 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kitakachofanyika Septemba, 2004. Ni matumaini yetu kuwa mapendekezo yao yatatoa fursa ya kukamilisha kazi ya kufanya mageuzi katika Umoja wa Mataifa. Hususan katika mageuzi hayo sauti ya nchi maskini inaweza kusikika zaidi na kupata fursa ya kufanya maamuzi katika taasisi muhimu ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika linaloshughulikia Wakimbizi Duniani (*UNHCR*), limeendelea kutoa misaada ya kibinadamu kwa wakimbizi wasiopungua 451,230 ambao ni karibu na nusu ya wakimbizi wote waliopo Tanzania. Kati ya wakimbizi 451,230, wakimbizi 293,661 wanatoka Burundi, 152,219 wanatoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na 3,381 wanatoka Somalia. Maendeleo ya amani yanayoonekana katika siku za hivi karibuni katika ukanda wa Maziwa Makuu (*Great Lakes Region*), yameongeza matumaini ya wakimbizi wengi waliopo nchini kurudi makwao, hasa wale wa Burundi. Kwa wakimbizi wa kutoka Kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inaelekea kutahitajika muda zaidi kabla ya kuanza zoezi la namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali ya usalama kuwa ya kuridhisha nchini Burundi, wakimbizi wengi wameonyesha nia ya kurudi nchini kwao. Wengi wanafanya hivyo.

Tangu kuanza kwa zoezi la kuwarudisha wakimbizi Burundi kwa hiari yao mwezi Machi, 2002 mpaka katikati ya mwezi Mei, 2004, jumla ya wakimbizi 109,520 wamerudi kwao, ambao kati ya hao, 41,453 wamerudi kati ya Januari na Mei, 2004.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuzi wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la kupeleka kikosi cha kulinda amani nchini Burundi kuanzia tarehe 1 Juni, 2004, kwa kipindi cha miezi sita, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (*UNHCR*), limeanza mipango kamambe ya kuwarudisha wakimbizi wa Burundi kwa wingi (*Mass Repatriation*). Hata hivyo, tunasisitiza kwamba ingawa matumaini ya kuwarudisha kwa hiari wakimbizi wa Burundi yamepamba moto, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia wakimbizi lisipunguze misaada yake ya kibinadamu (*Humanitarian Assistance*), pamoja na ulinzi katika kambi zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, ingawa kumekuwepo na Serikali ya kitaifa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, mategemeo ya kuwarudisha wakimbizi wa Kongo bado ni finyu. Hii inatokana na ukweli kwamba, wakimbizi wengi wanatoka katika Mikoa ya Kivu ambako bado hali ya usalama siyo nzuri. Hata hivyo, wimbi la wakimbizi kutoka huko kuingia nchini limepungua. Mwaka 2003, wakimbizi 5,600 ndio walioingia Tanzania kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kati ya Januari mpaka katikati ya mwezi Mei, 2004, ni wakimbizi 57 tu waliokuwa wameingia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Madola ni moja ya mashirika ya Kimataifa ambayo tumeyapa umuhimu wa juu kutokana na manufaa yake kwa nchi yetu. Tunaahidi kuendelea kushiriki kwetu katika Jumuiya hii. Tanzania ishiriki kikamilifu katika kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola kilichofanyika Abuja, Nigeria, Desemba, 2003. Bahati mbaya sana kwa sababu zisizoweza kuepukika Jumuiya ya Madola ilipoteza mmoja wa wanachama wake mashuhuri baada ya Zimbabwe kuacha uanachama. Ni tukio lililosikitisha wengi kwani kama ushauri wa nchi za *SADC* ungesikilizwa hali hiyo isingefikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo Tanzania ni kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati Maalum ya Mawaziri ijulikanayo kama *Commonwealth Action Group on Harare Declaration* au *CMAG* kwa kifupi. Kamati ina wajibu wa kufuatilia masuala ya demokrasia na utawala bora katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati Maalum ya Mawaziri wa Jumuiya ya Madola imeshafanya kikao cha kwanza tangu kuteuliwa kwake. Kikao hicho kilifanyika tarehe 22 Mei, 2004 Mjini London, Uingereza, ambapo kwa kauli moja tulimchagua Mheshimiwa Ademiniji, Waziri wa Mambo ya Nje wa Nigeria kuwa Mwenyekiti. *CMAG* ilizungumzia masuala kadhaa na kufanya maamuzi muhimu. Iliamua kuirejeshea Pakistan haki yake ya kushiriki katika Mabaraza ya Jumuiya ya Madola kwa masharti kuwa ifikapo Desemba, 2004, Rais Pervez Musharaf, aache kuwa Mkuu wa Majeshi ya nchi hiyo wakati pia ni Rais na Amiri Jeshi Mkuu. Kwa kipindi hiki kilichosalia, Pakistan itaendelea kuwa chini ya uangalizi wa *CMAG* katika kufuatilia utekelezaji wa makubaliano hayo. Aidha, katika mkutano huo tuliamua kuiondoa Fiji kwenye ajenda ya *CMAG* baada ya kutimiza masharti ya kurejesha utawala wa kidemokrasia.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Ushirikiano wa nchi za Kusini (*South Centre*) kiliendelea kuratibu shughuli zake kama ilivyokuwa imepangwa katika kalenda yake ya mwaka. Wizara yangu ilishiriki kwa ukamilifu kwenye mkutano wa pamoja wa Kituo na Wawakilishi wa kudumu wa Umoja wa Mataifa wa nchi wanachama wa Kituo ulioko Geneva. Mkutano huu ulifanyika tarehe 14 Novemba, 2003 huko Marakesh, Morocco. Lengo kuu la mkutano lilikuwa kuangalia jinsi ya kuimarisha utekelezaji wa masuala muhimu ya kimaendeleo katika nyanja za biashara, uwekezaji, mazingira, teknolojia na misamaha ya madeni na ufanikishaji wa malengo makuu ya Milenia. Mkutano pia uliweza kuweka mkakati mpya wa ushirikiano kwa kutilia maanani kwamba uwezo wa kimaendeleo unatofautiana baina ya nchi moja hadi nyingine, lakini unategemeana. Tanzania ina historia ya aina yake na kituo hiki hivyo basi tutaendelea kutoa mchango wetu wa hali katika kufanikisha shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililieleza Bunge lako Tukufu kuhusu maendeleo ya kazi ya Tume ya Kimataifa kuhusu Masuala ya Kijamii katika Utandawazi, ambayo Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alikuwa Mwenyekiti-Mwenza wake, pamoja na Rais Tarja Halonen wa Finland. Tume imekamilisha ripoti yake iitwayo, 'Utandawazi wenyewe Haki: kutoa Fursa Kwa Wote', ambayo ilizinduliwa rasmi mjini Geneva na London mwezi Februari, 2004. Ripoti imepokelewa vizuri sana, na wadau wengi wametaka mapendekezo yake yaweke mikakati ya utekelezaji katika ngazi zote Kitaifa na Kimataifa. Ripoti hiyo pia ilizinduliwa Kitaifa Jijini Dar es Salaam mwezi Machi 2004. Miiongoni mwa waliokuwepo katika uzinduzi huo ni baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru sana kwa kuja.

Mheshimiwa Spika, ripoti hiyo imewasilishwa rasmi katika Baraza la Uongozi la Shirika la Kazi Duniani na hatimaye katika Mkutano Mkuu wa Shirika hilo MJINI Geneva mwezi Juni, 2004. Mikutano yote hiyo iliiipokea vizuri sana Ripoti hiyo na mchango wa Rais wetu ulisifiwa sana. Mwezi Julai, Rais Mkapa aliwasilisha Ripoti ya Tume kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kule Addis Ababa. Viongozi wa Bara la Afrika nao wameipongeza sana Ripoti ya tume na kuitisha Azimio la kutaka mapendekezo yake, hususan yale yanayoihusu Afrika, yaungwe mkono na nchi zote na yale yanaoihusu Afrika, yaungwe mkono na nchi zote na yawe msingi wa msimamo wa pamoja katika kuendeleza na kulinda maslahi ya Afrika katika dunia ya utandawazi. Aidha, Azimio hilo limeitaka jumuiya ya Kimataifa, ikiwemo Umoja wa Mataifa, kuyazingatia mapendekezo ya ripoti hiyo kama njia mojawapo ya kuimarisha mikakati ya ushirikiano na kuhimiza maendeleo ya nchi zote duniani. Azimio hilo pia limetaka Ripoti hiyo iwe mojawapo ya nyaraka za msingi za kujadiliwa katika Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa umoja wa Afrika kuhusu Ajira na Kuondoa Umaskini katika Bara letu unaotarajiwa kufanyika mjini Ouagadougou, tarehe 8 - 9 Septemba, 2004. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Ripoti hii, ambayo ni mojawapo ya mafanikio makubwa ya Rais wetu, na kielelezo cha upeo wake mkubwa, imekuwa na mvuto wa pekee mionganoni mwa Serikali, mashirika ya kimaendeleo na wanaharakati wa maendeleo. Ripoti inajenga hoja ya utandawazi unaonufaisha watu wote, na unaopunguza athari zake. Ripoti

inabainisha kuwa mapambano ya kunufaisha watu wengi zaidi lazima yaanzie ndani ya kila nchi. Hapa ndipo ilipo changamoto kubwa kwetu kama viongozi na Serikali. Hatuna budi kuungana kama Taifa na kuazimia kunufaika na utandawazi na kuzikabili athari zake. Elimu na afya ni maeneo ambayo yatahitaji kipaumbele. Nafurahi kwamba, Shirika la Kazi Duniani linafanya mpango wa kuanzisha mradi wa mfano unaoekeleza baadhi ya mapendekezo ya ripoti. Mradi huo wa mfano utakuwa kielelezo cha yale ambayo kila nchi inaweza kufanya yenyewe kukabiliana na athari za utandawazi. Katika Bara la Afrika, Tanzania na Burkina Faso ndizo nchi zilizopendekezwa kwa majaribio ya utekelezaji wa mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, pia ameombwa na Waziri Mkuu wa Uingereza, Mheshimiwa Tony Blair, kuwa mjumbe katika tume ya Afrika yenyе lengo la kuandaa hoja zitakazomsaidia Waziri Mkuu huyo kuyapa msukumo mpya masuala ya kusukuma maendeleo ya Afrika na kupunguza matatizo ya Bara la Afrika atakapochukua uongozi wa Kundi la Nchi Nane Tajiri Duniani (*G8*) na nchi yake kuwa Rais wa Umoja wa Ulaya mwakani. Wazo la Waziri Mkuu, Tony Blair ni la kuungwa mkono kwani linatoa nafasi kwa nchi hizo nane (*G8*) na zile za bara la Ulaya kuyatazama kwa undani matatizo ya Afrika na kuchangia katika kuyapatia ufumbuzi. Ni heshima pekee kwamba, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa mara nyingine ametambuliwa kama kiongozi mahiri wa kusaidia jamii ya Kimataifa kuyatatua matatizo ya kimaendeleo yanayotukabili.

Mheshimiwa Spika, Makamishna wengine wanaoiunda Tume hii kutoka Bara la Afrika ni pamoja na Mheshimiwa Meles Zenawi, Waziri Mkuu wa Ethiopia, Mheshimiwa K. Y. Amoako, Katibu wa Tume ya Uchumi ya Afrika ya Umoja wa Mataifa (*ECA*), Prof. Anna Tibaijuka, Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (*UN-HABITAT*), Mheshimiwa Trevor Manuel, Waziri wa Fedha wa Afrika Kusini na Mheshimiwa Tidjane Thiam wa *AVIVA PLC*, Ivory Coast. Hii ni heshima kubwa kwa Bara letu la Afrika. Tunategemea Tume itazaa matunda mema.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa niliteuliwa kuwa Mwenyekiti Mwenza, pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje wa Finland, Mheshimiwa Dr. Erkki Tuomioja kuongoza *Helsinki Process High Level Group on Globalization and Democracy*. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati hii inaendelea na shughuli zake vizuri. Mkutano wa kwanza wa *Helsinki Group* ulifanyika Mjini Helsinki, Finland, Januari, 2004. Mkutano wa pili wa *Helsinki Group* utafanyika Dar es Salaam, Agosti 29 - 31, 2004. Kamati hii inategemea kukamilisha kazi yake Septemba, 2005, ambapo itakabidhi ripoti yake rasmi kwa *Helsinki Conference 2005: Searching for Global Partnerships*, mkutano ambao ni wa wadau kutoka kila pembe ya dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Tume ya masuala ya kijamii na utandawazi kukamilisha kazi yake, Kamati ya *Helsinki Process*, imekubaliana na *ILO* kusaidia kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Masuala ya Kijamii na Utandawazi ya *ILO*. Kwa namna fulani basi the *Helsinki Process* inatoa fursa ya kufuatilia utekelezaji

wa mapendekezo ya Tume ya Harlonnen na Mkapa. Pia itatoa fursa ya kuyaangalia baadhi ya mambo ambayo Tume hiyo haikuweza kuyaangalia.

Mheshimiwa Spika, kazi ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa dhidi ya mabomu ya ardhini imekuwa ikiendelea vizuri na kwa mafanikio makubwa. Katika kipindi cha mwaka huu, utekelezaji umefanyika katika awamu nne. Zoezi la kwanza lilifanyika Msata, Bagamoyo ambapo kiasi cha mabomu 9,837 yaliharibiwa. Zoezi la pili lilifanyika huko huko Msata ambapo kiasi cha mabomu 5,489 yaliharibiwa. Zoezi la tatu lilifanyika Monduli ambapo kiasi cha mabomu 4,338 yaliharibiwa. Zoezi la mwisho limefanyika hivi majuzi tu kunako tarehe 29 Julai, 2004 huko Msange Tabora ambapo kiasi cha mabomu 3,177 yameharibiwa. Hivyo basi, jumla ya mabomu ambayo Tanzania imeyateketeza ni 22,841. Kwa hiyo, Tanzania meteketeza kwa ukamilifu wajibu wake kwa mujibu wa Mkataba wa Ottawa. Isitoshe tumekamilisha kazi hiyo miezi tisa kabla ya wakati wa kufanya kuonyesha kiasi gani ulivyokuwa nchi ya kuaminika. Naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Mkuu wa Majeshi Gen. George Waitara kwa kazi nzuri na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi kwa uongozi wake. Wameiletea nchi yetu heshima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu silaha ndogo ndogo, Tanzania kwa kushirikiana na nchi majirani, imekuwa mstari wa mbele katika jitihada za kudhibiti ueneaji wa silaha ndogo ndogo. Mwezi Aprili, 2004, Mjini Nairobi, nchi za Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika ambayo Tanzania ni mwanachama, zilisaini Itifaki ya kupinga utengenezaji haramu, usafirishaji silaha ndogo ndogo, sehemu za vipuri na risasi zake. Wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani amba ni waratibu wa shughuli hii wanajiandaa kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya kuridhia Itifaki hiyo. Ni matumaini yetu kwamba, Bunge lako Tukufu litaridhia itifaki hiyo wakati itakapowasilishwa. Tunawapongeza Inspeksa Jeneral Omari Mahita kwa kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi kudhibiti ueneaji wa silaha ndogo nchini. Kadhalika tunapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Omari Ramadhani Mapuri na viongozi wenzake Wizarani kwa uongozi wao mzuri.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Wizara ambao lifanyiwa marekebisho mwaka jana bado haujapata kibali kutoka mamlaka husika ili uanze kutekelezwa. Juhudi zinaendelea kufanyika ili uweze kukamilika sambamba na mpango wa kimkakati wa muda wa kati wa utekelezaji (*Medium Term Strategic Plan*). Kuanza kutumika kwa muundo mpya wa Wizara, kutasaidia sana kutekeleza Sera mpya ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha, kutohana na ufinyu wa bajeti, mkakati wa utekelezaji wa Diplomasia ya kiuchumi (*Strategies for Implementing Economic Diplomacy*) utaanza na Balozi chache. Baadaye zikipatikana fedha tutazihusisha Balozi zingine fikra yetu ya jumla ni kuchagua miji michache duniani kwa mzunguko wa mwaka au miaka ambapo tutafanya maonesho ya kuitangaza Tanzania kwa uwekezaji, biashara na utalii. Tunakusudia kushirikisha wadau mbalimbali katika utekelezaji wa azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa utekelezaji wa Sera yetu mpya ya Mambo ya Nje unahitaji pia watumishi wenyewe stadi za kisasa, ujuzi na wenyewe uzoefu katika taaluma zao. Hivi sasa Wizara inakabiliwa na uchache wa watumishi hao. Juhudi za kupunguza uhaba huo zimeanza vizuri na zinaendelea. Vyema. Kuanzia mwaka huu wa fedha wa 2004/2005 hadi mwaka 2006/2007 tunategemea kuajiri watumishi wengine 20 zaidi ili kuziba pengo lililopo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupata watumishi wa ziada kwa njia ya kuajiri au uhamisho, Wizara itawaendeleza watumishi waliopo hivi sasa kitaaluma ili waweze kuhimili mabadiliko ya kazi zao. Mafunzo yatahusisha wafanyakazi waliopo Makao Makuu na katika balozi zetu. Mafunzo yatakayotolewa yatakuwa *Institutional Demand Driven* na siyo kwa matakwa ya mtumishi mwenyewe. Kwa kuanzia, Wizara imeteua watumishi ambao mwaka huu wa fedha watapewa mafunzo maalum ya kazi katika Chuo chetu cha Diplomasia, Kurasini na wengine nchi za nje. Aidha, Wizara inatarajia kuwashikiza maafisa wake kwenye Wizara nyingine za kisekta ili kuwapa ujuzi na uzoefu wa masuala ya uendeshaji wa uchumi na biashara ndani ya nchi. Kadhalika tunakusudia kufanya mazungumzo na Wizara za Mambo ya Nje za baadhi ya nchi rafiki tuweze kuwashikiza baadhi ya maofisa wetu kwa muda ili wajifunze mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza ya zoezi la kurekebisha kanuni za Utumishi wa Mambo ya Nje (*Foreign Service Regulations*) imekamili. Sasa tunaendelea na hatua ya pili ya kufikisha mapendeleko ya kanuni hizo kwenye vyombo vyya mamlaka Serikalini ili yapate ridhaa ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo tutalitilia maanani mwaka huu ni ununuzi au ujenzi wa nyumba katika Balozi zetu. Kwa mwaka huu wa fedha, tunakusudia kukamilisha ununuzi wa Jengo la Ofisi ya Ubalozi wetu London. Mipango inafanywa pia ili kuandaa mikakati ya kuwa na majengo yetu ya ofisi jijini New York, Nairobi, New Delhi na Moscow. Katika kutekeleza mkakati huu, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha (HAZINA) na Wizara ya Ujenzi na taadis za fedha nchini. Nia yetu, kama nilivyokwisha sema huko awali ni hatimaye tuwe na majengo yetu wenyewe katika Balozi zetu zote.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kuimarika. Ujenzi umeendelea vizuri katika mwaka 2003/2004. Juhudi hizo tutaendeleza katika mwaka 2004/2005 kwa kushirikisha pia wahisani. Lengo letu ni kuibadili sura ya Chuo ili ifanane na hadhi yake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Chuo kitaendelea kuimarisha mpango na mkakati wake wa maendeleo ambao unategemewa kukiwezesha Chuo kuwa kituo bingwa cha ushauri (*Centre of Excellence*) kwa Serikali nanchi za kanda kwa masuala ya diplomasia, stratejia na ushirikiano wa Kimataifa. Ili kufikia lengo hilo, Chuo kimeanza kujizatiti kwa ajira mpya ili kujenga uwemo wa utafiti na uchambuzi. Ajira zimelemta katika kupata vijana wanaoendelezeka na wenyewe hamasa ya kujiendeleza. Pia watumishi wa Serikali wastaafu wenyewe uzoefu na taaluma maalum wameajiriwa. Lengo ni kutoa mafunzo ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu, kwa nia

ya kuifanya Sera yetu mpya ya mambo ya Nje itekelezeke kwa ufanisi kwa kuwaoa watumishi waliopo na wapya watakaoajiriwa au watakaohamishiwa Wizarani. Nyanja za taaluma na vitendea kazi vinaimarishwa.

Aidha, Chuo kina maabara nzuri ya lugha ya Kifaransa. Chuo kimeendelea kutoa mafunzo katika programu zake za kawaida. Mafunzo ya kuwaoa na kuwaandaa mabalozi na maafisa mbali mbali wanaopelekwa nje yameendelea kwa ufanisi mkubwa. Idara ya utafiti imeimarishwa na ni matumaini yetu kuwa Idara hiyo itaanza kutoa matunda hivi karibuni. Pamoja na kushirikiana na vyuo rafiki katika kutoa mafunzo ya menejimenti ya ulinzi na usalama, Chuo kimeshiriki katika utafiti wa Utawala Bora na usalama kusini mwa Afrika. Utafiti huo umekamilika. Matokeo atatolewa katika semina maalum, ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge watalikwa kushiriki.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali ya Ufaransa na Serikali ya Jamhuri ya Korea kwa misaada yao kwa Chuo. Naishukuru Bodi ya Magavana ya Chuo kwa kukipa Chuo mwelekeo na msukumo mpya. Aidha, napenda kutambua mchango wa pekee uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa maendeleo ya Chuo. Mara kadhaa Kamati imekuwa mstari wa mbele kuhoji na kutetea maslahi ya Chuo na pia kutoa mawazo ya kukipeleka Chuo mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (*AICC*), kimeendelea kufanya kazi vizuri na mchango wake kwa pato la taifa na hususan Manispaa ya Arusha ni bayana. Kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004, kituo kimeweza kuwa mwenyeji wa mikutano ya Kimataifa 77 na ya Kitaifa 41 ilioingiza nchini wageni 15,060. Matarajio ya kituo ni kuongeza idadi ya mikutano kwa mwaka ujao na mingi ijayo kwa kujitangaza zaidi na kutoa huduma bora zaidi. Kufanya hivyo kunalenga kufanikisha kauli mbiu ya kituo ambayo ni “*We bring the World to Tanzania*”. Ili kufikia lengo hilo kituo kinalifanya kazi wazo la uwezekano wa kuwa mmiliki mwenza wa hoteli ya kisasa ya kitalii itakayokidhi mahitaji ya wageni wa mikutano na watalii.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 1 Agosti, 2003, Kituo kilitimiza miaka ishirini na mitano tangu kuanzishwa kwake kufuatia kuvunjika kwa Jumuia ya Afrika Mashariki. Sherehe za kuhitimisha miaka hiyo ziliadhimishwa rasmi katika juma la kwanza la mwezi wa tisa mwaka wa 2003. Pamoja na matukio mengi ya kufana katika sherehe hizo, Bodi ya Wakurugenzi, uongozi na wafanyakazi waliamua kujenga mnara wa kumbukumbu kwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kitendo hicho kilikuwa muafaka kabisa kwani kuwepo kwa chuo hicho kunatokana na maamuzi aliyofanya Baba wa Taifa wakati akiwa Rais wa nchi yetu. Kwa mara nyingine tena napenda kuitumia nafasi hii kuipongeza *AICC* kwa kufanya hivyo wakati wa kuadhimisha miaka 25 ya Kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Kituo katika kipindi cha miaka mitano ijayo kuendelea kuboresha zaidi kumbi za mikutano, kukarabati nyumba zake ili zilete pato kubwa zaidi na kuiendeleza hospitali yake kwa kuweka vifaa muhimu na vya kisasa kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wageni wa mikutano, jumuiya ya kimataifa na Wananchi wote. Lengo la Kituo bado ni lile lile la kutaka kuwa Kituo bora zaidi cha mikutano

katika Ukanda wa Nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika. Kituo kimeendelea kuzingatia utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa muda mrefu wa Kituo kama ulivyopitishwa na Bodi ya Wakurugenzi. Mpango huo pia, umebainisha kwa ufasaha mbinu za kuhimili ushindani.

Mheshimiwa Spika, naomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mara nyingine tena kituo kimepata hati safi ya ukaguzi wa hesabu zake kwa kipindi kinachoishia Juni, 2004. Katika kipindi cha 2004/2005, kituo kimepanga kuingiza Shilingi 4,074,318,149/= kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali na kupata ziada ghafi ya shilingi 1,066,969,592.00= . Nawapongeza Wafanyakazi, Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Julai, 2004 Wizara yangu ilipokea barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Kamishna Adadi Rajab, iliyomtuhumu Bw. Ismail Turde, Afisa Ubalozi wa Saudi Arabia, kwa ubakaji wa mfanyakazi wake wa ndani. Kwa kutambua kuwa mtuhumiwa alikuwa Afisa wa Ubalozi mwenye kinga za kidiplomasia, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, alituomba tufanye utaratibu wa kumwondolea mtuhumiwa kinga ili hatua za kukamilisha uchunguzi wa tuhuma hizo na hatimaye kumshitaki zichukuliwe. Kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Ushirikiano wa Kidiplomasia (*Vienna Convention on Diplomatic Relations, 1961*), ambao Serikali yetu iliuridhia tarehe 5 Novemba, 1962, kifungu nambari 31, kinainyima Serikali iliyompokea mwanadiplomasia wa nchi nyingine, mamlaka ya kumshtaki mwanadiplomasia huyo katika Mahakama zake kwa kosa lolote la jinai kwa kumvisha kinga ya kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kunukuu sehemu tu ya kifungu hicho kama ifuatavyo: “*A Diplomatic agent shall enjoy immunity from the criminal jurisdiction of the receiving state ...*”

Aidha, kinga hiyo ya kutoshitakiwa kwa kosa la jinai inaweza tu kuondolewa iwapo Serikali iliyomtuma mwanadiplomasia huyo itakubali kwa ridhaa yake kufanya hivyo. Hii imeelezwa kwenye kifungu nambari 32 cha mkataba huo huo kama ifuatavyo, nanukuu: “*The immunity from jurisdiction of Diplomatic agents and of persons enjoying immunity... may be waived by the sending state. Waiver must always be express.*”

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa na maoni ya Kamishna Adadi Rajabu, tarehe 8 Julai, 2004, Wizara ilichukua hatua ya kuuandikia Ubalozi wa Saudi Arabia na kuomba waondoe kinga ya kidiplomasia ya afisa wao huyo ili aweze kuchunguzwa na kushitakiwa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Pamoja na kufanya hivyo hapa Dar es Salaam tuliwapa taarifa ubalozi wetu huko Riyadhi, Saud Arabia, kuhusu tukio hilo la aibu na kuwataka wasaidie kufuatilia maombi yetu hayo na kuendeleza shinikizo.

Mheshimiwa Spika, terehe 13 Julai, 2004, tulipokea jibu kutoka Ubalozi wa Saudi Arabia hapa nchini, ukitujulisha kuwa Serikali ya nchi yao imeshindwa kumwondolea

kinga ya kidiplomasia mtuhumiwa wetu (*it has not been possible to lift Mr. Ismail Turde's diplomatic immunity*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea msimamo wa Serikali ya Saudi Arabia wa kukataa kumwondolea kinga ya kibalozi mtuhumiwa, mnamo tarehe 14 Julai, 2004, wizara ilifanya mawasiliano ya ndani ya Serikali kwa maana ya Wizara na Idara za Serikali yetu na kupata ushauri wa kisheria na kuamua la kufanya. Hivyo basi tukafikia uamuzi wa kumfukuza nchini tarehe 15 Julai, 2004. Uamuzi huo ulifikishwa Ubalozi wa Saudi Arabia na tarehe 19 Julai, 2004 mtuhumiwa aliondoka nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifikia uamuzi huo kwa kutambua ya kwamba haiwezi kumshitaki mtuhumiwa chini ya sheria za nchi yetu. Hata hivyo, tuliiatka Serikali ya Saudi Arabia kumshughulikia kisheria mtuhumiwa pindi atakapofika huko kwao kwa kuzingatia kifungu namba 31(4), ambacho kinairuhusu Serikali ya kwao kumshitaki mwanadiplomasia huyo kwa kosa la jinai alilolitenda kwenye nchi ya uwakilishi. Nanukuu kifungu hicho: “*The immunity of a Diplomatic Agent from the jurisdiction of the receiving state does not exempt him from the jurisdiction of the sending state.*” Ubalozi wa Saudi Arabia ulituahidi kuwa, kwa vyovytote vile, afisa huyo atashitakiwa kwa kitendo cha aibu alichokifanya na hasa kwa vile nchini mwao kitendo hicho ni kisa kikubwa sana ambacho akipatikana na hatia hukumu yake ni kifo. Kwa taarifa tulizopipata hivi karibuni ni kwamba mtuhumiwa yuko katika ulinzi mkali wa vyombo vya dola ya Saudia, akisubiri hatma yake kwa mujibu wa sheria za nchi hiyo. Tumeuagiza Ubalozi wetu Riyadh uendelee kulifuatilia jambo hili kwa ukaribu na kutuletea taarifa zipasazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kudhihirika kwamba mtuhumiwa hataweza kushtakiwa na kwamba kitakachotokea ni kumtimua tu, katika mashauriano swali kubwa likawa hivi ndugu yetu apoteze haki zake zote hivi hivi tu? Kwa mujibu wa sheria zetu mbakaji atahukumiwa kifungo pamoja na kumlipa fidia muathiriwa. Wazo likajitokeza kuwa juhudzi zifanyike angalau huyu dada yetu alipwe fidia. Jambo hilo likafuatiliwa na katika mazungumzo yaliyofuatia kati ya Balozi wa Saudi na muathirika, muafaka ulifikasiwa kuhusu fidia. Ubalozi umeahidi kutekeleza na umeshafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hii ni mara ya kwanza kwa tukio kama hili la aibu na la kusikitisha kutokea hapa nchini tangu uhuru wetu. Baada ya tukio hilo kutokea kumekuwepo na maneno na hata hisia kuwa Serikali kwa ujumla na hasa Wizara yangu, haikushughulikia ipasavyo suala hili. Siwalaumu waliofikiria hivyo, pengine tulikuwa hatujatoa ufanuzi vya kutosha. Naamini baada ya maelezo haya, tumetambua jitihada zilizofanywa na Serikali za kumdhilita mtuhumiwa na jinsi tulivyokwama kisheria kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa na sheria yetu wenyewe Na. 5 ya 1986 (*Diplomatic and Consular Immunities and Privileges Act No. 5 of 1986*), uliotambua mkataba huo na kuufanya kuwa sehemu ya sheria zetu. Kwa hakika hatungeweza kufanya zaidi ya yale tulio yafanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali, mimi binafsi na wenzangu wote Wizarani tumefadhaishwa na kusikitishwa na kitendo kiovu na cha kikatili alichofanya yule Afisa

wa Ubalozi wa Saudia. Tumempa pole dada yetu kwa mateso aliyo yapata. Tunaungana naye kusikitika kwamba haikuwezekana kumfikisha mtuhumiwa wake katika mahakama zetu akashuhudia mwenyewe haki inavyotendeka. Ni matumaini yetu kuwa wenzetu wa Saudia watamwajibisha ipasavyo mtuhumiwa huyo. Sisi tutaendelea kufuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, miongoni mwa kazi muhimu zilizopangwa kufanywa na Wizara yangu katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 ni pamoja na:-

- Kukusanya maduhuli;
- Kutekeleza mpango kamambe wa utekelezaji wa Sera mpya ya Mambo ya Nje na majukumu mengine ya Wizara (*Ministerial Strategic Plan*);
- Kutangaza maeneo ya uwekezaji, utalii na kutafuta masoko ya bidhaa zetu nje;
- Kuratibu utekelezaji wa mkakati wa Sera ya Mambo ya Nje kwa kuhusisha sekta binafsi;
- Kuratibu Tume za Pamoja za Ushirikiano;
- Kushiriki katika utatuzi wa migogoro katika nchi jirani;
- Kushiriki katika mikutano muhimu ya Kimataifa;
- Kuratibu ziara za nje za Viongozi wa Kitaifa;
- Kuajiri watumishi wapya;
- Kuwapa mafunzo watumishi;
- Kuimarisha uwakilishi wetu nje ya nchi;
- Kurekebisha kanuni za utumishi wa mambo ya nje (*Foreign Service Regulations*);
- Kukamilisha taratibu zinazohusu uwakilishi wa heshima;
- Kukamilisha kijitabu cha Kiongozi cha Mabalozi (*Ambassador's Handbook*); na
- Kuendeleza mipango ya kununua majengo ya Balozini.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2004/2005, kama nilivyoleza katika hotuba hii, sasa naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 33,592,295,600.00/=. Kati ya fedha hizo, Sh.

1,153,084,000/= tunaziomba kwa ajili ya mishahara na Sh. 32,439,211,600.00/= kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofî*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. HADIJA K. KUSAGA (k.n.y. DR. MHE. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa kazi kwa mwaka uliopita wa 2003/2004 na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kamati napenda kutoa salamu za rambirambi kwako pamoja na familia na Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kumpoteza ndugu yetu na rafiki yetu, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, ambaye alikuwa mkakamavu, mcheshi na mshiriki mzuri sana wa kazi za Kamati yetu. Aidha, Kamati imesikitishwa kumpoteza Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho za Marehemu wetu hawa mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, aidha, tunapenda kuwapa pole Wabunge wenzetu wengine waliopata majonzi ya kufiwa na ndugu zao na wale waliopata maumivu kwa ajali akiwemo Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mbunge wa Kuteuliwa na Mjumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje, walioshiriki kutoa maoni na kuandaa taarifa hii kwa mwaka 2004 ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mbunge wa Sengerema, ambaye ndiye Mwenyekiti, Mheshimiwa Peter Kabisa, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ussi Yahya Haji, Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Bernard K. Membe, Mheshimiwa Adelastella Mkilindi, Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Khadija Ngozi, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhani, Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na mimi ninayesoma taarifa hii, Mheshimiwa Hadija Kasola Kusaga, bila kumsahau Katibu wa Kamati hii, Ndugu Lawrence Makigi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwengine wa hali yetu binadamu, Kamati inawapongeza Wabunge mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Danhi Makanga, ambaye amechaguliwa kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki, kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Tunamtakia kila la heri.

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza pia Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhamwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Mheshimiwa Dr. Pus Ng'wandu, Mbunge wa Maswa na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kuchaguliwa kwao kuongoza Taasisi za Kimataifa na Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti maalum, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mjumbe wa *SADC-PF*. Wote hawa tunawatachia mafanikio katika majukumu yao hayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati inawapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika, tuliochagua hapa Bungeni tarehe 6 Februari, 2004, akiwemo Mheshimiwa Balozi Gertrude Ibengwe Mongella, Mbunge wa Ukerewe, ambaye alichaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika hapo tarehe 18 Machi, 2004, Mjini Addis Ababa, Ethiopia.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine tuliochagua kuingia katika Bunge la Afrika ni Mheshimiwa Dr. William Shija, ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati hii na Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Remedi Kissassi, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Dr. Aman Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini. Tunawatachia wenzetu hawa uwakilishi mzuri kwa umoja wetu mpya wa Bara la Afrika, ambalo linahitaji amani, ushirikiano na msukumo mpya katika maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 96(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2003, jukumu kubwa la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje ni kuisimamia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika maendeleo ya sera na utekelezaji wa kazi zote za Wizara, ikiwa ni pamoja na kazi za Balozi zetu nje ya nchi na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2003/2004, Kamati inapenda kuweka kumbukumbu muhimu za matukio yenye sura ya Kimataifa kwa Taifa letu katika kipindi hicho, matukio ambayo Wajumbe wameyafatilia kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kwanza, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ambaye ndiye Msemaji Mkuu wa mashirikiano yetu Kimataifa, alikamilisha na kukabidhi taarifa ya hali na athari za utandawazi duniani, akiwa ameshirikiana na Rais wa Finland, Mheshimiwa Tarja Halonen. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, kwa kazi na mchango wake huko Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pili, katika kipindi hiki Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na hivi karibuni alizuru na kukagua kazi zinavyofanyika katika Ofisi za Makao Makuu ya *SADC* huko Gaborone, Botswana. Taifa letu, eneo la *SADC* na Afrika kwa jumla linategemewa kufaidika na uongozi wake huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, Rais wa Namibia Mheshimiwa Sam Nujoma, alizuru Tanzania na kulihutubia Bunge letu tarehe 12 Julai, 2004 Mjini Dodoma kama ishara ya kuishukuru Tanzania kwa mchango wake katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika, nchi ya Namibia ikiwa mojawapo. Ujio huo wa Rais wa Namibia, ulitukumbusha Watanzania kazi kubwa na ya heshima aliyoifanya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika jitihada zake za kuleta ukombozi, heshima na maendeleo katika Bara lote la Afrika.

Mheshimiwa Spika, nne, Mkutano wa Mabalozi wa Tanzania ulifanyika Ngorongoro, Arusha pamoja na mambo mengine ulizungumzia mikakati ya Sera mpya ya Mambo ya Nchi za Nje, ambayo ilizinduliwa rasmi katika mkutano huo. Kwa mikutano ijayo, tunaiomba Wizara ishirikishe Kamati hii kwa kina zaidi pamoja na Kamati nyingine za Bunge kupitia Wenyeviti wao. Hiyo ndio itakuwa hatua mojawapo muhimu ya kutekeleza diplomasia ya kiuchumi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, tano, kwa mara ya kwanza tunashuhudia Bara la Afrika kupitia Umoja wake (Umoja wa Afrika), likiamua kuchukua hatua za kiulinzi na usalama (*Security and Peace Measures*), kuhusiana na mgogoro katika eneo la Darfur nchini Sudan, unaokisiwa mpaka sasa kuangamiza Wasudani Weusi karibu milioni moja. Huu ni mwanzo mzuri kwa umoja huu.

Mheshimiwa Spika, sita, vilevile Kamati ilisikitishwa sana na taarifa ya kuwepo kitendo cha Afisa wa Ubalozi wa Saudi Arabia hapa nchini, kumbaka msichana wa Kitanzania na kisha Serikali kutokekemea wala kuchukua hatua thabiti kwa kitendo hicho cha kinyama. Kamati inamtaka Waziri aeleze kwa nini Wizara yake imelifumbia macho suala hilo zito la kudhalilisha wanawake na Taifa letu kwa jumla. (*Makofi*)

SPIKA: Ameshaeleza.

MHE. HADIJA K. KUSAGA (k.n.y. MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE): Mheshimiwa Spika, wakati tunaandika taarifa hii, Waziri alikuwa bado hajaieleza Kamati.

SPIKA: Sasa si ungeiruka.

MHE. HADIJA K. KUSAGA (k.n.y. MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE): Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa napenda kueleza kuhusu maelekezo ya Kamati kwa Wizara kwa mwaka 2003/2004. Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje ilikutana Dar es Salaam tarehe 3 na 4 Juni, 2004 kujadili utekelezaji wa kazi za Wizara ya Mambo ya

Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2003/2004 na kuchambua mpango wa Maendeleo wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa Fedha wa 2004/2005. Kamati katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 ilielekeza mambo yafuatayo yatekelezwe:-

- (a) Wizara itoe mgao wa fedha katika Ofisi za Balozi zetu kila baada ya miezi mitatu.
- (b) Wizara ipewe fedha za maendeleo.
- (c) Mkakati wa kutekeleza sera ya diplomasia ya kiuchumi utengenezwe utakaoainisha nafasi ya kila mdau.
- (d) Wizara ifungue Ofisi za Kibalozi au Konsuleti katika nchi zenye manufaa makubwa kiuchumi kwa mfano Brazil na kadhalika.
- (e) Wizara ikamilishe kutafuta Hati Miliki ya Chuo cha Diplomasia kilichopo Dar es Salaam Wilaya ya Temeke.
- (f) Serikali itangaze zaidi vivutio vya nchi kwa ajili ya kutafuta wawekezaji watakaoshirikiana na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara ilikuwa imetengewa jumla ya Sh. 32,179,101,000/= kwa matumizi yake kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004. Kati ya hizo, Sh. 3,262,680,000/= zilipatikana kutokana na maduhuli ya Wizara. Inafurahisha kuona kwamba, maelekezo mengi ya Kamati yalitekelezwa na mengine yanafutiliwa kwa karibu. Ni dhahiri kabisa kwamba, kuanza kutolewa fedha za matumizi kwa Balozi zetu kwa robo mwaka kumepunguza madeni yetu nje na kuweka mfumo mzuri wa matumizi, hatua ambayo ilitokana na mapendekezo ya Kamati hii.

Aidha, hoja yetu ya umuhimu wa kuweka taratibu za matumizi ya fedha, ununuzi wa vifaa na utunzaji wa mali ya Taifa huko nje imezaa matunda kwa kuwa Wizara sasa imeweka mwongozo maalum wa matumizi ya fedha na utunzaji wa mali za Serikali katika Balozi zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, aliiambia Kamati kwamba, kwa mwaka 2004/2005, Wizara imepanga kutekeleza mambo makuu yafuatayo:-

- Kukusanya madhuli zaidi, pamoja na utarabitu wa *visa* za vibandiko;
- Kutekeleza mpango kamambe wa Sera ya Mambo ya Nje na majukumu mengine ya Wizara (*Ministerial Strategic Plan*);
- Kuongeza juhudhi zaidi katika maeneo ya uwekezaji na utalii, pamoja na kushirikiana kikamilifu na Timu ya kuitangaza nchi yetu (*Brand Tanzania Team*);

- Kushiriki katika utatuzi wa migogoro ya nchi jirani;
- Kushiriki katika mikutano muhimu ya Kimataifa;
- Kuratibu ziara za nje za Viongozi wa Kitaifa;
- Kuajiri watumishi wapya;
- Kuwapa mafunzo watumishi wapya na wa zamani;
- Kuratibu utekelezaji wa mkakati wa sera ya mambo ya nje kwa kuhusisha sekta binafsi;
- Kurekebisha kanuni za uwakilishi nje (*Foreign Service Regulations*);
- Kukamilisha taratibu na kanuni za uwakilishi wa heshima (Konseleti Utunuku/Mtunuku);
- Kuainisha uwakilishi wetu nje ya nchi;
- Kukamilisha Kitabu cha Mwongozo wa Mabalozi (*Ambassador's Hand Book*); na
- Kununua jengo la Ubalozi wetu London.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mipango hiyo Wizara imeomba Sh. 33,592,295,600/= kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kuchambua kwa kina utekelezaji wa Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, Kamati inaitaka Wizara kutumia vizuri mtandao ilionao kwa Ofisi za Balozi zetu katika kuhamasisha wawekezaji, kuvutia mitaji, kutafuta masoko kwa bidhaa za Tanzania, teknolojia, pamoja na kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu. Wizara inahitaji kuitangaza Tanzania nje ya nchi kwa nguvu zote na Serikali kwa jumla lazima itumie fedha katika kutafuta fedha kwa masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuyafanyia kazi maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara, Kamati imependeleza mambo yafuatayo yatekelezwe:-

(a) Kwa kuwa mfumo wa uchumi umebadilika sana duniani, tofauti na mazoea ya Watanzania wengi, Serikali iendelee kufanya mafunzo katika ngazi mbalimbali za uongozi na Wananchi kwa ujumla yatakayolisaidia Taifa letu kuelewa kwa pamoja matakwa ya mfumo huu mpya wa utandawazi, kama tulivyofanya wakati tunaweka mikakati ya kutekeleza Dira na Mipango chini ya Azimio la Arusha.

(b) Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ipange na kuendesha semina na warsha kwa Waheshimiwa Wabunge wote, pamoja na makundi mengne husika, juu ya Sera mpya ya Mambo ya Nchi za Nje na Mikakati iliyopo katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi. Aidha, ni muhimu kutumia vyombo vyaa habari katika kuielimisha jamii juu ya suala hili.

(c) Kwa kuwa mfumo wa uchumi wa utandawazi duniani unawagusa sana vijana, Serikali iwasaidie katika kuelewa kupitia mashule, vyuo, vyuo vikuu, vyombo vyaa habari na taasisi nyingine ili watafute na kutumia fursa zinazotolewa katika kufanya kazi, kudumisha nidhamu, kujielimisha na kushirikiana katika kujenga maisha yao.

(d) Serikali iendelee na azma yake ya kufungua Balozi mpya na Konsuleti katika maeneo na nchi muhimu kama vile Brazil na kadhalika ili utekelezaji wa sera ya diplomasia ya kiuchumi itekelezeke kwa tija. Ufunguzi wa Balozi mpya na Konsuleti uende sambamba na uteuzi wa Mabalozi Wanawake, nitarudia tena sehemu hiyo. Ufunguzi wa Balozi mpya na Konsuleti uende sambamba na uteuzi wa Mabalozi Wanawake ambapo wapo wenye uwezo, ili kuimarisha ushirikiano wetu wa kijinsia. Aidha, Serikali ianze kuchukua hatua za kutenga fedha za maendeleo kwa Wizara hii zitakazotuwezesha kujenga Balozi zetu au kununua nyumba katika nchi mbalimbali. Kwa mfano, India, Malawi, Kenya na nchi zingine. (*Makofit*)

(e) Serikali na Wizara iangalie upya muundo wa Wizara hii ambaa una Idara kubwa kubwa, muundo uliojishindilia na kusababisha kukosa ufanisi. Idara kubwa kubwa zimesababisha mawasiliano kuwa magumu na maamuzi kukawia kufanywa, kitu ambacho hakitusaidii katika hali mpya ya Kimataifa. Kamati inapendekeza idara zilizopo zigawanywe, zipewe Wakurugenzi wapya na hasa wanawake na vifaa ili ziweze kuwashudumia Mabalozi wetu nje na Balozi za ndani vizuri zaidi.

(f) Serikali kwa ujumla wake iondoe kasoro inayolalamikiwa sana na Balozi zetu nje kwamba barua na aina nyingine za mawasiliano hazijibowi upesi au kutojibowi kabisa, vitendo ambavyo hupelekea watu wanaopenda kuwekeza au kutembelea nchi yetu kukata tamaa kabisa.

(g) Mheshimiwa Spika, pia Kamati ilijadili suala la Watanzania kudhalilishwa wanapokwenda kuomba *visa* hasa katika Balozi za Nchi za Magharibi. Baadhi ya Balozi za nchi hizo wamekuwa na taratibu ambazo ni za udhalilishaji na zenye kuleta ugumu mkubwa katika upatikanaji wa *visa*, hali ambayo inalalamikiwa sana na Watanzania. Tunaitaka Wizara ilichunguze suala hili, ishauriane na wahusika na kasoro hii iondolewe. (*Makofit*)

(h) Katika ngazi ya shughuli za Umoja wa Afrika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia pendekoz lake la kusimamia na kuhakikisha kwamba, Kiswahili kinaanza kutumika katika shughuli za mikutano yake. Kwa hatua hii muhimu, tunamshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika aliyepeita na Rais wa Mozambique kwa kuwa mwanzilishi wa utaratibu huu. Tanzania sasa ikitumie

Kiswahili kama bidhaa yake ya kuuza nje. Kwa hiyo fedha zitengwe ili kutekeleza mikakati ya kuuza bidhaa hii Afrika na duniani. (Makofi)

(i) Mheshimiwa Spika, katika suala la shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati inarudia kushauri kwamba, kwa kuwa Mawaziri wanaohusika na majukumu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, wameonekana kuwa na kazi nyingi sana na hivyo kushindwa kufuatilia vikao na utekelezaji wa mikakati ya Maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha 2001 - 2005 kwa ukaribu, Marais wetu wateue Mawaziri watakaohusika na Jumuiya ya Afrika Mashariki tu, kama ambavyo Rais wa Kenya sasa amefanya.

(j) Aidha, Kamati inashauri kwamba, baada ya kutiwa sahihi Mkataba wa Umoja wa Ushuru wa Forodha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Agreement for the Establishment of East African Customs Union*), Bunge lipewe taarifa ya kina na lijadili kikamilifu kabla ya kufikiwa hatua ya Bunge kuridhia itifaki yake. Vilevile Kamati inazishauri Serikali zetu tatu za Jumuiya kupata kwanza uzoefu wa ushirikiano kwa nchi tatu kabla ya kuzikaribisha nchi za Rwanda na Burundi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa za utendaji wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati inapendekeza kwa Bunge lako Tukufu kwamba, taarifa hizo ziwe zinawasilishwa mara mbili kwa mwaka kwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje na kufikisha Bungeni mara moja kwa mwaka ili kujadiliwa na Bunge.

Kwa hiyo, Kiambatanisho cha IV cha Kanuni za Bunge kifungu 5(2), kibadilishwe ili kiweze kuruhusu Bunge kujadili kikamilifu taarifa ya shughuli za Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kanda ya Tanzania kila itakapowasilishwa Bungeni na Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati imekuwa ikijadili suala la matumizi ya maji ya Bonde la Mto Nile na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuweka wazi suala la ushirikiano katika kutumia rasilimali zilizomo katika bonde hilo. Kamati inaipongeza sana Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa hatua ambazo imeanza kuchukua kwa lengo la kuleta usawa na haki katika matumizi ya maji ya Ziwa Victoria. Kamati inashauri kuwa juhudhi zilizopo katika kutekeleza programu ya Maendeleo ya Ziwa Victoria ziendelee, maamuzi yafanywe na Wananchi waelimishwe juu ya matumizi ya Ziwa hilo ili wajikomboe na umaskini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ushauri na mapendekezo hayo, Kamati inasisitiza kwamba, ili kutekeleza vizuri sera yetu mpya ya diplomasia ya kiuchumi, Wizara na Serikali kwa ujumla, lazima ikubali kushirikisha wadau mbalimbali, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, wafanyabiashara na wataalam. Kutoshirikisha makundi mbalimbali nchini kutaendelea kudumaza sekta nyingi na kulikosesha Taifa mapato muhimu katika uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imeomba Sh.33,592,295,000/= kwa ajili ya matumizi yake kwa mwaka wa Fedha 2004/2005, fedha hizo zikiwa pamoja na maduhuli ya Sh.3,262,680,640/=,

Kamati imeyakubali maombi haya na sasa inaliomba Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha maombi ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Phillemon Luhanjo na wataalam wa Wizara, kwa ushirikiano mzuri waliouonyesha kwa Kamati pale Kamati ilipohitaji maelezo na ufanuzi wa shughuli za Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi wenu makini katika kuliendesha Bunge letu Tukufu. Pia nawashukuru sana Wenyeviti wenzangu wa Kamati za Bunge, pamoja na Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge, kwa ushauri wao mbalimbali wa kazi za Kamati yangu. (*Makofi*)

Vilevile namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka M. Mussa, Katibu wa Kamati Ndugu Lawrence Makigi na wasaidizi wake, Ndugu Brown Gideon, Ndugu Kelvin Njunwa na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kazi zao nzuri za kufanikisha taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, Kamati inaunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA - MSEAMJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Nami niungane na wenzangu katika kutoa pole kwa wafawa wa aliyekuwa ndugu yetu, Marehemu Mheshimiwa Yeteh Mwalyego na pia Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Aidha, natoa mkono wa pole kwa Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mbunge wa Pandani, kwa kufiwa na baba yake mzazi hivi juzi.

Pia napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Naibu wake kwa mashirikiano na maelekezo mazuri sana walionipa katika maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa hawa kama walivyoahidi Bungeni hapa katika Bajeti iliyopita kuwa milango ya Ofisi zao itakuwa wazi kwa ajili yangu, ni kweli kabisa wao na watendaji wao, wamekuwa wakinisaidia katika kazi. Wamenishauri vizuri na wamenishirikisha sana katika shughuli zote walizoona zinanihusu. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania tuna kila sababu ya kukienzi Kiswahili, kwani ndiyo lugha inayochangia kwa kiasi kikubwa kujenga umoja wetu, leo hata Mmasai ana

uwezo wa kuzungumza na watu wa Micheweni Pemba. Hii ni Hazina kubwa, lakini wataalam wanasema kwenye miti hakuna wajenzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, leo ndugu zetu wa Kenya wana wakufunzi wengi zaidi wa Kiswahili duniani ukilinganisha kuliko sisi pamoja na kwamba hakitumiki sana Kiswahili katika nchi yao, kiswahili wao kimeweza kuwaongezea mapato kwa kuweza kufundisha katika Mataifa mengine. Hivyo, tunaishauri Wizara iongeze juhudi katika kunyanya hadhi ya Kiswahili kwenye mawasiliano ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imefanya juhudi kubwa katika kunyanya hadhi ya Kiswahili katika mawasiliano ya Kimataifa, kwa sasa hatua ya kutumika Kiswahili katika Umoja wa Afrika ni hatua moja mbele. Hata hivyo, bado Taifa letu linapaswa kuongeza juhudi katika kuandaa tafsiri za misamati mbalimbali kama ya kisayansi, kiuchumi, kisiasa na kadhalika, ili kuongeza upana wa matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukajiuliza je, tumeandaa walimu wangapi kwa sasa wenyewe uwezo ambao wanaweza kutumiwa na nchi nyingine kufundisha katika ngazi za msingi na sekondari, ni chombo gani kipo, chenye jukumu la kukikuza, kukisambaza na hata kukipigia debe Kiswahili kama lugha ya kutumika Kimataifa ukiondoa BAKITA na TUKI pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam?

Aidha, tujiulize sisi wenye hapa ndani tunakitumiae Kiswahili katika shughuli rasmi kama mikutano ya Kimataifa inayofanyika. Je, tuna Wakalimani wangapi wenyewe uwezo kutafsiri Kiswahili katika lugha nyingine? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Kiingereza kinaleweka kwingi duniani lakini ili lugha yetu ipate hadhi inayofaa lazima viongozi wetu wakubwa wakitumie waziwazi kila inapobidi. Hivi hatusikii wenzetu wanavyotumia lugha zao kama Kiarabu, Kifaransa, Kichina, Kirusi, Kijerumani na kadhalika bila ya kuona haya! Tusipojiamini na kuchukua hatua za makusudi wenzetu watachukua nafasi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha na wakati fulani hata kutia mashaka kuona wapo watu wenyewe nyadhifa kubwa kabisa, katika nchi yetu wanaokwamisha maendeleo ya Kiswahili kwa makusudi tu. Kiongozi anayeaminikutoka katika damu yake kwamba Kiswahili hakiwezi kutumika kufundishia Fizikia, Kemia na Hisabati katika Kidato cha Kwanza ni wazi hawezu kuwa Balozi wa kukikuza Kiswahili. Hivi iliwezekanaje kufundisha masomo hayo kwa lugha nyingine?

Mheshimiwa Spika, ni ajabu pia kuona wanaokibeza na kukidhalilisha Kiswahili wapo pia ambao huenda kwa Wananchi au wanawazia kwenda kwa Wananchi kuomba kura, lakini wakiwa kwenye kampeni kamwe hawahutubii kwa Kiingereza! Kiswahili kwao wao kinakuwa “Lulu” kwenye kuomba kura kwa Wananchi na wakishapata madaraka ya kisiasa wanaanza kutumia nafasi zao kukinyanya Kiswahili! Umoja wa Afrika ungeweza kujengwa kwa urahisi kama tungeweza sisi wenye hapa Watanzania kukazania kukiimarisha Kiswahili. Waziri atueleze kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, amefikia wapi katika kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya Afrika?

Mheshimiwa Spika, sura halisi ya Muungano wetu katika ngazi za Kimataifa inapimwa kwa mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwakilishi wetu kwa pande zote mbili asilia za Muungano huu. Mimi mpaka sasa sijaelewa katika ngazi ya Ubalozi, ni Mabaloz wangapi wa Tanzania nje wametokea Zanzibar kwa mfano, ni watumishi wangapi katika ofisi zetu za Ubalozi na hata katika Wizara yenyewe na Idara zake wametokea Zanzibar? Ni vizuri Mheshimiwa Waziri, akatuelimisha juu ya haya.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujafanya mabadiliko ya Katiba ya Kumi na Moja ambayo hadi leo yananung'unikiwa kwa kiwango kikubwa, ukiangalia katika uongozi wa juu, uwakilishi ulikuwa unaridhisha sana na ndiyo hata muundo wa Tume ya pamoja ya fedha umezingatia hali hiyo.

Mheshimiwa Spika pale tunapozungumzia uwiano katika utumishi wa Muungano isionekane hata kidogo kana kwamba, tunadai jambo nje ya Katiba, maana kimsingi ukishakubali kuwa kuna Muungano, basi lazima kuwe na uwiano na ndiyo maana hata katika idadi ya Wabunge kuna uwiano pamoja na udogo wa Zanzibar katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue nafasi hii kuwaomba wale Wazanzibari wenzetu, wenyewe uwezo, wajitahidi kujitokeza katika kugombea nafasi mbalimbali za uajiri ndani ya Wizara za Muungano pale zinapotangazwa. Wizara hizo nazo ziangalie uwiano ili kupunguza manung'uniko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu bado haijaamua kuwekeza katika huduma za Kimataifa ambazo zinaweza kuchangia uthumi. Hivi *AICC* ya Arusha tu ndiyo suluhisho pekee la nchi yetu katika kuandaa mikutano ya Kimataifa?

Mheshimiwa Spika, leo tuna Rais wa Bunge la Afrika, tuijilize basi, kama wenzetu wataamua wakutanie Tanzania tutawaweka wapi, tutawalaza wapi na tutawaunganisha vipi na ulimwengu huu wa utandawazi wa sayansi na teknolojia? Yote haya ni mambo ambayo Wizara hii na Serikali kwa jumla, inabidi kuyazingatia sana au tutawapeleka kule *Diamond Jubilee* tu?

Mheshimiwa Spika, limekuwa ni jambo la faraja kwa Watanzania wote kuhusu uchaguzi na uteuzi waliouopata wenzao kuwa Rais wa Bunge la Afrika na Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Kambi ya Upinzani, inashauri sifa hizo ziwasaidie Watanzania, kitu cha kuwasaidia ni Wizara hii kwa kushirikiana na Viongozi hao kufungua ofisi zao hapa Tanzania ili kuongeza ajira kwa Watanzania wenzetu. Aidha, kushawishi mikutano iwe inafanyika Tanzania kitu kitakachoongeza utangazaji wa nchi yetu kibiashara, utalii na wasipeleke ofisi zao katika nchi za watu na kuwasahau Watanzania, sifa bila ya faida ni kazi bure!

Nampungeza sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Jumuiya ya *SADC*, kwa kuweza kufanya mkutano Tanzania kule Bagamoyo na kuweka Sekretarieti yake hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ili kunyanyua uchumi wa Bara la Afrika na kwa kuwa Tanzania inatumika kama mdomo wa kunyanyulia sauti za wanyonge Barani Afrika, umefika wakati sasa wa Wizara ya Mambo ya Nje kuanzisha ushawishi wa Kikanda katika kuunda umoja wa uzalishaji hasa kwa zile nchi zinazotoa madini ya aina moja, kama vile dhahabu, almasi na kadhalika. Hali hii itawezesha nchi hizi kushiriki vizuri katika *NEPAD*. Kama alivyoshauri Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Wizara ya Madini na Nishati kuhusu kitengo cha kuchambua na kuuza almasi ya Tanzania, nanukuu: “*TANSORT* iwe *Executive Agency* ili ifanye kazi ya kibiashara na ikiwezekana iweze kutoa huduma hiyo kwa nchi nyingine zinazozalisha almasi. Aidha, tunaishauri Serikali izungumze na nchi za Afrika zinazozalisha almasi ili tuunde umoja wetu chini ya mpango wa *NEPAD* kama *OPEC* ili tuweze kulidhibiti soko na uzalishaji wa almasi”.

Mheshimiwa Spika, hii ndio Wizara muafaka katika kuhakikisha yaliyosemwa hapo juu yanafanyiwa kazi kwa manufaa ya Nchi yetu na Wananchi wake. Namnkuu Rais Sam Nujoma wa Namibia alipokuwa akifungua kiwanda cha kutengeneza vito vyatya almasi alisema: “*To our brothers and sisters of neighbouring states, Angola, Botswana, South Africa. I hope this gives you inspiration to try to imitate what we have here*”.

Mheshimiwa Spika, kama Namibia wameweza kuanzisha kiwanda kinachowenza kujiendesha cha kukata na kutengeneza vito vyatya almasi zao wenye kwa nini sisi tushindwe? Kwa hiyo basi, umefika wakati kwa dhana hii kutekelezwa kwa vitendo na Wizara ya Mambo ya Nje kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini. Hili linawezekana na litasaidia sana kudhibiti na kupunguza uporaji wa rasilimali zetu, kupanua soko la ndani na kuimarisha soko la kimikoa (*Regional Market*). Nchi zinazotoa mafuta zina umoja wao pia upo mshikamano wa wazalishaji wakubwa wa kahawa duniani. Hivi kuna tatizo gani kwenye sekta hii ya Madini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuibuka kwa utandawazi ambako kumechochewa zaidi na kuimari kwa ubepari wa Kimataifa na hasa baada ya kwisha kwa vita baridi, kunalazimisha nchi changa, kama Tanzania yetu kujipanga upya katika suala zima la sera ya mambo ya nchi za nje. Uhai wa kiuchumi, kisiasa na kiulinzi, unategemea sana nguvu ya Tanzania na nafasi iliyonayo katika uhusiano wa Kimataifa. Wimbi la utandawazi linabainisha kuwa Mataifa egemezi na tegemezi kwa wakubwa wa dunia kama nchi yetu kuishi kwa kupokea mwelekeo unaodaiwa kuwa ndiyo sahihi kiuchumi, kibiashara, kisiasa na hata kijeshi.

Mheshimiwa Spika, utandawazi ambao kimsingi ni hatua au awamu ya kisiasa zaidi katika maendeleo ya ukoloni mamboleo, unalenga katika kumaliza kabisa kidogo kilichokuwa kimebakia katika uwezo mdogo katika kujiamulia mambo (*Self Determination*) kama Taifa. Uwezo wa kuendesha mambo yetu wenye na kujifanyia maamuzi muhimu kama Taifa huru (*Sovereignty*), sasa unazikwa kabisa na jambo hili linaloitwa utandawazi. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, ili kulipa heshima Taifa letu, Serikali ijitahidi kuwashirikisha Wabunge katika mambo ambayo tukiyakubali yasiyumbishe nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuimbika na kurembeka vizuri sana, dhana nzima ya diplomasia ya kiuchumi (*Economic Diplomacy*), inahitaji kuchukuliwa kwa umakini wa hali ya juu sana. Ikitibebwa kimsobemsobe dhana hiyo nzima inayo nafasi kubwa ya kuongeza umaskini wa Watanzania badala ya kuupunguza. Lengo kubwa la diplomasia ya kiuchumi ni kuchochea upatikanaji wa wawekezaji wa Kimataifa kuja kuwekeza Tanzania na kutafuta masoko nje ya nchi kwa ajili ya bidhaa za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu ushauri uliotolewa na Msemaji wa Kambi yetu kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utakaokuwa wajibu wa watu tunaowatuma kutuwakilisha nje ya nchi yeye alisema: “Kazi za Balozi zetu kwa kiasi kikubwa ziwe ni pamoja na kufanya *marketing* ya bidhaa zetu. Balozi atakayefaulu katika hili apewe tuzo na kupongezwa. Kama Balozi atashindwa kufanya kazi ya kuwaunganisha wafanyabiashara wa Tanzania ili watumie soko la nchi aliyopo, basi hiyo ni dhahiri kuwa atakuwa ameshindwa kuiwakilisha vizuri Tanzania nchi za nje na ni vyema akarejeshwa nyumbani haraka”.

Ni matumaini yangu kabisa kuwa ushauri huo utazingatiwa kwa makini kwani Wizara hii ndio inayowajibika kutekeleza hayo yote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kinachogomba hapa ni uwezo wa kisiasa na kiutawala wa Taifa maskini kama Tanzania kuyadhibiti makampuni makubwa ya kibepari ya Kimataifa (*Multinational Corporations*), ambayo ndiyo wawekezaji wakuu. Kinachojitokeza katika sekta ya madini nchini Tanzania ni kielelezo tosha cha kuonyesha namna Serikali isivyo na ubavu wa angalau kuwakemea wanaocheza rafu katika sekta hiyo. Michezo michafu katika zoezi la ubinafsishaji ni kielelezo kingine cha namna Serikali inavyozidiwa kete na hao wanaoitwa kuwa ni wawekezaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, siasa za soko huria ambalo huwa linayo nafasi kubwa ya kuwa soko holela, zinahimiza ujenzi wa uchumi unaojielekeza kukidhi matakwa ya nje ya Tanzania kuliko ndani ya Tanzania. Uuzaji wa mazao ghafî au nusu ghafî huko nje badala ya bidhaa zilizokamilika, unapunguza sana uwezo wa nchi yetu kujipenyeza katika soko lenye ushindani mkubwa, hasa Ulaya Magharibi, Marekani na kadhalika. Kuimarisha uwezo wa ndani ya Taifa wa kiuchumi na hasa katika eneo la uzalishaji ni muhimu sana kwa kujenga uwezo wa kuuza bidhaa nje na kwa faida.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ambayo ilikuwa ngangari katika miaka fulani ya sitini, miaka yote ya sabini, hadi karibu katikati ya miaka ya themanini, katika uimara wa sera yake ya mambo ya nchi za nje, chini ya uongozi imara wa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, sasa iko hoi kiuchumi na hata kisiasa na mfano mzuri wa msimamo ulionyeshwa na Rais Mstaafu wa Afrika ya Kusini, Mzee Mandela.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi sasa nchi yetu tumekuwa waoga hata pale tunapokataa hatuwezi kusema hadharani yaani tunachukua *low profile*, jambo hili halidhihirishi uwazi wa siasa yetu ya mambo ya nje na hivyo kupoteza kwa kiasi fulani

ukinara wetu. Tanzania imepoteza kabisa uwezo wake wa kushawishi mielekeo ya mambo hata katika Afrika Mashariki tu ukiondoa maeneo mengine ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika ya Afrika Mashariki, inazidi kutengemaa na yawezekana kabisa ikafika siku ya kutumia sarafu moja. Ili kukwepa matatizo yanayoifanya Uingereza iendelee kukwepa kutumia sarafu ya *Euro* katika Umoja wa Ulaya na hasa kwa kuhofia kuburuzwa kiuchumi na Mataifa yenyе nguvu kubwa za kiuchumi kama Ujerumani, ni lazima Tanzania ijipange kiuhakika.

Mheshimiwa Spika, utulivu wa kisiasa katika Kenya kwa sasa, unaelekea kuirejeshea Kenya nafasi yake ya kuongoza uchumi katika Afrika Mashariki. Bado Tanzania inaonekana kuwa namba tatu kiuchumi nyuma ya Kenya na Uganda. Ni lazima Tanzania ijenge sasa mazingira ya kuishi ndani ya Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki kama Taifa lenye misili imara ya kiuchumi na siyo Taifa goigoi lililo hoi kiuchumi, bila ya kujipanga vizuri kiuchumi, Nairobi itaendelea kuwa kiini (*core*) na Tanzania itaendelea kujibanza katika pembe ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, Serikali itafute muda wa kuwaelimisha Wabunge angalau juu ya zile kodi zitakazoanza za *East African Community*. Tunashukuru tumepewa makablasha leo asubuhi juu ya jambo hilo, lakini ni vizuri tukaelimishwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa wa kuipa Zanzibar nafasi kubwa zaidi na uhuru mkubwa zaidi ili ishiriki zaidi katika mahusiano ya Kimataifa pia ushirikiano wa Kimataifa. Kutokana na mkao wake kijiografia na pia historia yake na utamaduni wake, Zanzibar inaweza kubadilika sana kiuchumi na hasa kwa kutumia utalii na bandari zake, ikapata kwa haraka ufanisi ambao Mataifa kama Mauritius, Seychelles, Macao, Bahamas na kahdalika, yamepata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uhuru wa Zanzibar katika ushiriki wake kwenye siasa za Kimataifa na ushirikiano wa Kimataifa, usiishie kwenye kujiunga na Shirika la Chama cha Mpira la Africa tu (*CAF*), bali ujipambanue katika kukuza nafasi ya maendeleo ya kiuchumi ya Zanzibar, hasa kwa kupitia uwekezaji wa Kimataifa na diplomasia ya kiuchumi. Zanzibar ipewe nafasi ya kujiingiza zaidi duniani kwa lengo la kukuza zaidi maslahi yake ya kiuchumi na kisiasa. Kutumia mgongo wa Serikali ya Muungano tu hakutoi nafasi kubwa kwa Zanzibar kupambana na matatizo yake makubwa ya kiuchumi. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa wakati umefika wa kuifanya Zanzibar kuwa *Free Port* ili iwe Singapore ya *East Africa*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuona Mataifa yaliyokuwa mbele kabisa katika Bara letu katika kupigania haki za wanyonge duniani katika duru za Kimataifa, sasa yamegeuka na kuwa Mataifa ya kuwafagilia mabeberu wa dunia katika mambo mbalimbali ya Kimataifa. Nchi hizi zinaishi kwa kuchelewa na kusifiwa na wakubwa, wanapigishwa foleni na kupelekwa puta kama vile wao ni viranja tu na siyo watu wenye mamlaka ya kuamua mambo mazito, tena wakubwa hao wanafanya mambo hayo kwa staili ya ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, je, bado viongozi wa nchi zetu hawajajifunza jinsi vibaraka wakubwa walioishi duniani kwa kumwagiwa sifa kedekede na Serikali za Magharibi? Ni ajabu kuona hata mtu aliyekuwa nguzo ya kupambana na ubeberu kwa sauti kubwa sana sasa anaangia mbio mbio na hima hima katika ile tabia ya ahsante mzee. Inasikitisha pia kuona viongozi walioingia madarakani na gia kubwa za wanamapinduzi leo wamekuwa ni washika bango wa kutetea maslahi ya Mataifa makubwa katika eneo zima la Maziwa Makuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, dunia nzima ilishuhudia jinsi Marekani ambayo ni bingwa wa kuhubiri haki za binadamu na ni kinara wa kuwaadhibu wale wote wanaodaiwa kukiuka haki hizo, ikiwa ni pamoja na akina Slobodan Milocevic, Saddam Hussein, Mamwel Noriega na kadhalika, ikipata aibu ya karne, baada ya askari wake kuhusika moja kwa moja na utesaji na udhalilishaji mkubwa wa wafungwa wa ki-Iraq na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ya mwaka 2004, ni hii ambayo inajinyima yenye we uwezo wa kuyasimamia kidete masuala mengi ya Kimataifa, ilishindwa na imeshindwa kukemea na kulaani vikali utesaji na uuaji wa wafungwa katika Gereza la Abu Ghraib mjini Baghdad kule Iraq. Maguvu ya Mataifa makubwa ya kijeshi, kiuchumi, kiteknolojia, kisiasa na kidiplomasia, hayatoi sababu ya Tanzania kushindwa kulaani maovu mengi yanayofanywa na Mataifa makubwa. Umaskini usiwe sababu ya kushindwa kuyalaani Mataifa hayo kila yanapocheza rafu kwa makusudi kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, chokochoko za Rwanda dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (*DRC*), zinao mwelekeo wa kuliathiri Taifa letu kwa namna mbalimbali. Ukiiondoa uwezekano wa kuzalisha wakimbizi zaidi watakaoendelea kukimbilia Tanzania, *DRC* ni eneo muhimu katika maslahi ya kibiashara na kiuchumi ya Tanzania. Utulivu wa kisiasa katika *DRC* unayo manufaa mengi ya kiuchumi kwa Tanzania. Ni lazima sasa sera ya ulinzi (*Defence Policy*) ya Tanzania isaidiane na sera ya mambo ya nchi za nje (*Foreign Policy*) katika kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu yanayotishiwa na chokochoko za Rwanda dhidi ya *DRC*.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia ni lazima kiendelee kuwa na jukumu la kutoa ushauri wa kitaalamu na kuendeleza tafiti mbalimbali. Ushauri wa wataalamu wa Chuo hiki utaisaidia Wizara hii kujua Tanzania ijipenyeze wapi ili kufaidi kama Taifa kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani na hasa katika uwanja wa uchumi na biashara. Ni jambo la kutia moyo sana kwamba, Chuo hiki kipo katika juhudzi nzuri za kusajiliwa na Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu na kimepewa *Letter of Interim Authority* tangu mwaka 2002. Uhawia kibali hicho umeongezwa hadi mwezi Desemba, 2004 kabla ya hatua nyingine zitakazofuatia baadaye, ambapo Chuo kikijitahidi kitazipitia, kwa mfano, kupata hati ya usajili wa muda, hati ya usajili kamili na mwishowe kunyakua hati ya ithibati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kinga za Kibalozi (*Diplomatic Immunities*), ofisi za Kibalozi na makazi ya Mabalozi hayatakiwi kabisa kuwa vichaka vya kuficha watenda

maovu, Ubalozi na Udiplomasia ni kazi zenyenye hadhi kubwa sana duniani. Afisa yeote yule wa Ubalozi ni lazima awe ni mtu mwenye maadili bora na mwenendo bora. Ni lazima Serikali iwe macho na maafisa wa kibalozi wanaotumia ovyo nyadhifa zao na kwa hali hiyo kuwadhalilisha na kuwafedhehesha Watanzania. Sheria za Kimataifa siyo misahafu na hazitakiwi kutumiwa ovyo kwa kuwalinda Maafisa w Balozi wasiojiheshimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sera ya mambo ya nchi za nje ya nchi yoyote ile huwa ni uvushaji wa sera ya ndani ya nchi hiyo na kuipeleka nchi za nje. Sera ya mambo ya nje huwa ni kioo cha sera ya nyumbani. Daima sera ya nchi za nje huanzia ndani ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, bado Tanzania yetu ya leo hadi sasa haieleweki inafuata siasa ipi. Dalili hata zile za mbali kabisa za ujamaa kama itikadi hazipo, ubepari unaoonekana kujengwa ni ule wa kiuchwara na kipembezoni ambaoumekaa kiuchuuza zaidi kuliko ulivyokaa kiuzalishaji na kiuendelezaji sayansi na teknolojia. Siasa ya Tanzania kwa sasa ni ile ya bora liende na bora kumekucha. Upo upatupu, rafiki yangu mmoja aliniambia wanaita *vacuum*, mkubwa sana katika suala zima la mwelekeo wa kisiasa na kiitikadi ya Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi lazima uendane na kuwepo kwa kada ya Mabalozi na Wanadiplomasia wenyewe uelewa mpana kitaaluma wa mambo ya kibashara na kiuchumi. Lazima sasa tujiridhishe kwamba, Mabalozi wetu huko nje wameiva kitaaluma katika nyanja za biashara, uchumi, fedha, uwekezaji na kadhalika na wamesheheni shahada kama *MBA* za *Marketing, Finance, International Trade* na kadhalika. Kama kuna uwezekano si vibaya wakiwa hata na *Ph.D.* katika maeneo hayo. Digrii hizo kamwe zisiwe zile zilizopatikana kwa chap chap wakati fulani katika mazingira ya kutia shaka, eti kwa kisingizio cha kuwepo kwa *Internet*. Kwa mara nyingine tena, nasisitiza kwamba, ukada imara wa chama fulani na umwenzetu, usipewe nafasi ya kuwa sehemu ya vigezo vya kumteua mtu kuwa Balozi wetu nje ya nchi katika karne ya 21. Tunahitaji *Total Quality People (TQP)*, *these are people with character, integrity, good values and positive attitudes*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nafasi nyingi tulizokuwa nazo katika ofisi za Mashirika mbalimbali ya Kimataifa, Watanzania sasa wamekuwa wachache na wanazidi kupungua kadri tunavyokwenda mbele, mfano mdogo ni *ADB*, Tanzania ilikuwa na watumishi karibu 67 hapo nyuma sasa kuna habari kuwa wamebaki 12 tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atueleze kuna nini Watanzania wanashindwa kupata kazi katika Mashirika mbalimbali ya Kimataifa? Aidha, nafasi za masomo tunazopipata kupitia kwenye ushirikiano wa Kimataifa hatuzitumii vizuri kwa mfano, zipo habari kuwa Waziri wetu alipokwenda Urusi alipewa *Scholarships* kwa ajili ya Watanzania, hadi leo hatujasikia ni Watanzania wangapi wameenda kusoma kutokana na *Scholarships* hizo. Aidha, wanafunzi wetu wachache walioko nje, bado maisha yao sio mazuri na wengine hawasomi lakini wanalipiwa na

Serikali. Waziri atuletee Bungeni orodha ya wanafunzi walioko nje wanaolipiwa na Serikali yetu na mwaka waliokwenda na lini wanategemewa kurejea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Balozi nyingi hukusanya mapato lakini hayaingizwi kwenye vitabu na wakati mwingine hayafikishwi benki, mfano, *Bonn/Hamburg Consulate Rome, Denmark Consulate*, walikusanya kiasi cha shilingi 120,000,000/= lakini maelezo yake hayako wazi sana.

Mheshimiwa Spika, ununuvi wa Kompyuta zenyet thamani ya shilingi milioni 142 zilinunuliwa bila idhini ya Bodi ya Tenda ya Wizara kama inavyotakiwa na katika *Section 82* ya *Public Procurement Act* ya mwaka 2001. Wala hakuna ushahidi kwamba, Kompyuta 36 na vikorombwezo vyake viliingizwa kwenye vitabu na kwamba, zilifungwa na thamani yake ilikuwa ni Sh. 60,181,740/= na nyingine 30 ziliingizwa vitabuni lakini zilipokaguliwa hazikuonekana.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa Mawaziri siyo kuomba fedha tu, sisi ni nchi maskini na wao ndiyo wanaojibu hoja za Wabunge hapa ndani, hivyo, namwomba sana rafiki yangu Mheshimiwa Waziri ni lazima muwabane Maafisa Wahasibu katika kusimamia sheria na kanuni zote za fedha.

Mheshimiwa Spika, hizi ni zama za kupigana vikumbo katika duru za Kimataifa na ni mwenye uwezo wa kuhimili vishindo tu ndiye anayeshinda. Taifa letu ijijengee uwezo wa kuwa mshiriki sawa na anayeheshimiwa katika siasa za Kimataifa na siyo mtazamaji au msindikazaji. Tanzania ili iheshimike kama Taifa ni muhimu ifanye kila njia ijijengee uwezo mkubwa wa ndani ya nchi kwa kujitegemea kiuchumi. Kazi kubwa ya Serikali iwe ni kuwezesha na kujenga mazingira ya Tanzania kujijengea kwa haraka uchumi wa Kitaifa na unaojiendesha wenyewe na wenyewe muingiliano wa kisekta. Maendeleo ya kiuchumi ya Taifa lolote makini hutegemea sana uchumi wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, napenda sasa nitoe shukrani maalum na pongezi kama ifuatavyo: Namshukuru sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Kamati nzima ya Uongozi ya Kambi ya Upinzani, kwa uongozi wao wa busara ambao umetufanya sisi Wabunge wa Kambi hiyo, kutenda kazi zetu kwa mafanikio makubwa. (*Makofî*)

Aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika na wasaidizi wako, kwa kuliendesha Bunge letu kwa hekima na busara na hivyo kujijengea wewe binafsi heshima kubwa na kulifanya Bunge letu kuwa mfano wa Bunge lenye utulivu na nidhamu katika ukanda mzima wa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Naibu Waziri wake, pamoja na Watendaji wote wa Wizara yao, kwa umahiri wao na utendaji wao wa kazi bila kuchoka kwa muda wote. (*Makofî*)

Mwisho, nisimsahau Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Dr. William Shija, pamoja na Wajumbe wenzangu wote wa Kamati, kwa ushirikiano na msaada mkubwa wanaonipa kila wakati katika uchambuzi wa mambo mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na siyo tu kuwa mimi naunga mkono hoja hii, lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, waiunge mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa .

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbusha tu jambo moja, mwaka 1984, nilimleta mfanyabiashara mmoja mkubwa sana alitaka kufanya *investment* kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam. Alipofika pale alileta wataalam wake na akafanya *studies* ili kuifanya bandari ya Dar es Salaam iwe *Free Port*, baada ya kumaliza kufanya *studies* akaenda kumwona Rais Ali Hassan Mwinyi, akamwambia hivi: “Nchi yako ni nzuri sana ina rasilimali nyingi, ina watu wazuri, lakini bahati mbaya nje haijulikani, badilisha wale Mabalozi wa kisiasa weka Mabalozi wenye taaluma za kibiashara na za kiuchumi.”

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu na kuingia katika soko la kidunia, tunahitaji Mabalozi ambao kwa kweli wana uwezo mkubwa sana wa kuitangaza Tanzania na kusimamia sera zetu za Kitanzania kikamilifu. Kazi hii inahitaji kuandaliwa vizuri sana. Kwa hiyo, moja katika ombi langu kwa Wizara kama walivyosema waliotangulia ni kwamba, kuna haja ya kuchukua *measures* za dharura kuhakikisha kwamba, tuna Mabalozi wanaoweza kweli kuitangaza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako Ndogo ya Hesabu za Serikali ilikuwa London hivi karibuni. Nilipata nafasi *briefly* tu kukutana na Balozi. Lakini kwa *nature* ya Balozi yule aliyeko pale, ambaye kila dakika moja anakupa *statement* ambayo una hakika kabisa anadanganya, siwezi kutegemea kwa kweli katika kituo kile muhimu kabisa tukaweza kukuza biashara yetu. *Very I am sorry.* (*Makofî*)

Alifika mpaka kuikimbia Kamati yetu ya Hesabu za Serikali. Akamkimbia hata na Katibu wake Mkuu. Maana tulipomwuliza na yeze akasema amesikia ameondoka. Huwezi ukajenga uchumi kwa *with that type of ambassadors*, kabisa kabisa haiwezekani. Kwa hiyo, naomba kabisa tumshauri Mheshimiwa Rais, tupate watu ambao kwa kweli watasimamia uchumi wa nchi yetu katika ushindani huu tulionao sasa hivi. Watu ambao ni *serious*, ni *committed*, ndio tunaoweza tukasimamia uchumi wa nchi yetu. Sasa hilo ni moja ambalo ningependa niliseme hivyo. La pili, kwanza nawashukuru sana Wizara kwa kutoa *programme of action* kutokana na *policy* yetu ya Mambo ya Nje. Ni mwanzo mzuri sana angalau tuna dira tunajua ni wapi tufuate na tuulize kipi kimetendeka na kipi hakikutendeka. Napenda sana kuwapongeza kwa hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika programu hii kuna suala zima la kuendeleza ulinzi na usalama sio ndani ya nchi tu lakini pia na nchi zetu za majirani na Bara la Afrika kwa ujumla. Pindi uwe mfano lazima wewe mwenyewe uwe na amani na hicho ndiyo kitu kizuri cha Watanzania. Kwamba, nchi yetu imekuwa na amani na ndiyo maana watu wanakimbilia kwetu kuhifadhiwa, ndiyo maana hata tunaposimamia migogoro watu wanatuheshimu kwa sababu sisi wenyewe hatuna migogoro mikubwa. Mwanzo wa moto ni cheche, pale tunapoona cheche kama hatukuizima basi inawezekana hatimaye tukapata moto.

Nashukuru sana na nafurahi sana Rais wetu alivyoweza kwenda kifua mbele, mbele ya wenzake akiwaambia sisi Watanzania tuna uwezo huo wa kutatua migogoro yetu ya ndani. Hili lilitokana na mgogoro tuliokuwa nao tukautatua wenyewe tukapata muafaka. Ningependa sana kushauri Serikali na hasa kupitia Wizara hii, lazima tujitahidi muafaka utekelezwe kikamilifu. Hatuwezi tukafika mahali tukawa *champion* wa kuomba wenzetu waishi kwa amani kama sisi wenyewe tumeanzisha jambo zuri lakini hatimaye tumeshindwa kulisimamia. Jambo lolote zuri ni lile ambalo linadumishwa na si lile ambalo linafanywa mara moja na kuachwa. Kwa hiyo, ili tuwe na mwenendo mzuri kwa wenzetu, ni lazima tuhakikishe kabisa muafaka unatekelezwa na iwe ni kielelezo tunapokwenda mbele tunawaambia wenzetu sisi tumeweza kufanya hiki njooni mjifunze kwetu. Sasa kama hatukakamilisha kikamilifu, hatutoweza kufika mahali. Ili tukamilishe kikamilifu tuhakikishe kabisa moja ni kwamba, tunao uchaguzi uliokuwa huru na haki na mshindi atakayepatikana kwa njia ile ya haki, basi atangazwe kuwa mshindi bila matatizo yoyote. (*Makofit*)

Moja ni kuhakikisha kabisa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama havijishughulishi katika siasa, wanafanya kazi zao za kawaida na wale ambao wanataka kuingia kwenye siasa basi waingie kwenye siasa wakielewa kwamba, kutakuwa na uchaguzi uliokuwa huru na haki. Hilo litakusudia sana katika nchi yetu kuweza kusimamia maendeleo ya Taifa letu. Taifa lenye matatizo haliwezi kuendelea hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala zima la Kiswahili. Namshukuru sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, amelieleza vizuri na Kamati ya Mambo ya Nje nayo imeeleza vizuri. Lakini nataka kusema mfano wa pili. Nilikutana na mfanyabiashara mmoja kutoka *South Africa* akaniambia nyie Watanzania ni watu wa ajabu kidogo. Nikamwuliza kwa nini? Akaniambia hata kile kitu ambacho mnacho ninyi peke yenu duniani bado mnawangojea wengine wakupangieni bei. Nikamwuliza kitu gani? Akasema *Tanzanite* haipo popote ulimwenguni, lakini mmewaachia watu sasa wanakupangieni bei ya *Tanzanite*, kumbe mngekuwa na uwezo wa kujipangia bei ninyi wenyewe *Tanzanite* kwa sababu hakuna mwenye nayo.

Kwa hiyo na Kiswahili vilevile. Kiswahili ni peke yetu tulikuwa nacho. Sasa hivi kinachukuliwa na watu wengine, wao sasa ndio wanakitia thamani Kiswahili. Sasa hizi ni kasoro ambazo lazima tuzirekebishe. Kile ambacho ni chetu sisi wenyewe lazima tuwe na uwezo wa kujipangia bei sisi wenyewe wa kuweza kikitangaza sisi wenyewe, kuweza kukiiza sisi wenyewe. Leo mpaka upate mhuri wa *AFGEM* ya *South Africa*

ndio ione kane *Tanzanite* kwamba, ni *Tanzanite* halali. Sasa hii ni kasoro kubwa sana kwamba, hata chetu lazima tupate mhuri wa nchi nyingine au watu wengine pamoja na kwamba, wanatumia jina la kwetu hapa Tanzania. Sasa nasema hizi ni kasoro ambazo tunazifanya. Kwa hivyo, naomba sana hili suala la Kiswahili kiendelezwe na kitumike vizuri sana na hasa katika suala la Umoja wa Uhuru wa Kiafrika ambapo tumekubaliana Kiswahili ni moja katika lugha za Taifa.

Mheshimiwa Spika, la tano ni suala zima la *honourary consulates* tulionao. Nina haja ya kufanya tathmini kama kweli waliopo wanafanya kazi tulizozikusudia. Hata ukisoma taarifa tu za Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu utakuta hizo *honourary consulates* zina matatizo mengi sana. Mimi nafikiri kuna haja ya kufanya tathmini upya. Waliopo wanafaa kuwepo na kama hawafai kuwepo wanaondolewe watafutwe wengine. Lakini vilevile tupanue nyanja hiyo kwamba, wapo wafanyabiashara wazuri wa kigeni ambao wana hamu sana kuitangaza Tanzania na wana uwezo wa kuitangaza Tanzania. Nimewakuta ndugu zetu wa Ki-asia waliokimbia kutoka Uganda wako British Columbia pale Vancouver, wanaitangaza Uganda vizuri sana. Wamekuwa ni *honourary consulate* pale Canada. Sasa tunao watu wa aina hiyo wengi na Watanzania, *deplorger* wengi tu huko nje. Tuwatumie vizuri basi. Wengine wana uwezo mkubwa wanafundisha mahali pengine na wengine wameingia kwenye biashara kubwa kubwa. Juzi tulimwona msichana mmoja kwenye *TV* anaitwa Tausi anaweza kuwa Balozi mzuri tu wa Tanzania. Anaipenda nchi yake amejielimisha vizuri anaweza kuwa Balozi mzuri tu wa Tanzania.

Sasa nasema tuvitumie vipaji vya Watanzania tulionao nje ili kuikuza nchi yetu. Nchi nyingine wenzetu wana orodha hasa ya watu kama hao. Sisi sina hakika kama tuna orodha ya watu wetu ambao wana uwezo kama huo. Lakini lingine tumekuta nchi nyingi raia wao wanapopata matatizo huwa wanawafuutilia. Sisi tuna Watanzania wengi sana wana matatizo mengi sana. Lakini bado hatujui habari zao. Bado suala la kumthamini Mtanzania pale alipo halijafanyiwa kazi vizuri. Kwa *nature* ya Balozi zetu kila ukifika pale unaonekana kama mtu wa kuleta bughudha tu. Si kwamba ni mahali ambapo unaweza kupata msaada kwenu. Hiyo nasema ni kasoro moja. Nimekuta pale Ugiriki kuna Watanzania zaidi ya watatu wanalala tu barabarani na hawana msaada wa mtu ye yote na sehemu nyingine nyingi. Kweli wamekwenda kutafuta riziki, lakini kuna haja ya kuona na kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, kuna hawa wenzetu wana ozamia meli kwa mfano wanatafuta riziki. Hakuna ndani ya *organization* inayoweza kuwasaidia wao kupata ajira ya kwenye meli za kigeni. Sasa *organization* iliyopo inaachiwa iendelee yenye. Kwa wenzetu wengine akina Ma-Phillipino na kadhalika, wana *organization* kuhakikisha kabisa kama kuna *Panama Lines Ships* wanataka wafanyakazi wanawapelekea na mikataba inayo julikana na inaheshimika. Kuna Watanzania wengi sana wamekufa kwenye meli, wengine wamepigwa, wamenyima haki zao na hawana pa kulalamikia na hata Ofisi zetu hazina uwezo wa kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na haya machache, naomba kuiunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa, natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na msaidizi wake, kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika Wizara hii na kwa kipindi alichokaa ameonekana kuwa ni mtu wa Kimataifa na ametufanyia kazi kubwa na nzuri za Kimataifa na kutupatia heshima kubwa Tanzania. Nawapeni hongera nyingi sana. (*Makofî*)

Sifa za pili zimwendee Rais wa Msumbiji, Mheshimiwa Joachim Chissano, kwa kuwa mtu wa kwanza kabisa kukitangaza Kiswahili kwa kuhutubia Kimataifa kwa kutumia lugha ya Kiswahili ambapo Watanzania wenyewe lugha hiyo tulishashindwa kufanya hivyo. Ametupa changamoto kubwa kwamba sasa Kiswahili kama kilivyoamuliwa kianze kutumika Kimataifa bila kuona aibu. (*Makofî*)

Mwingine ni Mheshimiwa Sam Nujoma, Rais wa Namibia, aliyetutembelea hivi karibuni, ambaye amekuwa ni Rais aliyeona atoe shukrani kwa fadhila tulizowafanya za kuwakomboa. Ameona arudi nyumbani alikokuwa na kulikotokea uhuru wao na kuja kutushukuru. Naye pia nampongeza sana, naomba salamu zangu zifike kwao hawa wote wawili kupitia Wizara hii. (*Makofî*)

Lakini la pili ni lawama ambazo zimetolewa ni za kweli kabisa nazo ni kuhusu Mabalozi wa nchi zetu za nje hasa wale wa Kitengo cha Wizara yenye ya Mambo ya Nje, ukiacha watumishi wengine wanaotoka kwenye ofisi nyingine. Wale wamekuwa kama Miungu Mtu. Wanajiona wao ni bora zaidi kuliko Watanzania wengine, haya tumepata malalamiko kwa mfano London. London hapafai kabisa nadhani mnapaswa kubadilisha pale London hapafai, hapafai, ovyo. (*Makofî*)

Nimetembelea baadhi ya Balozi nyingi, sina haja ya kuzitaja nyingine huko nje. Lakini Balozi inayoongoza kwa ubaya zaidi ni ile ya London. Kwa kipindi kirefu Balozi yule alipokuwa ameteuliwa hakuwepo alikuwa anakaa huku Tanzania. Kwa hiyo, mara nyingi msaidizi wake ndiye alikuwa anafanya kazi. Kwa hiyo, Watanzania wengi wanaokaa eneo lile la Ulaya amba wanategemea Ofisi ile ya London, wamekuwa wakilalamika kwa mambo mengi sana. Kwa hiyo, tunaomba ile Ofisi mjaribu kuibadilisha. Wasidhani kwamba Watanzania wanapokwenda kwenye ofisi hiyo, maana yake ni watu wa kwenda kuombaomba tu, hapana wana matatizo wengine ya kimsingi kabisa jinsi ambavyo wanapaswa kusaidiwa jinsi gani wanavyokaa katika nchi hizo. Ni jinsi gani wanaweza kusaidiwa katika matatizo yao mbalimbali wale walioajiriwa na amba pengine wanafanya biashara zao na kadhalika. Wasidhani kila anayekwenda pale anakwenda kuombaomba.

Hata baadhi ya Wabunge wengi walotembelea Ofisi za Kibalozi zetu wamekuwa wakikimbiwa na Mabalozi wanadhani hata Wabunge wanaweza kuwa ni omboaomba, sasa huo ni ushirikiano gani. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ujaribu kulirekebisha hilo katika Ofisi zako.

Lakini naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Makame Rashid, ambaye yuko kule Malawi, Lilongwe. Yule mtu ni mtu mzuri kweli. Watanzania wengi waliokwenda kule wamekuwa wakimsifu. Mimi mwenyewe ni shahidi kwa sababu amekuwa akihaha katika miji ya Malawi kama vile Mzuzu, maeneo ya Karonga kule, Blantyre yenyewe na Sophia, akiwatafuta Watanzania ili wakae kwa pamoja wampe matatizo yao lakini kikubwa zaidi anataka afungue njia ya biashara kwa Watanzania, anasema anataka Watanzania watajirike maana yake kule fedha ziko nje na bidhaa nyingi zinatoka Tanzania kwenda kule.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ardhi ni shahidi wangu, maana yake yeye maeneo ya kule anapakana nao. Kwamba, hata katika eneo lile la Kaskazini mwa wanasema Malawi mfano, *Chitopa District*, kama isingekuwa Tanzania sijui tungefanyaje. Kwa hiyo, Balozi yule anasema anataka Watanzania wote, ameshaanza kuwakusanya anakaa nao vikao anawaelekeza nini la kufanya ili waweze kufaidika. Huyo ndio Balozi ambaye naweza nikamsifu kwa wazi wazi. Wale wa Ubalozi wa Kenya wanaotoka kwenye Mambo ya Nchi za Nje kwanza wana dharau halafu wanakimbia wageni. Kama sio wale maafisa wanaotoka kwenye Wizara nyingine ambao ndio angalau wanawakaribisha wageni napo pale tungekuwa tunaabitika kila wakati. Kwa hiyo, nawaambieni dhana ya Watanzania sio kwenda kuombaomba ni kwenda kujaribu kutafuta huduma za kweli kweli na ndio maana ya Ubalozi kuwepo kule. Mheshimiwa Waziri, unafanya kazi nzuri lakini hawa wenzako wanataka kukupaka matope bila sababu.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema kitu kingine ninaomba Wizara hii isaidiane na Wizara ya Kazi katika kitengo cha kuwatafutia Watanzania kazi nje. Unapowatafutia Watanzania kazi huko nje kwanza, unapunguza tatizo la kazi Tanzania. Lakini pili unawatafutia ujuzi mkubwa, yaani naweza nikasema kama kuwapa *U-TX*, kama Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, ambao walikaa huko nje na Watanzania wengine ambao siwezi nikawataja hapa muda wenyewe hautoshi, ambao wanapokuja Tanzania wanakuwa ni tunu kubwa na wanakuwa ni wafanyakazi wazuri sana, wanaotupatia ujuzi walioupata kutoka huko nje. Ndiyo faida ya kuwapeleka watu wetu wengi kwenda kufanya kazi huko nje. Hasa hawa ambao ni mahiri kwa Kiswahili nao ni vizuri tuwapeleke maeneo mengi ya nchi za nje maana Kiswahili kimetukuka waweze kufanya kazi ya kufundisha Mataifa. Wenzetu wa Bunge la *SADC* walikuwa wanafikiria wapendekeze kwamba, Kiswahili iwe ni lugha mojawapo ya kuongea katika *SADC*. Lakini pia wanasema watafute chuo ambacho kitafundisha Kiswahili. Wao wameanza kutafuta mawazo ya *ku-propose* hivyo sisi Watanzania tumekaa tu hatuoni umuhimu wa jambo hili sijui tunaona aibu ya kitu gani. Ni muhimu kwetu tujitahidi sisi wenyewe kuhakikisha kwamba, tuna-*promote* Kiswahili chetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Nje kwa kushirikiana na Wizara Maliasili na Utalii, wangeweza wakai-*promote* Tanzania kwa utalii na tukapata fedha nyingi sana. Kama kila Ubalozi ungekuwa na Kitengo kinachoshughulikia masuala ya utalii na kingekuwa na mtaalamu anayeshughulikia masuala ya utalii, tusingehangaika kupata fedha katika nchi yetu, maana nchi yetu ina kila kitu.

Kwa hiyo, Balozi nyingi hawana mpango kabisa na wala hawaoni thamani ya kutangaza utalii wetu. Mimi nadhani moja ya kazi kubwa pamoja na kazi waliyonayo lakini kazi ya pili kubwa ingekuwa ni kuutangaza utalii na awepo mtu anayeshughulikia masuala ya utalii. Iwe ndiyo kazi yake katika kila mikutano wanayokwenda kukutana wadokezwe masuala ya kiutalii katika maeneo wanapofanyia kazi. Pawe na urahisi wa watu wanaotaka kuja Tanzania wanapokwenda pale kwenye Balozi zetu, wawe na *brochures* za kutosha, wawe na *information* za kutosha ambazo zinalezea masuala mbalimbali ya vivutio vya Tanzania. Hicho hakifanyiki kwa sababu tumekuwa tukipata hayo malalamiko kutoka kwa watalii wenyewe na kutoka kwa baadhi ya watu wetu walioko huko nje kwamba hawafanyi hivyo.

Hapa naweza nikatoa pongezi kwa mtu mmoja anaitwa Bwana Abel ye ye yuko kule Japan anafanya kazi nzuri sana ya kututangazia utalii wetu. Kipindi fulani mwaka jana tulipokuwa huko Japan ye ye ndiyo alichukua vifaa vyake vyote na hata wale wanyama wa umbaumba na hata kanda zote zilizokuwa zimetengenezwa ni ye ye ndiye aliyekuja kuzitengeneza hapa Tanzania na anajaribu sana kuitangaza Tanzania na alishatengeneza *brochures* za Kijapan kwa ajili ya kuitangaza Tanzania utalii. Sisi Watanzania hatufanyi lolote ingawa Ubalozi wa pale Japan nao unajitahidi sana kutangaza utalii wetu. Wale naweza nikawasifu Balozi wa Japan Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusiana na visa za vibandiko. Hivi ni muhimu sana. Tumeona nchi zote karibuni za Ulaya, Marekani, Asia wanavyo. Hivi vinapunguza ubadhirifu mbalimbali wa ku-forge mambo ya visa na vile vile inatoa umuhimu wa wageni wanaokuja kuwa na uhakika zaidi kulikoni ule wa kupigapiga mihuri ambayo mtu yoyote anaweza aka-forge na hiyo mgeni anapokuja atapata matatizo kwamba huu sio mhuri ambaio ni sahihi. Lakini uwepo na ushirikiano kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Mambo ya Nje kuhusu visa kwa watalii wanapokuja waweze kupunguziwa au ikiwezekana kufutiwa kabisa ili tuweze kupata watalii wengi wanaokuja Tanzania kuja kutuungezea mapato.

Lingine ni watumishi wa Ubalozi wanapokuwa huko nje wajitahidi kujinoakili zao yaani wasome, wasirudi kama walivyokwenda. Wengine wakienda wanakaa tu pale kutazama raha za mijji na kadhalika au kutafuta mambo yao wajitajirishe hawataki kujinoakili kupata elimu nyingine za Kimataifa. *AICC* jengo letu pale limejaa ofisi nyingi za Kimataifa. Kwa hiyo, kulundikana kule bado pia sio kuzuri sana, jengo moja wao kujaa pale. Wizara ione umuhimu wa kutafuta ardhi na kujenga Makao Makuu ya Muungano wetu wa Afrika ili mlundikano uliopo pale *AICC* uondoke. Pia Mahakama hii ya Mauaji ya Halaiki ya Rwanda nayo ione umuhimu wa kujengewa ofisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja kwamba, Tanzania itakuwa ni Mjumbe katika Kamati ya Usalama ya Umoja wa Mataifa katika miaka miwili kuanzia mwaka ujao? Sasa nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, atuelezee hii ina maana gani hasa kwa upande wa kifedha kwa maana ya Balozi wetu pale New York, lakini pia watumishi wa Ubalozi hapa?

Mwisho, kuna watu wetu waliotekwa katika eneo la Karema kule Mpanda Mwambao mwa Tanganyika, eneo la Nkasi na eneo la Sumbawanga Vijijini upande wa kule Kasanga kwenye *DRC*. Wale watu mpaka leo hatujui hatima yao. Mheshimiwa Waziri, tunaomba tufahamu watu wa Mkoa wa Rukwa wale watu wakoje, wako hai ama iko ikoje?

Lakini pia tunashukuru kwa sababu eneo pia lile angalau bado matukio yapo lakini angalau kidogo hali imeshaanza kutulia tulia na tunaomba msukumo wa kutuongezea vifaa zaidi kama vile boti ziwepo katika maeneo yetu, watuongezee magari ya kijeshi pale ili waendelee kulinda eneo lile la Mwambao.

Mwisho, kufungua *corridor* ya kibashara katika eneo lile la Tanganyika na *DRC* ili Wananchi wa eneo hilo waweze kufaidika na biashara kwa maana ya Tanzania nzima. Tunaomba Wizara hii muongee na nchi ya *DRC*, waone uwezekano wa kufungua eneo hilo la barabara kwa kushirikiana na Tanzania kwa kiwango cha lami kuitia maeneo ya Kasanga na maeneo ya Kipili na pia kuweka vituo vya Bandari ili tuweze kufungua *corridor* ya biashara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi ninaunga mkono kabisa Wizara hii maana yake imejitahidi kufanya kazi kubwa na nzuri na kutuletea *image* nzuri ya Tanzania huko nje ya nchi kutokana na Mawaziri hawa kuwa makini zaidi na kuwa ni watu wa Kimataifa. Naunga mkono. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nina shughuli nyingine, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Spika, aje anipokee Kiti.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. REMIDIUS EDINGTON KISSASSI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache katika hii, Ofisi yetu inayoshughulikia Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Awali ya yote, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Abdulkader Shareef, pamoja na Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuliwakilisha Taifa letu, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nitoe salamu zangu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyetutoka hivi karibuni na Wananchi wote wa Ulanga Mashariki tunawapa pole sana na tunawaombea Mungu wawe na moyo wa subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda sana nimpongeze sana Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kulitangaza jina la Tanzania katika nyanja za Kimataifa. Pamoja naye Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Alhaj Aman Abeid Karume, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Kiongozi, pamoja na Viongozi wote, Mawaziri pamoja na Wabunge, kila wanapokuwa nje kwa kweli wanajitahidi kulitangaza

Taifa letu. Taifa letu linang'aa sana katika nyanja za Kimataifa. Hongereni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuwa Tanzania sasa hivi tulishapata changamoto. Kiswahili kuanza kutumika katika Mikutano ya Kimataifa ambayo imeanza katika Mkutano wa juzi uliofanyika kule Addis Ababa ni changamoto kwa Mabaraza yetu ya Kiswahili Tanzania Bara na Visiwani kuanza sasa kushawishi watu wengi kutumia Kiswahili na tuone fahari basi kukitumia Kiswahili kila kinapowezekana na lakini vilevile tuendelee kutafuta na kuwafunza wakufunzi wengi ambao watakitungaza Kiswahili na kutoa elimu kwa Wananchi wengine wa Afrika na Dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali ya Tanzania kwa kujiunga na huu mpango wa *NEPAD (African Pan Review Mechanism)*. Mpango huu ambao ulinubuniwa na Viongozi wetu wa Afrika unalenga katika kujiangalia na kujikosoa wenyewe ndani ya Afrika katika mambo mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa Serikali zetu na masuala ya Utawala Bora. Hivyo, hii ni hatua muhimu sana kuwa kama nchi zote za Afrika zitajiunga na *APRM* wakawa wanajichunguza wenyewe, ina maana tayari tunakuwa tunafanya mkakati wa kujikosoa ndani kwa ndani. Lakini sio hivyo tu, ina maana sasa hivi nchi za Afrika zitakuwa na mbinu ambazo zinafanana za kujikombao kiuchumi, kiutamaduni na kadhalika. Kwa hiyo, nahimiza nchi nyingine za Afrika ziingie katika mpango huu wa *APRM* ili tuanze kupata maendeleo haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la uchumi wa Kijiografia. Ndani ya Tanzania yenyewe kwanza ni muhimu kutambua maeneo ambayo yana *economic advantage* katika nyanja mbalimbali. Mfano ambao ningependa kutoa leo ni wa nafasi ya Zanzibar katika uchumi wa Tanzania na katika uchumi wa Afrika. Zanzibar ni visiwa, tumebarikiwa kuwa na maeneo ya bahari tena ambayo yana kina kirefu. Changamoto ninayopenda kuitoa ni kuwa katika mkakati wa Tanzania kiuchumi ambao ndio mkakati wa sera za nje sasa hivi basi tuangalie namna gani tutawezesha Zanzibar ambao tayari wameshaanza kuwa na sera ya kuwa na Bandari huru iwekeze zaidi ili iwe kivutio kwa wawekezaji wa nje kwenye masuala ya *Free Port*. Haitoshi kusema kuwa, Zanzibar iende peke yake. Tulishakubaliana hapa kuwa masuala ya Nje, Ushirikiano wa Kimataifa, masuala ya Muungano, kwa hiyo ioneokane basi mkakati wa makusudi wa maamuzi kuwa kwa kweli inapokuja katika masuala ya *Free Port Development*, basi zile nguvu zinapelekwa Zanzibar ili Zanzibar kama walivyosema wenzangu, labda Dubai au sijui ng'ambo ya Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la uwiano. Hiki chombo cha Muungano Mambo ya Nje ni vizuri basi wale wafanyakazi wanaofanya kazi mle waonekane angalau wanaonyesha ile sura ya Kimuungano. Mabalizi ioneokane wapo wanaotoka Visiwani na Bara. Wale wafanyakazi wenyewe watendaji katika ofisi mbalimbali kama katika Ubalozi na hata katika Mashirika ya Kimataifa zile nafasi zitawanywe katika mgawanyo ambao unakubalika. Si vizuri kila wakati tukapata sehemu moja inanung'unika kwamba, zile nafasi za ajira hazipatikani au kuna watu wanabinywa hapa na pale. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri aliangalie ni kuwa Zanzibar tumekubali kuwa iwe na ofisi nyingi za Naibu Kibalozi au ofisi ndogo za Ubalozi. Sasa ile ofisi ya Mambo ya Nje iliyoko Zanzibar haionyeshi ile sura ya Kimungano lakini vilevile hata hadhi yake sio ya kuonyesha hii ni Ofisi ya Ubalozi wa Mambo ya Nje. Kwa hiyo, napendekeza pale kwa kuwa kuna maeneo yamejengwa tayari kwa kujengwa Ofisi ya Muungano zenye sura za Kimungano basi Mambo ya Nje nayo wajenge Ofisi moja ambayo itakuwa na hadhi. Kwanza, ile Ofisi iliyoko pale ni ya kukodisha. Kwa hiyo, ni vizuri ikijengwa Ofisi ndogo moja nzuri ya Mambo ya Nje pale Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la wakimbizi. Watanzania tumeshaelewa mambo yetu mengi yameharibika ya kiuchumi kwa sababu ya wakimbizi. Wengi wamekuja wametuhabiria mazingira yetu na kadhalika. Mheshimiwa Rais wetu aliwahi kutangaza mkakati kuwa ni vizuri Afrika sasa tukawa na utaratibu ambao wakimbizi watabakia katika nchi zao wasivuke mipaka.

Kwa hiyo, kama ni wakimbizi kutoka Rwanda, basi watengewe eneo ndani kwao mle na ufanywe utaratibu wa kuwalinda, lakini wasije huku wakaanza kuwashumiza wenzao. Sasa mimi nasisitiza sana kuwa mkakati huu ufanyiwe kazi ili wakimbizi katika Afrika wabakie katika zile zile nchi zao wasaidiwe ili wapatane waweze kuendesha nchi zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kuchangia ni suala la ushirikiano wa kiuchumi baina ya nchi za Kiafrika. Tumeanza na Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunayo *SADC*, wenzetu Kaskazini wanayo *COMESA*. Sasa hivi tunayo *AU* na tunatumia chombo cha *NEPAD*.

Rai yangu ninayotoa ni kuwa tujaribu sana kwanza kuwashirikisha Wananchi wenyewe waone umuhimu wa hizi Jumuiya. Isiwe ni Jumuiya za Viongozi. Hizi ni Jumuiya za kuwashirikisha wale Wananchi wa chini na namna ya kufanikisha hilo, moja katika mkakati iwe ni kuachia wawe na *free movement*. Wawe na utaratibu ambao hawatabughudhiwa sana wakaenda kwenye nchi nyingine kwenye masuala ya biashara, utamaduni na kadhalika.

Tuwatie moyo wawe na mwingiliano wa hali ya juu ili waone sababu za kwenda nchi nyingine kufanya biashara. Sasa hivi tumekaa tunang'ang'ana hapa hapa na nchi yetu kumbe kuna nafasi nyingi katika nchi za jirani na kadhalika.

Natoa wito kwa nchi za Kiafrika kuendeleza miundombinu ya barabara, masuala ya mawasiliano kwa njia ya simu na kadhalika, masuala ya umeme kushirikiana ili Afrika iweze kufanya *leapfrog* katika suala la uchumi. Hatuna haja ya kuanza ku-reverse the wheel kila wakati wenzetu wameshafanya hilo na sisi tunajaribu kufanya hilo hilo. Sisi tuna nafasi ya kuchupa. Tutumie teknolojia hizi mpya za Sayansi ili tupate maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema tena kuwa naunga mkono hoja hii na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba na mimi nichangie hoja ya Wizara hii ya Mambo ya Nje. Awali ya yote, nampongeza sana Waziri wa Mambo ya Nje kwa kazi nzuri anayofanya na juhudi mbalimbali ambazo zimeonekana kwa kipindi chote ambacho amekuwa kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio mimi tu nimeamua kumpongeza, lakini nampa na salam nyingine kwa Wizara yake kutoka Misri kwa Balozi, wanashukuru sana Watanzania kununua nyumba. Kule Misri sasa tuna nyumba ya Tanzania ambayo inakaliwa na Balozi na Ofisi nzuri wanayo na mimi mwenyewe nimeiona. Kwa hiyo ametuma hizo salam nipongeze Wizara kwa jumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache lakini nafikiri muhimu ni katika kuunganisha Afrika, tumekuwa na kigugumizi na ninamwomba Waziri kwa kweli Askari wa Mwavuli alijengee hoja sana hili. Tumekuwa na kigugumizi cha namna ya kuunganisha Afrika. Amerika kuna *United State of America*, Ulaya kuna *European Union* na *Soviet Union*. Hapa kwetu tuna *African Union* sio sahihi. Nasema sio sahihi kwa sababu imekuwa African Union kwa jina lakini sio katika utekelezaji, not in activity. Kwa sababu gani? Utakuta huku Kusini sisi Tanzania tunasema tuko *SADC*, tayari tumeshajitenga, hapa katikati kuna *COMESA* na huku Magharibi tuna *ECOWAS*. Sasa utenganisho huo utatuwia vigumu sana tuje kuwa na *a good African Union*.

Ninapenda na ninapendekeza tuwe na sauti moja na kama hatuwi na sauti moja katika Afrika hatutakwenda. Afrika sasa hivi kuna vita. Kuna vita Congo, Sudan na Ethiopia kuna ugomvi wa hapa na pale. Lakini sisi Tanzania tunasema tunasuluhisha, lakini hatuangalii chanzo cha magomvi haya. Sisi tunapoambiwa kwamba silaha za kwenda Kongo zinapita hapa hapa Tanzania, sijui kama tunazona au hatuzioni! Lakini tunakuja baadaye tunataka kusuluhisha ugomvi na wakati mwingine silaha za kwenda Kongo kupigana zinapitia katika nchi yetu. Ningetaka Wizara hii iwe makini katika mambo haya kwamba, kutokana na udhaifu huu wa kutenganisha Afrika kwa kutugawa, kwani hawa wakubwa ambao wanahitaji kuendelea kututawala kiuchumi ndani ya Afrika hawatapenda kusikia kwamba Afrika inaungana.

Kwa hiyo, ili tuweze kuliona vizuri, ningeshauri pamoja na bidii ya Wizara hii, kwa nguvu zote iangalie upya mawazo ya Marehemu Nkhurumah, iangalie upya mawazo ya Marehemu Julius Kambarage Nyerere na iangalie upya mawazo ya Mwamar Gadaffi ambao wana mawazo mazuri ya kuunganisha Afrika na kwa maana kwamba, walikwishaona matatizo ya hawa mabeberu wanaopenda kutugawa sisi ili wao watutawale kiuchumi na vilevile inafikia mahali wanatutawala kisiasa. Wala tusikatae hilo la kisiasa maana kuna mikopo mingine walilettea masharti ya kisiasa tukaikataa. Kwa hiyo, jambo ninalolizungumza ni mambo ambayo yapo, tusiweke utani hapa! Tunazungumzia *serious* katika mchango wa Bunge. Ni mambo ambayo yapo yanatendeka na yanatumiza sisi Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yanatumiza namna gani? Leo hii tunapangiwa bei ya nafaka zetu tunazozalisha huko Ulaya, hatukuweza kuungana tukawa na soko letu moja la Afrika ambalo tunaweza kujidai. Afrika ni tajiri ukilinganisha na nchi nyingine. Lakini kwa sababu hatuko wamoja, tunaletewa silaha tunapigana halafu baadaye wanakuja wanasema ngoja tukawasuluhishe wale wakati silaha ndio wao wameleta. Ukimwuliza yule anayepigana hela amepata wapi ya kukaa huko msituni, kumbe anapokea kwa mkono wa nyuma namna hii na sisi tunawaangalia. Bila kuwa wamoja katika Afrika hii, bila kuchukua mawazo ya hawa watu mashuhuri duniani niliozungumza kwamba sasa tuendeleze hili jambo la kuunganisha Afrika. Tuombe hawa *ECOWAS*, *COMESA*, *SADC* tuwaambie mambo ya kujitenga ni nini? Mabaya! Kwani kuna nini? Tukifanya kitu kimoja tukavunja vyote hivyo si Waafrika sisi? Si *continent* yetu? Tuwaambie na wakikataa basi wataonekana baadaye mbele ya vizazi vyetu kwamba, wao ndio waliokataa na watakuja kulaanika baadaye. Lakini kwa sasa sisi tuwe kidete kufanya hilo.

Ninaamini katika mazungumzo yangu, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kuna wakati alikwenda *South Africa*, kulikuwa na Mkutano na alizungumza vizuri sana na ndio maana nikamsifu hapa. Nafikiri ataendeleza hilo la Muungano na kushirikiana na hao na kupiga vita hao wanaotu-induce sisi kupigana wenyewe kwa wenyewe. Sio kweli kwamba watu wanajianzia tu kupigana, wanapewa vihela kwa mkono wa nyuma halafu wanaleta vita wanasema Waafrika wanapigana wenyewe kwa wenyewe. Je, tuna kichaa sisi Waafrika?

MBUNGE FULANI: Hatuna.

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Hatuna kichaa, tuna akili zetu timamu, lakini sasa wengine wanapenda hela zaidi wanachukua fedha kwenda kumpiga Ngawaiya, Zanzibar wanataka kupigana na Tanzania hivyo hivyo. Lakini tukiwa macho, hayo mambo yote yatapotea. (*Kicheko*)

Nina uchungu sana na suala la kilimo na nimelisemea kwa sababu Rais wetu alivyokuwa anazungumza katika Mkutano wa *SADC* alizungumza akatoa mapendekezo katika Kikao hicho kwamba tutenge ndani ya Bajeti yetu asilimia 10 iingie kwenye kilimo. Sasa sifahamu alikuwa anamwambia nani. Yeye alikuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa *SADC*, sasa sijui alikuwa anawaambia nani na makubaliano hayo yatakekelezwa na nani na nimeunga mkono hiyo hoja kwamba kweli asilimia kumi ya Bajeti yetu iingie kwenye kilimo, lakini alikuwa anamwambia nani? Kwa nini tusitekeleze sisi ikawa ni mfano kwa hizi nchi nyingine ambazo ni za *SADC*? Tuseme sasa hapa kama alivyotekeleza Rais wetu kwamba sasa asilimia 30 watakuwa Wanawake ndani ya Bunge na amelitekeleza hilo. Sasa na hili kwa kuwa ni yeye, amesema hii asilimia kumi ya kuingia kwenye kilimo ndani ya Bajeti yetu sasa tunaanza Tanzania kuonyesha mfano na nyie wengine mfuate.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kinachotuumiza sisi katika Afrika ni umasikini na huu umasikini ni lazima tukubaliane kwamba ni wa kujitakia. Ni kitu gani

tumekosa Afrika? Ardhi tunayo, maji tunayo, Maliasili dhahabu tunayo, almasi na tanzanite, huko Kongo wanapigana vita kumbe ni almasi wanaiba. Sasa tusipokuwa kitu kimoja Kongo watakuwa peke yake, Tanzania itakuwa peke yake, tutakuwa masikini, tutaendelea kudhalilika na kudharauliwa. Ndiyo sababu nilisimama hapa nikasema kwamba, kutokana na Ripoti ya Afrika kwamba, jangwa sasa hivi kutoka kwenye asilimia 20 ya jangwa ndani ya Afrika, sasa hivi wametangaza kwamba jangwa ndani ya Afrika limeshakaribia asilimia 40. Sasa tusipokuwa kitu kimoja tukawa sambamba, mwisho Afrika yote itakuwa jangwa pamoja na hali nzuri ya maji tuliyonayo. Lakini tukiwa kitu kimoja, kwa mfano, Misri walisema wako tayari kuleta wataalam wa maji kwa Tanzania kuja kuelimisha namna ya kutumia maji yetu vizuri zaidi. Walisema wako tayari. Lakini vilevile Rais Gadafi wa Libya, aliwahi kusema kwamba yuko tayari kujenga Bunge la Afrika kwa pesa zake. Sasa nayo hiyo sijui kama Waziri hakuipata, kama ameipata, wazo hilo limefikia wapi? Kwa sababu sikusikia akijibowi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi kubwa sana katika Afrika, kwa mfano, *South Africa* inatusaidia sasa hivi, tumekubaliana. Tusiogope kusaidiwa na hizi nyingine. Hapa katikati sijui kuna balaa gani? Misri ni Kaskazini, wako tayari kutusaidia na sisi hapa katikati tuwe ngangari tujisaidie na sisi wenyewe. Afrika itakuwa kitu kimoja na tunaweza sasa tukaendelea na hawa wakubwa wakatuogopa. Leo wana-determine price ya korosho, kahawa na bei ya mazao yetu. Lakini tukiwa kitu kimoja kama wataalam walivyosema, mtakapokuwa na sauti moja Afrika, ndipo mnawenza kufanya jambo na wenzenu wakawaogopa. Basi, niseme kwamba hilo la kuweka hali yetu iwe kitu kimoja, basi liungwe mkono katika misingi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, narudia kumwomba Waziri na Wizara hii achukue jukumu la kuangalia Balozi zake zote kama ilivyoangalia Balozi ya Misri na kuangalia mambo yanayohusu Afrika na vile vile umahiri wa Waziri auendeleze, kwani nafasi yake ni nafasi kubwa sana, hata Rais Mkapa alikuwa ni Waziri wa Mambo ya Nje, leo amekuwa Rais. Kwa hiyo nafasi aliyokuwa nayo ni ya Kimataifa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. CHIFU ABDALLAH S. FUNDIKIRA: *When Honourable Thomas Ngawaiya was speaking he referred to the President of Libya as Hayati which is incorrect. I don't think we should allow that to go into Hansard. He is still alive. (Laughter)*

NAIBU SPIKA: *Honourable Thomas Ngawaiya, could you clarify on this? May be you got news this morning.*

MHE. THOMAS NGAWAIYA: *Okay, let me clarify this. I didn't say that he is dead. I said Nkhurumah and Nyerere, but Mwamar Gadaf, I just mention that he is the one... No, I couldn't say.*

NAIBU SPIKA: Honourable Chief Abdallah Fundikira, I heard what he says. He said he is alive but the other two were not alive. May be you didn't pick your point correctly. (Applause)

MHE. OMAR S. CHUBI: Mmenikoroga kweli kweli! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kusema machache juu ya hoja hii. Pamoja na kwamba kuna mtafaruku umeniingia kwenye ubongo, lakini nitajitahidi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda na mimi niwaunge mkono wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi wanayoifanya ambayo imeweka Tanzania katika nafasi nzuri kwenye Jumuiya ya Kimataifa. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, aendelee na hali hiyo ili na sisi tuweze kujulikana.

Nikienda kwenye hoja, nataka kidogo nipate maelezo kutoka kwa Maafisa wa Wizara, matumizi ya ukumbi wa watu mashuhuri pale Uwanja wa Kimataifa Dar es Salaam. Hivi karibuni kumetokea *circular* kwamba, viongozi wanaotumia ule Ukumbi hawaruhusiwi kuwasindikiza watoto wao au kuwapokelea. Lakini wakati wa kusafiri, viongozi wanaposafiri na watoto, watoto watumie *ordinary lounge*, mke na mume watumie *VIP lounge*. Hiki ni kitendawili, nafikiri ni vizuri tuwekane sawa. Labda iwe specified kwamba, viongozi kadhaa ndio watumie na wengine wa *level* kadhaa ndio wasitumie. Kwa sababu mpaka sasa bado wakubwa wanatumia ule uwanja kwa madhumuni hayo ya kuwapokea na kuwasindikiza watoto wao. Kwa hiyo, hilo nafikiri tungewekana sawa.

La pili, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, afanye kila linalowezekana kabla Bunge hili halijamalizika ili kutuwezesha kujua masuala ya Kimataifa, kwa mfano, masuala ya kiprotokali. Suala la posho haliwezi kuzingatiwa, tunachozungumza, tuelenze ni jinsi gani watu wanapokwenda kwenye Mikutano ya Kimataifa waweze kuambatana na hali hiyo. Kwa sababu mimi nataka niseme tu ukweli, nilikwenda kwenye Kikao kimoja nilipata ngekewa, *High Level Ministerial Conference on Aviation Security Montreal Canada* ilikuwa tarehe 19 - 21 Februari, 2002. *Ile Conference procedure* kwa kweli unamaliza wenzako wanafunga Kikao wewe hata huelewi unakwenda wapi. Sasa haya masuala yanatisha. Sasa ukiwa mwenzangu mimi unatoka mahali kama nilipotoka wakakupachika kwenye hiyo *delegation*, ukienda kule hata ukirudi huwezi kutoa ripoti. Sasa tungeomba tuelenze, maana yake Waziri ameja na mambo yote ya duniani, sasa na sisi akitumwagia kidogo yatatusaidia. Hayo mambo ya kutuwezesha watu wana wasiwasi, mimi sioni kama ni suala la msingi. Kwa hiyo, ningeiomba Waziri angefanya utaratibu huo ili na sisi tuweze kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimebobea kwenye masuala ya kidiplomasia, Membe ndio kabisa mwenzangu amefanikiwa kupata hata Bodi, mimi Ubunge unakwisha sina hata Bodi moja. Lakini Bodi yangu ni mimi mwenyewe na nina moja ile ya International Public Relation Association London, nakwenda kwa mwaka mara moja na Bodi ya familia yangu. Namshukuru Mungu kwa kunijalia hilo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo linaniuma, Mheshimiwa Waziri amesema tutumie fursa kama ile ya *AGOA*, ambayo tumeongezewa muda mpaka mwaka 2015. Lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri, wale waambata wa kiabiashara kwenye Balozi zetu watusaidie kutuletea orodha ya sasa hivi ya bidhaa zinazohitajika kule kwa sababu hizi anuanza za kwenye *E-Mail* nyingi ni *fake*. Wengine wamekufa, unapoteza kama shilingi laki tatu kwa *communication* lakini unaambiwa yule mtu labda amekufa au alifungwa. Kwa hiyo, tunaomba hasa Ubalozi wa Japan tunapoelekea kwenye Uchaguzi, tunaweza kujianaa vizuri kama tunaweza kufanya biashara na Japan. Kwa hiyo, hilo tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atupigie ndogo ndogo tupate hiyo habari.

Suala la utalii kama alivyozungumza Mheshimiwa Ponsiano Nyami, sisi tatizo letu tuna Bajeti finyu. Wenzetu wa Kenya sidhani kama wamebadilisha lakini Alhamisi au Jumapili kuanzia saa 5.30 ya saa za kule London, wanaunguruma mpaka saa 6.30, *one hour* wanatangaza utalii. Sina uhakika kama waambata wetu walioko pale London kwa upande wa kutumia *BBC* wanafanya nini. Kama hali hiyo haipo basi, Mheshimiwa Waziri, ningombaa atufanyie maarifa ili na sisi utalii wetu ueleweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, wakati wa enzi ya Marehemu Mwalimu Julius Kambarage alipokuwa anasafiri, Marehemu alikuwa na tabia ya kwenda na Waziri wa Mambo ya Nje, *delegation* yake inaambatana na Wenyeiti wa Chama wa Mkoaa, Waheshimiwa Wabunge, bila kujali wa Kamati gani, lakini utamaduni huo kama upo siuelewi. Sijifagilii, maana hatujakuta watu wanaokwenda kwenye misafara kama hiyo na kama wapo, basi wangetangazwa na sisi tuwaalize wenzetu mmepata nini huko ili na sisi tuelewe kinachoendelea. Tunaomba basi tutazamwe inapokuwa kama suala linalokwenda kuzungumzwa na *delegation* ipo, basi *Foreign Minister* aweke watu wake kumi wakiwemo Wabunge, wanamsindikiza, akirudi wanakuja wote. Hiyo *culture* inafanyika dunia nzima! Kwa hiyo, naona hilo sio jambo la ajabu. Naomba Mheshimiwa Waziri, aliweke sawa sawa. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, sisi kama Waheshimiwa Wabunge, nisisitiza kwamba, kwa sababu *protocol is a ceremonial accepted rules which governs events*, bila kujua masuala ya protokoli tunaibika. Maana yake sisi wote tunasafiri, wengine kwa tiketi zetu, wengine kwa tiketi za Mheshimiwa William Lukuvi, lakini tunasema kwamba, kujua itifaki ni suala la muhimu sana na hilo linazingatiwa. Utakuta mambo mengine yanaborongwa, kabla mkubwa fulani hajasema mwingine amesharukia. Tumekwenda kwenye Mikutano kwa mfano, mwaka 2003, *CPA* Afrika Nairobi, tumejiweka mahali pabaya sana kwa sababu ya kutojua masuala ya kiitifikasi. Hili nalisisitiza kwa bidii zote kwamba, lazima tufanyiwe hivyo. (*Makofii*)

Halafu mwisho, kama Mwenzangu alivyopongeza baadhi za Balozi, mimi nataka kumpongeza Dr. Ben Moses. Ni Balozi mfano, kwa sababu wanapokuja viongozi kwa *level* kama sisi Wabunge, mimi nadhani wangetupokea Maofisa tu, lakini yeze alijitoa muhanga akaja kutupokea mwenyewe na tumeshirikiana naye kwenye Mikutano mpaka tumeondoka. Lakini sehemu nyingine unaweza ukalala hata siku tatu, nne, Balozi unamsikia tu kwa jina. Anakuja kama anasikia Mheshimiwa Rais anakuja au Makamu

wa Rais au Waziri Mkuu. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba, Mheshimiwa Balozi Ben na timu yake ni watu ambao wanastahili pongezi za dhati kabisa bila kutaka kusema maneno mengine. (*Makofsi*)

Halafu mwisho, nimpongeze ndugu yangu, Balozi Mchumo, kwa kuchukua nafasi ya Kimataifa. Mimi nampongeza kwa dhati lakini watu wengine watani zangu hawaelewi. Pia nampongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Waziri wa Biashara na Masoko, Mheshimiwa Thomas Ngasongwa, kwa kufanya kampeni ya nguvu kabisa mpaka kumwezesha Balozi akapata na Tanzania kuwa miiongoni mwa nchi ... (*Kicheko/Makofsi*)

Halafu wa mwisho nimpongeze ndugu yangu Balozi Cisco Ntiro, kwa nafasi aliyoipata ya *Chief Protocol*. Kiutawala ile ni nafasi kubwa hapa duniani. Namwombea Mwenyezi Mungu, amwendeleze ili kesho na keshokutwa aweze kupanda. Kwa hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofsi*)

MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, sina budi kuwapongeza Mawaziri wote wawili, waliotuletea kitabu hiki kizuri kilichojaa mambo mengi, pia na wataalam wao wote kwa ujumla. Kwa hakika nina machache tu ya kuchangia na kwa vile naunga mkono hoja, kwa hiyo, nitakuwa sina mengi zaidi isipokuwa kuyaboresha baadhi ya mambo madogo madogo. (*Makofsi*)

La kwanza, nataka kuzungumza jambo ambalo sijui kama limepata ufumbuzi au bado, lakini silisikii. Tulikuwa na Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki ambayo imevunjika na sasa hivi tumeiunda nyingine, lakini wafanyakazi waliokuwa katika kipindi kile mpaka leo wanateseka, wamepewa Shilingi mia tano tano wamekataa. Lakini sasa hivi sijui nini kinaendelea kwa ajili ya wafanyakazi wale wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Namwomba Mheshimiwa Waziri, hili alifuatilie na alitolee uamuzi. Sio kisingizio kwamba, suala hili liko Mahakamani ikawa watu wanaohusika hawajui haki zao. Ni kweli kwa wakati huu sio vizuri kuwapa pesa za muda ule kwa sababu zilikuwa chache na zingefaa wakati ule lakini kwa sasa hivi lazima itazamwe ili wafaidike kwa sababu ni Watanzania tu ndio wamepata matatizo lakini nchi zetu mbili wamepata faida nzuri. Hilo ni la kwanza.

La pili hivi sasa katika dunia tumekuwa tukisikia habari za kijana mmoja yule aliyekamatwa Pakistan kuhusiana na mambo ya ugaidi. Sijui Serikali yetu inafuatilia vipi kuhusu kijana yule. Hofu yangu ni kwamba, kijana yule hayuko peke yake, hiyo sio siri. Wako wengi ambao wamekwenda kupata mafunzo kama yale ya ugaidi. Nia yao kwa kweli sio siri, tunapokaribia katika shughuli nzito na wataanza kurudi na kutuletea matatizo. Sijui Serikali kwa hili wameliangalia vipi. Yule aliyekwisha kamatwa nini usemi wa Serikali na wale vijana ambao bado wapo wengi nje? Lengo lao karibu na uchaguzi watarudi na kwa bahati nzuri au bahati mbaya, jana katika kuchangia Serikali imeombwa kwamba, Majeshi yasioneokane uwanjani wakati wa Uchaguzi. Kwa hiyo, naomba Serikali hilo waliangalie ili tusipate matatizo wakati wa Uchaguzi.

Jambo lingine ambalo nataka kulichangia ni kwamba, sasa hivi kuna vijana wa Tanzania wengi sana wapo Uingereza, wako na Afrika ya Kusini. Kwa kweli Uingereza sijakwenda kama rafiki yangu, Mheshimiwa Omar Chubi, lakini Afrika ya Kusini nimekwenda nimewakuta vijana wa Kitanzania wana dhiki kubwa sana hata hawawezi kupata chakula chao. Wako kule, wanahangaika, ukitua wewe Mtanzania ndio wanakuvalamia ili uwasaidie wapate kuishi. Serikali hili wameliangalia vipi? Serikali inajua?

Kama hawajui hiyo ni taarifa, tafadhali hilo lifuatilieni ikiwezekana wale vijana wetu warudi, wasikae katika hali ambayo inasikitisha kule.

Jambo lingine ni kwamba kuna Watanzania hasa wa upande mwingine kule, wengi wamekimbia kule wanaita kujilipua, wako Uingereza. Kwa kweli hatujui hatima yao, maana siku unaskia kwamba wengine wamekamatwa, wamefungwa au wanataka kupelekwa Mahakamani. Serikali na Serikali wanafanya nini kuhusu vijana wale ambao wako wengi kule kwamba wana tabu, wengine wanasema wanakwenda kutafuta maisha. Si vibaya ikiwa watakwenda kwa utaratibu mzuri.

Lakini utaratibu walioendea, wanasema wenyewe wa kujilipua. Wakifika kule wanajigeuza kuwa Wasomali, bahati yule mtu anayefanyia usaili sijui Msomali na anaweza kuwa Mwingereza. Hajui Kiarabu, hajui lugha ya kwetu, akifika pale anaulizwa wewe Msomali, anasema mimi Msomali. Hebu sema Kisomali, anasoma *Kulhuwa Allahu*. (*Kicheko/Makofsi*)

Sasa yule hajui anaona hii ni lugha, hajui kwamba ile ni matatizo makubwa sana kwa vijana wale. Hebu Mheshimiwa Waziri, vipi kuhusu vijana hawa ambao kwa kweli wanatuabisha, kwa sababu Tanzania hakuna matatizo hayo yanayosemwa.

Jambo lingine ambalo nahitaji kulichangia ni hili, sasa mambo mazuri, tunaona baadhi yake yanayohusu Muungano yanatengenezwa. Tunaomba yazidi kutengenezwa. Lakini kutokana na hadhi ya Ofisi yako mambo ya nje na uhusiano wa kimataifa, kule upande wa pili hakuna Ofisi. Bunge wameanza kujenga Ofisi na Ofisi ya Makamu wa Rais inajengwa na wewe tafadhali jitahidi upate mahali ujenge Ofisi. Unapoingia wewe na tai yako hiyo kama unavyopendeza hivyo, ijulikane hiyo Ofisi yako. Usiache ile nyumba iliyokuwa inatumiwa na kiongozi wa *HIZBU* kama watu hawajui, nyumba ile kiongozi Ali Musibu, ndiyo alikuwa anakaa katika nyumba ile ambayo sasa ni Ofisi yako, haileti sifa nzuri. Ijengwe nyumba ambayo italingana na hadhi ya nchi yetu, ili watakapokuja wageni Sheikh Abdulkader Shareef, anavyowapeleka ajue hapa ni Zanzibar. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu uwiano wa wafanyakazi wa Jumuia ya Afrika Mashiriki. Hivi nchi zetu zimeungana ni jambo zuri, tunaomba liendelee. Lakini Tanzania bahati ina sehemu mbili. Ina sehemu ya Zanzibar na ina sehemu ya Tanzania Bara. Wanapiga kelele mimi sijaweza kuangalia, wanapiga kelele kwamba kwa upande wa pili hakuna mtumishi kutoka Zanzibar hakuna. Kwa hiyo, hili tulifute mapema apelekwe mtumishi. Nafasi imeshapatikana. Mwenzetu

Mheshimiwa Omar Chubi, keshatoka, maana yake wasiwasi wake umeshamwondoka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yule bwana ameshapata kazi nje. Sasa hatuombi, tunasema ni kuchangia tu na kutoa fikra kwamba nafasi ile hebu mtafuteni kijana kutoka upande wa pili, ashike nafasi ile, wapo wasomi wanaoweza ku-*maintain* nafasi ili apewe nafasi ile, ili haya maneno madogo madogo yaondoke, ili turekebishe zile kero za muungano. Kwa kweli ukifanya hivyo, itakuwa tena maneno hapa kwamba Jumuiya ya Afrika Mashiriki hatumo. Nini uwiano wa upande wa pili, kumbe nia ipo na uwezo upo. Hebu tusaidie hilo. Tafuta kijana mzuri ambaye ana uwezo lakini awe CCM. Ni lazima, sharti moja liwe ni hilo.

Narudia Mheshimiwa Waziri kuptitia kwa Mheshimiwa Naibu Spika, mchague kijana mwenye elimu, mwenye uwezo, mwenye shahada na sifa ya mwisho awe lazima ni CCM, sio vibaya, ni lazima, siwezi kuogopa kusema hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nia yangu ni kumtahadharisha Mheshimiwa Waziri kwamba wako vijana wetu wanapata shida huko nje, Uingereza wanapata shida na Afrika Kusini wanapata shida kubwa sana hata na Ugiriki wako wanapata shida kabisa, wanalala katika mapipa, chakula chao cha dhiki, na hali kwetu salama usalimini, hakuna matatizo. Tunatembea mpaka usiku, tunalala kwenye *disco*, tuna kila kitu hatuna tatizo. Kwa hiyo, uwarudishe wale huku kwetu ikiwa wanaendelea kupata dhiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. NJELU E. M. KASAKA: Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Nina mambo kama matatu tu madogo ambayo nitayachangia hapa. Lakini kabla sjafanya hivyo ningependa na mimi kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki, ambaye alifariki hapa Bungeni mwezi uliopita na pia nitoe rambirambi kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyengo, ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu kutoka Mkoani kwetu Mbeya. Namwomba Mwenyezi Mungu azipokee roho zao na kuzihifadhi mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ningependa nichukue pia nafasi hii kumpongeza Balozi Ali Mchumo, kwa kupewa nafasi aliyoipata katika Shirika moja maarufu sana hapa duniani ambako yeye amepata nafasi hiyo.

Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuiwakilisha nchi yetu katika masuala ya nchi za nje. Wameifanya kazi nzuri ambayo inatuletea sifa, wanatuwakilisha vizuri na kwa kweli tunaenda vizuri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo matatu ambayo nitayachangia, la kwanza katika hotuba yake amezungumzia matatizo mengi ambayo yanayolikabili Bara la Afrika,

Kongo, Rwanda, Burundi na wapi ambako kuna matatizo. Lakini nataka nizungumzie suala la Daful kule Sudan. Kwa kweli sio mgogoro ule wa kawaida kama unavyofahamu kwamba Kongo wanapigana na makundi, wenyewe kwa wenyewe au kama wanavyopigana Burundi wenyewe kwa wenyewe. Hapa kuna tatizo la msingi ambalo inaonekana Wasudan wenyewe asili ya Kiarabu wakisaidiwa na Serikali wanawaua Wasudani walio weusi, naweza kusema hivyo, wanauwa walio weusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inachukua sura tofauti na migogoro mingine tunayoifahamu katika Bara la Afrika. Hapa kuna *race* moja inaondoa *race* nyingine ndani ya nchi yao mle na kwa bahati mbaya sana kwa taarifa zote tunazopata ni kwamba hawa *Janjaweed Militia* wanasaidiwa na Serikali.

Hata baada ya kutolewa taarifa kwamba Serikali ya Sudan ichukue hatua na kwamba kama itakubali na kwamba yenyewe haishiriki lakini taarifa zimeendelea kuonyesha kwamba bado wale *Janjaweed Militia*, wanasaidiwa na Serikali pia na kupewa silaha. Magazeti yameonyesha kwamba hata wale wananchi walipokwenda kutoa taarifa kwenye Vituo vya Polisi, Polisi wa Serikali hawasaidii chochote, hawajibu, wahaendi kusaidia kuwakinga wale wananchi wa sehemu zile na taarifa zilizopo ni kwamba tayari karibu watu 50,000 wameshauawa na katika makambi yale ya wakimbizi wanasema karibu watu 40 wanakufa kila wiki.

Sasa najiuliza na mimi ningependa nijue Serikali za Kiafrika linalichukuliaje suala hili? Wanauchukulia kama ni mgogoro wa kawaida au ni mgogoro maalum ambao unahitaji *attention* kwa nchi za Kiafrika? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishasoma katika historia kwamba watu weupe walipofika Australia na New Zealand walifanya kazi ya kutaka kuwaondoa watu weusi kabisa wanaoishi New Zealand ambao wanaitwa Aborigins pamoja Gulamaoli wa New Zealand na Australia, Aborigins wa Australia na Maori wa New Zealand. Tunazo taarifa pia kwamba kulikuwa na mauaji ya namna hiyo katika nchi za Amerika ya Kaskazini na Amerika ya Kusini watu wetu walipokwenda huko. Haya yapo katika historia.

Sasa nashangaa yanatokea katika enzi zetu wakati ambapo na nchi za Kiafrika zilishapata Uhuru na jambo kama hili tunanyamaza. Tunachukulia ni mgogoro wa kawaida. Kwa hili tunafanya kosa kubwa sana katika nchi za Kiafrika. Walichukulie suala hili kama ni tatizo maalum ambalo linahitaji mkakati maalum na ushirikiano wa nchi zetu za Kiafrika na kuiambia Serikali ya Sudan kwamba kinachofanyika pale ni kibaya wakisimamishe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusione aibu kuwaambia wenzetu, Serikali ya Sudan kwamba kinachofanyika ni kibaya hakipaswi kuendelea na tuonyeshe wazi nchi za Kiafrika zionyeshe wazi kwamba zinachukizwa na kitendo cha kikundi kimoja ambacho kimegawanya kwa misingi ya rangi, kinaua watu weusi na Serikali yetu ya Tanzania ambayo imekuwa mstari wa mbele katika masuala mengi siku za nyuma za kusimamia haki na kutetea haki za wanyonge sasa hili ni moja ya masuala ambayo yapo mbele yetu

ni vizuri sisi kama Watanzania tukawa na msimamo au na taarifa na kauli maalum kuonyesha kwamba hatukubaliani na vitendo vya namna hiyo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka nilizungumzie linahusu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki zamani tulikuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipozinduliwa mwaka 1967 pale Arusha nchi nyingi waliomba uanachama, licha ya nchi zetu hizi tatu za Afrika Mashariki pia nchi nyingine kama vile Somalia na Sudan na Rwanda pamoja na Ethiopia wakati ule waliomba kuwa wanachama. Lakini tukaweka vikwazo vingi vya kuwachelewesha kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa karibu miaka 10 tulibaki peke yetu nchi tatu hizi, Kenya, Uganda na Tanzania. Matokeo yake tulipokuja kugombana sisi wenyewe katika Afrika Mashariki ikawa rahisi sana kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvunjika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi au nina matumaini kwamba kama Somalia, Ethiopia na nchi zote ambazo zilikuwa zimeomba uanachama wangekuwa ni wanachama wakati ule ugomvi kati ya Uganda na Tanzania peke usingesababisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvunjika. Sasa tulipoianzisha upya hivi karibuni nchi ya Rwanda waliomba, Burundi waliomba kuwa wanachama. Ni vizuri nashukuru kwamba tumeweka masharti ya kujiunga, mojawapo ikiwa ni kuzingatia masuala ya utawala bora na demokrasia katika nchi inayotaka kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki, jambo zuri sana na mimi naliunga mkono.

Sasa nchi ya Rwanda imeomba wamesharudisha amani ya kutosha katika nchi yao na sasa hivi wameshafanya uchaguzi, wana Bunge lililochaguliwa na wana Rais aliyechanguliwa. Nilikuwa nafikiri ni wakati muafaka kuanza kufikiria maombi ya nchi kama hizo. Rwanda waliomba, sisi tulikwenda mwaka 2003, Spika aliongoza ujumbe, tulikwenda Rwanda na moja ya ombi lao kubwa ilikuwa ni kwamba wanaomba waruhusiwe kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki na inazekana kabisa kuwaingiza katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inaweza kuwa ni kigezo kimojawapo ya kupunguza migogoro ndani ya nchi zao ambayo inatokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapojiunga katika Jumuiya kubwa zaidi ambayo ina masharti yake ya kuwa mwanachama wake inabidi uyatekeleze masharti yake na kwa maana hiyo, unaleta amani na utulivu ndani ya nchi hizo. Naamini kabisa nchi ya Rwanda wakiwa katika Jumuiya ambayo ni jumuiya ambayo ni kubwa zaidi kuliko walivyo katika nchi yao ndogo inawezekana kabisa ikawasaidia kudumisha amani ambayo wameanza kuipata sasa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuwatenga inawezekana ni kama ni chanzo cha kusababisha waingie kwenye migogoro na vurugu ambazo wanajaribu kuziepuka ambazo na sisi wote tungependa zisiwepo kwa sababu nchi majirani inapokuwa kwenye matatizo na sisi tunapata matatizo makubwa. Kabla ya amani haijarudi Rwanda tulikuwa na wakimbizi wengi kutoka Rwanda hapa. Tunashukuru sasa amani imepatikana na wakimbizi hao sasa wamesharudi makwao.

Leo iko migogoro kule Burundi, tunao wakimbizi wengi hapa kutoka Burundi, Mikoa ya Kagera na Mkoa wa Kigoma wanabeba mzigo mzito wa wakimbizi kutokana na vurugu zinazotokea ndani ya nchi ya Burundi. Kwa hiyo, ni vizuri sana tukaanza kuangalia masharti yetu pale wanapotimiza masharti yanayotakiwa basi tuwa-*admit* moja ni kama nchi ya Rwanda tungefikiria kui-*admit* katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kama vigezo ambavyo viliwekwa mojawapo ikiwa ni utawala bora na uchaguzi Serikali iliyochaguliwa kiraia sasa wana Serikali kama hiyo.

Jambo la tatu, hili linahusu mambo ya ndani ya Wizara yenewe. Kulikuwa na malalamiko hivi karibuni yalitokea kwenye ripoti ya *Auditor General* na vyombo vyahabari vikaandika andika hapa kwamba kuna mgogoro wa ununuzi wa nyumba ya ununuzi Italia, kule Roma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huu ultokana na kwamba waliomba fedha kama *Euro* milioni tatu wanunue nyumba ya Ubalozi. Lakini habari za kutoka huko zinasema kwamba ununuzi ule haukufanyika inavyopasa, haukufanyika vizuri una mgogoro. Zimetumika *Euro* milioni moja badala ya *Euro* milioni tatu, wanaauliza hizo milioni mbili ziko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemekana nyumba yenewe haina hati. Kwa nini lilifanyika hilo? Tunaambiwa pia kwamba *transaction* yaani taratibu za manunuzi hizo hazikufanyika, yaani hakuna risiti. Leo ni wakati muafaka kwa Wizara hii kuondoa kile kiwingu ambacho kimetanda kwenye suala hili. Mtuondoe wasiwasi, nini kimefanyika katika ununuzi wa nyumba ya Balozi Roma. Ni kweli hela zimetumika vibaya, ni kweli manunuzi hayakufanyika inavyotakiwa? Ni kweli hiyo nyumba haina hati?

Mheshimiwa Naibu Spika, tungependa Mheshimiwa Waziri alifafanue hili kwa faida yetu sisi wote na kwa faida ya Wizara yenewe. Ni vizuri masuala kama haya yanapojitokeza Serikali itaje wazi wazi, kwa sababu hata Mkaguzi alitia mashaka, Mkaguzi Mkuu wa Serikali alitilia mashaka *transaction* hii na alipajaribu kuhojiwa na Waandishi wa Habari yeche aliitioa akasema kwamba siyo suala lake kulizingumza kwenye vyombo vyahabari ambayo nakubaliana naye ni sahihi. Siyo kazi yake kuzungumza kwa kuititia vyombo vyahabari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa nadhani ni mahali pazuri sasa kutumia nafasi hii kuweza kulieleza hilo kwa uzuri zaidi na kuepusha mambo mengine yanayofanana na hilo. Tungependa sisi, najua Balozi zetu nyingi zinazo matatizo ya majengo, wamekuwa na matatizo ya Ofisi katika sehemu mbalimbali. Hiki kitendo cha kutenga fedha na kuanza kununua nyumba za mabaloz kwa ajili ya ubalozi wetu ni kitendo kizuri ambacho tunakiunga mkono. (*Makofî*)

Lakini tungependa mambo kama yanavyofanyika yafanyike katika hali ya uwazi na ukweli na pia yafanyike kwa hali ya kuepuka ama ubadhifuru au ujanja ujanja wa aina nyingine yoyote ambayo inaweza kusababisha kuleta hasara kwa Serikali kutokana na vitendo vyahabari ya watumishi wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipenda nizungumzie haya matatu ambayo natumaini Waziri atakapokuwa anamalizia ana-*summarize* Wizara yake basi atapata muda wa kuyatolea maelezo. Lakini lile la kwanza kwa kweli ni vizuri sana nchi za Kiafrika zisione aibu, hili suala la kuoneana aibu ndani, kwa sababu tu nasema ni mambo ya ndani, mambo ya ndani yanapovuka mipaka lazima tukatae.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Umoja wa Nchi za Kiafrika wa sasa *African Union (AU)* ya sasa imelikataa hilo kwa sababu kwamba mambo mengine yaachiwe ndani, kusema ni mambo ya ndani kama yakivuka mipaka tunasema hapana hilo limezidi siyo mambo ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, liletwe linatuhusu sisi wote na kwa kweli katika hili suala Daful katika Sudan sio suala la nchi moja tena. Tulione ni suala la nchi zetu sisi sote na tulilaani kwa sura ambayo litakujanayo tulilaani na tusilikubali kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naiba Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge muda wa kipindi hiki cha asubuhi umeishia hapo. Lakini kabla sijasitisha shughuli za Bunge, ningependa tutakapokutana tena jioni ataanzia Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, kwa dakika zake tano. Halafu hapo nitawataka watoa hoja Mheshimiwa Naibu Waziri uanze kujibu hoja wakati huo.

Baada ya maelezo haya sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie Wizara hii muhimu kwa Taifa letu na nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na nataka nimthibitishie kwamba naiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndio kioo cha Taifa letu nje ya nchi yetu hii ya Tanzania, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu hotuba yake *im-cover* maeneo yote ambayo kwa kweli yaliwajibika kuweza kufahamika na Watanzania. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia nataka nitoe pole kwa Mheshimiwa Rais kwa *operation* ya pili aliyofanyiwa na namwombea dua Mwenyezi Mungu amjalie apone. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuwapongeze Madaktari kwa kweli waliochukua juhudhi ya kuweza kumhudumia Mheshimiwa Rais wetu na matumaini yanayonekana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumza, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo ambayo ameyatoa kupitia hotuba yake juu ya yule Mtanzania mwenzetu ambaye aliaithirika na kile kitendo cha kubakwa.

Kwa kweli tukio lile liliwasikitisha Watanzania wengi na kwa kupitia vyombo vya habari tuliwaona wengi sana waliokuwa wanalisikitikia lile tendo na kulaani. Pamoja na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri, yamekatisha tamaa lakini tunashukuru kwamba ametwambia atalipwa fidia na Ubalizi ule wa Saudi Arabia. Lakini naitaka Serikali pamoja na vipingamizi vizito vilivyokuwepo ambavyo vinatukinga kwamba hatuwezi kumshtaki yule Afisa Ubalizi wa Saudi Arabia, lakini tuangalie hii fidia isije kuwa ni kifuta jasho. Lile tukio ni kubwa, kwa kweli yule Mtanzania mwenzetu kabaki hana la kufanya tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikinukuu Chama chetu asisi cha *TANU* kinasema kwamba: “Malengo makuu ya *TANU* yalikuwa ni kukataa fedheha na kutawaliwa.” Mtanzania mwenzetu huyu amekumbana na fedheha kubwa sana. Tunaamini kwamba magazeti karibu yote ya nchi hii yameandika *story* ile na tunaamini taarifa hizi inawezekana zipo mpaka Saudi Arabia na Mataifa mengine ambayo yanafuatilia.

Kwa hiyo, Serikali iweze kumsaidia sana kijana huyu, isiwe apewe kifuta jasho bali aweze kupewa fidia ambayo itamwendeshea maisha yake. Vile vile niwatake wasomi wetu nchini na wanasheria waweze kumsaidia kwa yale maeneo ambayo yatawezekana kwamba aweze kupata haki inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kuchangia kwa kweli nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Katika ukurasa wa 64 Mheshimiwa Waziri ametwambia, uhusiano na ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine katika mabara na dunia ni mzuri. Nathibitisha kwamba ni sahihi.

Mheshimiwa Waziri akaendelea kusema kwamba ushirikiano huo na Mataifa ni mkubwa na tunaona kuna uhusiano mkubwa na Mataifa yote makubwa ya dunia na nchi zote wahisani na mashirika yale ya fedha. Kwa hiyo, kama ingekuwa Wizara hii haikuwa na uwezo mkubwa wa kuweza kusimamia majukumu yake, kwa kweli tungefeli kama Taifa. Kwa hiyo, nataka kuthibitisha kwamba namuunga mkono Mheshimiwa Waziri juu ya suala hili ambalo kwa kweli amelizungumzia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Waziri ameelezea kuhusu Umoja wa Afrika. Kwanza nachukua nafasi hii kuupongeza Umoja wa Afrika kwa kukubali kwamba lugha ya Kiswahili iwe ni moja katika lugha sita ambazo zinatumika katika Umoja huo. Mimi nilikuwa nashangaa sana baadhi ya wasomi wanapokataa kwamba Kiswahili hakiwezi kutumika, mimi nakataa sana na nina vigezo, lakini

tunashukuru wenzetu wa Chuo Kikuu, kitu hiki wamekiona. Sasa kama baadhi ya wasomi wa Chuo Kikuu wamekubali, viyi wengine watakuwa wanapinga? Tusiangalie maslahi ya binafsi bali tuaangalie maslahi ya Taifa.

Waafrika wamejua siri moja kubwa ya Tanzania kufanikiwa kuwa na umoja ni lugha ya Kiswahili ambayo inazungumzwa nchi nzima. Hivi karibuni sisi tukizungumza na ule ujumbe kutoka Kenya wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ulinzi na Usalama walituthibitishia kwamba sasa hivi wana sera maalum katika shule za msingi juu ya kufundisha lugha ya Kiswahili na wanafundisha mpaka katika vyuo vyao vikuu.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashangaa, lakini tunaushukuru Umoja wa Afrika kwamba wamekubali kuitumia lugha ya Kiswahili kuwa ni moja kati ya lugha sita. Mimi nilikuwa najua kuwa itafika mahali watakiri kwa sababu Umoja wa Afrika sasa hivi wamekubali na wamekiri kwamba Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kwamba ni kiongozi aliyekuwa muhimu kwa Bara hili la Afrika na tunaambiwa kama njia moja ya kumuenzi Mwalimu ni kufuata ule ushauri wake na Mwalimu ndiye alitangaza kwamba Kiswahili ndio lugha ya Taifa la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu lingine nilimsikia Waziri wa Mawasiliano wa Libya akilaumu kile kikao cha Mawaziri wa Shirika la Reli kilichofanyika hapa Tanzania kwamba *speech* ya Tanzania ilisomwa kwa Kiingereza. Yeye alitumaini kwamba hotuba ile ya Waziri wetu wa Tanzania ingesomwa kwa Kiswahili na Libya wanasomesha katika Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia suala hili mpaka lugha yetu ya Kiswahili ikaingia katika Bara la Afrika. Nami nataka nimhakikishie kwamba kwa matumaini makubwa sasa Afrika inaweza ikaendelea kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu naamini mawasiliano yakiwa ya pamoja tutaweza kuelewana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie katika ukurasa wa 47. Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la ugaidi, nataka nimpongeze sana kuliingiza katika hotuba yake. Amesema katika hotuba yake kwamba ugaidi bado ni tishio kubwa kwa amani na usalama wa dunia, hata katika taarifa ya habari ya saa saba nilisikia katika Sauti ya Ujerumanu suala hili wamelizungumza hivyo. Vile vile katika taarifa ya habari ya *Radio One* wamem-quote Rais George Bush amekiri kwamba sasa hivi ugaidi ni hatari kubwa sana kwa Taifa lake la Marekani.

Kwa hiyo, tunauona uzito wa suala hili. Lakini mbali ya hapo mimi nataka nije pale ambapo kwa kweli linanisikitisha kidogo. Mheshimiwa Waziri anasema matukio ya kigaidi yameendelea kutikisa sehemu mbalimbali za dunia na kusababisha kuongezeka kwa hofu mionganoni mwa watu. Hebu tuaangalie yalitokatoka viyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini matatizo yote ya ugaidi haya inasemekana kwamba Mataifa yote makubwa yaliulea ugaidi kwa muda wa miaka mingi sana na madhara haya yote tunayoyapata ni kutokana na Mataifa makubwa kutokuwa wakweli, walipanda mambo ambayo sasa hivi yanaathiri dunia.

Kwa hiyo, sasa hivi ipo haja kwa Taifa letu, kwa Bara la Afrika na Umoja wa Mataifa kuangalia namna gani wataweza kulizima suala hili, si kutumia nguvu. Wakae, wazungumze, waweze kupata *solution* ya kusaidia dunia, vinginevyo kama tutakwenda hivyo wanavyokwenda Marekani hatutofika. Wao wenyewe sasa hivi wanatafuta *solution* ya namna gani watajikwamua. Kwa hiyo, hili nataka Mheshimiwa Waziri popote atakapokaa, ajaribu kuwasaidia wenzetu kuwapa maelekezo ni namna gani tutaondoa tatizo la ugaidi katika dunia, sio kwa kutumia nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo kwa kweli ndilo nililokusudia hapa kulizungumza. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie sana. Ninukuu gazeti la Majira mwishoni mwa mwezi uliopita, simlaumu Mwandishi wa Habari, kama kuna mtu ambaye anawaheshimu Waandishi wa Habari ni mimi pamoja na walimu wote ambao wanatoa elimu yao mashulenii na maeneo mengine yote. Hawa ni watu muhimu sana na mara nydingi sana ninapozungumza, nazungumza kwamba nchi yoyote kama itakuwa na Waandishi wa Habari na Walimu inaweza ikafikia maendeleo iliyokusudia na kama tulivyosema katika Ibara ya 18 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba mwananchi yejete anayo haki ya kupata habari na mfano sahihi *Radio Tanzania* inarusha habari mbalimbali, watu wanajua tu Bunge linavyoendelea na wananchi wanajua nini Wabunge wao wanafanya. Kwa hiyo umuhimu wa habari naujua, sitaki nimlaumu Mwandishi huyu, lakini amesema nini.

Amesema kwamba: “Mtanzania gaidi mbaroni Pakistan, Mtanzania mwenye asili ya Kisiwa cha Pemba bwana Ahmed Khalifan Khairan, ametajwa kuwa mtuhumiwa muhimu wa mlipuko wa mabomu katika ofisi za Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania na Kenya mwaka 1998.” Imenistua kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, gazeti lilishasema kwamba Mtanzania, sisi Pemba ni sehemu ya Tanzania, unatufananisha na Marekani. Masikitiko yangu ni ku-point kwamba Mtanzania mwenye asili ya Pemba, mnatusaliti na Marekani, ile nchi mbaya sana. (*Kicheko/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Unaogopa?

MHE. OMAR MJAKA ALI: No, siogopi nazungumza *serious* Mheshimiwa Naibu Spika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niishukuru *Radio Tanzania* usiku ule ule kupitia taarifa ya habari ya saa mbili ilisema kwamba nanukuu: “Serikali imethibitisha kuwa mtuhumiwa wa ugaidi aliyekamatwa Pakistan, Ahmed Khalifan Khairan ni Mtanzania aliyezaliwa Zanzibar mwaka 1974, huko Kiembe Samaki. Pia amesoma katika shule ya Vikokotoni na amesoma kidato cha tano katika shule ya Ufundji Mbweni.” Tuchukue ipi?

Kwa hiyo, ni vizuri mambo haya, tukachukua jukumu kama la Tanzania. Kama ni kupata lawama, tupate kama Watanzania. Mimi silalamiki kusema kwamba ni

Mtanzania mzaliwa wa Zanzibar, *okay*, tunajua kwamba Pemba na Unguja ni sawasawa. Lakini uki-point kwamba mwenye asili ya Pemba, mnatusaliti. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza uwazi kabisa, sifanyi masihara, tumemwona Marekani alivyoiumiza Iraaq, alivyowateketeza Wairaqq, ndio. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa hili.

MBUNGE FULANI: Asikubali kwamba ni Mzanzibar?

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikatai kama ni Mzanzibar, lakini ku-quote kwamba ni mzaliwa wa mahali fulani inatumiza na kwa kutumia hili naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongeza majeshi na vyombo vyaya usalama katika Kisiwa cha Pemba mara moja. Hii nasema kwa sababu ninaamini taarifa ambazo vyombo vyetu vimewasilisha Serikalini itatunusuru. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niki-quote vyombo vyaya habari vinasema kwamba kabla ya Muungano wetu Uingereza ilikuwa ivamie Zanzibar. Waandaaji wa mpango ule ambao waliuita *Zanzibar Action Plan (ZAP)* na walishaanzisha mgogoro ambaoungesababisha kupatiwa ufumbuzi kutokana na msaada wa kijeshi na pia ufumbuzi wa mgogoro ule ulishaamuliwa kwani waandaaji wa mpango huo walikwenda kuonana na Rais wa Kenya wakati ule na akaonyesha kukubali na wakazungumza kwamba yumkini Mwalimu Julius Nyerere na Milton Obote, wangekubaliana na mpango ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie Mwalimu alivyotuokoa sisi na inasemekana na maamuzi yake yalishafanywa kwamba Zanzibar ingegaiwa katika nchi moja ya Bara au zaidi *it means* Unguja ingekuja Bara na Pemba ingekwenda Kenya, *sure* kabisa. Huu mpango uliandaliwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri sasa Serikali kupitia tatizo hili ikaangalia vijana wote wa Kitanzania waliopo nje, kuona wanafanya nini na nani aliywapeleka, *intelligence* yetu sasa ifanye kazi, tupate jibu mapema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu kijana amekamatwa na silaha mbili *AK47*, kupitia taarifa ya habari ya leo ile *diskette* ya *computer* yake imeonyesha maeneo ambayo ingelipuliwa Marekani katika kipindi hiki. Ndio sauti ya Ujerumanî imetangaza. Amesimama kwa muda wa saa kumi na mbili yule kijana ndani ya nchi ya watu, saa kumi na mbili wamewazuia Pakistan. Kwa hiyo, suala la ugaidi lazima liwekewe nguvu ya pamoja ili kuwanusuru Watanzania wetu. Kwa bahati nzuri Naibu Waziri alikaa Ubalozi pale Uingereza, pale wapo wengi, sasa tunataka tujue wale vijana wanafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nalizungumza hili sio kama nafanya masihara, ni kujaribu kuweka umoja wa Taifa letu na naamini kwamba huyu kijana wa miaka thelathini hawezi kufika tu kule moja kwa moja, lazima aliandaliwa, lazima alipelekwa na kama alivyosema Mheshimiwa Abdulkader Shareef, hapa hayupo peke yake, wapo wengi sana. Tulipitisha mara moja hapa Muswada fulani kuhusu fedha ambazo ni, lakini

inawezekana siku hizi tunasema labda fedha haramu, lakini wenzetu wanazitumia pesa haramu kwa maeneo mengine.

Huyu kijana amekamatwa na fedha nyingi sana za kigeni ndani ya chumba chake. Kwa hiyo, kama Taifa, watu wa Wizara ya Mambo ya Nje lazima mwangalie Watanzania wanafanya nini kule nje, kama hawana kazi, warudishwe mara moja katika nchi hii, tuna ardhi kubwa waje walime hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili nalizungumza kwa dhati kabisa, lazima tuwasaidie Watanzania wetu, hatuwezi kuwaacha wakayumba katika dunia, wakaharibu sifa ya nchi yetu. Tushukuru Mashirika ya Kimataifa, Mtanzania yule kwa kweli kama ingekuwa ni ile Marekani ya zamani, sasa hivi tungakuwa hatuna misaada, tungelifumua mfumo mzima wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii ili nitoe pongezi zangu kwa Wizara hii kutokana na kazi nzuri inayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mambo mawili ambayo ni kero kwa Watanzania. Kwenye ukumbi wa watu mashuhuri (*VIP Lounge*), kumetokea tangazo kuwa watumiaji wa ukumbi huo hawaruhusiwi kutumia na watoto wao wakati wa safari. Baba na Mama watumie ukumbi huo, watoto wapite kwenye ukumbi wa kawaida. Hii maana yake nini? Mbona hadi leo viongozi, Mawaziri na Mabalozi bado wanawasindikiza na kuwapokea watoto wanaosoma nje? Endapo hoja hii imetokana na wachache wanaoutumia vibaya ukumbi huo, kwa nini tuadhibiwe wote katika suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la *Visa* za Uingereza na Marekani. Kumetokea matatizo mengi kiasi cha kufikia kudhalilishwa wakati wa kuomba *visa* ya nchi hizo. La kushangaza, raia wa nchi hizo hupata *visa* za chee watakapo *visa* hizo, ili watembee Tanzania na wengine hupewa *visa* kwenye uwanja wa ndege wa Dar es Salaam. Je, hii ina maana gani? Kwa nini na sisi tusiwe wagumu kutoa viza za kuingia nchini kwetu? La kusikitisha, Balozi zetu zinazingatia kupata mapato bila kuwachuwa waombao *visa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika wa Wizara kufanya mikutano wa wadau kuhusiana na tabia za Maofisa wa Balozi hizo ili wasiwe wasumbufu katika utoaji wa *visa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naulizia *Order of Precedence. Satos Guide on Diplomatic Rules - Viena Convention on Order of Precedence*, katika hali ya kushangaza kuona kiitifikasi, Mbunge yuko namba 14, je, hii ipo duniani kote?

MHE. AZIZA SLEYUM ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Mimi nachangia kwanza kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa *VIP*, naomba Waziri atueleze kuhusu utaratibu wa Kimataifa uliopo kuhusu matumizi ya *VIP* hasa pale viongozi wetu wanapokwenda baadhi ya nchi, inakuwa ni vigumu wao kutumia maeneo ya *VIP*. Kwani *VIP* yetu hutumika nao kwa kila kiongozi bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha viwanja vya ndege. Tunaomba kuchangia kuhusu suala la uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Kimataifa ili watalii waweze kushukia Tanzania na kuongeza pato katika nchi yetu, Kiwanja cha Kimataifa cha Kilimanjaro ambacho inasemekana kitakuwa Arusha. Pia kiwanja cha ndege Mbeya ili kuweza klusaidia kwa nchi za *SADC* kupata nafasi ya kutua na kupunguza usumbufu na kuleta hadhi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *visa*, sitachoka kulalamikia kuhusu suala la *visa* kwa kurudia tatizo. Katika baadhi ya Balozi katika nchi hii kuna udhalilishaji ambao naomba sana hii kero isiwepo kabisa. Kuna nini huko mpaka kukawa na matatizo zaidi kwa zaidi? Kilio changu kila siku na kila bajeti niliko na ninaamini hakuna lisilo na mwisho kama yatapigwa kelele na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa umahiri na ushirikiano na nchi za jirani. Ndiyo maana tunapata misaada kutoka nchi nyingine. Hiyo inatokana na uimara wa viongozi wa Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. BENARD K. MEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza niunge mkono hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa hotuba nzuri iliyopitia utendaji na mafanikio ya Wizara hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo napenda niombe kwamba wakati umefika kwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuhamasisha wawekezaji ili tuwe na Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Dar es Salaam, ili mikutano mikubwa inayohusu masuala ya amani na usuluhishi wa migogoro na ile ya kiuchumi, iweze kufanyika. Tusiwe watu wa kuhudhuria mikutano ya nje tu. Tukumbuke kuwa mikutano ya Kimataifa ina faida zake kiuchumi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii.

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa furaha na bashasha nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, Mabalozi wetu wote wa nchi za nje, pamoja na wale Mabalozi waliokuwa

humu humu ndani ya nchi kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya kwa kulitangaza Taifa letu la Tanzania ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii imebainishwa katika vielelezo vilivyotolewa na Wizara hii pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ambayo kwa kiasi kikubwa imeelezea juhudhi hizo na maelezo ya kina ya shughuli zake. Naendelea kuipongeza Wizara kwa shughuli zake hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano wa Kimataifa tulio nao Tanzania na nchi za Nje, ni jambo la kutia moyo na ni kweli kabisa ni mfano kwa dunia nzima. Ushirikiano ambao kwa kiasi fulani unakuza uchumi wa nchi yetu Tanzania, ikiwemo Zanzibar hasa katika biashara na utalii. Hata hivyo, ningependa kwa kiasi fulani nitoe mchango wangu ambao bado naona unanitatiza na kutaka Mheshimiwa Waziri anielimishe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya nne pamoja na nyongeza ya kwanza ya Mambo ya Muungano kati ya mambo yaliyoorodheshwa, ni mambo ya nchi za nje mawili na mikopo na biashara ya nchi za nje nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaona popote katika Katiba hii, palipozungumzia kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa. Sasa hapa Mheshimiwa Waziri atanielimisha vipi na hali ya Wizara hii kuitwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa! Huu Ushirikiano wa Kimataifa, kwa upande wa Zanzibar una sehemu gani katika Wizara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu haya na kutegemea kuwa Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha, atanipatia maelezo. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mabalozi, ni vigezo gani vinavyotumika ili mtu kuitwa Balazo, hata kama hana nchi anayoiwakilisha? Vigezo gani vinavyotumika kwa nchi yetu kuweka Balozi nchi kadhaa na kuacha nchi zingine hata kama nchi hizo zina uhusiano mzuri sana na nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nafasi ya Wabunge kutembelea Balozi zetu. Wizara hii ina mpango gani kamambe ili kuwezesha baadhi ya Wabunge kutembelea nchi za nje kama Wabunge, siyo Kamati kama Wabunge, kuona na kujifunza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wageni wanaozagaa nchini. Ukaribu na upole wa Tanzania utatuponza. Wizara hii ingeangalia upya uraia wa baadhi ya wafanyakishara wakubwa nchini kama ni Watanzania kweli au wana uraia mara mbili, ili waamue uraia wa aina moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu siasa za nje. Kwa nchi ambazo zina vurugu, tusione soo, tuachane nao. Muda mwingi Tanzania tunajifanya kimbelembele kusuluhiha migogoro ambayo ni sugu na kwa Mataifa ambayo ya vurugu.

MHE. BEATUS R. MAGAYANE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuitangaza Tanzania katika nyanja ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudzi za Serikali ya Tanzania katika kuleta amani eneo la Maziwa Makuu. Hili ni jambo muhimu katika kuleta amani hata kwa Tanzania yenyewe. Lakini nchi hizi zina unafiki sana na mara nyingi si wawazi wa kusema yale wanayokusudia. Nashauri Serikali yetu iwe makini katika kuzikaribisha Rwanda, Burundi na *DRC* kuwa wanachama wa *EAC*, kwani *agenda* ya *Hima Supremacy* bado inazungumzwa sana sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wetu amekwishatoa changamoto kuwa wakimbizi watunzwe katika maeneo salama ndani ya nchi zao, ni vema baada ya wakimbizi wa Burundi na Rwanda kurudishwa, Serikali yetu ifunge mipaka ili wasirudi tena na Jumuiya ya Kimataifa iwahudumie katika nchi zao badala ya kuja Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na vitendo vya mauaji na uporaji wa mali za Watanzania, vinavyofanywa na Majeshi ya Burundi hasa katika vijiji vya mpakani, na hata kuwateka nyara Watanzania na hata kuwaua. Ni vema Serikali ichukue hatua za makusudi za kuorodhesha vitendo hivi na kudai fidia kutoka Serikali ya Burundi, kwani inaweza kuthibitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na makundi mbalimbali ya kiuchumi na kisiasa ndani ya Afrika, *ECOWAS*, *SADC*, *COMESA*, *EAC*, *Arab League* na kadhalika, kunadhoofisha Umoja wa Afrika. Pia kuna mgongano mkubwa kati ya *NEPAD* na *AU* na kuna makundi ya Kimataifa yanayotuyumbisha kupitia makundi haya. Ni vema tuwe na *agenda* moja kama Afrika kupitia *AU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ichunguze kwa makini viongozi wa Vyama vya Upinzani ndani ya nchi za Burundi na nyingine zinazotuzunguka kwani wengine si viongozi, kwani hutumiwa tu kudhoofisha juhudzi za amani katika nchi husika. Kuendelea kuwatambua kutaendeleza vita katika nchi hizo na sisi tutaonekana kuwa sehemu ya migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuboresha uhusiano mzuri kati ya Tanzania na nchi zingine duniani pamoja na Mashirika yote ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anazofanya katika kuleta amani kwa nchi ambazo bado zina migogoro mikubwa kama

Burundi, Rwanda, Kongo na kadhalika. Amekuwa mstari wa mbele kuwapatanisha, akishirikiana na viongozi wa nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali ya usalama kutia matumaini nchini Sudan kati ya Serikali na wapiganaji wa *SPLM*, sasa hivi umezuka mgogoro mkubwa wa *DARFUL* ambako wanamgambo wa Kiarabu (*Janjaweed Militia*) wanawakataa wananchi weusi wa Sudan. Namwomba Mheshimiwa Waziri asaidie katika kutafuta amani sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nyuma kulitokea tuhuma ya kwamba Ofisi zetu wa Balozi mbalimbali walikuwa wanatoa *passport* nyingi, lakini mapato yalikuwa hayarudishwi hapa nchini. Nashukuru sana kwa utaratibu mpya ulioanzishwa wa kutoa Hati za Kusafiria na utaratibu wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kufanikisha Mkutano Mkuu wa *SADC* uliofanyika hapa kwetu. Hata hivyo, bado mnayo kazi kubwa ya kufanya kwa sababu Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa alichaguliwa kuongoza *SADC* na watendaji wake wakuu ndiyo nyie. Sina wasiwasi mtafanikisha majukumu yote vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Tanzania imechaguliwa kugombea kwenye Baraza la Usalama. Hiyo ni heshima kubwa sana tuliyopewa na wenzetu. Hata hivyo, kuchaguliwa huko kutakubaliwa tu endapo nchi za Ulaya na Marekani zitaunga mkono. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais, uzunguke kote Ulaya, Marekani na kwingineko kuomba wahusika watunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa juhudhi anazozifanya kuujenga upya ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hata hivyo, kuna ule mpango wa kutafuta fedha za kujenga mtandao wa barabara za Uganda, Kenya na Tanzania. Naona sasa hivi kama umesimama. Nakuomba Mheshimiwa Waziri utie msukosuko ili fedha hizo zipatikane kwa faida ya wananchi wote wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Kamati za Utendaji za *ALGAK*, *ULAA* na *ALAT*, tilitia saini Mkataba wa Ushirikiano wa Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji katika nchi zetu tatu na mkataba huo ndiyo uliothibitisha kabisa kwa Muungano wa Afrika ya Mashariki. Sasa ni wa wananchi wenye tofauti na Muungano uliovunjika mwaka 1977, ambao sana sana ulikuwa unahusisha Viongozi na Serikali husika. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atumie uwezo wake ili Mawaziri na Makatibu Wakuu husika wapewe nafasi kwenye Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki na Kamati ya Katibu Wakuu.

Narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutanguliza kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa juhudini kubwa za Kimataifa ambazo zinaendelea kwenye maeneo mengi duniani. Tanzania imejulikana kwa umaarufu kwa ajili ya uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Waziri kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Benjamin William Mkapa, kwa juhudini zake za kuitangaza Tanzania na kutetea ukweli na kuthubutu kuitetea Tanzania kusamehewa madeni yake. Umaarufu wake nchi yetu, umefahamika duniani. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, amekuwa Balozi mzuri wa kumsaidia Rais kwenye ziara mbalimbali, jambo ambalo limeonyesha uwezo wake mkubwa kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaarufu wa nchi yetu ndiyo umewapa Wajumbe ambao wanachaguliwa kwenye nafasi mbalimbali kuwa viongozi. Kwa mfano, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki ni Mtanzania, Rais wa Bunge la Afrika vile vile ni Mtanzania. Wengine ni Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu na wengine wengi. Rais wetu ameshiriki kwenye vikao vingi vya kusuluhisha migogoro ya nchi mbalimbali na kuwa mfano mzuri Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Mabalozi wetu walioko nchi nyingi duniani, watangaze uchumi wetu kiutalii, madini na mali nyingine ambazo zinapatikana Tanzania, ili uchumi wetu uimarike. Kwani nchi jirani zinatangaza nchi zao kuliko Tanzania. Kwa mfano, mbuga za wanyama nyingi zinatangazwa ziko Kenya, jambo ambalo siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kuimarisha uhusiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Hongera sana.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kuwapongeza kwa kazi nzuri ya kuitangaza nchi yetu nje Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba baada ya mageuzi ya kiuchumi, kitiikadi na mabadiliko ya kidunia (utandawazi), Wabunge hawana uzoefu wa kwenda na mabadiliko hayo kwa kuwapa semina na mafunzo mbalimbali, na hata kuwatemeza mara kwa mara kujifunza na kupata uzoefu katika nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya *AU* kukubali kuongeza Kiswahili kama lugha rasmi, Wizara iwe na mpango wa kuwawezesha Watanzania wengi kufundisha na kufanya kazi nje ya nchi za Kiafrika na hata Afrika penyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuendelea kuwapongeza sana watumishi wote wa Wizara hii, waendeleze juhudini nchi tajiri zione huruma kufuta madeni na kutoa misaada isiyo na masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. FRANK M. MUSSATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kipindi cha 2003/2004. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu, mwaka 2004/2005 uwe na mafanikio makubwa zaidi. Hata hivyo, ninayo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bidii zaidi za kuleta amani eneo la Maziwa Makuu, kwa sababu Tanzania ndiyo inaumia kuliko Mataifa yote ya Maziwa Makuu, kutokana na matatizo katika eneo hili kwa kulazimika kupokea wakimbizi. Naiomba Wizara iongeze juhudini za kupatanisha na kuleta amani katika eneo hili, ili wakimbizi warudi kwao na wakazi wa maeneo haya waweze kuishi kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Jumuiya ya Kimataifa iombwe kwa nguvu zote kuwafuta machozi wakazi wa Mkoa wa Kigoma kwa mzigo mkubwa walioubeba kwa zaidi ya miaka 30 ku-*host* wakimbizi kwa niaba ya Taifa la Tanzania. Msaada wa pekee unatakiwa kuboresha miundombinu hasa kimawasiliano, ili barabara zilizoharibiwa na magari ya wakimbizi, ziimarishwe kwa kuwekwa lami. *UNHCR* watakiwe kusaidia kupeleka umeme wa grid Mkoani Kigoma ili wakazi waweze kuanzisha miradi ya kiuchumi na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wageni kutembelea maeneo ya pembezoni. Naiomba Wizara hii ibadilishe mtindo uliopo wa wageni wengi watembeleao nchi yetu kupelekwa maeneo yaliyoendelea kama vile Arusha na Kilimanjaro na badala yake waelekezwe kwenye Mikoa ya pembezoni hasa Kigoma na Rukwa ambako ndiko kwenye umaskini uliokithiri. Tanzania isitangazwe tu kwa kuutaja Mlima Kilimanjaro kama mlima mrefu kuliko yote Afrika, bali vile vile kuwa Ziwa Tanganyika ni la pili kwa kina kirefu duniani kote na lina dagaa wa pekee duniani kote na Meli ya *MV Liembu* yenye umri unaokaribia miaka 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NEPAD* inafanya nini hasa nchini kwetu? Ningependa kujua nchi yetu mpaka sasa imefaidika vipi na inategemea kufaidika vipi katika siku za usoni kutokana na *NEPAD!* Aidha, ningependa kujua mpango wa kuendeleza barabara toka Tunduma kuititia Sumbawanga, Mpanda, Kasulu, Nyakanazi hadi Bukoba kwa fedha za Jumuiya ya Afrika Mashariki, umefikia wapi au sisi tunaoishi maeneo ya barabara hiyo tuwe na mategemeo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Waziri wa Mambo ya

Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, pamoja na wasaidizi wake kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nichangie kwa kumshukuru Waziri kwa kuliweka wazi tukio la aibu lililofanywa na Afisa Ubalozi wa Saudi Arabia la ubakaji. Naelewa fika mawasiliano ambayo yamekuwepo kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu tukio hilo na nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kumtaka Mwanadiplomasia huyo aondoke nchini baada ya Serikali ya nchi yake kukataa kumwondolea kinga ya kidiplomasia na kuitaka nchi yake imshughulikie kwa mujibu wa Sheria za Saudi Arabia, ni uamuzi sahihi kwa mujibu wa sheria za Kimataifa na sheria zetu. Aidha, *quite diplomacy* iliyotumika kuwezesha mwathirika kulipwa fidia, hayo ni ya kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo ninalo ni kwamba Serikali imechukua muda mrefu kulitolea maelezo tukio hilo na hivyo kutoa mwanya kwa vyombo vingine kulidandia na kuliteka nyara. Hata hivyo, ni kheri kuchelewa kufika kuliko kutokufika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *precedents* za huko nyuma tunazo, ikiwa ni pamoja na *container* la mizigo la aliyekuwa Balozi wa Indonesia hapa nchini, ambalo likutwa na nyara za Serikali kinyume na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku za usoni iwapo matukio kama haya yatatokea, nashauri Serikali ifanye hima katika kutoa maelezo na ufanuzi mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kama nilivyoanza kwa kuwapongeza kwa dhati kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii katika nyakati tulizo nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nia moja naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Wizara imefanya mambo mengi ya Kitaifa na Kimataifa. Yote yaliyotendeka yamelipa Taifa letu heshima kubwa. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wote, tunazidi kuwatia moyo ili wapige hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo/pendekezo la Mheshimiwa Rais wetu alilowahi kulitoa kuhusu Wakimbizi kwamba, ifikie mahali au wakati ambapo Wakimbizi wabakie katika nchi zao. Aidha, iendelee kupendekezwa kwa jumuiya ya Kimataifa kutenga maeneo ya Wakimbizi ndani ya nchi husika na hivyo kupewa misaada yote wakiwa nchini mwao. Faida zake ni pamoja na kwanza, kuwa rahisi kurudi makwao mara baada ya vita, pili, kuepusha mzigo wa Wakimbizi kwa nchi isiyo na mgogoro isiyohusika na mgogoro na inawapokea, tatu, kuepusha uharibifu wa mazingira kwa nchi ambazo zinawapokea Wakimbizi na nne, kuepusha mashaka/chuki kati ya nchi inayotoka

Wakimbizi na ile inayowapokea kwamba pengine wanawasaidia Wakimbizi hao mifano ipo, na huleta mapambano.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimimwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri ya kina na undani iliyosomwa kwa ufasaha na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya katika kujenga mahusiano na ushirikiano mzuri baina ya nchi yetu, majirani zetu, Afrika na Dunia kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunafurahia na kushangilia Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki ningeomba isiwe jumuiya ya viongozi bali ya wananchi hivyo iwepo mikakati ya wazi ya wananchi wa nchi hizi kuelimishwa ili waielewe na hivyo kuweza kutumia fursa zote zilizo ndani ya Katiba ya Jumuiya. Kwa mfano ni wananchi wangapi wanaojua namna ya kupata *passport* ya Afrika, ni wananchi wangapi wanajua na wanaweza kutumia fursa zilizopo za biashara baina ya nchi hizi tatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakimbizi nakuomba Jumuiya ya Kimataifa ijaribu na izidi kuelewa matatizo na athari kubwa zilizojitokeza na zinazoonekana hadi sasa na pengine zitaendelea kuwapo kwa muda mrefu katika maeneo walijotumia Wakimbizi wa Rwanda Burundi na *DRC* ili waendelee kutoa msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili nydingi na mazingira yaliharibiwa na hadi sasa hayajarudia hali ya kawaida. Silaha nydingi walizoingia nazo Wakimbizi sasa ndizo zinaleta mateso kwa raia wasio na hatia. Utekaji, ujambazi na mauaji yamekuwa jambo la kawaida, sasa wamekuwa tishio kwa mali na maisha ya wenzao na haya yote ni matokeo ya ujio wa Wakimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja ya Wakimbizi kutengewa eneo ndani ya nchi zao ili kupekana na hayo niliyoyaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizidi kumpongeza Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja.

MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza Waziri Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Naibu wake, Mheshimiwa Abdulkader Shareef na Katibu Mkuu, Bwana Luhanjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza na kumshukuru Mhehsimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Matumizi ya Kiswahili katika *African Union*. Aidha, nashukuru kwa kuona baadhi ya viongozi wa Afika kutumia Kiswahili katika Mkutano huo wa Kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliarifiwa kuwa wakalimani wetu walipata matatizo makubwa katika kutekeleza kazi zao. Naomba kama hili ni kweli, Serikali ichunguze ni nani aliyesababisha usumbufu huo na hatua kali zichukuliwe kwa wahusika hao ambao nadhani walifanyi njama hizo kusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara yetu ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, iombe nafasi katika vyuo vya kufundisha ukalimani na utajurumani ili watu wetu wa Afrika ya Mashariki wajifunze taaluma hii katika lugha za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara yetu isibweteke katika safari hii ndefu ya kukiwezesha Kiswahili kutumika katika medani ya Kimataifa. Hivi hatuwezi kushawishi pia Kiswahili kitumike katika vikao vya SADC na Afrika ya Mashariki? Aidha, nashauri vikao vyote vinavyofanyika nchini Tanzania vya Kimataifa, Kiswahili kitumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana pia katika dhifa za Kitaifa Kiswahili kikatumika kama alivyofanya Rais wetu Mheshimiwa Benjamin Mkapa, hivi karibuni alivyotembelewa na Rais wa Namibia, Sam Nujoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilivyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mabalozi pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyofanywa na Wizara hii kwa kipindi cha miaka minne ni nzuri sana na napenda nikubali kwamba Mheshimiwa Waziri ni aina ya askari wa mwavuli ambao Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, amekuwa anazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kufungua Ubalozi nchini Malawi. Hii ni hatua muhimu katika kupata jawabu la kudumu kuhusu utata wa mpaka wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mpaka kati ya Malawi na Tanzania linaweza kutatuliwa kwa ushirikiano wa vitendo wa kiuchumi na Kijamii. Nashauri swala la kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi kati ya Malawi na Tanzania na hasa wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iwezeshe ili wakazi wa Mbinga na wale wa Malawi wafanye biashara halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana hali ya ushirikiano kati ya wananchi wanaoishi mipakani hususan Kenya, Uganda na Tanzania. Nashauri Serikali iweke utaratibu wa kukuza ujirani mwema kwa nchi zote zinazopakana na nchi yetu.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa hotuba yake nzuri na ya kusisimua ambayo imetolewa asubuhi hii. Uchambuzi wa hali ya juu hasa kuhusu utandawazi umefanyika na kwa kweli kutolewa kwa kitabu kiitwacho *A Fair Globalization - Creating Opportunities for all*, kilichotolewa na World Commission on the Social Dimension of Globalization ni ushahidi tosha kuwa Wizara hii iko *serious* na mambo yake. Hongera sana kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nichukue fursa hii, kukumbushia suala la mpigakura wangu mfanyakishara *Mr. Joel E. Mchomvu*, ambaye alitapeliwa na mfanyakishara wa Afrika ya Kusini ambaye alikuja kumkamata kwenye *Trade Fair*, Dar es Salaam na Serikali kuingilia kati na kuahidi kuwa itawasiliana na Ubalanzi wa Afrika ya Kusini ili dola 12,000 zilizochukuliwa na mfanyakishara huyo wa Afrika ya Kusini ambaye hakurejesha bidhaa (*supplies*) kama walivyokubaliana na *Mr. Mchomvu* ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, kwa namna ambavyo amekuwa akilihangainia suala hili bila kuchoka. Bado tuna matumaini makubwa na jitihada za Serikali na ni imani yetu kuwa haki itatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa na kwa niaba ya jimbo langu la Siha naunga mkono hoja hii.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza kabisa ni kuipongeza Wizara hii kwa mipango yake mizuri iliyoipangia katika kipindi hiki, mfano ni ule wa kuwaita Mabalanzi wake wote na kuwafanya semina za uwajibikaji, hivyo kutoa changamoto katika ofisi zao, ni matumaini yangu si muda mrefu *impact* yake tutaiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa pili ni kukipongeza kitengo cha Itifaki kwa mipango yao mizuri ambayo inaonekana kabisa inafanana na nchi zilizoendelea, pamoja na pongezi hizi zipo dosari ndogo ndogo ambazo inafaa ifanye marekebisho mfano mdogo ni hivi majuzi tu mwandishi wa habari alivyokunjwa na vyombo vyaya dola hivyo kuonekana katika suala la Itifaki halikutayarishwa vizuri hivyo watu wengine kukoseshwa haki zao za msingi katika shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu namna gani nchi yetu inapaswa kujitangaza, pamoja na kwamba Balozi zetu zipo duniani lakini wasiwasi

wangu labda ni kuhusu uwezeshwaji ambao siyo siri kwa namna yeote utangazaji unahitaji gharama. Je, Wizara imetenga fedha hizo? Pamoja na utangazaji huu lakini mimi nahisi bado tutoe fursa kuajiri makampuni yenyeye uzoefu wa kibiashara katika sera hii yenyeye taaluma na mbinu mzunguko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarimu wetu lazima uwe na mipaka na hasa katika uvunjaji wa sheria za Kimataifa na katika kulinda haki za binadamu, haiwezekani Balozi au mtumishi wa Kibalozi avunje sheria hatimaye sisi (Wizara) tukaikingia kifua na kumtetea mhalifu, mfano mdogo Kashfa ya Balozi wa Saudia Arabia ambaye alibaka na hatimaye alipata fursa ya kuondoka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo yote katika mikakati ya Wizara hii chuo cha Diplomasia lazima kitengewe fedha zaidi ili kiweze kuboresha sifa zinazoweza kukidhi haja ya matakwa ya Wizara hii kwa hivi sasa na baadaye, badala ya kutegemea kuchota wataalm wengine nje ya wenye sifa ya Ubalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Wizara hii ipongezwe wakati Mheshimiwa Rais wetu alipokuwa nje kwa matibabu Uswiss, kwa taarifa zao walizokuwa wanazituma nchini, hii ilichangia kiasi kikubwa cha kuongeza utulivu wa matumaini kwa kiongozi wetu, zoezi hili limetupatia sifa kubwa sana katika taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeingia katika Bunge muhimu la Afrika, naishauri Wizara hii pamoja na Wabunge wetu walioingia katika Bunge hilo wanazo sifa zote, naiomba Wizara hii iwapatie semina za kutoa michango katika uwanja huu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa mara ya pili kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa mpango huu mzuri wa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongozi hizi, vile vile niwaombee kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwatia nguvu, upendo na mshikamano katika kutekeleza majukumu yao siku hadi siku kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa *Visa*, naipongeza Serikali kwani imekuwa ikijitahidi kutoa huduma zinazoridhisha kwa Watanzania hususan suala la upatikanaji wa *Visa* uliotokana na mahusiano mazuri kati ya nchi yetu na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mahusiano haya bado kumekuwepo na matatizo kwa baadhi ya nchi kutoa *Visa* kwa Watanzania wanaopata nafasi za kwenda kusoma, biashara za Kimataifa, ama kwenda kwenye matibabu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifanye juhudi za kidiplomasia ili kulegeza au kuondoa masharti yasiyokuwa ya msingi katika upatikanaji wa *Visa* hizo ili kupunguza gharama za usafiri na kuondoa vikwazo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuzindua Diplomasia ya Kiuchumi katika nchi yetu. Hivyo basi, naiomba Serikali ihakikishe inaboresha ofisi za Mabalozi wetu huko nje ya nchi ili kuziwezesha Balozi zetu kupata nguvu ya namna ya kutekeleza Diplomasia ya Kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu katika Balozi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano wa *SADC*, napenda kuchukua nafasi hii kwa namna ya pekee kuipongeza Serikali kwa kudumisha mahusiano mazuri na nchi mbalimbali duniani zikiwemo nchi za *SADC*. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya *SADC* jambo ambalo limeijengea heshima Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ushirikiano tulionao na nchi za *SADC*, lakini kumekuwepo na minong'ono ya chini chini kutoka nchi zilizo Kusini kabisa mwa Afrika mfano, Botswana, Swaziland na kadhalika kwamba kwa nini Tanzania inajita ni mwanachama wa *SADC* wakati yenyewe iko Afrika Mashariki na wanajumuia yao ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hizi zimekuwa zikidai kwamba *SADC* ni kwa ajili ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika tu. Je, Serikali inalijua hilo na kama inalijua inasema nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikishwaji wa Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kusema kwamba Serikali yetu imekuwa na mahusiano mazuri na nchi mbalimbali za Afrika na dunia kwa ujumla na imeshiriki mikutano mingi na makongamano ya Kimataifa na mafanikio yake tunayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haiioni kwamba ziara za Serikali kuitia Wizara hii kuna kila sababu ya kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge kila inapotokea ili na wao wajifunze?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia mchango wangu napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati Waziri, Mheshimiwa Jakaya Kikweta, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, Katibu Mkuu, Ndugu Phillemon Luhanjo, Wakurugenzi, Mabalozi wetu pamoja na wafanyakazi wengine wa Wizara hii na Taasisi zake kwa hotuba nzuri na kazi nzuri sana ya kuiwakilisha na kuitetea nchi yetu katika mambo ya nje na uhusiano wa kimataifa. Sera, mikakati na mipango ya utekelezaji na mtazamo kwa jumla ni kwa mujibu wa Dira ya Taifa letu na Ilani ya Uchaguzi ya CCM

ya mwaka 2000. Hatua hizi zinaleta matumaini makubwa kwa wananchi na kuiweka Tanzania katika nafasi nzuri katika ramani ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mbalimbali tuliyoyapata katika nyanja za Diplomasia na Ushirikiano wa Kimataifa ni ushahidi wa kutosha kuhusu hatua kubwa tunazopiga mbele hasa katika heshima inayopewa nchi yetu kwa viongozi wetu mbali mbali, akiwemo mpendwa Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kupewa nafasi za juu za uongozi wa Taasisi na asasi za kidunia na kikanda. Tuendelee kuzitumia vyema nafasi hizi kuzidi kuiongezea sifa na manufaa Tanzania, hasa katika zama hizi za utandawazi. Matumizi ya Kiswahili ni njia moja ambayo tunaweza kuitumia kwa manufaa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Diplomasia ya kiuchumi ni sera sahihi ya kuinua na kuendeleza uchumi wa nchi yetu na ustawi wa jamii iwapo hatua thabiti zitachukuliwa katika utekelezaji wa sera hii. Naipongeza Wizara kwa hatua ambazo Wizara imekwishakuchukua mpaka sasa. Mikakati na hatua za utekelezaji wa sera mpya ya mambo ya nje na semina iliyofanywa kwa Mabalozi wetu ni hatua nzuri za mwanzo ambazo hazina budi kufuatiliwa kwa jitihada kubwa ili kuleta mafanikio yanayotarajiwa. Nimefarajika kufahamu kwamba Wizara itaendeleza kuajiri watu wenyе sifa zifaazo na kuwapatia mafunzo ili wawe watendaji bora na watetezi hodari.

Mafanikio ya sera hii pia yatategemea sana nguvu zinazotolewa na hatua za makusudi za kufanikisha sera hii. Hatuna budi kutambua kwamba shughuli za kkitangaza nchi, kuvutia uwekezaji, kukuza mauzo ya bidhaa zetu mahiri bali pia kadha za kutosha. Hapana budi tukiri kwamba bila kuwekeza vyta kutosha haitawezekana kuvutia wawekezaji au wanunuzi wa bidhaa na huduma majirani zetu wa Kenye wanatumia takribani US \$ bilioni moja kwa mwaka kwa ukuzaji wa utalii pekee.

Kwa kuwa hivi sasa Wizara na Taasisi zinazohusika na kuvutia uwekezaji na ukuzaji wa mauzo ya Tanzania kwa jumla ni nyingi, hapana budi pakawepo utaratibu thabiti wa kuratibu na kusimamia kwa pamoja shughuli hizi mahali pamoja hapa nyumbani na katika Balozi zetu mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ushindani ni kichocheo kizuri cha maendeleo, nashauri Balozi zetu mbalimbali na pia Wizara na Taasisi mbali mbali zingewekewa malengo na kuzawadiwa pale wanaofanya vizuri kama motisha. Pia napendekeza kwamba mafanikio hayo ndiyo yawe moja ya vigezo vikuu vyta kuwapandisha vyeo wale wenyе mafanikio mazuri na kuwachukulia hatua za nidhamu wale wasiofanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na Waziri, Waziri wa Nchi au Naibu Waziri atakayesimamia masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri katika kutekeleza malengo mliyojiwekea kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 na nawapongeza watendaji wote wa Wizara na Balozi zake na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kuwa Watanzania wanaposafiri kwenda London, Uingereza wanapata shida maana ukipewa dola hapa ukifika Uingereza thamani ya fedha hizo inakuwa nusu kwa hiyo, anaishi maisha ya nusu, nusu. Nimeona kuwa hata watumishi wetu wanaofanya kazi Uingereza wanaishi maisha magumu sana. Ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa Watanzania wanaosafiri kwenda Uingereza wawe wanalipwa *Sterling Pounds* badala ya *US dollar*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali na Wizara kwa kuwa wanapewa fedha za kutosha na kuyalipa madeni yote ambayo yalikuwa yanadaiwa na waliotukopesha. Hii imetujengea heshima huko nje ya nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nilikuwa New Delhi, India ilionekana Wizara haitoi fedha za kutosha katika kushughulikia maonyesho ya biashara na kwamba wanaopewa kushughulikia swala hili hawana Elimu za kutosha, ni vyema wanaotakiwa kushughulikia maswala haya wawe na uzoefu na Elimu ya kutosha kushughulikia maswala ya Viwanda na Biashara (Uchumi). Kutokana na mwelekeo wa sasa kuhusu kuboresha uchumi ni vyema sasa Wizara ikaliwekea mikakati ya kutoa fedha za kutosha katika *ku-promote* biashara, Viwanda, Utalii, Uwekezaji, Wizara ishirikiane na Wizara zote katika kuhakikisha na kuweka msimamo wa kuboresha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara haina tabia ya kujibu barua zinazoandikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuwapongeza kwa utekelezaji wa malengo waliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Ushirikiano wa Kimataifa.

Kwanza kabisa napenda kutoa pondezi kwa kushirikiana na Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza mwenzetu Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki, kwa ushindi wa kishindo. Tunajua kazi ilikuwa ngumu, lakini ukivaa shati la CCM siku zote ni rahisi kupita. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kutoa mkono wa rambirambi kwa kupotelewa na ndugu zetu wawili kwa ghafla, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye alikuwa jirani yangu hapa Dodoma, milango yetu inaelekezana uso kwa uso. Kwa hiyo, tokea kufariki sasa hivi hatuonani asubuhi nikitoka. Vile vile ndugu yetu Marehemu Mheshimiwa Kapteni Theodos Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi na awape faraja familia na jamaa wa Marehemu. *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuwaambia wananchi wa Majimbo hayo mawili kwamba watapatiwa Wabunge wengine imara wa CCM. (*Makofii*)

Vile vile nawapa mkono wa rambirambi ndugu zetu waliofiwa na wazee wao Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda. Pia Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na watoto wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi na awape subira waliofiwa. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa wanakamati wa Kamati ya Mambo ya Nje kwa msaaada wao mkubwa wa kutupa mwongozo na kutushauri vizuri. Lakini pongoza za pekee natoa kwa Mheshimiwa Hadija Kusaga, kwa kuwasilisha maoni ya Kamati vizuri sana kwa ufasaha na kwa kujiamini kabisa.

Vile vile, napenda kumshukuru ndugu yangu Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Waziri aliyesalia kivulini, ndugu yangu Khalifa Suleiman Khalifa, napenda kumpongeza kwa mchango wake na ushirikiano wake mkubwa aliokuwa anatupa siku zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, mwisho kabisa na wala sio mwisho kwa umuhimu ni kumshukuru Katibu wetu Mkuu mchapakazi Ndugu Luhanjo, pamoja na Wakurugenzi wote, Mabalozi na maofisa. Sisi kwa kweli ni bomba kusema tu, wao ndio watayarishaji wa mambo yote tuliyokuwa nayo hapa. Kwa hiyo, tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajaribu kama niwezavyo kwa muda mfupi niliokuwa nao kuchangia baadhi ya maswali na mengine nitamwachia Mheshimiwa Waziri.

Nitaanza na mambo mawili, matatu, kutoka kwa wanakamati. Katika mapendekezo yao mojawapo wanasema wakigusia hili suala la Saudi Arabia lililotokea hivi karibuni au mfanyakazi wa Saudi Arabia kwamba Serikali kutokelea wala kuchukua hatua thabiti kwa kitendo cha kumbaka msichana wa Kitanzania na kwamba Kamati ya Mambo ya Nje inamtaka Waziri atoe maelezo ni kwa nini amelifumbia macho suala hilo zito ambalo linamdhalilisha mwanamke pamoja na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nasi kwamba maelezo aliyatoa Mheshimiwa Waziri leo asubuhi yameeleza kwa ufasaha kabisa hatua kwa hatua mambo ambayo Wizara yetu ilifuatilia, haikupuuza hata kidogo na wala hakukuwa na njia nyingine ya kulishughulikia suala lile zaidi ya vile tulivyofanya. Tunabanwa na sheria za Kimataifa, hatuna njia nyingine. Jambo ambalo tunaweza kuongezea hapa ni kwamba tulitaka kuhakikisha mambo mawili makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza tulitaka kuhakikisha kwamba yule mtu akirudi kwao Serikali itamshughulikia ipasavyo na jambo hilo kwa kweli Balozi wa Saudi Arabia amekuwa kila siku anatwambia huyu mtu alitakiwa arudi jana ili apatiwe

adhabu ipasayo ambayo kwetu sisi, anasema yeye, adhabu kali inaweza kufikia kifo. Kwa hiyo, tulitaka tupate maelezo wazi kabisa kutoka Ubalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kutaka kujua endapo atakwenda mshtakiwa yule au aliyefanya kosa lile Saudi Arabia na mwathirika akataka kufungua kesi kule, je, inawezekana? Serikali ya Saudi Arabia wametwambia ndio inawezekana na wao wapo tayari kutoa msaada wote akienda kule ashtakiwe yaani mwathirika akafungue mashitaka kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, lilikuwa ni suala la kuhakikisha basi angalau kabla ya kuondoka, huyu dada yetu anapata kitu angalau cha kujisadia baadaye na hilo Balozi wa Saudi Arabia alishirikiana nasi vizuri na ipasavyo. Wakakaa pembeni, wakazungumza pande mbili na ukapatikana muafaka na fidia ikatolewa na tukaridhika.

Kwa hiyo, tunasema hayo ndio mambo ambayo yalitufanya kidogo tucheewe. Lakini taarifa tulikuwa tukizitoa, hatukuzitoa kwa maana ya kuitisha mkutano na Waandishi wa Habari, lakini tulikuwa tukitoa kadri zilivyokuwa zinaweza kutolewa na hasa kwa vile mazungumzo mengine yalikuwa yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba suala hili hatukulifumbia macho, tulilivalia njuga lakini kwa mujibu wa sheria na taratibu na kitu kilicho muhimu kwetu sisi kuliko yote baada ya yote hayo, ni heshima ya yule dada yetu ambaye aliathirika. Ilikuwa lazima tumlinde, lazima abakie kuwa hajulikani, si vizuri baada ya maafa yake yaliyomfika akawa anatolewa hadharani na kila mtu sasa aanze maneno yake mbalimbali. Kwa hiyo, hayo ndio tuliyofanya na kulikuwa hakuna njia nyininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati vile vile inasema kwamba Wizara itumie vizuri mtandao ulio nao wa Ofisi za Balozi zetu ili kuhamasisha wawekezaji, kuvutia mitaji na kutafuta masoko kwa bidhaa za Tanzania, kutafuta teknolojia na kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchini mwetu.

Napenda kusema kwamba hizo ndizo kazi zetu za kila siku mchana na usiku, ndio majukumu tuliyoyavalia njuga na ndiyo tunayoyafanya kazi kila siku. Sasa pengine linalohitajika zaidi hapa ni kushirikiana vizuri zaidi na wenzetu wa sekta nyininge mbalimbali, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Maliasili na Utalii na wote wengine ili kufanikisha jambo hili. Hayo pia tunayafanya na katika sehemu ya mkakati wetu tuliojipangia katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje hayo ndio tuliyojipangia moja baada ya moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la Wizara kuitangaza Tanzania nje ya nchi kwa nguvu zote na kuhusu hilo Serikali kwa jumla itumie fedha katika kufuatilia suala hilo. Nasema haya vile vile ni mionganoni mwa tunayoyafanya. Lakini hivi karibuni Mheshimiwa Rais kwa kutambua kwamba kuna uwiano mkubwa kati ya kuitangaza Tanzania na majukumu tunayoyafanya sisi katika Wizara yetu, ndio maana akanichagua hata mimi mwenyewe

kuongoza timu ndogo inayoitwa *Brand-Tanzania* yaani ni timu ya kujenga jina la Tanzania nje ya nchi. Mtu akisikia Tanzania anaelewa nini, kwa sababu sio tu mtu akisikia Tanzania aelewé ni nchi ya kutanzua matatizo, ni nchi tulivu, ni nchi ya amani, ni nchi iliyokuwa Afrika ya Mashariki. La hasha, aelewé kwamba Tanzania kuna mbuga za wanyama, kuna fursa chungu nzima za biashara, ni nchi iliyotulia, ni nchi makini, ina sera makini na ni nchi ambayo haina ugomvi si wao wenye kwa wenye na wala si baina yao na watu wengine. Hicho ndicho kitu kimvutie mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama leo ukitajiwa Marekani, basi jina hilo linakuwa ni mfano wa rajamu yaani ni *Trade Mark*, ni kitu ambacho ukisikia tu jambo la kwanza linalokuja kichwani mwako ni nchi ya kwenda kufanya biashara, ni nchi iliyendelea kwa teknolojia, ni nchi yenye fursa nyingi. Ukisikia Uingereza, Malkia, ni nchi yenye Bunge, lakini ni nchi yenye mambo ya kibashara na kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mbali na kuitangaza kwa kila siku lakini lazima sote tuitangaze kwa namna moja. Kwa maana ya kwamba tukitoka nje kuitangaza sio kila mmoja anakwenda na njia yake na kutangaza anavyotaka yeye. Lazima tuitangaze Tanzania kwa sura moja, kwa kauli moja, kwa mtindo mmoja ili tupeleke message moja tu nje. Sio mmoja katokea anatangaza Kilimanjaro, mwingine anakwenda kutangaza mambo ya kuhifadhi mazingira ambavyo vitu vinagongana. Kuhifadhi mazingira ni jambo muhimu, lakini lazima linapotangazwa liwiane na kutangaza utalii, liwiane na kuleta viwanda katika nchi, liwiane na kualika watu kuja kuwekeza katika mambo ya biashara, mambo ya ukulima na kadhalika. Kwa hiyo nasema, hilo ni suala ambalo Mheshimiwa Rais ameliona na kutuungezea jukumu na sisi tumelichukua kwa mikono miwili na tumelivalia njuga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wanasema Serikali iendelee kufanya mafunzo katika ngazi mbalimbali za uongozi kwa wananchi kwa jumla itasaidia Taifa hili kuelewa kwa pamoja matakwa ya mfumo mpya wa utandawazi kama tulivyofanya wakati tunaweka mkakati wa kutekeleza dira ya mipango chini ya Azimio la Arusha. Tunasema hili ni wazo zuri na tumelipokea na tutalifanyia kazi na kwa hakika mkakati wetu vile vile unazungumzia masuala hayo kama Kamati ilivyopendekeza. Kwa hiyo, ni jambo la kutukumbusha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia suala lingine lililopendekezwa na Kamati hapa kwamba Serikali iwasaidee vijana kuelewa utandawazi duniani kupitia shule, vyuo, vyuo vikuu, vyombo vyahabari na kadhalika. Ni wazo zuri tumelipokea, lakini nina mambo mawili hapa pia napenda kusisitiza, kwamba ripoti ya Tume ya *ILO* ambayo Mheshimiwa Rais ndiye alikwenda kushirikiana na wenzake kuiongoza, imeweka mikakati, dira na mipango mbalimbali ya kueleza hayo hayo ambayo yameelezwa hapa.

Kwa hiyo, kilichosalia kwetu sisi kama ni Wabunge, kama watu wa taasisi, kama watu wa Serikali, ni kujaribu kila mmoja kutazama ripoti hiyo inasema nini na kutekeleza wajibu wake na utakuta kwamba kutoa mafunzo kwenye vyuo, vyuo vikuu, vyombo vyahabari na kadhalika ni mojawapo ya mikakati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna kitu kinaitwa *Helsinki process* au mchachato wa Helsinki na mchachato huu unaongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania na Waziri wa Mambo ya Nje wa Finland. Pengine ni *coincidence* tu kwamba ile ripoti ya *ILO* iliongozwa na Marais na huu mchachato wa Helsinki sasa unaongozwa na Mawaziri wa nchi hizo mbili. Kama ni *coincidence* tu au ni mpango wa makusudi na ni jambo la kufurahisha kwa sababu *Helsinki process* ni ufuatiliaji wa kina zaidi kutoka ngazi za chini ya utekelezaji wa masuala yale yale ambayo yalisimamiwa na Tume ile ya Utandawazi na ripoti yao waliyoitoa.

Kwa hiyo, mambo haya mawili yanasaidia katika kutoa na kuelimisha watu mbalimbali kujua athari za utandawazi na vipi utandawazi unaweza kugeuzwa ukawa utandawazi wenye manufaa na haki kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati imependekeza Wizara ipange na kuendesha semina na warsha kwa Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na makundi mengine husika juu ya sera ya mambo ya nje na mikakati iliyopo katika kutekeleza Diplomasia ya kiuchumi. Aidha, ni muhimu kutumia vyombo vyaya habari katika kuelimisha jamii juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, semina za kuelimisha masuala yaliyokuwa muhimu mionganoni mwake sera ya mambo ya nje, utandawazi, umoja wa forodha, Itifaki, hata mchakato wa Helsinki ndiyo masuala ambayo kwa kweli tumejipangia kuyafanya.

Kwa hiyo, tumepokea ushauri huu na tutaufanyia kazi kama ipasavyo. Tutaangalia suala la gharama kama semina hizi zikifanywa mbili au tatu kwa pamoja kwa sababu kuifanya semina kila mmoja peke yake ina gharama zake, lakini tutaliangalia na tutalitekeleza. Tunawaahidi Waheshimiwa Wabunge tutawashirikisha. Siku za nyuma tulikwisha kuwashirikisha katika mengine lakini tutaendelea zaidi kuwashirikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inasema Serikali iendelee na azma yake ya kufungua Balozi mpya katika maeneo ya nchi muhimu kama vile Brazil na kadhalika ili utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya kiuchumi iweze kuleta tija. Tunapenda kusema kwamba kama tungekuwa na fedha za kutosha tungefungua Balozi kila nchi duniani na tungezifungua zaidi hasa katika nchi ambazo zina mahusiano makubwa na sisi kibiasara. Lakini ukosefu wa fedha ndiyo unatufanya tusiwezi kufanya hivyo.

Kwa hiyo, tumelipokea hili lakini lazima tupange na tuchague kutokana na fedha chache tulizokuwa nazo. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri alisema kwamba tungefungua pengine Ubalozi Oman, sababu za msingi tulizielezea mwaka 2003 na vilevile Oman wametuahidi kwamba watasaidiana nasi kwa kila njia ili sisi tufunge kule na wao Ubalozi mdogo wao hapa Tanzania waupandishe hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Visa*, hili limekuwa ni sugu sana na Balozi hizi za nje ni kweli. Kwa kweli lazima tukubali kwamba utaratibu mwingine wanaofuata

ni wa kudhalilisha na kunyanyasa watu wetu na jambo hili hatuwezi kulivumilia sana. Lakini vilevile lazima tukubali kwamba nchi hizi zina hiari ya kufanya hivyo na ni mamlaka yao wenyewe na wana sababu zao hatuwezi kuwatia shemere. Kinachotakikana ni sisi kukaa, tukazungumza nao kwa taratibu na kuwaeleza kwamba haya mambo mnayoyafanya mnaweza kuyafanya kwa ubinadamu na kwa njia ya busara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikiwa bado wataendelea itabidi na sisi tutafute njia nyingine ya kufanya na ikiwa njia ya kufanya ni kurudi kwenu hapa na kutaka sisi mtupe mwongozo kama Taifa tufanye nini tutorudi kwenu Bungeni lakini hatutaki tufike huko.

Kwa hiyo, bado tutaendelea kuzungumza na wenzetu hawa kwamba kwa kweli taratibu walizoziweka nyingine ni za kunyanyasa na kudhalilisha hazikubaliki lazima tukae kitako tutafute njia ya kuzitanzua. Haiwezekani hata kidogo kwa sababu wanaofanyiwa ni ndugu zetu na watu kutoka hapa, mbona nchi nyingine wao hao hao wanapowapatia *Visa* hawafanywi hivyo? Kwa hiyo, nasema muendelee kushinikiza. Kamati ya Mambo ya Nje iliwaita baadhi ya Mabalozi hawa na iliwaeleza vizuri na sisi tutaendelea. Hatutaki kufika mpaka kuanza kutukanana au kuchukuliana hatua za ulipizaji kisasi. Lakini ikibidi mwisho wake itabidi tufike huko, hatutaki kufika huko, ikibidi kufika, tutafika kwenu kuwaulizeni mtupe ushauri wa kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naona wakati umenikimbia sana sikutaraji kwamba wakati utapita hivi kwa haraka. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliopata nafasi ya kuchangia na kuunga mkono hoja niliyoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa maandishi na kwa kuzungumza hapa ndani ya Bunge. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge 10 wamechangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge 14 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Hadija Kusaga ambaye aliwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Lucas Selelili, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Aziza Sleyum

Ali, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa na Mheshimiwa Bernard Membe. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Mengi ya mambo waliyosema ni mambo ya ushauri ambayo mimi na wenzangu tumeyapokea na tutaendelea kuyafanyia kazi. Wametoa sifa nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu ni za kweli yeche ndiye mwanadiplomasia *number one* sisi wengine wote tupo kumsaidia na kumwezesha kurahisisha kazi yake. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje. Pendekazo la kwanza au suala la kwanza lilikuwa rai kwamba Wizara katika Mikutano ijayo ya Mabalozi iishirikishe Kamati ya Mambo ya Nje na pia Wenyeviti wa Kamati nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni pendekazo tumelipokea tunasikitika kwamba safari hii hatukufanya hivyo, lakini pengine ni kwa sababu nzuri tu. Sisi kwa fikra yetu tuliona kwamba huu ni Mkutano wa kazi. Mabalozi wanakutana kila baada ya kipindi fulani kutafakari jinsi wanavyotenda kazi zao za kuihudumia nchi yetu. Ni kama vile kuna wakati wa Wakuu wa Mikoa wanakaa, Wakuu wa Wilaya wanakaa na watendaji wengine wanakaa. Sasa haikutujia katika mawazo yetu kwamba katika mkutano wa kazi kama huo kwamba Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje nao wawepo kwenye mkutano. Kwa kweli tulitaka uwakilishi kwa mtu mmoja lakini nadhani pia nayo kulikuwa na matatizo kidogo katika uwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kwamba ni jambo ambalo tutaona tutakavyolitengeneza vizuri zaidi, kwa sababu Mabalozi si wengi sana wako 29 tu na pengine Kamati yetu ya Bunge ya Mambo ya Nje ina wajumbe wengi kuliko idadi hiyo ya Mabalozi. Ndiyo maana tukasema kwamba tukipata uwakilishi wa mtu mmoja unaweza ukatosheleza ndiyo fikra zetu. Lakini kama kuna mawazo bora zaidi tutakaa tutazungumza tuone kama kuna namna bora zaidi ya kuwashirikisha wengine katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na pongezi kwa *African Union* kwa jinsi ilivyoshughulikia suala la Daful, ni kweli baada ya kutokea tatizo la Daful Mwenyekiti wa *African Commission*, Alfa Cornel alikwenda, baadaye alikwenda Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kufanya *assessment* ya hali wakarudi, taarifa ikatolewa, Baraza la Amani na Usalama likakaa na yakaamriwa kufanyika mambo mawili.

Kwanza, kusimamia mazungumzo yatakayoleta suluhu na la pili, ni kupeleka kwanza *observers mission* kujaribu kuangalia na kupeleka wanajeshi wale ambao ni *observers*. Haya yamefanyika na baadaye kumekuwepo na uamuzi wa Baraza la Usalama la Umoja la Mataifa likiitaka Serikali ya Sudan ichukue hatua kali zaidi itimize wajibu wake ipasavyo katika kuhakikisha kwamba mauaji yale yanasi mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Njelu Kasaka, kweli ni jambo la kusikitisha na ni jambo la aibu kwamba katika jamii hiyo hiyo moja watu

wanauana kwa rangi ya ngozi zao na yote hayo katika Umoja wa Afrika yamesimamiwa vizuri na yamekemewa na masikitiko yameelezwa na Serikali ya Sudan imetakiwa kutimiza wajibu wake ipasavyo. Wameahidi kufanya hivyo hebu tongoje tuone baada ya Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kama hakutokuwepo na utekelezaji na kama hakutakuwepo na utekelezaji chombo ambacho kinaweza kikachukua hatua madhubuti ni Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Mimi nadhani jambo lenyewe linasimamiwa vizuri nadhani tuliachie hapo lilipo.

Kuwekuwepo pia na pendekozo au maelekezo ya kwamba Wizara itumie vizuri mtandao uliopo wa Mabalozi hicho ndicho tunachokifanya, kwa kweli ndicho kitivo chetu cha kufanya kazi na sisi tunachoomba tu wenzetu wengine wote wakitumie, wako tayari pale ukiwatuma watakutumikia, usipowatuma wakati mwingine wao wenywewe watachukua *initiatives* zao na ndiyo maana tumesema kwamba sisi tutachokifanya mwaka huu tutajaribu kuona katika ufinyu bajeti tuliyokuwa tuchague Miji michache duniani mwaka huu tuweke *focus* ya kuitangaza Tanzania.

Kwa hiyo, watu wa watalii watakuwepo, wa madini watakuwepo, wa biashara watakuwepo na kila mmoja atakuwepo kwa pamoja tutatengeneza mkakati wa kuitangaza Tanzania. Sasa hii nadhani itatusaidia. Lakini bado kitivo kitakuwa ni Ubalozi katika nchi hiyo. Kama tulivyosema mwaka huu tukifanya Mji huu, mwaka ujao tunafanya katika Mji mwingine pengine baada ya miaka mitano, sita katika Bara nzima tunaweza tukawa tumefanikiwa kufanya hivyo. Kwa hiyo, ni ushauri ambao tumeupokea na sisi tunadhani tutakwenda nalo vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na pendekozo la kufanya semina. Semina za kuelimisha kuhusu masuala muhimu. Hilo jambo tumelipokea na tutakwenda kulifanya kazi kwa sababu ni vizuri pia watu wakayajua masuala kwa uhakika ili waweze kukusaidia na tunakusudia kuanza na *Custom Union* kabla ya kwenda kwenye mambo mengine yoyote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na suala la kufungua Ubalozi Brazil, hili tunalo kila mwaka. Sisi kwenye Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa tungependa kuwa na Balozi nyingi sana. Kwa hiyo, ni kama vile ukiwa unahubiri na sisi ni kwamba umeshawahubiria waliokwishaamini. Tatizo kubwa kwa kweli ni uwezo wa kifedha wa Serikali kwamba hatuwezi kuwa Balozi kila mahali na kwa hiyo na sisi pamoja na hali yetu ya kutaka tuwe na Ubalozi kila mahali bado tukubali kwamba pale ambapo Serikali itakapojenga uwezo ndipo tutakapoweza kufungua Ubalozi. Kwa hiyo, ombi tumelipokea lakini tutakapowezeshwa tutatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuteua Mabalozi wanawake tumelisikia na hili nalizungumza kila wakati kwa kweli na Mheshimiwa Rais anasikia tulikuwa na Balozi mmoja sasa tunaye wa pili. Mimi nina hakika kwamba kazi imeanza ya utekelezaji tuombe nafasi tu nadhani tutaendelea vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekozo la kwamba Wizara ipatiwe fedha za maendeleo. Kweli sisi katika Wizara tungependa sana na tunaombwa kila wakati lakini

kwa hali tu ya fedha tunakosa fedha za maendeleo. Nina hakika hapo uwezo utakapokuwa umepatikana tutapata fedha za maendeleo, lakini tunashukuru kwamba pale inapokuwa ni lazima kupata kitu Mheshimiwa Rais amekuwa anatusaidia sana kuweza kusaidiwa.

Kuhusu muundo wa Wizara sasa tunafanya zoezi hilo na ushauri walioutoa Kamati wameutoa wakati muafaka na mapendekezo yao tutayazingatia. Tatizo la kutokujibu barua hili kwa kweli ni tatizo la kweli na Balozi zetu zinalalamika sana hasa wanapowasiliana na Idara nyingine za Serikali kutokupata majibu mpaka tumewambia kwamba wakipeleka watuletee na sisi nakala ili tuweze kuwasaidia kufuatilia. Wakati mwingine mambo ya haraka yanachelewa kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, amezungumzia Kiswahili, alivyosema ni sawasawa. Sasa tufanyeje kuhusu Kiswahili na wengi wamelizungumzia suala la Kiswahili. Tukitangaze zaidi Kiswahili ni kweli. Rai kwamba sisi tukae na Wizara zinazohusika tutafanya hivyo. Hatua hii ya kwanza tuliofanikiwa kwa kweli ilikuwa ni hatua ngumu sana sisemi uongo. Tulitoa pendekozo hilo kwenye Mkutano wa Mawaziri Durban, Mawaziri wakalikubali tukawapeleka Wakuu wa Nchi wakakubali, tulipofikia kwenye hatua za sasa ya kuingiza uamuzi ule katika Katiba ya *African Union*, hapo pakaanza matatizo kweli kweli na kukawa na nguvu kubwa ya kukataa Kiswahili kisiingie. Hakuna haja ya kutaja nchi nyingine ni marafiki zetu sana huwezi kuamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tume-*struggle*, kubwa tumekipitisha katika vikao vitatu mpaka cha mwisho cha nne pale Addis Ababa, nikawa nawauliza mwenzangu nyie kama mnaona tabu kukiingiza Kiswahili na mnaweka masharti magumu ya kukiingiza, lugha gani ya Kiafrika nyingine itaingia, lakini tulipata *support* ya nchi nyingine ambazo hatukuzitegemea kabisa kama Senegal na Mali. Hatimaye tumeweza kufika hapo tulipofikia. Lakini hata baada ya uamuzi huu bado kukawa na watu pale wana-foot drag katika kuingiza Kiswahili nashukuru sana.

Naomba nitamke kwamba huyu Mwenyekiti wa sasa wa *African Commission*, Alfa Cornel nilipokwenda kumwona mwaka 2003 mwezi Septemba, tulipokutana New York tumezungumza akasema anataka Kiswahili Waziri kianze mwezi Julai, kwenye *African Union* na kweli. Tukakubaliana kwamba sisi tuanze gharama za kwanza halafu tutaendelea na namna ya kusaidiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nimtaje mtu mmoja hatukumtaja Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, baada ya kupata makubaliano ya msingi kwamba Kiswahili kitatumika nili-*constitute* Kamati na kwa kufahamu umahiri wake wa lugha ya Kiswahili yeye nilimpa Uenyekiti wa hiyo Kamati naye amefanya kazi nzuri sana mpaka tuweza kupata watu waliokwenda kukisimamia na kufanya tafsiri kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, wakati mwingine unaweza ukapata sifa, lakini wako wengine hasa avumaye papa baharini kumbe wengi wapo, ndiyo msemo wa Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kweli kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, ndiyo imewezesha Kiswahili hatimaye kuweza kutumika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, limekuwepo suala la ajira katika Wizara hasa kwa upande wa Wazanzibari wako wangapi, Mabalozi wako wanne, watumishi Maofisa wako 23 ni kidogo ingawaje si kidogo sana, lakini tunafanya jitihada. Tumejitahidi sana kujaribu kuongeza watumishi kutoka Zanzibar. Naomba nilieleze hili taratibu zetu za kawaida tunatangaza nafasi hizi watu wanaomba, waombaji kutoka Zanzibar wamekuwa kidogo na wale ambaو wamekuwa wanaomba katika mitihani tunayoifanya hii kupitia ile TUMEAJIRI imekuwa kwa kweli wengi hawafaulu.

Kwa hiyo, tukafanya uamuzi pale Wizarani kwamba sasa tukienda kwa *style* hii itafika mahali *Foreign Services* ya Tanzania itakosa Wazanzibar. Tufanya maombi rasmi kuiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itupatie Maofisa kutoka kule ili wapate ajira kwenye Serikali ya Muungano halafu tuwawekee kwenye *category* wanayostahili. Kwa sababu pia ya uchache wa Maofisa, wale Maofisa wazuri wange-fit sana nao pia Zanzibar wanahitajika.

Kwa hiyo, imetuchukua muda mrefu sana, lakini nashukuru mwezi uliopita tulipata majina 12 ambayo sasa tunayafanyia kazi tuone nani watakaofaulu waweze kuingia kwenye ajira. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tumekuwa tunalishughulikia si kwamba ni jambo tunalipuuza. Nimewaelezeni matatizo ambayo tumekuwa tunayapata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini *AICC* tu peke yake si ndiyo iliyopo. Maana ndiyo ukumbi wa mikutano uliokuwepo na ndiyo maana tumetoa wito sisi watu wawekeza jamani katika kujenga kumbi, watu wawekeze katika kujenga mahoteli ambayo yana kumbi za mikutano, mikutano itapatikana, lakini ikibaki *AICC* hakuna pengine pa kupeleka mkutano na hakuna mtu wa kulaumu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tukawahimize watu wetu kwenye Majimbo yetu huko ili wawekeze katika kumbi za mikutano ili mikutano iende kwingine zaidi ya *AICC*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania si kinara tena, hili si kweli nimeelezea kwa kiasi gani sasa hivi Diplomasia ya Tanzania inang'ara. Mimi nadhani hili halina ubishi sifa tumezieleza na dalili zipo za kutosha tu. Orodha ni ndefu sana ukichukua akina Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Wenyeviti huko watu wengi tu. Lakini yote ni kuonyesha kwamba kwa kweli tuko katika mstari wa mbele kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kujipanga kuzuia kuburuzwa, mimi nasema hakuna mtu anayeweza kutuburuzwa sisi pamoja na umaskini wetu, tunapenda sana hali ya Utaifa wetu kuburuzwa hilo toa wasiwas. Mtu ukiona tumekubaliana naye ameturidhisha kwa hoja, lakini kwamba atatuburuza haiwezekani. Kwa hiyo, nasema tutakubaliana naye kama tunaridhika kwamba maslahi yetu pale yapo. Sasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki nilichokisema jamani kilichotengenezwa ni kwamba ukiwa na bidhaa unaweza ukaiuza Kenya bila ya ushuru, unaweza kuiuza Uganda bila ya

ushuru, suala kubwa ni wewe kuwa na bidhaa hakuna mtu wa kuja kukutengeneza bidhaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sisi wenyewe sasa tutazalishé bidhaa za kuuza kwenye hilo soko. Sasa hili ni letu sisi wenyewe ndilo ambalo nasema jamani tuchangamke tujipange vizuri ili tuweze kunufaika vinginevyo watanufaika wengine sisi tutalaumu na kwa sababu siku hizi Serikali haifanyi biashara suala kubwa kwa upande Serikali ni kutegenenza mazingira yatakayowawezesha wafanyabiashara kuwekeza katika uzalishaji na utoaji wa huduma zitakazouzwa katika soko la Afrika ya Mashariki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kushindwa kulaani maovu, hiyo si kweli kila palipotokea matatizo tumeeleza msimamo wetu kuhusu Iraq, Marekani na Waingereza walipokwenda pale bila ya ridhaa ya Umoja wa Mataifa, tumeeleza *position* yetu kuhusu Israel, ila tunachokisema ni kwamba watu wasitegemee kwamba kila pakitokea tatizo asubuhi tunatoa tamko sasa kazi hiyo kwa kweli itafika mahali itatushinda. Tunatoa matamko pale ambapo tunadhani sasa imefika wakati muafaka kusema hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukitokea mlipuko Baghdad mnatoa tamko, ikitokea Jerusalem mwishowe itafika mahali watu watachoka na matamko. Lakini nasema kwamba kuna mambo ya msingi mnafoka tu sasa kufoka kutazidi mno ni vizuri pia useme mara machache ili utakaposema watu wawe na hamu ya kusikia. Taarifa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa leo wanamsema nani mkishafika hapo watu pia watakuwa wanawakebehi. Kwa hiyo, nasema mtuelewa hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Ulinzi kusaidiana na sera ya Mambo ya Nje kwa *nature* yake Jeshi ni chombo cha Sera ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ina kazi ya kulinda nchi dhidi ya nchi nyingine yenyewe hiyo ni *element* ya *Foreign Policy*. Kwa hiyo, sisi tuna ushirikiano wa karibu sana kuna Kamati yetu tu ya ndani ambapo ni sisi watu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ndiyo Mwenyekiti na wenzetu wa Jeshi la Ulinzi na Idara ya Usalama wa Taifa tunakutana mara kwa mara chini ya Uenyekiti wetu sisi kuchambua masuala mbalimbali haya ya Kitaifa na kuweka msimamo kama nchi msimamo uwe upi, hawa wana habari hizi na hizi na tunachanganya na zetu sisi tunafanya sana hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawahakikisheni kwamba kuna a lot of linkage na kufanya kazi pamoja kati ya vyombo vyetu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ya Mashirika ya Kimataifa kwa nini Watanzania ni kidogo. Watanzania ni kidogo kwa sababu tunajua lugha moja tu Kiingereza. Mashirika mengi ya Kimataifa yanataka watu wanaojua lugha mbili mbili na Watanzania inapofika mahali kwamba anatakiwa mtu *by bilingual that the end cap*.

Sasa nadhani ni vizuri tuangalie ni namna gani tunaweza ku-*improve own our curriculum so that* Watanzania wengi wanapata lugha ya pili ili iweze kuwa rahisi kuajiriwa kwenye Mashirika ya Kimataifa. Ndiyo maana unawakuta wa Cameroon wengi kwa sababu wao nchi yao ni *bilingual*. Kwa hiyo, nasema ni vizuri labda kwa sababu ya Kiswahili *African Union* labda, lakini kama Umoja wa Mataifa tutayapata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Visa* limezungumzwa nadhani limeelezwa vizuri. Jamani ni tatizo la kweli. Tulizungumza mwaka jana hapa na tumechukua hatua tumewapelekea barua Mabalozi za *protect*, ku-*protect* jinsi wanavyowatendea watu wetu kuwa si vizuri. Wako wamekuja jamani mbona mnafanya hivi tukasema tufanyeje sisi kama hivi ndivyo mnavyofanya, wakasema mnajua pale mlangoni kuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna mambo ambayo tumekuwa tunaendelea kuzungumza nao ila wenzetu hawa bwana ni wagumu. Si vizuri sana kusema kwamba wana ukaidi, lakini ni wagumu kwa kweli kusikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuchanganya hayo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyachangia kwa maandishi yamejumuika. Lakini niyazungumze baadhi katika muda uliobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Chubi amezungumzia ukumbi wa *VIP*, kwa nini watoto hawaruhusiwi kuja. Ukumbi ule una viti 28 tu yaani ukiona *delegation* ya Waheshimiwa Wabunge sita hivi pameshajaa kabisa. Ndiyo maana kweli ukatolewa ushauri kwamba jamani ehee kama watoto hebu jamani wapite katika taratibu nyingine ni lile lile kwa sababu ya nafasi yenyewe ni ndogo.

Sasa kama tutafanikiwa huko mbele safari tukajenga *VIP* kubwa zaidi tutawenza kwenda na watoto na wajukuu, mimi nafikiri itafika katika *stage* hiyo. Kwa sababu ya *stage* ya sasa mimi naomba tuvumilie kwa sababu kwa kweli nafasi pale ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Visa* limezungumzwa ambalo tumekwishalieleza. Mheshimiwa Remidius Kissassi amezungumzia Ofisi ya Zanzibar ambayo pia ameizungumzia rafiki Mheshimiwa Mohamed Adully Ally, tujenge Ofisi mpya. Tuseme kwamba tumelisikia hatuwezi kusema ndiyo ama hapana, lakini tumelisikia tuachieni tuone kama kuna uwezekano huo. Lakini nyumba ile tulipewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sasa kama historia yake, lakini sasa aliyeondoka si kaondoka na nyumba imekuwa mali ya Serikali. Lakini kwa sababu ya historia hiyo aha bwana wee, ngoja tuone tunachoweza tukafanya kwenye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa hatimiliki wa kiwanja cha Chuo cha Diplomasia, tumepiga hatua, *originally* Chuo kile kilikuwa cha Msambiji, kwa hiyo, hati zile zilikuwa mikononi mwa Msambiji, baadaye tumekifanya kuwa Chuo cha Diplomasia chetu sisi na wao ikawa kila tukifutilia wenzetu *somehow* zile hati wame-*misplaced*. Kwa hiyo, wameshaandika *affidavit* kuthibitisha hiyo na wenzetu wa

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, wanatusaidia wamekwishatoa matangazo tayari nadhani baada ya muda tutakuwa tumepata hati kamili ya Chuo chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Chubi, amezungumzia juu ya *Protocol* anasema hivi *Geneva Convention* ina utaratibu wa *Protocol*, mbona Wabunge katika orodha tunakuwa wa kumi na nne, lakini wanasema zile *organs* ziko tatu na Bunge ni sehemu ya hiyo na katika nchi tunasema yuko Rais, yuko Makamu halafu Spika, lakini Wabunge wale ni wa kumi na nne katika orodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila nchi inatengeneza utaratibu wake. Sasa kwa utaratibu wetu wa Tanzania pale ndipo alipo Mbunge. Ni jambo ambalo tunawenza tukakaa tukazungumza na tukawaambia hawa wanaotengeneza hizi taratibu labda tukaweza tukawekwa mahali pengine zaidi ya hapo. Tulivyo sasa tukubali hivyo lakini hakuna maelekezo ya kidunia kwamba mfanye hivi. Maelekezo ya kidunia yatakuwepo Rais lazima atakuwa ni wa kwanza na kama mahali kuna Mfalme, Mfalme atakuwa *number one*. Mnaanza kumtaja *His Majesty and Excellency is present*. Huu ndio utaratibu za himaya. Lakini hizi nyingine huku nani amekuwa *slotted* wapi hiyo inategemea taratibu za nchi zinavyokwenda. Kwa hiyo, naamini kwamba iko siku pengine tukikaa kutazama upya tutaweza pengine Waheshimiwa Wabunge kuwa mahali pengine pazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Eliachim Simpasa amezungumzia habari ya Wakimbizi. Hili limezungumzwa sio tu na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Beatus Magayane na hasa suala kubwa ni kwamba huko nyuma Rais alizungumzia suala la Wakimbizi walindwe katika nchi zao wanazotoka. Zitengenezwe *safe...* baina ya nchi zao ili waangaliwe huko.

Ni kweli tumelizungumza sana Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, anakumbuka katika Mkutano wa mwisho pia tumezungumza suala hilo. Ni jambo linalofanyika, lakini pia linafanyika katika mazingira maalum. Ila kwa mazingira tuliyokuwa nayo sasa Wakimbizi wetu wengi wanatoka Burundi. Burundi imeshaanza kupata amani. 95% ya *countries pacify* na Wakimbizi wameshaanza kurudi kwa kasi nzuri.

Mimi nadhani kwa sasa hivi suala letu kubwa ni sisi na Serikali ya Burundi na *UNHCR* tukashirikiana vizuri kuongeza kasi ya Wakimbizi kurudi kwao. Pengine masuala haya baada ya muda si mrefu yanaweza pia yasiwe ni suala la kuzungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Njelu Kasaka, amezungumzia Rwanda na Burundi kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wakati huo kuna pendekeso kwamba kutoka Kamati yetu ya Bunge ya Mambo ya Nje ikisema kwanza jamani sisi wenyewe watatu tuzoeane, tujijenge halafu ndio waingie wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wetu wa nchi zetu tatu wameshatamka rai yao ya kutaka Rwanda na Burundi ziingie. Sasa hivi taratibu zinafutiliwa juu ya Rwanda na Burundi kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa

masharti ya mkataba uliokuwepo. Sasa masharti yale ya mkataba yanazo sifa nyingi. Tutakapokaa na kuchambua tunaweza tukaona ipi iko tayari sasa na ipi itafuatilia.

Kwa hiyo, ni masuala ambayo yamekuwepo yanashughulikiwa itaonekana ni lini itaingia. Sisemi kwamba ni kesho lakini sidhani kwamba ni muda mrefu kutoka sasa. Ila lazima nikiri kwamba mawazo yako hayo mawili wako wanaosema waje sasa na wako wanaosema wasubiri kidogo na wako wanaosema wasije kabisa hata hayo pia ni yapo. Lakini nadhani hiyo ya busara tukiwapata wenzetu wa Rwanda na Burundi eneo letu linapanuka. Lakini lini waingie kwa masharti gani, kwa taratibu gani hayo ni maamuzi ambayo sisi ambao sasa hivi ni wanachama ndio tunaofanya uamuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo, anasema kuna minong'ono watu wanauliza kwa nini Tanzania iko *SADC* sio nchi ya Kusini badala ya kuwa Afrika ya Mashariki? Unajua historia ya *SADC* ilianza kama *The Southern Africa Development Coordination Conference*. Uamuza wake ulifanyika Arusha. Mwenyekiti wa uamuza ule alikuwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wakati ule akiwa Rais wetu. *Background* yake ni kwamba wakati ule nchi za *frontline* zilipokuwa zinaongoza harakati za mapambano. Yalipokuwa sasa yanaseoga kuna baadhi ya nchi zilikuwa ni muhimu sana ili uweze kufanikiwa kuangusha makaburu ufanikiwe kuangusha na wengine. Lakini nchi hizi zinaitegemea Afrika ya Kusini kiuchumi. Ndipo ukatokea uamuza kwamba ili tufanikishe hizi harakati za ukombozi tutengeneze utaratibu utakaoziondoa nchi hizi katika kuitegemea Afrika ya Kusini ili wasiwe na kigugumizi katika kusaidia harakati za ukombozi, ndipo ikaamuliwa kwamba tuanzishe hii *Southern African Development Coordination Conference* na ndiyo maana wakati huo utakuta zaidi ilikuwa ni kujenga uwezo na ndiyo maana shughuli zote zilikwenda kwenye sekta. Wanaangalia sekta ya nishati, barabara na kadhalika, ambapo sasa hivi ndio tuna Jumuiya kwa maana tunajenga hasa zaidi tunafikiria kujenga soko.

Kwa hiyo, ndiyo historia yake na ndiyo maana huwezi ukaitengeneza *SADC* bila ya Tanzania kuwemo. Imeanza uamuza umefanyika katika *Frontline States* lakini wakakubaliana wakati ule kwamba Marehemu Seretse Khama ashughulikie *economic wing* na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ashughulikie *The Political and therefore the military wing also* katika harakati za ukombozi.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo historia yake na historia hiyo ina manufaa, ina umuhimu wake na ni muhimu kui-*maintain*. Sasa hivi tumeingiza mpaka Mauritius iko Kusini, nadhani hivi sasa Madagascar wanaweza kuwa ndio *the next in line*. Sasa nasema hii iko Kongo kwenye *SADC*. Kwa hiyo, nasema yako maneno haya na mimi nayasikia lakini nadhani hoja zake si za msingi. Wako watu ambao wakikuchukia basi wanaweza kutafuta lolote lile wakalisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Leonard Derefa amezungumzia malipo ya posho za safari kwa watumishi wanaokwenda kikazi nchini Uingereza walipwe kwa *Sterling Pound* badala ya *US Dollar* kwa vile maisha ni ghali sana. Pia wafanyakazi wetu katika ubalozi walipwe mshahara kwa *Sterling Pound* badala ya *dollar*.

Mimi nasema ukilipa kwa *Dollar*, *Pound*, *Euro* kinachotakiwa wakulipe kiasi ambacho kitakuwezesha kupata *Pound* ile. Nadhani hili ndilo la msingi, kwamba kama ulistahili kulipwa *Pound 100* sasa kama *dollar 172* ndiyo *Pound 100* ulipwe *dollar 172* ili ukienda Uingereza uweze kupata *Pound 100*. Nasema hili ndilo suala la msingi. Hivyo hivyo kwa mishahara ya watumishi wetu na mengineyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Serikali inafuatilia vipi suala la kupambana na ugaidi hasa wakati wa kuelekea Uchaguzi Mkuu. Kwanza huyu Bwana Ahmed Khalfan Khairan. Imetoka kwenye vyombo vya habari vya Kimataifa amekamatwa. Siku hiyo *BBC* wakanahoji, nikawaambia jamani na mimi nimeona sasa hivi kwenye *flash* tu kwenye *CNN*. Kwanza lazima tuthibitishe kama kweli ni Mtanzania. Maana wako watu wanatembea na *passport* za Tanzania, wapo Watanzania wana *passport* za Somalia. Wengine wanajiita Warundi, wakati mmoja kuna Watanzania walikufa karibu saba pale Pakistan kwenye nyumba moja, *I don't know what happen*. Walikuwa wanaishi pale kama Wanyarwanda lakini Watanzania wenzao ndio wakatupigia simu *hallow*, wale ni Watanzania lakini wanaishi pale kama Wanyarwanda.

Kwanza sikia aliyekamatwa na *passport* ya Tanzania, wewe unasema unaanza kuhangai kama Mtanzania lakini tumeangalia kwenye rekodi zetu ni kweli Ahmed Khalfan Khairan ni Mtanzania. Yeye huyu ni mmoja wa washukiwa wakuu wa ulipuaji wa Ubalozi wa Marekani pale Jijini Dar es Salaam na aliondoka nchini tarehe 5 Agosti, 1998, siku mbili kabla ya tukio lenyewe kutokea. Aliondoka kwa jina la bandia na amekuwa anaishi katika majina ya bandia. Alikuwa anasoma mpaka *Form Five*, akatoroka ameingia kwenye harakati hizo. Mwenzake ndiyo yule mwingine aliquja akakamatwa *Cape Town* ameshafungwa maisha. Sasa nasema na mwingine ambaye yupo hapa Mahakamani na anashtakiwa.

Kwa hiyo, ni kweli kama wanakwenda huyu kwenda kule sio mtu aliyechukuliwa kwa ajili ya kwenda kujifunza ugaidi huyu tayari alikwishakuwemo. Maana kilichomkimbiza hapa ni kwamba alikwishajua kwamba tayari na inaaminika kwamba huyu ndiyo aliyekuwa ana ile gari ya *Nissan* iliyotumika kwa ajili ya *bombing*. Kwa hiyo, nasema ni Mtanzania mwenzetu. Sasa tunafanya nini kuhusu Watanzania walioko nje wako wengi kweli. Wengi hawa wanaganga njaa. *The majority of them are economic refugees*. Ni *Economic refugees* lakini akifika pale anasema unajua Zanzibar pale, sisi tumekaa kule Zanzibar tunateswa sana sisi wa Chama cha Upinzani. Basi unamwangalia unasema wewe unateswa kwa Chama cha Upinzani mbona Seif Shariff anarudi. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe unasema kama kweli Zanzibar kuna operesheni ya watu wa *opposition* basi wa kwanza kukimbia angekuwa Seif Sharif, lakini Seif Shariff yupo. Khalifa Suleiman Khalifa yupo, lakini mtoto wa Khalifa yuko London anasema amekimbia mateso ya kisiasa. Nasema ni vitu ambavyo kwa kweli wanajaribu kutafuta mwanya wengine baada ya kushindwa hivyo wanajiita Wasomali, Warundi wanafanya hivyo. Kwa hiyo, kuna mambo hayo. Nadhani walio wengi mimi sidhani kwamba ni watu ambao hatari kwa usalama wetu si wengi, si wengi. Lakini na sisi pia kazi ya Balozi ni kuangalia masuala ya usalama pia tunayaangalia. Wakati mwingine

ndio nataka kuiongeza hapa muielewe hekima iliyowafanya watu wakaingiza *Geneva Convention* na ile *Diplomatic Immunities*. Kwa sababu wako watu wanafanya hiyo kazi.

Sasa katika kufanya hiyo kazi ukakosea mahali. Sasa mtu wetu akikosea mahali tusingependa sisi akifika pale anapelekwa kwenye Mahakama ile. Watatuambia yeye amefanya hivi wanasema muondoeni *immunity*, hatutaki, mfukuzeni, anafukuzwa. Nasema nayo ina historia yake sio sana kwa matatizo haya. Lakini nasema hatuna wasi wasi huo na wale ambao wanafanya vitendo na sisi tunayo jitahada ya kuwajua. Kwa hiyo, nasema wengi ni *economic refugees* lakini kama wapo ambao ni hatari na sisi watu wetu walioko kule watatusaidia kuwajua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipewa dakika 40 naona zinaisha. Sasa zilizobakia nimalizie kwa hizo dakika mbili zilizobakia. Niseme tu kwamba jamani mmetupa ushauri mwingi ambao tutaufanyia kazi. Hata wale ambao hatukuweza kuwajibu hapa tutawapatia majibu ambayo tutayatoa. Sasa nimalizie kwa hili la ununuzi wa jengo la ofisi yetu ya Rome.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001/2002 Wizara ilinunua jengo la ofisi ya Ubalozi, *Counsel* katika Ubalozi wa Rome katika jitihada za kuondokana na tatizo la kupanga majumba ya watu huko nje na pia kupunguza gharama za kuendelea kulipa pango la nyumba kila mwaka. Ununuzi wa jengo hili zilifuata taratibu zote za ununuzi wa majengo ya Serikali kwa kuzishirikisha Wizara za Ujenzi, Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Fedha. Jengo lilifanyiwa tathmini na wataalamu wetu hao na kukubaliana na ununuzi wa *Euro 3,098,741.40*. Tarehe 6 Machi, 2002 fedha za awamu ya kwanza katika Ubalozi wa Rome zilipelekwa nazo ilikuwa ni shilingi 700,000,000/=. Tarehe 28 Juni, 2002 zilipelekwa shilingi 120,000,000/=. Mwishoni, tarehe 26 Agosti, 2002 tena zikapelekwa shilingi 1,000,000,000/= jumla ya fedha zilizokuwa zimepelekwa zikafikia shilingi 2,900,000,000/=. Baada ya hapo Ubalozi wetu ulitekeleza taratibu zote za ununuzi wa jengo husika na kumlipa mwenye nyumba kiasi hicho cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulitokea hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kweli hoja 142.6.7. Mkaguzi Mkuu alihoji Wizara ya kuwa alipofika Ubalozi wetu Rome kukagua hakuona hati yoyote ya jengo hilo. Lakini napenda kueleza kuwa hati ya nyumba hivi sasa ipo Ubalozini nakala imeletwa Wizarani kwa ajili ya hifadhi na pia Mdhibiti Mkuu ameshapelekewa nakala ya hati hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo niombe radhi tena kwa wale ambao sikuweza kuyajibu masuala yao hapa lakini tunawahakikishia kwamba tutayajibu kwa maandishi. Baada ya kusema maneno hayo naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i>	2,025,139,700/=
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	327,164,200/=
Kifungu 1003 - <i>Foreign Affairs Office Zanzibar</i>	173,037,900/=
Kifungu 1004 - <i>Policy and Planning</i>	465,726,200/=
Kifungu 1005 - <i>International Cooperation</i>	1,740,021,100/=
Kifungu 1006 - <i>Europe and America</i>	238,304,500/=
Kifungu 1007 - <i>Asia and Australia</i>	229,945,200/=
Kifungu 1008 - <i>Africa and Middle East</i>	1,981,471,800/=
Kifungu 1009 - <i>Regional Cooperation</i>	1,237,019,200/=
Kifungu 1010 - <i>Protocol</i>	2,323,673,900/=
Kifungu 1011 - <i>Legal Services</i>	203,417,900/=
Kifungu 2001 - <i>Embassy of Tanzania - Addis Ababa</i>	564,199,200/=
Kifungu 2002 - <i>Embassy of Tanzania - Berlin</i>	768,807,700/=
Kifungu 2003 - <i>Embassy of Tanzania - Cairo</i>	586,494,900/=
Kifungu 2004 - <i>Embassy of Tanzania - Kinshasa</i>	597,986,600/=
Kifungu 2005 - <i>High Commission of Tanzania - Abuja</i>	511,337,100/=
Kifungu 2006 - <i>High Commission of Tanzania - London</i>	1,479,663,900/=
Kifungu 2007 - <i>High Commission of Tanzania - Lusaka</i>	689,299,800/=
Kifungu 2008 - <i>Embassy of Tanzania - Maputo</i>	500,344,000/=
Kifungu 2009 - <i>Embassy of Tanzania - Moscow</i>	926,287,800/=
Kifungu 2010 - <i>High Commission of Tanzania - New Delhi</i>	800,320,200/=
Kifungu 2011 - <i>Permanent Mission To the Un - New York</i>	1,974,149,000/=
Kifungu 2012 - <i>High Commission of Tanzania - Ottawa</i>	774,341,900/=
Kifungu 2013 - <i>Embassy of Tanzania - Paris</i>	972,773,700/=
Kifungu 2014 - <i>Embassy of Tanzania - Beijing</i>	708,787,700/=
Kifungu 2015 - <i>Embassy of Tanzania - Rome</i>	978,392,000/=
Kifungu 2016 - <i>Embassy of Tanzania - Stockholm</i>	912,176,900/=
Kifungu 2017 - <i>Embassy of Tanzania - Tokyo</i>	1,336,468,300/=
Kifungu 2018 - <i>Embassy of Tanzania - Washington</i>	1,193,876,200/=
Kifungu 2019 - <i>Embassy of Tanzania - Brussels</i>	838,755,000/=
Kifungu 2020 - <i>Permanent Mission To the UN - Geneva</i>	1,146,792,000/=
Kifungu 2021 - <i>Embassy of Tanzania - Kampala</i>	475,502,000/=
Kifungu 2022 - <i>High Commission of Tanzania - Harare</i>	485,653,700/=
Kifungu 2023 - <i>Embassy of Tanzania - Nairobi</i>	597,857,900/=
Kifungu 2024 - <i>Embassy of Tanzania - Riyadh</i>	493,720,800/=
Kifungu 2025 - <i>Embassy of Tanzania - Pretoria</i>	693,496,500/=
Kifungu 2026 - <i>Embassy of Tanzania - Kigali</i>	379,327,300/=
Kifungu 2027 - <i>Embassy of Tanzania - Abu-Dhabi</i>	393,723,600/=
Kifungu 2028 - <i>Embassy of Tanzania - Bujumbura</i>	525,550,600/=

Kifungu 2030 - *Embassy of Tanzania - Lilongwe* 341,287,700/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu iyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, haijapata kutokea. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa sababu kuna mwenzetu anataka kutoa hoja baada ya kuahirisha Bunge, sasa namwita *Chief Whip* atoe hoja hiyo ya kuahirisha Bunge.

KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 21 kifungu kidogo cha (6) naomba Bunge lako Tukufu liahirishwe kabla ya muda wake hadi kesho saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

HOJA BINAFSI

HALI MBAYA YA USALAMA ILIYOKO WILAYANI KASULU

MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maeleo binafsi ya kutaka ufanuzi kuhusu hali mbaya ya usalama iliyoko Wilayani Kasulu. Maeleo haya yanatolewa chini ya Kanuni ya 21(9) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za hivi karibuni wananchi wa baadhi ya maeneo ya Jimbo langu la Uchaguzi la Kasulu Magharibi na Mji wa Kasulu katika ujumla wake wamekuwa wakiishi katika hali ya mashaka mashaka kutokana na kuzorota na kukosekana kwa hali ya usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mifano michache ili kuthibitisha ukweli huo. Tarehe 16 Juni, 2004 majira ya usiku Ndugu Juma Hungu na nduguye kwa nyakati tofauti walivamiwa na majambazi na kupigwa kwa marungu, kukatwakatwa kwa mapanga na kuporwa mali zao kadhaa. Tarehe 16 Juni, 2004 siku hiyo hiyo majira ya usiku tena majambazi walimvamia Ndugu Ndeka, mkazi wa Mdyanda Kasulu na kumpora fedha na mali nyingine kisha wakapiga risasi hewani na kutokomea porini.

Aidha, tarehe 28 Julai, 2004 majambazi waliteka gari aina ya *Coaster* mali ya Ndugu Fanuel Ntabaliba na kumpora kiasi cha shilingi 485,000/= na mali nyingine nyingi zikiwemo simu za mkononi. Katika tukio hilo watu wafuatao walipigwa risasi na marungu sehemu mbalimbali za miili yao na natoa mifano ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu Paschal Kababaye alipigwa risasi mguu wake wa kushoto na kuporwa shilingi 60,000=/. Mwenyekiti wa Serikali ya Mwayaya alivunjwa mguu wake wa kushoto kwa kupigwa rungu na kuporwa shilingi 44,000=/. Aidha, Ndugu Elias Banebangu, *VEO* wa Kijiji cha Mwayaya aliumizwa kwa kuteguliwa bega lake la kulia na kuporwa shilingi 45,000/= na Ndugu Fanuel Kasogota, wakati huo aliporwa shilingi 205,900=.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Julai, 2004 Ndugu William Rubvingagiza wa Mjini Kasulu naye alivamiwa na majambazi na kuporwa mali zenye thamani ya shilingi 1,971,000=/. Aidha, maduka mengine ya wafanyakishara Mjini Kasulu kama vile duka la Bwana Dunia na Bwana Isaya Doya, nayo yalivunjwa na mali iliyopotea thamani yake haikupatikana mpaka tulipopata taarifa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali hii ni mifano michache tu ya matukio ya wananchi kupigwa na kuporwa mali zao. Kinachowashangaza wananchi na mimi Mbunge wao ni utendaji wa Jeshi la Polisi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iweje matukio yote hayo yatokee na Polisi wapo wasichukue hatua zozote kwa mujibu wa kazi zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni tafsiri yangu mimi na mtu mwingine yeyote anayeguswa na matukio hayo kuwa ama Polisi hawafanyi kazi yao, ama hawajali kufanya kazi yao kwa sababu wanazofahamu wao wenyewe kwa mfano doria inayofanywa na Polisi katika eneo hilo ni kuanzia saa 1.30 hadi saa 2.00 usiku kitu ambacho hakiwezi kueleweka na wananchi wanaopenda amani na utulivu. Aidha, Kituo cha Polisi ambacho kinapaswa kuwa wazi wakati wote hufungwa saa 1.30 usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiwasiliana mara nyingi na Wizara husika na kuwaeleza juu ya kukerwa kwa wananchi wa Kasulu dhidi ya vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya Askari wa Jeshi la Polisi hususan kutolinda raia na mali zao, kutowatendea haki hata pale raia wanapopeleka mashtaka kwenye Vituo vy'a Jeshi hilo pamoja na yale ya kuwabambikizia kesi na kuwaweka ndani kwa muda mrefu bila kuwafungulia mashitaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa hali ya usalama katika Wilaya ya Kasuli inazidi kuwatia hofu kubwa wananchi wake hasa pale ambapo Mitaa mingi husikika milio ya bunduki lakini hawapati maelezo yoyote wala kujulishwa hatua zilizochukuliwa kuhusu wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na matukio hayo, nataka maelezo kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa nini hali hiyo iendelee kuwa hivyo na kusababisha wananchi kuendelea kutokuwa na imani na usalama wa maisha yao na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka tamko la Serikali kuhusu hatua zitakazochukuliwa kudhibiti hali hiyo mbaya katika Wilaya ya Kasulu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo haya yanayohusu usalama wa raia na mali zao kwa raia wote wa Wilaya ya Kasulu, Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani sana, ahsante sana. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, tumeyapokea maelezo ya Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi. Katika maelezo yake anataka ufanuzi wa kina juu ya mambo mengi ambayo ameyaeleza na maadam anataka ufanuzi wa kina, kwa kweli tutahitaji muda wa kuandaa hayo maelezo na tutakuja kuyatoa kwenye Bunge hili katika Mkutano wake unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hatutasubiri kutoa maelezo katika kuchukua hatua ambazo zitahakikisha kurejea kwa amani katika Jimbo la Kasulu, mara moja tutaagiza ulinzi uimarishe katika Wilaya, tutatafuta taarifa za hao askari ambao wanafanya ulegevu na tukiwabaini tutachukua hatua zinazopasa. Lakini maelezo ya kina tutakuja kutoa katika Bunge lijalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya kuahirisha Bunge.

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Saa 12.34 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano tarehe 4 Agosti, 2004 saa tatu asubuhi*)